RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia Juni 30, 2013

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.
Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja
Kumb. Na. FA.27/249/01/2012/13 Tarehe 28/03/2014

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
DAR ES SALAAM.

Yah: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Juni 30, 2013

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 48 cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninayo heshima na taadhima kuwasilisha kwako ripoti kuu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 juni, 2013 kwa taarifa na hatua za utekelezaji. Nimetoa mapendekezo ambayo kama yatatekelezwa, yanaweza kutumika ili kupunguza dosari zilizojitokeza na kurekebisha sababu zilizopelekea kutokea kwa mambo yaliyoripotiwa katika taarifa hii.

Nawasilisha,

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Yaliyomo

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania..... xv

TAFSIRI/VIFUPISHO.....xvii

Dibaji.....xix

Shukrani.....xxii

Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Taarifa ya Ukaguzi xxv

SURA YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI NA MAMBO YA UJUMLA 1

1.2 Viwango vinavyotumika vya Ukaguzi na taratibu za utoaji taarifa 6

1.3 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi 9

1.4 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 12

SURA YA PILI..... 17

2.1 Maana ya Hati za Ukaguzi 17

2.2 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi katika Halmashauri 22

SURA YA TATU 29

3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA 29

3.1 Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka iliyopita 29

3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). 32

SURA YA NNE 37

4.0 TATHMINI YA HALI YA FEDHA ZA HALMASHAURI..... 37

4.1 Ukaguzi wa Bajeti..... 37

4.2 Mwenendo wa Makusanyo ya mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa 38

4.3 Fedha zilizotolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa 40

4.4 Fedha zilizotolewa pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti 41

4.5 Matumizi yaliyofanyika bila kuwepo katika bajeti 44

4.6 Mwenendo wa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri ikilinganishwa na matumizi ya kawaida 46

4.7 Ruzuku ya matumizi ya kawaida isiyotumika..... 47

4.9 Fedha ambazo hazikutumika miaka iliyopita hazikujumuishwa kwenye bajeti ya mwaka huu (2012/2013) wa fedha..... 49

4.10 Makusanyo Pungufu katika vyanzo vikuu vya mapato ya ndani 50

SURA YA TANO 53

5.0 MASUALA MUHIMU YALIYOJIRI KATIKA UKAGUZI WA HESABU NA TATHMINI YA UDHIBITI WA NDANI..... 53

5.1 Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na masuala ya utawala bora 53

5.3 Usimamizi wa Fedha..... 78

5.4 Usimamizi wa Rasilimali watu 84

5.5 Usimamizi wa Mali 106

5.6 Mapitio ya usimamizi wa Matumizi.....114

5.7 Masuala Mengine 126

SURA YA SITA.....133

6.0 Ukaguzi wa Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo (LGDG) 133

6.1 Ruzuku ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ..133

6.2 Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) 141
6.3 Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuthibiti UKIMWI (NMSF) 2008-2012 (NMSF)/TACAIDS 145
6.5 Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana 151
6.6 Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)..... 152
6.7 Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) 154
6.8 Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 156
6.9 Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF) 157
6.10 Mpango mkakati wa Miji Tanzania (TSCP) 158
6.11 Fedha za Miradi ambazo hazikutolewa..... 159
6.12 Miradi ambayo haijatekelezwa 160
6.13 Miradi iliyokamilika lakini haitumiki 161
6.14 Miradi ambayo haijakamilika 161
SURA YA SABA 165
7.0 Usimamizi wa mikataba na manunuzi 165
7.1 Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za manunuzi..... 165
7.2 Ufanisi wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU)..... 166
7.3 Tathmini ya usimamizi wa mikataba na ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi, na huduma katika Serikali za Mitaa 167
SURA YA NANE 177
8.0 KAGUZI MAALUM 177
8.1 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum 177
8.1.5 Halmashauri ya Wilaya ya Ileje 191
8.2 Mambo ya kujifunza katika Kaguzi Maalumu zilizofanyika mwaka huu 202

SURA YA TISA 207
9.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 207
9.1 MAJUMUISHO YA JUMLA 207
9.2 MAPENDEKEZO 214
9.3 Mapendekezo kwa Serikali kupitia kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 220
VIAMBATISHO 229

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na.1: Idadi ya Wakaguliwa 10
Jedwali Na.2: Upotoshwaji katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwaka..... 15
Jedwali Na.3: Halmashauri zilizorekebisha taarifa za fedha kwa miaka mitano mfululizo kufuatia ukaguzi uliofanyika 15
Jedwali Na.4:Hati za Ukaguzi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitano 23
Jedwali Na.5: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotelewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ripoti ya mwaka wa fedha 2011/2012: 30
Jedwali Na.6: Mwenendo wa masuala yaliyosalia kwa miaka mitano mfululizo katika ripoti za kila Halmashauri..... 30
Jedwali Na.7:Muhtasari wa masuala yaliyosalia katika ripoti za ukaguzi maalum..... 32
Jedwali Na.8: Mwenendo unaoonesha bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya makusanyo halisi..... 39
Jedwali Na. 9: Mwenendo wa fedha ambazo hazikupokelewa.... 42
Jedwali Na.10: Mwenendo wa fedha za maendeleo ambazo hazikupokelewa..... 43
Jedwali Na.11: Matumizi yaliyofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kuwepo kwenye bajeti 45
Jedwali Na. 12: Mwelekeo wa mapato ya ndani dhidi ya matumizi ya kawaida 46
Jedwali Na.13: Mwenendo wa ruzuku ya kawaida ambayo haikutumika kwa miaka mitano mfululizo..... 47
Jedwali Na.14: mwenendo wa fedha ambazo hazikutumika za miradi ya maendeleo 49
Jedwali Na.15: Orodha ya Halmashauri ikionesha makusanyo pungufu ya Kodi ya Majengo..... 51
Jedwali Na.16: Halmashauri zenye mkaguzi/wakaguzi mmoja au wawili 58

Jedwali Na.17: Orodha ya Halmashauri ambazo hazijaweka kumbukumbu katika daftari la mihadi na matumizi 66
Jedwali Na.18: Orodha ya Halmashauri ambazo zina Masurufu yasiyorejeshwa 68
Jedwali Na. 19: Orodha ya Halmashuri ambazo hazijaanzisha sheria ndogo ndogo kwa baadhi ya vyanzo vya mapato 73
Jedwali Na.20: Ulinganifu wa masuala ambayo hayakusuluishwa 80
Jedwali Na.21-Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya zamani kwenda Akaunti mpya 82
Jedwali Na.22: Orodha ya Halmashauri zenye mapungufu katika upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi (OPRAS)..... 85
Jedwali Na.23: Idadi ya Halmashauri ambazo hazitunzi/ kuboresha rejesta za watumishi 88
Jedwali Na.24: Halmashauri zilizolipa mishahara zaidi ya fedha walizopokea 93
Jedwali Na.25 : Idadi ya Halmashauri zinazoonesha watumishi wenye tarehe za kuzaliwa zisizo sahihi katika orodha kuu ya mishahara Hazina 94
Jedwali Na.26:Muhtasari wa makato yasiyowasilishwa katika taasisi husika..... 96
Jedwali Na.27: Stakabadhi zisizowasilishwa za kupokelea mishahara isiyolipwa na makato ya Kisheria yaliyolipwa 98
Jedwali Na.28: Karadha za mishahara zisizorejeshwa 99
Jedwali Na.29: Halmashauri ambazo zina watumishi ambao hawapo kwenye utumishi na hawajafutwa kwenye orodha ya mishahara ya Hazina.....101
Jedwali Na.30: Idadi ya Watumishi wanaokaimu nafasi za Wakuu wa Idara kwa muda zaidi ya miezi sita katika Halmashauri mbali mbali.....104
Jedwali Na.31: Wafanyakazi na zaidi ya moja namba ya hundi .105
Jedwali Na.32: Orodha ya Halmashauri ambao zina Mali, Vifaa na Mitambo lakini hazikufanyiwa tathminini. 109
Jedwali Na.33: Orodha ya Halmashauri ambazo zina mali ambazo hazina Hati miliki 112

Jedwali Na.34: Orodha ya Halmashauri ambazo thamani ya Mali, Vifaa na Mitambo zimeonyeshwa pungufu au zaidi katika taarifa za fedha 113
Jedwali Na.35: Orodha ya Halmashauri zenye matumizi yasiyo na Hati za malipo 116
Jedwali Na.36: Orodha ya Halmashauri ambazo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji zilikosekana 117
Jedwali Na.37: Orodha ya halmashauri zilizofanya uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambazo hazijarejesha 120
Jedwali Na.38: Mwenendo wa fedha zilizohamishwa ndani ya Halmashuri bila kurejeshwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) .. 121
Jedwali Na.39: Kiasi cha posho za wito wa dharura ambazo hazijatumika katika mwaka wa fedha 2012/2 123
Jedwali Na.40: Orodha ya Halmashauri na kiasi kilicholipwa kabla kufanyiwa ukaguzi wa awali na kukosa idhini sahihi ya kufanya malipo 125
Jedwali Na.41: Orodha ya Wahisani wa Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 134
Jedwali Na.42: Mapokezi ya fedha za LGDG katika Serikali za Mitaa 135
Jedwali Na.43: Mwenendo wa fedha zisizotumika kwa miaka miwili..... 136
Jedwali Na.44: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuchangia 5% ya fedha za ruzuku toka na mapato ya ndani 137
Jedwali Na.45: Malipo yasiyo na viambatanisho Sh.700,562,352 138
Jedwali Na.46: Manunuzi ya bidhaa bila kuwa na nukuu za bei 139
Jedwali Na.47: Mwenendo wa fedha zisizotumika kwa miaka mitatu 140
Jedwali Na.48: Mwenendo wa fedha za CDCF ambazo hazikutumika 141
Jedwali Na.50: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuibua Miradi ya CDCF 143

Jedwali Na.51: Orodha ya Halmashauri zilizotumia fedha za CDCF kwa matumizi ya kawaida 144
Jedwali Na.52: Mlinganisho wa wastani wa bakaa za fedha za NMSF kwa miaka mitatu.....146
Jedwali Na.53: Mwenendo wa bakaa za fedha za CHF kwa miaka mitatu mfululizo 147
Jedwali 54: Malipo yaliyofanya kinyume na miongozo ya CHF.....148
Jedwali Na. 55: Orodha ya Halmashauri zilizokuwa zinaidai Bima ya Afya 150
Jedwali Na.55: Fedha ambazo hazikuombwa toka NHIF 150
Jedwali Na.57: Mwenendo wa fedha zisizopelekwa kwenye mfuko wa Wanawake na Vijana 151
Jedwali Na.58: Orodha ya Halmashauri zenye fedha za MMEM ambazo hazikutumika 153
Jedwali Na.59: Mwenendo wa fedha za MMEM ambazo hazijatumika 154
Jedwali Na.60: Orodha ya Halmashauri zenye bakaa ya fedha za PFM.....155
Jedwali Na.61: Mwelekeo wa Halmashauri ambazo hazikutumia fedha za PFM.....155
Jedwali Na.62: Mlinganisho wa bakaa ya fedha za MMES kwa miaka mitatu.....157
Jedwali Na.63: Bakaa ya fedha za EGPAF 158
Jedwali Na.64: Fedha ya TSCP ambayo haikutumika mpaka mwishoni mwa mwaka.....159
Jedwali Na.65: Fedha za Miradi ambazo hazikutolewa 160
Jedwali Na.66: Miradi iliyokamilika na viwango hafifu.....163
Jedwali Na.67: Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni 168
Jedwali Na.68: Mwenendo wa Ununuzi wa bidhaa na huduma uliofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni 169
Jedwali Na.69 : Manunuzi kwa watoa huduma za Ugavi ambao hawajaidhinishwa 170

Jedwali Na.70: Mwenendo kwa miaka miwili wa manunuzi kutoka kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa 170
Jedwali Na.71: Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya Manunuzi bila ushindani wa wazabuni 171
Jedwali Na.72: Mwenendo wa Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni.....172
Jedwali Na.73: Orodha ya Halmashauri ambazo vifaa vyake havikuingizwa katika leja 173
Jedwali Na 74: Mwenendo wa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la vifaa kwa miaka miwili.....173
Jedwali Na.75: Orodha ya Halmashauri ambazo zililipia vifaa lakini bado havijapokelewa.....174
Jedwali Na.76: Mwenendo wa Bidhaa zilizolipiwa lakini hazijapokelewa 175
Jedwali Na.77: Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za mikataba na miradi.....176

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) kama ilivyofafanuliwa zaidi na vifungu Na. 45 na 48 vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (ilivyorekebishwa 2000) na kifungu Na.10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Dira ya Ofisi

Kuwa kituo cha ubora katika ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma

Lengo la Ofisi

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

Zingatio kwa Wadau	Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamanduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.

© Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Hata hivyo, baada ya taarifa hii kuwalishwa Bungeni, taarifa itakuwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hautakuwa na kikomo.

TAFSIRI/VIFUPISHO

AFROSAI - E	Muungano wa asasi kuu za Ukaguzi katika nchi za Afrika zinazotumia lugha ya kiingereza
ASDP	Programu ya maendeleo ya Kilimo na Mifugo
BoQ	Mchanganuo wa gharama za Kazi
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CDCF	Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo
CDG	Ruzuku ya miradi ya maendeleo
CHF	Mfuko wa afya ya jamii
DADPS	Mpango wa maendeleo ya Kilimo wilayani
HBF	Mfuko wa pamoja wa afya
H/M	Halmashauri ya Manispaa
H/W	Halmashauri ya Wilaya
IFAC	Shirikisho la kimataifa la wahasibu
IFMS	Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha
INTOSAI	Shirika la kimataifa la asasi kuu za ukaguzi
IPSAS	Viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma
ISA	Viwango vya kimataifa vya Ukaguzi wa hesabu
ISSAIs	Viwango vya shirika la kimataifa la asasi kuu za ukaguzi
Kif.	Kifungu
LAAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa
LAPF	Mfuko wa Pensheni wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa
LGA	Mamlaka za Serikali za Mitaa
LGCDG	Ruzuku ya miradi ya maendeleo ya Serikali za Mitaa
LGDG	Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa

LGFM	Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009
LGRP	Mpango wa maboresho ya Serikali za Mitaa
MMAM	Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi
MMEM	Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi
MMES	Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari
MSD	Bohari ya Madawa
MTEF	Mpango wa kati wa Matumizi ya Fedha za Umma
NAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
NHIF	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
NMSF	Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI
NSSF	Mfuko wa hifadhi ya huduma ya jamii
OPRAS	Mfumo wa wazi upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi
OR-MUU	Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma
OWM –TAMISEMI	Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PFM	Usimamizi shirikishi wa misitu
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
PMU	Kitengo cha usimamizi wa manunuzi
PPF	Mfuko wa pensheni wa watumishi wa mashirika ya umma
PPRA	Mamlaka ya udhibiti wa manunuzi ya umma
PSPF	Mfuko wa pensheni wa watumishi wa umma
SIDA	Wakala wa maendeleo ya kimataifa wa Sweden
TACAIDS	Tume ya kudhibiti UKIMWI
TASAF	Mfuko wa maendeleo ya jamii Tanzania
TRA	Mamlaka ya mapato Tanzania
VAT	Kodi ya ongezeko la thamani
WSDP	Mpango wa maendeleo wa sekta ya maji

Dibaji

Ninayo heshima kuwasilisha taarifa yangu ya mwaka ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013.

Ripoti hii ni majumuisho ya taarifa za ukaguzi katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 juni,2013 kwa muhtasari, ambapo maelezo ya kina ya taarifa hizo yanapatikana katika taarifa za Halmashauri zilizotumwa kwa waheshimiwa wenyeviti wa Halmashauri na Maafisa masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2000), kifungu Na.48 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na kifungu Na.34 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii ina lengo la kuwajulisha wadau wetu ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mahakama, wahisani, Asasi za kiraia na jamii kwa ujumla, kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ripoti hii inatoa matokeo ya ukaguzi wa jumla juu ya hali ya utendaji wa kifedha wa Serikali za Mitaa na kama zimefuata sheria, kanuni na viwango vya kimataifa vya

uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) kwa mwaka husika.

Mamlaka za Serikali za Mitaa, zilipewa nafasi ya kupitia na kujadiliana na wakaguzi kuhusu matokeo ya ukaguzi kwa kupitia Taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa wakati wa ukaguzi na katika vikao vya mwisho vilivyofanyika baada ya ukaguzi. Ningependa kukiri kuwa, majadiliano na wakaguliwa yalikuwa na umuhimu mkubwa. Ofisi yangu inatarajia kufuatilia katika muda muafaka juu ya maamuzi yatakayotolewa na Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 kuhusiana na mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti hii.
Ukaguzi wa mwaka huu wa fedha umegusa jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 140 katika nchi. Nina furaha kukuarifu kuwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini zimekaguliwa na ofisi yangu.

Ni vema ikaeleweka kwamba, wakati Ofisi yangu inatoa taarifa juu ya utekelezaji wa sheria mbalimbali, kanuni na miongozo, na udhaifu katika mifumo ya taarifa za fedha na udhibiti wa ndani katika taasisi za sekta ya umma na hasa Serikali za Mitaa, mwenye jukumu la msingi kabisa kwa ajili ya kutengeneza mfumo wenye ufanisi wa udhibiti wa ndani na mfumo wa uzingatiaji sheria ni Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zina majukumu mbalimbali kwa ajili ya utoaji wa huduma muhimu na utawala bora kwa wananchi wa maeneo yao. Ili kutimiza majukumu haya, zinapaswa kukusanya mapato kwa njia ya kodi, leseni, ada na mapato mengineyo. Katika kutekeleza suala

hili, umadhubuti katika usimamizi wa fedha ni muhimu ili Serikali za Mitaa ziweze kuleta ushawishi kwa umma kuwa mapato hayo yamepokelewa kwa kufuata sheria na kutumika ipasavyo kwa matumizi yaliyokusudiwa.
Ningependa kutambua mchango wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ikiwa ni moja ya Kamati muhimu ya usimamizi ya Bunge kwa ajili ya kuchukua jukumu muhimu la kufuatilia taarifa za kaguzi zilizopita pamoja na mapendekezo, na kwa ajili ya kufanya ziara na kufuatilia matumizi ili kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana katika miradi iliyotekelezwa.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote waliotengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba na kupelekea kukamilika kwa wakati taarifa ya jumla ya Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013

Natumaini kwamba, Bunge litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za muhimu katika kuifanya Serikali kuwajibika kwa ajili ya usimamizi wake wa fedha za umma na utoaji wake wa huduma bora za umma kwa Watanzania ambao inawahudumia. Katika suala hili, nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa taarifa hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Dar es Salaam,
28 Machi, 2014

Shukrani

Ripoti ya mwaka ya ukaguzi kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni 2013 imekamilika kwa mafanikio. Mafanikio haya yamefikiwa kwa sababu ya msaada na ushirikiano nilioupata kutoka kwa wadau mbalimbali.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake yote, Bunge na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuisaidia ofisi yangu na kuchukua kwa umakini masuala yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu za ukaguzi kwa lengo la kuboresha uwajibikaji katika ukusanyaji na utumiaji wa fedha nchini.

Pia,ninawiwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) kwa juhudi kubwa katika kusisitiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma kwa kutoa maelekezo kwa kila Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya ukaguzi yanatekelezwa na kuhakikisha ukaguzi unahitimishwa kwa wakati, katika kuwasisitizia wakaguliwa kuwa wanatakiwa wafuate kalenda ya mwaka ya Ukaguzi.

Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa wale ambao walinitengenezea mazingira mazuri ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Napenda kuwashukuru watumishi wote wa ofisi yangu kwa juhudi zao na kwa mara nyingine tena, kuwezesha ripoti kutoka ndani ya muda wa kisheria. Kwa moyo wa shukrani nyingi,

ninawiwa kuishukuru familia yangu pamoja na familia za watumishi wa ofisi yangu kwa uvumilivu waliokuwa nao kwa kipindi chote ambacho hatukuwa nao ili kutimiza majukumu haya ya kikatiba.

Vilevile, shukrani zangu za dhati ziende kwa jumuiya ya Wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO). Serikali ya Sweden kupitia mradi wa SIDA, Benki ya Dunia kupitia mradi wa PFMRP, Sekretarieti ya AFROSAI-E, Ofisi ya ushirikiano ya Ujerumani kupitia mradi wa GIZ ambao unafanya mafunzo kuhusu kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini, na wote wenye mapenzi mema waliochangia katika kufanikisha mageuzi ndani ya Ofisi yangu. Michango yao katika kuendeleza Watumishi, mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na ununuzi wa vitendea kazi vingine kama magari imekuwa msaada mkubwa sana katika mafanikio ya Ofisi yetu.

Pia, ninawiwa kuwashukuru wadau wetu wengine wote ikiwa ni pamoja na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Maafisa Masuuli wote wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya msaada uliohitajika na ushirikiano mkubwa waliotupatia.

Nitakuwa mchache wa shukrani kama sitatambua jukumu la vyombo mbalimbali vya habari katika kuujulisha umma wa Tanzania juu ya matokeo na mapendekezo yaliyopo katika Ripoti yangu.

Pia natoa shukrani kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kutumia utaalamu wao katika ukaguzi na kujituma wakati wote wa ukaguzi na kuweza kufanikiwa kukamilisha kazi ambayo imebainishwa katika ripoti hii

inayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa 140 katika nchi yetu. Juhudi kubwa katika kazi imewezesha ripoti hii kukamilika na kuwasilishwa Bungeni kwa wakati.

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa namna ya kipekee watanzania wote tunaowatumikia kwa ujumla. Nawasisitizia kwamba waendelee kupenda na kuhimiza juu ya uwazi na uwajibikaji katika kusimamia ukusanyaji na matumizi mazuri ya fedha na rasilimali za Umma.

Wakati tunatambua michango ya wadau wetu wote, sisi pia tunaahidi kuendelea kuchangia katika kukuza uwajibikaji na uzingatiaji wa thamani ya fedha katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma.

Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Taarifa ya Ukaguzi

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Ukaguzi wa taarifa za fedha ni uchunguzi huru wa mahesabu ya fedha na kutoa taarifa za sekta za Umma.

Sehemu hii ya ripoti inatoa maelezo ya jumla ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kufuatiwa na mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi pamoja na muhtasari wa mapendekezo.

1. Maelezo ya matokeo ya ukaguzi

Ukaguzi wa kisheria wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za mitaa 140 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013 umekamilika. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi upo katika ripoti hii na masuala haya kwa kirefu yamefafanuliwa katika taarifa zilizopelekwa kwa Menejimenti na Wenyeviti wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

- **Mwelekeo wa jumla wa hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Sehemu hii inaonesha tathmini ya mwelekeo wa hati za ukaguzi kwa miaka ya fedha ya 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013. Madhumuni ya mwelekeo huu ni kuonesha kiwango cha utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano ukiwemo mwaka wa fedha husika.

Mwelekeo wa Hati zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo

Hati	Hati Zinazori-dhisha		Hati zenye shaka		Hati Zisizoridhisha		Hati Mbaya		
Mwaka	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Idadi ya Halmashauri
2012/13	112	80	27	19	1	1	0	0	140
2011/12	104	78	29	21	0	0	1	1	134
2010/11	72	54	56	42	5	4	0	0	133
2009/10	66	49	64	48	4	3	0	0	134
2008/09	77	58	55	41	1	1	0	0	133

Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya Halmashauri kutoka mia moja thelathini na nne (134) katika mwaka 2011/12 hadi mia moja arobaini (140) katika mwaka 2012/13, hakuna mabadiliko makubwa kwenye aina ya Hati zilizotolewa kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo juu.

Hali inayoonekana hapo juu ni taswira ya kiwango kidogo cha maboresho katika mchakato wa uwajibikaji wa Serikali za Mitaa nchini. Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na Programu ya maboresho ya Serikali ya Mitaa (LGRP), Serikali kuchukua uzito katika utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na utekelezaji wa matumizi ya mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) kwa kutumia Epicor toleo la 9.05 katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

- **Mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Kutokana na mwenendo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitano, yameonekana mambo yafuatayo:

i) Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na saba (17) zimeendelea kupata Hati zinazoridhisha kwa miaka mitato (5) mfululizo, ambazo ni Halmashauri za wilaya

ya Bukoba, Muleba, Biharamulo, Misenyi, Kisarawe, Mufindi, Hai, Siha, Lindi, Simanjiro, Masasi, Tandahimba, Maswa, Iramba, Muheza, Serengeti na Nachingwea.

ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa sita (6) zimefanikiwa kupata Hati zinazoridhisha ukilinganisha na miaka iliyopita ambapo zilipata hati zenye mashaka na zisizoridhisha. Halmashauri hizo ni Halmashauri za wilaya ya Makete, Monduli, Mvomero, Sikonge, Halmashauri ya Mji wa Korogwe na Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam.

iii) Halmashauri ya Jiji la Arusha imeendelea kupata Hati isiyoridhisha na mbaya kwa miaka mitano mfululizo.

iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa nne (4) zimeshuka kwa mwaka huu wa fedha ambapo zimepata Hati zenye Mashaka ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo zilipata Hati zinazoridhisha. Halmashauri hizo ni Halmashauri za Manispaa ya Bukoba na Shinyanga, Halmashauri za wilaya ya Shinyanga na Bariadi.

Mafanikio haya kwa Mamlaka za serikali za Mitaa yamechangiwa na sababu zifuatazo:

- Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda (MB) aliwaagiza viongozi wakuu wa tawala za Mikoa juu ya kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa Menejimenti za Halmashauri husika
- Kuhusishwa kwa Wakuu wa Mikoa katika kuhakikisha na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali. Hii inajumuisha kuongoza vikao vya Baraza la Madiwani vinavyojadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- Kumekuwepo na uboreshaji wa taarifa za fedha zilizotolewa na Halmashauri kulingana na viwango vya

Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSASs).

- Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imefanya kazi kubwa katika kuhimiza uwajibikaji kwa Maafisa masuuli wa Serikali za Mitaa ambazo hazikufanya vizuri.
- Kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za mitaa kumekuwa na maboresho kidogo katika mfumo wa udhibiti wa ndani na kutekeleza matakwa ya sheria na kanuni.

2. Muhtasari wa mambo muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2012/2013 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mapungufu na madhaifu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ni pamoja na yafuatayo:

Mapendekezo ya Kaguzi zilizopita ambayo hayajatekelezwa

(i) Ripoti Kuu

Majibu ya Serikali pamoja na Mpango wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya mwaka uliopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2012 yamepokelewa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa Barua Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya 25 Juni, 2013.

Katika kupitia majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali imebainika kwamba, kati ya mapendekezo thelathini na tatu (33) yaliyopelekwa mwaka wa fedha 2011/2012, ni mapendekezo mawili (2) tu sawa na asilimia 6 ndio yaliyotekelezwa, mapendekezo kumi na saba (17) sawa na asilimia 52 utekelezaji wake bado unaendelea na mapendekezo kumi na nne (14) sawa na asilimia 42 bado hayajatekelezwa kabisa.

(ii)Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Katika kukamilisha na kujibu Ripoti ya ukaguzi kwa Taarifa za Fedha zilizoishia tarehe 30 Juni 2012, Mlipaji Mkuu wa Serikali hakuweza kujibu maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kinyume na kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008.

Hata hivyo hakuna majibu ya mapendekezo kumi (10) yaliyowasilishwa hadi wakati wa uandishi wa ripoti hii (Machi, 2014). Kwa maoni yangu, nasisitiza kuwa, hatua stahiki zichukuliwe na Serikali ili maoni yote ya Ukaguzi yashughulikiwe kwa ajili ya kuleta ufanisi na uwajibikaji katika Halmashauri za Serikali za Mitaa.

(iii) Ripoti za Halmashauri mbalimbali

Kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa mia moja arobaini (140) zilizokaguliwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa mia thelathini na moja (131) zilikuwa na masuala 6340 yenye jumla ya Sh.341,081,810,170 yanayohusu miaka ya nyuma ambayo hayajatekezwa. Pia kuna masuala mbalimbali ambayo hayakuthaminishwa kama vile mapungufu ya mfumo wa udhibiti wa ndani katika Halmashauri. Mapendekezo 2857 sawa na asilimia 45 yanayoweza kuthaminishwa yametekelezwa, mapendekezo 1460 sawa na asilimia 23 yanaendelea kutekelezwa na mapendekezo 2023 sawa na asilimia 32 bado hayajatekelezwa kabisa.

(iv) Kaguzi maalum

Katika Kaguzi zilizopita, jumla ya kaguzi maalum kumi nne (14) zilifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na nne (14) ni majibu ya Mamlaka saba (7) ndio yamepokelewa na masuala

mbalimbali yaliyojitokeza katika taarifa za kaguzi maalum yanaendelea kushughulikiwa na taasisi mbalimbali za kiuchunguzi kwa mujibu wakifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008. Mamlaka za Serikali za Mitaa saba (7) bado hazijajibu mapendekezo yaliyotolewa.

Hoja za Ukaguzi kwa mwaka husika

(i) Utayarishaji wa Taarifa za Fedha ambao siyo sahihi

Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa mia moja na mbili (102) zilizowasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi, zilikuwa na makosa mbalimbali kama vile, baadhi ya tarakimu kuoneshwa pungufu au zaidi na vilevile taarifa za Fedha zilizoandaliwa kutokuwa sahihi.

Kwa ujumla, makosa yaliyobainishwa ni kuwa Taarifa za fedha zilioneshwa pungufu kwa Sh.149,589,875,934 ambayo ni asilimia 6 ya matumizi yote na kuoneshwa zaidi kwa Sh.159,706,365,768 ambayo ni asilimia 7 ya matumizi yote. Kutokana na wingi wa makosa haya, Mamlaka za serikali za Mitaa zilifanya marekebisho ya taarifa za fedha na kuzileta tena kwa ajili ya ukaguzi.

(ii) Tathmini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani na Utawala bora

- **Udhaifu katika mfumo wa kihasibu-Epicor toleo la 9.05**

  Katika mwaka husika, Serikali za Mitaa walifanya taratibu za uhasibu kupitia Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) kwa kutumia mfumo wa kihasibu wa Epicor toleo la 9.05 chini ya usimamizi wa OWM-TAMISEMI. Kwa hali hii, Halmashauri zimefungiwa kompyuta tu kwa ajili ya kuingiza taarifa mbalimbali na kuidhinisha tu, lakini udhibiti wa mfumo mzima upo OWM-TAMISEMI ambapo kumbukumbu za taarifa za Serikali za Mitaa zote zinahifadhiwa.

Hata hivyo baada ya kupitia mfumo huo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa sabini na nane (78) tumebaini utendaji duni wa mfumo huo ambao unahitaji kuboreshwa ili kutoa taarifa za uhahika kwa watumiaji wa taarifa za fedha. Mapungufu yafuatayo yamebainika:

- ❖ Intaneti isiyo ya uhakika ambayo inapelekea ucheleweshaji wa kuingiza taarifa za kihasibu kwenye mfumo, hatimaye kuchelewa kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.
- ❖ Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitumii moduli zote ambazo zipo kwenye mfumo, na hivyo kupelekea kazi nyingi za kihasibu kufanyika nje ya mfumo kama vile kuandaa taarifa za wadeni, wadai, hesabu za bidhaa (inventories) na mali za kudumu. Kwa hali hii, taarifa za fedha haziwezi kutengenezwa moja kwa moja ndani ya mfumo wa kihasibu.

- **Mifumo mingine ya kihasibu inayotumika Halmashauri zaidi ya mfumo wa Epicor**

  Ilibainika kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama haikuwa inatumia mfumo wa Kihasibu wa Epicor, badala yake ilikuwa ikitumia mfumo mwingine wa kihasibu unaojitegemea (Quick use). Hii ni kinyume na maelekezo kutoka OWM-TAMISEMI kupitia barua yenye Kumbukumbu Na. GB.174/389/01/34 iliyotumwa kwa Halmashauri zote tarehe Aprili 30, 2012 ambayo ilieleza matumizi ya akaunti sita kwa kutumia mfumo wa kihasibu wa Epicor na pia waraka wa mwaka wa fedha 1999/2000 kutoka OWM-TAMISEMI ambao unazitaka Halmashauri kutumia mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS).

- **Utendaji duni wa Kamati za Ukaguzi katika Serikali za Mitaa**

  Kamati ya Ukaguzi ni chombo cha utawala bora kinachosaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutimiza majukumu yake ya usimamizi wa mchakato wa taarifa za fedha na mfumo wa udhibiti wa ndani.

  Katika kutathmini utendaji wa Kamati ya Ukaguzi, imebainika kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa tisini (90) zimeonekana zikiwa na utendaji duni wa kamati za ukaguzi kwa sababu zifuatazo:

  - ❖ Hakukuwa na ushahidi kuwa kamati za ukaguzi zinatoa usimamizi huru wa mipango ya ukaguzi wa ndani, rasilimali za ukaguzi zinazohitajika na kupatanisha mahusiano ya Mkaguzi na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
  - ❖ Kamati ya Ukaguzi hazikuweza kusimamia utendaji mzuri wa ukaguzi wa ndani, suala la rasilimali zinazohitajika na utoshelevu wa programu za ukaguzi.
  - ❖ Hakuna uthibitisho kwamba kamati za ukaguzi zimehakikisha matokeo ya ukaguzi wa ndani na nje yanatoka na mapendekezo yote yanafanyiwa kazi.
  - ❖ Katika Halmashauri za wilaya tatu (3) ambazo ni Mvomero, Masasi na Urambo, kamati za ukaguzi zimekutana mara moja tu kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Hivyo hawakutekeleza majukumu yao ya kimsingi.

- **Tathmini ya Usimamizi wa vihatarishi**

  Sampuli ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hamsini na tano (55) zimeonesha kuwa hazina nyaraka rasmi zinazoelezea tathmini iliyofanyika juu ya Usimamizi wa vihatarishi na kutambua vihatarishi vilivyopo na

vinavyoweza kujitokeza na kuathiri utoaji wa huduma wa Halmashsuri.

- **Kuzuia na Kudhibiti Udanganyifu**
  Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina nyaraka na mpango wa kuzuia udanganyifu ulioidhinishwa na hakukuwa na taratibu za kutambua mianya ya udanganyifu na kukabiliana na hatari hizo.

- **Utoaji wa huduma endelevu**
  Mamlaka za Serikali za Mitaa sabini na nane (78) zina kesi 636 za kisheria ambazo hazijaisha zenye jumla ya madai ya Sh.74,410,741,026. Kiasi hiki kinaweza kuathiri bajeti na utoaji wa huduma wa Serikali za Mitaa endapo walalamikaji watashinda kesi hizo.

(iii) Udhaifu katika usimamizi wa mapato kutoka vyanzo vya ndani

Usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Serikali za Mitaa bado ni changamoto. Muhtasari wa mapungufu yaliyoonekana katika eneo hili kwa mwaka huu wa ukaguzi ni pamoja na yafuatayo:

- Vitabu vya vya stakabadhi za kukusanyia mapato 1234 kutoka Mamlaka za serikali za Mitaa hamsini na moja (51) havikuwasilishwa na hivyo havikuweza kukaguliwa.
- Jumla ya Sh.6,710,548,469 zilikusanywa na Mawakala wa kukusanya mapato kwa niaba ya Mamlaka za serikali za Mitaa hamsini na nane (58), lakini kiasi hicho bado hakikupelekwa Halmashauri.
- Mapato ya ndani ya Mamlaka za serikali za Mitaa thelathini na moja (31) yenye jumla ya

Sh.585,502,820 yaliyokusanywa na wakusanyaji mbalimbali, hayakuthibitika kupelekwa benki wala kuwasilishwa katika Halamashauri husika.

- Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hamsinin na nne (54) umebaini kuwa jumla ya kiasi cha Sh.7,710,147,415 hakikukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani.

- **Kukosekana kwa sheria ndogondogo za Mapato ya ndani**

  Ukaguzi wa mwaka husika umebaini kuwa, Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na nane (18) hazikuwa na sheria ndogondogo zinazoongoza ukusanyaji wa mapato kutoka minara ya mawasiliano, ushuru wa huduma na ushuru wa mabango.

- **Upembuzi yakinifu juu ya ukusanyaji wa mapato haukufanyika**

  Katika mwaka huu, imebainika kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ilikasimisha makusanyo ya mapato ya Stendi ya mabasi na maegesho ya magari kwa Wakala kwa kipindi cha miezi minane kwa bei ya mkataba ya Sh.9,600,000 na Sh.2,750,000 kila mwezi kwa mtiririko huo.

  Hata hivyo, uchunguzi wa vitabu vya stakabadhi vya kupokelea mapato ya ushuru wa stendi na maegesho ya magari ulibaini kwamba kwa mwaka huu wa fedha jumla Sh.224,425,000 zilikusanywa na Wakala, lakini kiasi cha Sh.98,800,000 sawa na asilimia 44 ndicho kilichopelekwa Halmashauri kulingana na mkataba waliokubaliana na Sh.125,625,000 sawa na asilimia 56 kilibaki kwa Wakala. Hii inaonesha kwamba Halmashauri haikufanya upembuzi yakinifu ambao ungesaidia kujua kiasi kitakachokusanywa na kiasi kitakacholetwa halmashauri.

(iv) Udhaifu katika usimamizi wa Fedha

Usimamizi na udhibiti wa fedha ni muhimu ili kuhakikisha fedha zote zinazotokana na mapato zinakusanywa vizuri, kupelekwa benki na kuweka kumbukumbu zake katika vitabu vya fedha vya Halmashaurika husika. Mambo yafuatayo yalibainika katika mwaka 2012/2013:

- Udhaifu katika suluhisho za benki ulibainika katika Mamlaka za serikali za Mitaa thelathini na saba (37). Hii ni pamoja na Sh.5,864,183,413 ikiwa ni mapato katika vitabu vya fedha za Halmashauri lakini hayapo katika taarifa za benki. Pia hundi zenye thamani ya Sh.16,842,008,917 kutoka Halmashauri mbalimbali zililipwa na kuingizwa kwenye vitabu vya halmashauri lakini hazikuwasilishwa benki kwa ajili ya malipo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013. Pia, hundi zilizochacha zenye thamani ya Sh.107,345,185 hazijafanyiwa marekebisho kwenye vitabu vya Halmashauri.
- Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na mbili (12) hazikuhamisha fedha kiasi cha Sh.498,497,315 toka akaunti za zamani kwenda akaunti sita za sasa. Hii inamaanisha kuwa Halmashauri zimeendelea kutumia akaunti za zamani, kinyume na maelekezo toka OWM-TAMISEMI.
- Kaguzi za kushtukiza za fedha taslimu hazikufanyika katika Mamlaka za serikali za Mitaa thelathini na tatu (33).
- Masurufu ya jumla ya Sh.327,685,362 katika Mamlaka za serikali za Mitaa ishirini na tano (25) bado hayajarejeshwa mpaka wakati wa Ukaguzi.
- Mamlaka za serikali za Mitaa ishirini na tatu (23) zimeshindwa kuweka kiwango cha juu cha fedha taslimu anachotakiwa kuwa nacho Mtunza fedha wa Halmashauri.

(v) Mapungufu katika usimamizi wa matumizi

Udhibiti wa mfumo wa matumizi ni muhimu ili kuhakikisha kwamba gharama zote zilizotumika zimelipwa kwa usahihi na kuingizwa vizuri kwenye vitabu vya fedha. Mambo muhimu yaliyoainishwa katika mwaka 2012/2013 ni pamoja na:

- Malipo yenye nyaraka pungufu yalibainika katika Mamlaka za serikali za Mitaa sitini na saba (67) yenye jumla ya Sh.3,514,703,776.
- Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na tisa (19) kati ya mia arobaini (140) zilizokaguliwa zilifanya malipo yenye jumla ya Sh.8,063,469,984 ambayo hayakuwa na hati za malipo zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, na hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi.
- Jumla ya Sh.292,058,967 zilizokaguliwa kutoka katika Mamlaka za serikali za Mitaa tisa (9) zimelipwa kwa taasisi mbalimbali lakini fedha hizo hazikuthibitika kupokelewa kutokana na kukosekana kwa stakabadhi za kukiri mapokezi ya fedha hizo.
- Matumizi yenye jumla ya Sh.2,061,468,497 yalifanyika katika vifungu ambavyo siyo sahihi katika Mamlaka za serikali za Mitaa arobaini na tano (45) bila kuidhinishwa na Kamati za Fedha za Halmashauri husika.
- Kwenye sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na nane (18), jumla ya Sh.2,058,258,530 zilihamishwa kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyengine kama mikopo ya ndani inayopaswa kurejeshwa ili kutekeleza shughuli zilizokusudiwa, lakini mpaka mwaka wa fedha unaisha fedha hizo hazikurejeshwa kwenye akaunti husika.
- Kwenye sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa tisa (9), jumla ya Sh.1,119,360,501 zililipwa bila ya kupitishwa na Afisa Masuuli na wakuu wa idara husika. Kwa upande mwengine jumla ya Sh.1,205,767,982 zililipwa na Mamlaka za serikali

za Mitaa kumi na nne (14) bila kupitia ukaguzi wa awali.

(vi) Mapungufu katika menejimenti ya rasilimali watu na udhibiti wa mishahara

Menejimenti ya Rasilimali watu na udhibiti wa mishahara bado ni changamoto katika Halmashauri nyingi ambayo inahitaji usimamizi wa kina. Kama ilivyotolewa taarifa katika miaka ya nyuma, hata katika mwaka huu, madhaifu mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- **Uhaba wa Rasilimali watu**

  Katika mwaka wa ukaguzi, Mamlaka za serikali za Mitaa sabini na tatu (73) zilichaguliwa kama sampuli wakilishi ambapo ilionekana kwamba ikama zilionesha mahitaji ya watumishi 183,095 lakini idadi halisi iliyopo ilikuwa ni 143,111 tu na kusababisha kuwepo kwa upungufu wa watumishi 39,984 sawa na asilimia 22 ya idadi inayotakiwa.
- Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na sita (16) hazikutathimini utendaji kazi wa watumishi wao kinyume na Kanuni D(62-63) ya Kanuni za kudumu za watumishi wa umma, 2009. Hata hivyo, tathmini hizo zimekuwa zikifanyika tu pale watumishi wanapotakiwa kupanda vyeo. Kutofanyika kwa tathmini ya utendaji kazi, kunapelekea kukosekana kwa ufanisi katika ufuatiliaji wa utendaji wa watumishi.

Kutoandaliwa vema rejista ya watumishi

- Kwenye sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na moja (11) imebainika kwamba rejista ya mishahara isiyolipwa haina taarifa za kutosha kama vile namba ya kumbukumbu ya mfanyakazi na

sababu ya kutolipwa mshahara hazijajazwa kwenye rejista hiyo.

- Mishahara yenye jumla ya Sh.708,377,338 inayohusiana na watumishi waliofariki, wastaafu na watoro katika Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na sita (16) haikuwasilishwa Hazina. Pamoja na hoja hii ya ukaguzi kurudiwa kila mwaka, tatizo linaonekana kuwa sugu. Hii imetokea pamoja na kuwa serikali imeanzisha na kutumia mfumo wa Lawson.
- Mishahara yenye jumla ya Sh.832,448,998 ililipwa kwa wafanyakazi walioacha kazi, waliokufa, waliostaafu na walioachishwa kazi. Hii imeonekana katika Mamlaka za serikali za Mitaa thelathini na nane (38). Hili ni ongezeko ikilinganishwa na Sh.693,132,772 zilizohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa 43 zilizohojiwa mwaka uliopita. Pia makato ya mishahara yenye jumla ya Sh.482,405,746 yamelipwa kwenye taasisi mbalimbali kama vile mifuko ya pensheni, taasisi za fedha, mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kama makato ya wafanyakazi hao.
- Ukaguzi wa mishahara uliofanywa katika Mamlaka za serikali za Mitaa thelathini na tatu (33) ulibaini kuwa jumla ya wafanyakazi 3,650 wanapokea mishahara yao chini ya 1/3 na wengine wanakatwa mshahara wote, kinyume na Waraka No.CCE.45.271/01/87 wa tarehe 19, Machi,2010 iliyotolewa na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya utumishi wa Umma ambao unakataza makato ya mshahara wa mtumishi wa serikali kuwa zaidi ya 2/3 ya mshahara wa kila mwezi. Hii inaonekana kuna maboresho ukilinganisha na idadi ya wafanyakazi na idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizohojiwa katika mwaka uliopita.
- Ukilinganisha mishahara iliyolipwa na fedha za mishahara zilizopokelewa kutoka hazina katika

mwaka wa fedha 2012/13 imebainika kuwa, kuna fedha kiasi cha Sh.184,174,087 kilitolewa zaidi.

- Pamoja na suala hili kuoneshwa kwenye taarifa za miaka iliyopita, pia mwaka huu wa fedha katika sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na tano (15) ilibainika kuwa, tarehe za kuzaliwa za wafanyakazi zilikuwa si sahihi. Tarehe za kuzaliwa kwa watumishi zilionekana kuwa 1/1/1700, 1/1/1900 and 1/1/2012.
- Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa Halmashauri ya wilaya ya Mbozi na Halmashauri ya Mji ya Geita zilikuwa na watumishi sitini na sita (66) na sabini na mbili (72) wa mikataba kwa mfuatano kinyume na Kanuni D.30 (2) na A.1 (27) ya Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.
- Kwenye sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa thelathini na moja (31) ilibainika kuwa watumishi 166 wanakaimu nafasi za ukuu wa idara, vitengo au Afisa masuuli kwa zaidi ya miezi sita kinyume na Kanuni D. 24 (3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa umma, 2009.
- Namba ya utambulisho ya mtumishi ni namba ya kipekee inayomtofautisha mtumishi mmoja na mwingine. Kwa hali hiyo, haitegemewi mtumishi mmoja kuwa na namba ya mtumishi zaidi ya moja. Hata hivyo, uchunguzi wa mfumo wa mishahara ulibaini kuwa katika Mamlaka za serikali za Mitaa sita (6), watumishi ishirini na tano (25) wana namba mbilimbili tofauti za utambulisho wa mtumishi, hivyo kupelekea wafanyakazi hao kulipwa mishahara mara mbili kila mwezi. Huu ni ubadhirifu wa fedha za Serikali.

(vii) Mapungufu katika uendeshaji wa mambo ya fedha

- **20% ya fedha za Vijijini ambazo hazikutumwa**
  Kwenye sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa hamsini (50) ilibainika kwamba, jumla ya Sh.2,445,264,248 hazikutumwa kwenye Vijiji husika kama fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa na Serikali. Hii inamaanisha kwamba, kazi za maendeleo ya Vijiji hazijatekelezwa kama ilivyopangwa.

Fedha za ruzuku ambazo hazikupelekwa mashuleni

- Ukaguzi wa fedha za ruzuku za shule katika Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na saba (17) ulibaini kuwa, jumla ya Sh.1,356,500,282 zilipokelewa na Mamlaka za serikali za Mitaa hizo ikiwa ni fedha za ruzuku za shule. Lakini fedha hizo bado hazijapelekwa shuleni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali hivyo kuchelewesha utoaji wa huduma zilizokusudiwa. Pia jumla Sh.498,509,950 zilitumika kwenye matumizi yasiyohusiana na matumizi ya fedha za ruzuku ya shule kama vile kulipa posho.

- **Upungufu wa walimu na miundombinu ya shule za msingi na sekondari**
  Mapitio ya utendaji wa elimu katika shule za Msingi na Sekondari yamebaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuwa na miundombinu ya shule ya kutosha katika shule za msingi na sekondari. Ukaguzi pia umebaini kuwa, shule za msingi na sekondari, zina upungufu wa walimu ambao huathiri sana ubora wa elimu. Tatizo hili limepelekea nchi kushindwa kufikia lengo la kitaifa la uwiano wa 1:45 (Wanafunzi 45 kwa mwalimu mmoja). Muelekeo unaonesha kwamba walimu wengi hawaripoti katika vituo vyao vya

kazi hasa vijijini kutokana na miundombinu duni iliyopo vijijini.

- **Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)**

  Jumla ya kiasi cha Sh.2,591,012,939 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo hazikutumika katika sampuli ya Mamlaka za serikali za Mitaa sitini na sita (66) hivyo malengo ya kuanzisha Mfuko hayakutimia. Zaidi ya hayo, Mamlaka za serikali za Mitaa kumi na mbili (12) hazikuandaa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa taarifa ya kiasi kilichopokelewa na kutumiwa kwa kila Kamati ya kuchochea Maendeleo ya jimbo kama ilivyoagizwa katika Kifungu 7 (3) cha Sheria ya Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009.

- **Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)**

  Ukaguzi uliofanyika juu ya usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii katika Mamlaka za serikali za Mitaa arobaini na sita (46) zilizochaguliwa ulibaini kuwa Mamlaka hizi zilikuwa na bakaa ya Sh.2,070,366,726, hivyo malengo ya kuanzisha mfuko huo hayakutumia.

  Salio kubwa la fedha mwishoni mwa mwaka linawanyima haki walengwa kunufaika na huduma za afya zilizokusudiwa. Kwa upande mwingine, kiasi cha Sh.149,411,700 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa saba kilitumika kutekeleza shughuli ambazo hazihusiani na malengo ya mfuko huo kama vile malipo ya mshahara na posho kinyume na waraka Na.2 wa mwaka 1997 uliotolew na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kiasi hicho bado hakijarejeshwa kwenye akaunti husika.

- **Mfuko wa Wanawake na Vijana**
  Ukaguzi uliofanyika katika Mamlaka za serikali za Mitaa sitini na nane (68) umebaini kuwa, Sh.10,905,858,533 zipo katika akaunti za Halmashauri na hazikutolewa kama mikopo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana, hivyo kurudisha nyuma maendeleo wanawake na vijana.

- **Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)**
  Katika Halmashauri kumi na tatu (13), jumla ya Sh.1,138,230,899 hazikutumika kwa ajili ya MMEM hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha.

- **Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES)**
  Jumla ya Sh.21,869,260,499 zilitolewa kwa Mamlaka za serikali za Mitaa sitini (60) kwa ajili ya utekelezaji wa maendeleo ya elimu ya sekondari kwa malengo ya kuongeza ubora wa elimu na kupanua wigo wa wanafunzi kupenda kuendelea na masomo ya sekondari. Hata hivyo, jumla ya Sh.11,207,808,727 sawa na asilimia 51 ndizo zilizotumika na kubakia na kiasi cha Sh.10,661,451,772 sawa na asilimia 49 ya fedha zote zilizopokelewa ambazo hazijatumika hadi mwisho wa mwaka 30 Juni, 2013.

(viii) Usimamizi duni wa Miradi ya Maendeleo

Sampuli ya miradi mitatu (3) ya maendeleo ya wafadhili ambayo ni Mradi wa kudhibiti UKIMWI (NMSF), Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi

(MMAM) na Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGCDG) ilionesha kasi ndogo ya utekelezaji kwa kuwa na kiasi kikubwa kisichotumika cha Sh.2,333,558,283 kwa Mradi wa kudhibiti UKIMWI (Mamlaka za serikali za Mitaa 58), Sh.10,975,907,846 kwa Mradi wa Maendeleo ya afya ya Msingi (Mamlaka za serikali za Mitaa 81) na Sh.38,615,006,253 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za serikali za Mitaa 99). Utekelezaji wa Miradi kwa kiwango cha chini ina maana kwamba, idadi kubwa ya shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kikamilifu au hazikutekelezwa kabisa. Kwa ajili hiyo basi, huduma/ malengo yaliyotarajiwa na Halmashauri kwa jamii husika yamecheleweshwa. Hii pia inaweza kupelekea marekebisho ya bajeti katika siku zijazo kwa sababu ya uwezekano wa kupanda kwa bei kutokana na athari za mfumuko wa bei.

- **Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM)**
  Ukaguzi katika Mamlaka za serikali za Mitaa nane (8) ulibaini kuwa jumla ya Sh.119,054,705 hazikutumika mpaka mwisho wa mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa mradi shirikishi wa misitu

(ix) Changamoto katika utekelezaji wa Bajeti

Katika kupitia na kujiridhisha kama Mamlaka za serikali za Mitaa zimetumia fedha kulingana na Bajeti iliyoidhinishwa, nimebaini mapungufu yafuatayo:

- Bunge lilipitisha bajeti kwa baadhi ya vifungu vya fedha za maendeleo vyenye jumla ya Sh.673,590,626,951 katika Mamlaka za serikali za Mitaa mia moja kumi na nne (114). Hata hivyo, Sh.420,283,949,168 tu sawa na asilimia 62 ndizo zilizopokelewa na Mamlaka za serikali

za Mitaa husika, na kufanya kuwepo upungufu wa Sh.253,306,677,783 sawa asilimia 38.

- Pia fedha kwa ajili ya Matumizi ya kawaida zilitolewa pungufu kwa Sh.275,403,246,117 sawa na asilimia 13 katika Mamlaka za serikali za Mitaa tisini na tisa (99). Bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa Sh.2,102,969,648,522, wakati kiasi cha fedha kilichopokelewa na Halmashauri kilikuwa ni Sh.1,827,566,402,405 tu sawa na asilimia 87.
- Mpaka mwisho wa mwaka, Sh.243,677,063,440 sawa asilimia 36 ya fedha za Maendeleo zilizokuwepo hazikutumika. Kiasi hiki kinahusisha Mamlaka za serikali za Mitaa mia moja thelathini na nane (138).
- Katika mwaka husika Sh.146,328,309,031 sawa na asilimia 5 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizokuwepo hazikutumika. Kiasi hiki kinahusisha Mamlaka za serikali za Mitaa mia moja thelathini na tisa (139)

(x) Kutozingatia sheria na Kanuni za manunuzi

Katika kupitia na kujiridhisha kama Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazingatia Kanuni za Manunuzi, nimebaini mapungufu yafuatayo:

- Nyaraka muhimu zimekosekana kwenye mafaili ya mikataba kama vile mikataba, orodha ya vifaa vya ujenzi (BOQ), Makisio ya Mhandisi na vyeti vya malipo.
- Manunuzi yaliyofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na nane (18) nje ya Mpango wa manunuzi yenye thamani ya Sh.5,923,884,834.
- Kwenye sampuli ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na tatu (13) manunuzi yenye thamani ya Sh.254,040,434 yalifanyika bila kuwepo ushindanishi, kinyume na Kanuni 63 ya Kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2005.

- Manunuzi yenye thamani ya Sh.344,129,357 yalifanyika bila kupitishwa na Bodi ya zabuni. Hii inahusisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na sita (16)
- Ukaguzi wa bidhaa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na nane (18) ulibaini kuwa bidhaa zenye thamani ta Sh.665,721,997 hazikuingizwa kwenye daftari la vifaa bidhaa kinyume na Agizo la 54(3) la Memoranda ya fedha za serikali za mitaa ya mwaka 2009.
- Bidhaa zenye thamani ya Sh.150,649,237 ziliagizwa na kulipiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa tisa (9), lakini bidhaa hizo bado hazijapokelewa kinyume na na Kanuni 122 (1) ya Kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2005.

xi) Matokeo ya kaguzi maalum

Masuala mbali mbali yalijitokeza katika Kaguzi Maalum sita (6) zilizofanyika katika mwaka husika. Mamlaka za Serikali za Mitaa hizo ni Halmashauri za Wilaya ya Meru, Mpanda, Ileje, Mufindi, Geita na Halmashauri za Manispaa ya Bukoba. Matokeo ya Kaguzi hizo maalum ni kama yalivyoainishwa hapa chini:

Mfumo wa Udhibiti wa ndani na masuala ya Utawala bora

Mapungufu yaliyobainika katika eneo hili ni pamoja na yafuatayo:

- Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kutunza vifaa vya stoo na matumizi yake.
- Kutokuwepo kwa idhini kabla ya kufanya malipo.
- Kukosekana kwa nyaraka zilizofanyia malipo na nyaraka nyingine muhimu kama vile vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato, hati za malipo, stakabadhi za kukiri mapokezi na viambatanisho vingine vya matumizi.
- Malipo ambayo yamefanyika kwa shughuli zisizohusika.

- Bidhaa zilizoagizwa na kulipiwa lakini hazijaletwa Halmashauri.
- Kutokusanya na kuwasilisha mapato kwa Halmashauri kutoka kwa makampuni ya madini, wakala na wakusanyaji wengine wa mapato.
- Malipo ya madeni kwa wadai ambao hawakuwa wametambuliwa katika hesabu za mwaka uliopita.
- Uhamisho wa ndani wa fedha ambazo hazijarejeshwa.
- Manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanyika kwa fedha taslimu badala ya hundi.
- Mkandarasi kuwasilisha dhamana ya utendaji wa kazi (performance bond) ya kughushi kutoka benki bila Halmashauri kujua.

Usimamizi wa Manunuzi

Mapungufu yaliyobainika katika eneo hili ni pamoja na yafuatayo:

- Manunuzi na mabadiliko ya mikataba isiyoidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
- Hakukukuwa na ushindanishi wa zabuni katika zabuni ya ukusanyaji wa mapato na manunuzi ya bidhaa na huduma.
- Kutokufuata mpango wa mwaka wa manunuzi.
- Utoaji wa zabuni ya kukusanya mapato usiofuata taratibu za manunuzi kwa kumpa mzabuni ambaye atakusanya mapato kidogo badala ya mzabuni atakayekusanya mapato mengi.
- Manunuzi yaliyofanyika kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa.
- Halmashauri zilinunua vifaa tiba kwa wazabuni wengine bila kupitia Bohari kuu ya Madawa (MSD) kwa ajili ya kuthibitisha kutokuwepo kwa vifaa tiba hivyo.

Usimamizi wa Mikataba na Miradi

- Malipo yaliyolipwa kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazijafanyika.
- Fedha za miradi hazijahamishwa kwenda kwenye akaunti husika za miradi.
- Malipo ya fedha za awali kwa wakandarasi zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa.
- Malipo yaliyolipwa zaidi ya mikataba kwa watoaji wa huduma ya ushauri yaliyotokana na madiliko ya thamani ya fedha za kigeni.
- Upotevu wa fedha za Umma uliotokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa kutosha wa fedha zilizohamishwa kwenda ngazi za Vijiji na Kata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.
- Halmashauri ziliingia kwenye mikataba bila ya kuwepo matakwa ya kisheria ambayo yanaonesha haki na wajibu wa kila upande.

Usimamizi wa Rasilimali Watu

Vibali vya kujaza nafasi za watumishi zilizo wazi havikuombwa na Halmashauri. Pia, watumishi wa muda waliajiriwa bila ya kupata idhini kutoka Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

1. **Muhtasari wa Mapendekezo**

   Mbali na mapendekezo ya kina yaliyotolewa kwa kila menejimenti ya Halmashauri kupitia ripoti za menejimenti katika mwaka huu wa Ukaguzi, ninapendekeza mapendekezo yafuatayo:

   (a) Ninarudia pendekezo langu la mwaka uliopita kuwa OWM-TAMISEMI ianzishe mpango mkakati wa kubakiza watumishi kwa lengo la kupunguza wimbi la wafanyakazi kuacha kazi na kufikiria utoaji wa

motisha maalum kwa madhumuni ya kuhamasisha watumishi kufanya kazi katika Halmashauri zilizopo pembezoni. Nafasi nyingi za ajira zilizo wazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zipo katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na maeneo ya mijini.

(b) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kufanya tathmini upya wa mchakato wa maandalizi ya bajeti ili kuwawezesha kupata bajeti iliyo sahihi zaidi inayoweza kufikiwa na kuhakikisha kwamba mianya yote ambayo inaweza kupelekea hasara ya upatikanaji wa mapato inatambuliwa na hatua stahiki za kurekebisha zinachukuliwa. Pia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo dhidi ya bajeti ili kusaidia katika uandaaji wa bajeti sahihi.

(c) Serikali kuu kupitia OWM-TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kwamba fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo zinapelekwa katika Serikali za Mitaa kwa wakati na Serikali za Mitaa zinapaswa kuongeza ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kupunguza kiasi cha fedha zisizotumika mwishoni mwa mwaka. Inasisitizwa kwamba fedha ambazo hazijatumika katika mwaka husika zikasimiwe upya au kuingizwa katika bajeti ya mwaka husika na kutumika katika shughuli zile ambazo hazikukamilika katika mwaka uliopita.

(d) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakumbushwa kuomba idhini kutoka kwa mamlaka husika kwa ajili ya kubadili mgawanyo wa fedha kama inavyoagizwa kwenye Agizo la 22(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ili

kuepuka matumizi yasiyoidhinishwa ambayo yanaathiri utoaji wa Huduma wa Halmashauri kwa jamii iliyokusudiwa.

(e) Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI zinashauriwa kufanya upembuzi yakinifu mara kwa mara wa upatikanaji wa vyanzo vya mapato vilivyopo na fursa mpya zilizopo ili kubaini vyanzo vikuu vya mapato kwa ajili ya mipango sahihi na kuhakikisha kuwa mapato kutoka vyanzo vyote vya mapato yanakusanywa kwa ufanisi. Pia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuanzisha mikakati endelevu ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato.

(f) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kutunga sheria ndogo za vyanzo vyote vya mapato ya ndani vilivyopo kwenye mamlaka zao ili kuhakikisha kwamba kuna nguvu za kisheria katika ukusanyaji na ufuatiliaji kwa wale wanaokiuka sheria.

(g) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuimarisha udhibiti wa ndani wa vyanzo vya mapato vilivyobinafsishwa kwa Mawakala wa ukusanyaji mapato, ikiwemo kuimarisha usimamizi wa mikataba na kuhakikisha malengo ya Halmashauri yanafikiwa. Zaidi ya hayo Halmashauri zinapaswa kuwa na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu wa mapato yaliyokusanywa na Mawakala ikiwepo kupitia utendaji kazi wao kwa kufanya uchunguzi mbalimbali na kupitia taarifa zao za fedha.

(h) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuimarisha udhibiti wa ndani wa usimamizi wa rasilimali watu kwa kuboresha taarifa za watumishi mara kwa mara katika Mfumo wa

usimamizi wa taarifa za rasilimali watu (HCMIS) ili kupata taarifa sahihi za mishahara.

(i) TAMISEMI inashauriwa kupitia changamoto zote zinazoukabili mfumo wa Epicor toleo la 9.05 na kuja na suluhisho endelevu kwa kuwa kuna udhibiti mzuri kwenye mfumo wa Epicor ambao unaweza kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi ikiwemo kuandaa taarifa za fedha na mgawanyo wa kazi katika matumizi ya fedha za umma. Aidha, Mamlaka za serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha kuwa kuna utunzaji madhubuti wa nyaraka za miamala mbalimbali na kufuata sheria na kanuni katika kuidhinisha na kutunza nyaraka za miamala.

(j) Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Serikali kuu kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali wanashauriwa kuchunguza na kufanya suluhisho na benki husika ili kuhakikisha kwamba fedha zilizopo kwenye akaunti za zamani zinahamishiwa kwenye akaunti mpya kama ilivyoagizwa na TAMISEMI. Pia Mlipaji Mkuu wa Serikali anashauriwa kuidhinisha kufungwa kwa akaunti zote za benki za zamani ambazo bado zinatumika na Serikali za Mitaa.

(k) TAMISEMI kwa kushirikiana na ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali wanatakiwa kuongeza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uandaaji wa taarifa za fedha zinazozingatia viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSASs) kwa njia ya mafunzo. Pia OWN - TAMISEMI na Mhasibu Mkuu wa Serikali wanashauriwa kuweka mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa Serikali za Mitaa ili kuhakikisha na kujiridhisha kuwa Halmashauri zote zimefanikiwa

kutumia kikamilifu viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSASs) na kuandaa taarifa za fedha zinazozingatia viwango hivyo.

(l) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuanzisha udhibiti ulio bora na taratibu za uhakika kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wake kabla ya kuziwasilisha kwa ajili ya ukaguzi.

(m) TAMISEMi inashauriwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara ili kujenga uwezo kwa watumishii wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanao husika katika kuandaa taarifa za fedha kutoka kwenye mfumo wa Epicor toleo la 9.05 kwani toleo la Epicor ni jipya kwa Watumishi wengi wa Serikali za Mitaa na ina matumizi mengi yaliyofungamana katika mfumo huo.

(n) Mamlaka za Serikali za Mitaa wakishirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi wa umma (PPRA) wanashauriwa kuimarisha vitengo vya usimamizi wa manunuzi ya umma na michakato ya manunuzi ili kupata thamani ya fedha. Hili litafanikiwa kwa kuwa na wafanyakazi wa kutosha na wenye sifa stahili watakaozingatia Kanuni za Manunuzi ya umma.

(o) Mamlaka za Serikali za Mitaa wakishirikiana na Mamlaka ya kusimamia Manunuzi ya umma (PPRA) wanashauriwa kufanya mafunzo kwa wafanyakazi wa kitengo cha manunuzi, wajumbe wa Bodi ya zabuni, wakuu wa idara, afisa masuuli na Madiwani ili kujenga uwezo wa sheria za manunuzi ya umma na Kanuni zake.

(p) Serikali kuu kupitia TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Mafunzo Stadi wakishirikiana na Mamlaka za

Serikali za Mitaa wanashauriwa kuanzisha mikakati itakayoboresha miundombinu ya shule ikiwa ni pamoja na kuwa na idadi ya walimu wa kutosha ili kuongeza na kuimarisha ubora wa elimu. Pia Serikali Kuu inashauriwa kutenga fedha za kutosha katika ujenzi wa miundombinu kama vile ya afya, malazi, usafiri, mabweni, maabara na maktaba za shule hasa katika ngazi za Vijiji.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI NA MAMBO YA UJUMLA

1.1 Mamlaka na Madhumuni ya Ukaguzi

1.1.1 Mamlaka ya kufanya Ukaguzi

Taarifa hii imetolewa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 45(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambavyo vinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa Mkaguzi wa mapato na matumizi yote ya Serikali ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kukagua na kutoa taarifa, angalau mara moja kila mwaka, juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa za fedha zilizoandaliwa na maafisa wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; taarifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha zinazotayarishwa na Katibu wa Bunge.

Pia, kifungu cha 45 (5) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua fedha, uwekezaji au mali nyingine ambazo zinamilikiwa au zilizo chini ya udhibiti wa Halmashauri; kuwa na fursa wakati wowote ya kukagua hesabu, vitabu, hati za malipo na nyaraka zote zinazohusiana na mapato au malipo ya Halmashauri.

Aidha, kifungu cha 48 (1), (2) na (4) cha Sheria Na. 9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandaa na kusaini taarifa ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni mizania ya hesabu za mwaka na taarifa nyingine zinazohusiana nazo, ambapo nakala moja ya kila taarifa pamoja na mizania ya hesabu na taarifa nyingine zinazohusiana zitapelekwa kwa Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye anatakiwa kuziwasilisha kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

Kifungu hicho pia kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kubainisha kila kifungu cha matumizi ambacho kimetumika bila kufuata Sheria au kuidhinishwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pia anapaswa kubainisha mapungufu au hasara ambayo imetokea ama kwa uzembe au mtu yeyote kushindwa kutoa taarifa ya matumizi ya fedha alizokabidhiwa. Pia suala lingine ni kuthibitisha kiasi cha matumizi yaliyofanyika kinyume na sheria, matumizi yenye upungufu au hasara ambayo haijaoneshwa vitabuni.

Hesabu za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizowasilishwa kwa ukaguzi zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSASs), pamoja na sehemu ya (iv) ya Sheria Na.9 ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), na pia kulingana na Agizo la 31(4) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, 2009 kama msingi wa utayarishaji wa taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Orodha kamili ya taarifa za hesabu zilizotayarishwa kwa kutumia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma ambayo inatakiwa kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi inajumuisha:

(a) Taarifa ya Mizania ya hesabu;
(b) Taarifa ya mapato na matumizi;
(c) Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji;
(d) Taarifa ya mtiririko wa fedha;
(e) Taarifa ya uwiano wa bajeti na matumizi halisi kama yalivyojitokeza;
(f) Taarifa ya uwiano wa bajeti na matumizi halisi kwa kila idara;
(g) Maelezo ya ziada yanayofafanua mambo yaliyopo katika taarifa za hesabu zilizotayarishwa.

Ili kuhakikisha kunakuwepo uwazi na uwajibikaji, Kifungu cha 49 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kama ilivyosisitizwa kwenye Agizo 31 (9) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutangaza katika Ofisi zake au kwa kadri itakavyoelekezwa na Mkuu wa Mkoa kutangaza taarifa zifuatazo katika eneo lake:

(i) Muhtasari wa taarifa jumuifu ya Mizania ya hesabu na taarifa ya mapato na matumizi zilizokaguliwa.
(ii) Taarifa yoyote inayohusu hesabu husika na iliyosainiwa na Mkaguzi katika kipindi cha miezi sita baada ya kufungwa kwa mahesabu ya mwaka au katika kipindi cha miezi sita baada ya kupata taarifa ya ukaguzi au kadri itakavyokuwa.

Nakubalianaa kuwa, kufuatwa kwa misingi ya utaarishaji wa Hesabu na kuchapishwa kwa hesabu na taarifa za ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni fursa nyingine kwa Mamlaka hizo kuongeza mawasiliano kwa upana zaidi na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma.

1.1.2 Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Majukumu yangu kama Mkaguzi ni kutoa maoni katika hesabu zilizowasilishwa yanayotokana na ukaguzi wangu. Nimefanya ukaguzi wa hesabu kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) na ulijumuisha mambo kama taratibu za ukaguzi wa hesabu ambazo kwa utashi wangu niliona kuwa ni muhimu katika mazingira yanayohusika. Viwango hivi vinanitaka nizingatie mahitaji ya kimaadili, nipange na kufanya ukaguzi ili kupata uhakikisho wa kutosha kuwa taarifa za fedha hazina kasoro.

Ukaguzi wa hesabu ulijumuisha kufuata taratibu ili kupata ushahidi unaothibitisha kiasi cha fedha kilichotumika na kuonyeshwa katika taarifa za fedha. Taratibu zilizochaguliwa zilitokana na mtazamo wa mkaguzi, uliojumuisha kutathmini viashiria vya kuwepo kwa mapungufu katika taarifa za fedha ama kutokana na ubadhirifu au makosa. Katika kufanya tathmini ya viashiria, nilizingatia mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri husika katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa ya fedha ili kuweka njia sahihi za ukaguzi, na sio kwa ajili ya kutoa maoni juu ya ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri.

Ukaguzi pia ulihusisha kutathmini usahihi wa sera za uhasibu zilizotumika na usahihi wa makadirio ya kiuhasibu yaliyofanywa na wenye dhamana ya uongozi , pamoja na kutathmini uwasilishaji wa jumla wa taarifa za fedha.

Vile vile, kifungu Na. 10 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kinataka nijiridhishe kwamba, hesabu zimeandaliwa kwa mujibu wa viwango vya kihasibu vinavyofaa na kwamba; tahadhari muhimu zimechukuliwa kulinda ukusanyaji wa mapato, kupokea, kutunza, kuuza, kutoa na kufanya matumizi sahihi ya mali za umma, na

kwamba sheria, miongozo na maelekezo husika yamezingatiwa kwa umakini na matumizi ya fedha za umma yamekuwa yakiidhinishwa vizuri kwa kufuata taratibu.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 44 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni ya 31 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Bidhaa, Ujenzi, huduma zisizo za kiushauri na uuzwaji wa mali za serikali kwa zabuni) za mwaka 2005 zinanitaka kutoa taarifa ya mwaka ya ukaguzi nikieleza endapo mkaguliwa ametekeleza au hajatekeleza masharti ya Sheria na Kanuni zake.

1.1.3 Madhumuni ya ukaguzi

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni huru juu ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 na kubainisha kama hesabu hizo zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa kulingana na misingi ya utayarishaji wa hesabu, ikiwa ni pamoja na:

- Kuhakikisha kuwa fedha zote zimepokelewa na kutumiwa kwa matumizi halali kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa kufuata Kanuni zinazosimamia matumizi ya fedha za na Serikali kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa.
- Kuhakikisha kuwa mapato yote yaliyokusanywa yameingizwa vyema katika vitabu.
- Kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu, vitabu, rejista, taarifa za fedha na taarifa mbalimbali zimetayarishwa vizuri zikionesha miamala yote na bakaa husika.
- Kuhakikisha kwamba vitu vyote muhimu vilivyo kwenye taarifa za fedha vinawasilishwa na kutolewa taarifa vizuri.

- Kufanya tathmini na kupima mifumo mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kubaini uimara na ubora wa mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwa ni pamoja na udhibiti wa teknolojia ya mawasiliano.
- Kutathmini hatari inayoweza kutokea kutokana na makosa ya kiukaguzi.
- Kuhakikisha kuwa malengo yaliyotarajiwa au mafanikio yamepatikana na kwamba malengo yaliyowekwa na Bunge au chombo kingine kilichoidhinishwa yamefikiwa.
- Kufanya tathmini ili kuona kama Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata taratibu za manunuzi kama zilivyoelezwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004, pamoja na Kanuni zake za mwaka, 2005.
- Kuhakikisha kuwa utawala bora umejengeka katika kufanikisha shughuli za kila siku za Halmashauri na katika kutekeleza malengo yote kwa ujumla na jinsi menejimenti inavyosimamia masuala ya kijamii na mazingira.

1.2 Viwango vinavyotumika vya Ukaguzi na taratibu za utoaji taarifa

1.2.1 Viwango vinavyotumika wakati wa Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi kuu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Afrika la Asasi Kuu za Ukaguzi (AFROSAI), na Shirika la Afrika la Asasi Kuu za Ukaguzi - kwa nchi zinazozungumza lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E) ambazo zinasaidiana katika kubadilishana utaalamu na uzoefu kati ya nchi wanachama duniani katika ukaguzi wa taasisi za Umma.

Ikiwa ni mwanachama wa Asasi hizo za kimataifa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inawajibika kutumia viwango vya ukaguzi

vilivyotolewa na INTOSAI ambavyo ni viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vilivyotolewa na Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa (IFAC) wakati wa ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

1.2.2 Taratibu zinazotumika kutoa taarifa

Hatua mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kabla ya kutoa taarifa hii ya mwaka. Kwa hiyo basi, ni vyema kubainisha hatua zote za ukaguzi kwa watumiaji wa taarifa hii ili waweze kuifahamu na kujua taratibu zinazotumika katika kuikamilisha. Hatua hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kutoa barua ya kuanza ukaguzi kwa mkaguliwa inayoeleza madhumuni na mawanda ya ukaguzi, na maeneo yanayotarajiwa kufanyiwa ukaguzi na kuelezea kazi na majukumu ya mkaguzi na kazi na majukumu uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa.

(ii) Kuandaa mpango mkakati wa ukaguzi unaoonesha mwelekeo mzima wa ukaguzi, vigezo vitakavyotumika katika hatua za mwanzo za kutathmini Halmashauri inayokaguliwa.

(iii) Kufanya kikao cha kwanza na uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kabla ya kuanza ukaguzi. Kikao hiki kinatoa nafasi ya kuueleza uongozi madhumuni na malengo ya kufanya ukaguzi na kinampa nafasi mkaguliwa kuelezea maeneo ya ukaguzi.

(iv) Kuanza ukaguzi wa awali kwa lengo la kupunguza ukubwa wa kazi na muda utakaosaidia katika kukamilisha taarifa ya ukaguzi mapema.

(v) Kutoa taarifa kwa uongozi wa Halmashauri kwa kipindi cha kati inayoonesha matokeo ya ukaguzi ikiwa ni pamoja na hoja za ukaguzi na kutoa nafasi

kwa uongozi wa mkaguliwa ili kuweza kujibu hoja hizo.

(vi) Kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa kujiridhisha kwamba zimeandaliwa kwa kufuata misingi ya utayarishaji wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(vii) Kufanya kikao cha mwisho na Uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi kwa kuwajulisha matokeo ya ukaguzi na kuwapa nafasi ya kutoa maoni yao kabla ya taarifa ya mwisho ya ukaguzi haijatolewa.

(viii) Kutoa taarifa ya mwisho ya ukaguzi kwa Uongozi wa Halmashauri inayokaguliwa kwa kuujulisha Uongozi wa Halmashauri iliyokaguliwa mambo yote yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi zaidi ya kuyashughulikia. Hatua hii pia ni ya msingi katika kutayarisha taarifa ya mwaka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(ix) Kuandaa taarifa Kuu ya mwaka ya Mamlaka za Serikali za Mtaa na kuiwasilisha Bungeni kupitia kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(x) Kufuatilia matokeo ya ukaguzi yaliyotolewa katika taarifa kama ilivyoainishwa katika Kifungu Na.40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kwa kubainisha na kutoa taarifa kama kila Mkaguliwa ameandaa mkakati wa kuyatekeleza mapendekezo yatokanayo na ukaguzi au ametekeleza mapendekezo yaliyotolewa, pamoja na kuonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi katika taarifa ijayo ya Ukaguzi kama inavyotakiwa na Kifungu Na.40 (4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Kwa kifupi mchoro ufuatao hapa chini unaonesha hatua zinazofuatwa wakati wa ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa:



1.3 Idadi ya Halmashauri zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

1.3.1 Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, kulikuwa na Mamlaka za Serikali za mitaa 140 Tanzania Bara ambazo zilikaguliwa na kutolewa taarifa ya ukaguzi kwa kila Halmashauri husika. Mamlaka hizi za Serikali za Mitaa zina hadhi tofauti kuanzia Halmashauri za Wilaya hadi Halmashauri za Jiji kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 1: Idadi ya Wakaguliwa

Na.	Halmashauri	Jumla	Asilimia (%)
1.	Halmashauri za Jiji	5	4
2.	Halmashauri za Manispaa	18	13
3.	Halmashauri za Miji	10	7
4.	Halmashauri za Wilaya	107	76
	Jumla	**140**	**100**

1.3.2 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kuna jumla ya Halmashauri 140 ambazo zinakaguliwa na Ofisi 28 za Ukaguzi zilizopo mikoani kote Tanzania Bara. Ofisi za Ukaguzi Mikoani zinaongozwa na Wakaguzi Wakazi ambao wanasimamiwa na Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kila Kanda. Kwa madhumuni ya Ukaguzi unaofanyika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini, Ofisi hizo zimegawanywa katika Kanda tano. Ofisi za Kanda zinaongozwa na Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kila Kanda ambao wanasimamiwa na Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Divisheni ya Serikali za Mitaa. Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Divisheni ya Serikali za Mitaa anawajibika moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoonekana katika Sehemu ya Muundo wa Ofisi hapa chini:


Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Naibu Mkaguzi Mkuu
Wizara
Naibu Mkaguzi Mkuu
Hesabu za Taifa
Naibu Mkaguzi Mkuu
Mamlaka za serikali za Mitaa
Naibu Mkaguzi Mkuu
Mashirika ya Umma
Naibu Mkaguzi Mkuu
Ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalum
Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu
Kanda ya Pwani
Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu
Kanda ya Dar
Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu
Kanda ya Kati
Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu
Kanda ya Ziwanza
Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu
Kanda ya Kusini
Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu
Kanda ya Kaskazini
Morogoro
Mtwara
Lindi
Coast
Kinondoni
Ilala
Temeke
Dar es salaam
Dodoma
Singida
Tabora
Kigoma
Kagera
Mara
Shinyanga
Geita
Simiyu
Mbeya
Ruvuma
Iringa
Rukwa
Njombe
Katavi
Arusha
Kilimanjaro
Tanga
Manyara

1.4 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

1.4.1 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa na kuripoti taarifa za fedha

Uongozi wa kila Halmashauri una wajibu wa kuandaa na kuonesha kwa usahihi taarifa za fedha na kuanzisha mifumo ya udhibiti wa ndani ambao uongozi utaona unafaa ili kuwezesha kuandaa taarifa za fedha ambazo hazina dosari kutokana na udanganyifu au makosa mengine.

Kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) imeainisha kuwa, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina wajibu wa kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu zinazohusu:

(a) Mapato na matumizi ya fedha na miamala mingine katika mamlaka
(b) Mali na dhima; mapato na matumizi ya mamlaka

Kifungu kilichotajwa hapo juu kimefafanuliwa katika Agizo la 11 mpaka la 14 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 inayotaka Halmashauri kuanzisha na kusimamia udhibiti wa ndani wa shughuli za Halmashauri. Kwa nyongeza, Agizo la 31 linazipa majukumu menejimenti za Halmashauri kuandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, miongozo inayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs).

Pamoja na majukumu ya uaandaaji wa taarifa za hesabu, Kifungu cha 49 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya 1982 (Iliyorekebishwa 2000) na Agizo la 31 (9) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 vinaitaka

kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kuchapisha taarifa za fedha zilizokaguliwa katika ya maeneo yao ya uwajibikaji.

Aidha, Agizo la 31(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 na Kifungu cha 45(4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa, 2000) inamtaka kila Afisa Masuuli kuandaa taarifa za mwisho za Hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi tarehe 30 Septemba au kabla ya tarehe hiyo kila mwaka.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013, Halmashauri ziliwasilisha hesabu zao kulingana na tarehe iliyokubalika kisheria au kabla ya tarehe 30 Septemba 2013.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa taarifa hizo za fedha imebainika kwamba, kuna baadhi ya hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ziliwasilishwa aidha zikiwa na makosa mengi au kutooneshwa kabisa kwa mambo mengine muhimu. Inawezekana kuwa Hesabu hizo ziliwasilishwa tu kwa lengo la kutimiza wajibu wa kisheria wa kuwasilisha taarifa za fedha kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi huku waliowasilisha taaifa hizo wakijua fika kuwa hazikuwa sahihi.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo mia moja na mbili (102) ziliwasilisha taarifa za fedha zikiwa na makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuonesha tarakimu katika mahesabu ambazo ni zaidi au pungufu ikilinganishwa na tarakimu zilizotakiwa kuoneshwa katika taarifa hizo za fedha. Kwa ujumla taarifa hizo zilizowasilishwa awali zilionesha jumla ya kiasi cha Sh.149,589,875,934 pungufu ya kiasi ambacho kilitakiwa kuoneshwa sawa na 6% ya matumizi yote na kiasi cha Sh.159,706,365,768 kilioneshwa

zaidi ambacho ni sawa na 7% ya matumizi yote ya fedha kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini. Orodha kamili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo taarifa zake za fedha zilionesha tarakimu zaidi au pungufu imeoneshwa katika **Kiambatisho (i).**

Jedwali Na.2: Upotoshwaji katika Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Mwaka

Maelezo	Kiasi kilichooneshwa pungufu (Sh.)	Kiasi kilichooneshwa zaidi (Sh.)
Jumla ya matumizi	2,347,629,365,375	2,347,629,365,375
Jumla ya makosa	149,589,875,934	159,706,365,768
Asilimia (%)	**6%**	**7%**

Kutokana na makosa hayo yaliyopelekea kuoneshwa kwa kiasi pungufu au zaidi katika taarifa hizo za fedha, Mamlaka za Serikali za Mitaa husika zilirejeshewa taarifa za fedha zilizowasilishwa hapo awali kwa minajili ya kuzifanyia marekebisho na baadaye ziliwasilishwa tena kwa ajili ya ukaguzi.

Mwelekeo wa taarifa za fedha zilizorekebishwa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ni kama ufuatao:

Jedwali Na. 3: Halmashauri zilizorekebisha taarifa za fedha kwa miaka mitano mfululizo kufuatia ukaguzi uliofanyika

Mwaka wa fedha	Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa	Idadi ya Halmashauri zilizoleta taarifa za fedha zilizorekebishwa	Asilimia
2012/13	140	102	73
2011/12	134	67	50
2010/11	133	60	45
2009/10	134	44	33
2008/09	133	24	18

Mwelekeo wa taarifa za fedha zilizorekebishwa katika kipindi cha miaka mitano mfululizo hapo juu unaonesha kuwa, kuna ongezeko kubwa la Halmashauri ambazo zilirejeshewa taarifa za hesabu zilizowasilishwa hapo ili kuzifanyia marekebisho na baadaye kuziwasilisha tena kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo imejitokeza kwa sababu ya kutokuwepo kwa mafunzo ya kutosha kwa watumishi ili waweze kuandaa hesabu kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs) na uhamisho wa watumishi ambao wamebobea kwenye kuandaa taarifa kwa kufuata Viwango vya kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

Idadi kubwa ya makosa na marekebisho yaliyofanywa kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na masuala ya uhasibu yanayohusiana nayo yanaashiria kuwa jitihada za dhati zinahitajika ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zinakuwa sahihi na zinazoonesha mambo yote yanayotakiwa.

Ninapendekeza kuwa, katika miaka ijayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zianzishe mchakato wa uhakiki na udhibiti wa ubora katika maandalizi ya taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa hizo kabla hazijawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Pia, OWM-TAMISEMI inatakiwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara katika kujenga uwezo wa watumishi wanaoandaa taarifa za fedha.

SURA YA PILI

2.0 Hati za Ukaguzi

Katika kutekeleza matakwa ya Kisheria, ninawajibika kutoa uhakikisho kwa wadau wa Mamlaka za serikali za Mitaa kwamba, taarifa za fedha zilizotayarishwa na Halmashauri zinatoa picha halisi ya matokeo ya shughuli zilizofanyika, ikiwa ni pamoja na mtiririko wa fedha pia mali na madeni ya Halmashauri kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Maoni ya ukaguzi yanatolewa kwa wadau kama uhakikisho wa usahihi wa taarifa za fedha za Halmashauri pamoja na uzingatiaji wa taratibu zinazotakiwa.

2.1 Maana ya Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayoeleza kama taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya taaluma ya uhasibu na mambo yote muhimu, kwa mujibu wa misingi inayotumika katika uandaaji wa tarifa hizo. Hati ya ukaguzi pia inazungumzia kama taarifa za fedha zilizowasilishwa zina maelezo ya kutosha katika kuelezea vizuri na kwa upana zaidi taarifa hizo ili ziweze kueleweka kwa watumiaji.

2.1.1 Aina ya Hati za ukaguzi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na Viwango vya Shirikisho la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs), zifuatazo ni aina za Hati za Ukaguzi ambazo zinatolewa kama kipimo cha ubora/udhaifu katika utayarishaji wa taarifa za fedha:

2.1.1.1 Hati inayoridhisha

Hati ya aina hii inatolewa wakati nimeridhika kuwa, taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetayarishwa

kulingana na misingi ya utaarishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, utoaji wa hati inayoridhisha haumaanishi kwamba Halmashauri ina mfumo safi kabisa wa udhibiti wa ndani. Hati hii ina maana kwamba hakuna jambo lolote nililoliona ambalo lingesababisha kutolewa kwa hati yenye shaka. Kila Halmashauri iliyopata aina hii ya hati imeandikiwa taarifa nyingine ya ukaguzi kwa ajili ya menejimenti inayoeleza masuala ambayo yasipoangaliwa, yanaweza kuisababishia Halmashauri kupata hati yenye shaka miaka ijayo.

2.1.1.2 Hati yenye shaka

Hati yenye shaka inatolewa iwapo ninaridhika kuwa, taarifa za fedha hazikuonesha usahihi, kutokukubaliana na uongozi au kukwazwa kwa mawanda ambapo athari yake ni kubwa lakini si muhimu na kwamba ukiacha athari zilizopelekea kutoa hati yenye shaka, taarifa za hesabu zimetengenezwa kulingana na misingi ya utayarishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa hivyo hazihitaji kutolewa hati isiyoridhisha.

Kwa maana nyingine, Hati yenye shaka inatolewa endapo kuna kutoelewana na Uongozi katika sehemu moja au zaidi ya taarifa za fedha lakini makosa hayo hayaathiri eneo lililosalia la taarifa za fedha na halisababishi taarifa za fedha kwa ujumla wake kuonekana zina makosa.

2.1.1.3 Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale ninapokuwa na uthibitisho wa kutosha kwamba, kuna kiasi kikubwa cha kutokukubaliana na menejimenti na kuna madhara makubwa kwenye taarifa za hesabu kutokana na ama kutofuata taratibu za fedha zilizowekwa au taarifa za hesabu zilizowasilishwa hazina maelezo ya kutosha ambayo

yanawezesha taarifa za fedha kuelezeka vizuri na kwa upana zaidi kwa watumiaji.

2.1.1.4 Hati mbaya

Hati mbaya hutolewa wakati ninaposhindwa kupata taarifa na uthibitisho wa kutosha kufanya niweze kukagua na kutoa maoni na hivyo kushindwa kutoa maoni juu ya tarifa za fedha zilizowasilishwa.Hali hiyo inaathiri kwa kiasi kikubwa tarifa za hesabu kiasi kwamba ninashindwa kutoa maoni yangu juu ya hesabu husika.

2.1.2 Vigezo au mambo yanayopelekea kutoa hati yenye shaka

Vifuatavyo ni vigezo au mambo ambayo yanaweza kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa hati yenye shaka:

(a) Kukwazwa kwa mawanda ya Ukaguzi kwa kushindwa kupata taarifa na nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi.

(b) Mambo ambayo yanaendana na kutokufuata sheria na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na:
   i) Utayarishaji wa taarifa za fedha ambao haukufuata misingi ya utayarishaji wa taarifa za fedha.
   ii) Uingizaji wa taarifa katika vitabu vya fedha ambao haujafuata taratibu zinazostahili.
   iii) Taarifa muhimu na za msingi zinazoathiri vitabu vya fedha.

(c) Kutokubaliana na Menejimenti kwamba kuna madhara makubwa kwenye taarifa za fedha kunatokana na kasoro za kiuhasibu au nyinginezo zilizobainishwa na mkaguzi.

2.1.3 Masuala muhimu ambayo hayaathiri maoni ya ukaguzi

Kwa kawaida baadhi ya masuala ambayo ni muhimu kwa wadau kuyajua hayaruhusiwi kuwekwa wazi katika sehemu ya maoni ya ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi.

Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa masuala haya, yameruhusiwa kuoneshwa kama masuala yenye msisitizo au masuala mengine tu chini ya aya ya maoni kama nilivyoeleza hapa chini;

2.1.3.1 Masuala ya msisitizo na masuala mengine

Masuala ya msisitizo na masuala mengine ambayo mkaguzi anaona yanafaa yanawekwa kama mawasiliano ya ziada kupitia katika ripoti. Kwa kawaida mkaguzi anaeleza bayana kuwa masuala haya ni ya msisitizo tu na hayaathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa.

(a) Kutoa uelewa kwa watumiaji wa hesabu zilizoandaliwa kuhusu suala au masuala yaliyooneshwa ndani ya taarifa za fedha, kwamba ni muhimu kwa watumiaji katika kuelewa taarifa za fedha na kwamba masuala hayo ya msisitizo yasiposhughulikiwa vyema yanaweza kuathiri hesabu katika miaka inayofuata.

(b) Kutoa uelewa kwa watumiaji wa hesabu katika suala au masuala yale yaliyo oneshwa kwenye taarifa za hesabu ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuuelewa vizuri ukaguzi, majukumu ya wakaguzi au ripoti ya ukaguzi.

2.1.3.2 Masuala ya msisitizo

Wakati mwingine, nimejumuisha aya inayohusu masuala ya msisitizo ili kuweka bayana masuala ambayo hata kama yameoneshwa vyema katika taarifa za fedha, kwa mtazamo wangu, yana umuhimu na ni ya msingi kwa watumiaji wa taarifa za fedha. Nyongeza ya aya ya masuala hayo yenye msisitizo hayaathiri maoni ya ukaguzi. Aya ya masuala yenye msisitizo inajumuishwa pale panapokuwa na mazingira yafuatayo:

- Kuonesha juu ya mambo yanayoweza kuwa na athari ambayo ufumbuzi wake unategemea matukio ya baadaye ambayo hayako ndani ya uwezo wa Halmashauri, na ambayo yanaweza kuleta athari katika taarifa za fedha, kwa mfano matokeo ya masuala yaliyo mahakamani au yale yanayohitaji kushughulikiwa kisheria.
- Kuweka angalizo juu ya mambo mengineyo yaliyooneshwa katika taarifa ya utekelezaji ya mkaguliwa ya mwaka ambayo ni muhimu kuyafanyia marekebisho lakini Mkaguliwa hakufanya hivyo.
- Kuonesha masuala yanayoathiri taarifa za fedha na ambayo yaliyooneshwa katika taarifa za fedha lakini kutokana na umuhimu wake, ni vyema watumiaji wa tarifa hiyo wawe na uelewa wa masuala hayo kama vile janga kubwa lililotokea au linaloendelea kutokea na kuleta madhara makubwa ya hali ya kifedha katika Halmashauri.

2.1.3.3 Masuala mengine

Aya ya masuala mengine inahusu mambo ambayo hayakuoneshwa katika taarifa za fedha na kwamba kwa mtazamo wa mkaguzi ni muhimu mtumiaji wa taarifa za fedha kuelewa ukaguzi, majukumu ya mkaguzi na ripoti ya mkaguzi.

Endapo nitaona inafaa kuwasilisha masuala mengine kuliko yale yaliyooneshwa katika taarifa za hesabu, nitatumia aya ya masuala mengine kwa masuala hayo yenye kichwa cha masuala mengine, ambayo itakuwa baada ya aya ya hati ya ukaguzi na masuala yenye msisitizo kama yapo. Masuala mengine yapo katika sehemu tofauti ya ripoti ya mwaka ya ukaguzi ili kutenganisha wazi wazi kutoka katika majukumu ya mkaguzi, na hati ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha na masuala mengine yaliyokuwa na angalizo katika aya zilizotangulia za msisitizo wa masuala. Mifano ya masuala mengine ni pamoja na kutofuata sheria na udhaifu katika udhibiti wa ndani.

2.2 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi katika Halmashauri

2.2.1 Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sehemu hii ya ripoti ni kwa ajili ya kuonesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2008/2009 hadi 2012/2013. Umuhimu wa taarifa hii ni kuonesha mwelekeo wa hali ya utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Hati za ukaguzi zilizopata kwa miaka mitano imeoneshwa katika **Kiambatisho (ii).**

Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka ya fedha 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013 umeoneshwa hapa chini:

Jedwali Na.4:Hati za Ukaguzi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitano

Miaka	Hati Zinazori-dhisha		Hati zenye shaka		Hati Zisizoridhisha		Hati Mbaya		
	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Idadi ya Halma-shauri
2012/13	112	80	27	19	1	1	0	0	140
2011/12	104	78	29	21	0	0	1	1	134
2010/11	72	54	56	42	5	4	0	0	133
2009/10	66	49	64	48	4	3	0	0	134
2008/09	77	58	55	41	1	1	0	0	133

Kwa ujumla wake inaonesha kumekuwa na maendeleo ya ubora wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa kuzingatia kuongezeka kwa idadi ya Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kutoka 134 katika mwaka 2011/2012 hadi 140 katika mwaka wa fedha 2012/2013.

2.2.2 Mchanganuo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kutokana na mchanganuo wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka mitano, yafuatayo yamebainika:

i) Halmashauri kumi na saba (17) zimeendelea kuwa na hadhi ya kupata Hati zinazoridhisha kwa miaka mitano. Halmashauri husika ni H/W Bukoba, H/W Muleba ,H/W Biharamulo, H/W Misenyi, H/W Kisarawe, H/W Mufindi, H/W Hai ,H/W Siha, H/W Lindi , H/W Simanjiro , H/W Masasi , H/W Tandahimba, H/W Maswa H/W Iramba H/W Serengeti, H/W Muheza na H/W Nachingwea.

ii) Halmashauri sita (6) zimefanya vizuri ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo zilipata Hati zenye shaka na Hati isiyoridhisha na kwa mwaka huu wa fedha zimepata Hati zinazoridhisha ambazo ni H/WMonduli,

H/W.Makete, H/W Mvomero, H/W Sikonge, H/Mji Korogwe na H/Jiji Dar es salaam.

iii) Halmashauri ya Jiji la Arusha imeendelea kupata Hati yenye shaka kwa miaka mitano mfululizo

iv) Halmashauri nne (4) zimeshuka ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo zilipata Hati inayoridhisha lakini katika ukaguzi wa mwaka 2012/2013 zimeweza kupata Hati yenye shaka ambazo ni H/M Bukoba, H/W Shinyanga, H/M Shinyanga na H/W Bariadi

2.2.3 Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopata Hati zisizoridhisha na zenye shaka na sababu zilizopelekea kupata hati hizo

Katika mwaka husika wa ukaguzi, kulikuwa na Halmashauri moja (1) iliyopata hati isiyoridhisha, Halmashauri ishirini na saba (27) zimepata Hati zenye Shaka na hakuna Halmashauri iliyopata hati mbaya. Mchanganuo wa mambo ambayo yalikuwa ni vigezo katika kutoa Hati yenye shaka kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (iii)**

Kutokana na Kiambatisho hicho, baadhi ya mambo yaliyokuwa ni kigezo cha kutoa Hati zenye shaka ni haya yafuatayo:

(i) Maduhuli

- Vitabu vya makusanyo ya maduhuli havikuwasilishwa ukaguzi kwa uhakiki
- Mawakala wa ukusanyaji wa mapato kutowasilisha mapato kwenye Halmashauri husika

(ii) Matumizi

- Hati za malipo na viambatisho vyake havikuwasilishwa kwa ukaguzi hivyo kudhibiti mawanda ya ukaguzi
- Matumizi yasiyo na viambatanisho
- Malipo ya mishahara pamoja na makato kwa watumishi wasio katika utumishi wa umma

(iii) Mali za kudumu

- Thamani ya mali zilizofanyiwa tathmini bila kuwa na viambatanisho
- Tofauti zisizosuluhishwa kati ya urari wa hesabu pamoja na taarifa za fedha
- Thamani ya majengo, mitambo na vifaa kuoneshwa pungufu

(iv) Mali za muda mfupi

- Wadaiwa wa Halmashauri kuoneshwa pungufu
- Kutofanywa usuluhisho wa bakaa ya fedha na fedha za maendeleo ambazo hazikutumika katika tarifa ya matumizi ya mitaji
- Wadai ambao hawakuweza kuthibitishwa

(v) Madeni

- Wadaiwa wa Halmashauri kuoneshwa pungufu
- Wadaiwa wa Halmashauri klutoweza kuthibitishwa

Menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani katika utoaji wa taarifa za fedha ikiwa ni pamoja na kufuata miongozo ya uandaaji hesabu kutumia "IPSAS accrual basis" pamoja na taratibu na kanuni za fedha ili hesabu zitakazowasilishwa zikidhi viwango vilivyowekwa.

- Pamoja na kutolea taarifa katika mwaka uliopita, bado kumekuwa na Mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufariki, kuachishwa kazi, watoro na watumishi waliohamishiwa utumishi wao sehemu nyingine. Malipo haya yalifanyika kupitia kwenye akaunti zao binafsi za benki, Serikali haikunufaika kutokana na malipo ya jinsi hii.
- Thamani ya Vifaa, magari na mitambo iliyofanyiwa uthamini kwa mara nyingine ilioneshwa kwenye tarifa za fedha bila kuwa na kiambatanisho.
- Thamani ya Vifaa, magari na mitambo ilioneshwa pungufu kwenye taarifa za fedha.
- Kuwepo kwa tofauti ya hesabu isiyosuluhishika kati ya urari na taarifa za fedha.
- Malipo ya mishahara, na yale yanayohusiana na makato ya kisheria kwa ajili ya watumishi walitoroka, wastaafu na waliofariki.
- Hati za malipo pamoja na viambatanisho vyake havikupatikana kwenye makabrasha yake na hivyo kukwaza mawanda ya ukaguzi.
- Baadhi ya hati za malipo hazikuwa na viambatanisho vya kutosha na hivyo kufanya ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
- Kulikuwa na upotoshwaji kwa kuonesha wadai na wadaiwa pungufu.
- Kuwepo kwa tofauti isiyosuluhishika kati ya bakaa ya fedha taslimu na ile iliyooneshwa kwenye taarifa ya matumizi ya maendeleo.
- Hapakuwa na michanganuo ya wadaiwa, hivyo ukaguzi ulishindwa kuthibitisha uhalali na usahihi wa taarifa hizo.
- Mawakala wa kukusanya mapato kutowasilisha makusanyo yatokanayo na mapato ya Halmashauri na

hivyo kuisababisha Halmashauri kushindwa kutoa huduma kwa wananchi wake.

- Kutowasilisha kwa Idadi kubwa ya vitabu vya kukusanyia mapato kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo, kiasi cha mapato yaliyokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo hayakuweza kuthibitika.
- Vifungu vya matumizi vililipiwa kimakosa kutoka vifungu vingine na hivyo kupotosha taarifa za fedha zilizoletwa.

Mapungufu yote yaliyoainishwa hapo juu yalisababishwa kwa kiasi kikubwa na mambo yafuatayo:

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuimarisha mifumo ya Udhibiti wa Ndani, kutokana na kuwa, udhaifu mwingi niliouonesha hapo juu umetokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Maeneo muhimu ya kuzingatiwa ni kama ifuatavyo:

- Mafunzo endelevu juu ya IPSAS ni suluhisho kwa baadhi ya mapungufu yaliyobainishwa hapo juu. Viwango vya Kimataifa vinabadilika kila mara, hivyo kuna haja ya mafunzo hayo kuwa endelevu kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi.

SURA YA TATU

3.0 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

Sehemu hii inajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya awali ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa Halmashauri husika.

3.1 Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka iliyopita

3.1.1 Mapendekezo katika Ripoti ya jumla ya Ukaguzi

Kifungu cha 40(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kupokea majibu kutoka kwa Maafisa Masuuli na baada ya hapo kuwasilisha kwa Waziri anayehusika na mambo ya fedha ambaye atapeleka mbele ya Bunge. Pia, Mlipaji Mkuu anawajibika kuwasilisha nakala jumuifu ya majibu na mpango wa utekelezaji kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Pia, kifungu cha 40 (4) kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujumuisha hali halisi ya utekelezaji wa mpango kazi katika ripoti ya ukaguzi wa mwaka unaofuata. Majibu juu ya masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa mwaka wa fedha uliomalizika Juni 30, 2012 yalitolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa barua yenye Kumb. Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya tarehe 25 Juni 2013. Hali halisi ya masuala ambayo yanahitaji ufuatiliaji kwa ajili ya utekelezaji umeonyeshwa katika **kiambatisho (iv)**

Jedwali hapa chini linaonesha muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ripoti ya mwaka wa fedha 2011/2012.

Jedwali Na.5: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotelewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ripoti ya mwaka wa fedha 2011/2012:

Mwaka	Idadi ya Mapendekezo	Yaliyotekelezwa	%	Yaliyo katika hatua ya uteke-lezaji	%	Yasiyoteke-lezwa
2011/12	33	2	6	17	52	14

3.1.2 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa katika Ripoti ya kila Halmashauri

Wakati wa kaguzi zilizopita, mapendekezo mbalimbali ya msingi yalitolewa. Kati ya Hamashauri 134, Halmashauri 131 hazikutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita yenye jumla ya Sh.341,081,810,170 kama inavyoonesha katika **kiambatisho (v).**

Jedwali hapa chini linaonesha kwa muhtasari hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa katika kaguzi za miaka iliyopita kuanzia mwaka 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012 kama ifuatavyo:

Jedwali Na.6: Mwenendo wa masuala yaliyosalia kwa miaka mitano mfululizo katika ripoti za kila Halmashauri

Mwaka wa fedha	Idadi ya Halmashauri husika	Hoja za ukaguzi zilizosalia ambazo zilithaminishwa (Sh)
2011/2012	131	341,081,810,170
2010/2011	131	78,489,936,013
2009/2010	130	105,263,165,967
2008/2009	129	122,128,377,615
2007/2008	126	53,463,558,647
2006/2007	112	32,903,395,306

Kutotekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni dalili kuwa mifumo ya ndani ya udhibiti katika Halmashauri haijaanzishwa vizuri ili kuhakikisha kuwa ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali unafanyika kwa wakati. Hii inapelekea kujirudia kwa hoja ambazo zimetolewa na wakaguzi kwa miaka ya nyuma.

3.1.3 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa katika Ripoti za Kaguzi Maalum

Kifungu 36 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinaeleza kuwa, iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona kuwa kuna jambo lolote lihusulo fedha au mali ya umma ambalo inabidi Bunge lijulishwe pasipo kuchelewa, ataandaa taarifa maalumu kuhusiana na jambo hilo na kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni kupitia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika mwaka wa ukaguzi uliopita, mapendekezo mbalimbali yaliyotokana na hoja za kaguzi maalum yalitolewa katika Halmashauri 14. Hata hivyo, kati ya Halmashauri 14, Halmashauri 7 zimewasilisha majibu ambayo yanaendelea kufanyiwa uchunguzi, na Halmashauri 7 bado hazijawasilisha.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali za Serikali katika ripoti za ukaguzi maalum inaonyeshwa katika **kiambatisho (vi).**

Jedwali hapa chini linaonesha muhtasari wa hoja za ukaguzi maalum ambazo hazijajibiwa katika kaguzi za miaka iliyopita kuanzia mwaka 2008/09, 2009/10, 2010/11 na 2011/12.

Jedwali Na.7:Muhtasari wa masuala yaliyosalia katika ripoti za ukaguzi maalum

Mwaka wa fedha	Idadi ya Halmashauri husika	Hoja za ukaguzi zilizosalia ambazo hazikuthaminishwa	Hoja za ukaguzi zilizosalia ambazo zilithaminishwa (Sh.)
2011/2012	14	302	66,471,126,999
2010/2011	13	69	31,408,213,793.00
2009/2010	7	40	43,012,029,632.00
2008/2009	8	8	2,532,943,672.00

3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Sehemu hii inatoa maelezo kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kama inavyohitajika katika Kifungu cha 40(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma ya mwaka 2008 ambacho kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa majibu na mpango wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yakizingatia udhaifu uliobainika na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge za Usimamizi.

Tarehe 6 Disemba Mwenyekiti wa LAAC aliwasilisha ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ikijumuisha mapendekezo muhimu juu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Hata hivyo, hadi wakati wa kuandika taarifa hii Marchi 2014, hakuna majibu yaliyopokelewa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali juu ya mapendekezo 10 yaliyotolewa na Kamati ya Bunge kama inavyooneshwa hapa chini:

3.2.1 Udhaifu katika usimamiaji na utekelezaji wa sheria za Manunuzi ya Umma

Kamati ya Bunge ilipendekeza kuwa Sheria za manunuzi ya Umma na kanuni zake zifuatwe na zizingatiwe ili kuwezesha manunuzi yanayofanyika kuwa na thamani na tija. Pia Kamati za Ukaguzi ziimarishwe na ziwe zinawasilisha taarifa zake kwa wakati.

3.2.2 Udhaifu katika usimamizi wa miradi

Kamati ilipendekeza kuwa Wataalam wanaohusika na usimamizi wa miradi mbalimbali watembelee mara kwa mara maeneo ambayo miradi inatekelezwa na kuepukana na tabia ya kubaki ofisini tu.

3.2.3 Kuanzishwa Kwa Miradi na Jamii husika

Kamati ilipendekeza kuwa miradi yote inayowahusu jamiii ni vyema ishirikishwe ili isiwe na mashaka na pia iweze kuitunza na kuiendeleza miradi hiyo.

3.2.4 Kutothaminiwa kwa Michango ya Wananchi katika miradi ya Maendeleo

Kamati ilipendekeza kuwa ni muhimu michango inayotolewa na wananchi ioneshwe katika hesabu za Halmashuri husika, kwa kufanya hivyo kutawapa moyo wananchi na kuwahamasisha kwa kuona juhudi zao na michango yao inatambuliwa na kuthaminiwa.

3.2.5 Kuchelewa kuwasilisha taarifa za Utekelezaji wa Miradi

Kamati ilipendekeza kuwa Maafisa Masuuli wazingatie maelekezo yatakayowawezesha wakaguzi kukagua utendaji na utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa kipindi kinachokaguliwa na kuioanisha na taarifa nyingine za fedha. Pia Maafisa Masuuli wawe wanafanya ziara kwenye miradi husika ili kutathmini hali halisi ya miradi na mafanikio yaliyofikiwa. Hii itawasaidia wakaguzi katika kutathmini uwepo wa thamani ya fedha katika miradi iliyotekelezwa na Halmashauri husika na kutoa taarifa juu ya matokeo ya tathmini hiyo.

3.2.6 Weledi wa Madiwani katika kusimamia Shughuli mbalimbali za Halmashauri

Kwa kuwa Halmashauri inatekeleza shughuli mbalimbali ambazo zinahusiana na taaluma tofauti tofauti, Kamati inapendekeza kuwa Madiwani wajengewe uwezo ili wawe na weledi juu ya yale wanayoyasimamia katika Halmashauri zao. Maslahi na mazingira ya kazi yaboreshwe ili waweze kusimamia vyema fedha za Umma katika Halmashauri zao. Pia pawepo na mpango mkakati wa kuwajengea uzalendo Waheshimiwa Madiwani ambao ndio wasimamizi wakuu wa fedha za Umma.

3.2.7 Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato

Kamati ilibaini madhaifu mengi katika ukusanyaji wa mapato hasa kwa kutumia mawakala na kupendekeza yafuatayo:

- Mikataba kati ya mawakala na Halmashauri iandaliwe kisheria kwa kumshirikisha Mwanasheria wa Halmashauri, sambamba na kulinda maslahi ya Halmashauri husika.
- Mipango sahihi na thabiti ifanywe kabla ya kufikia uamuzi juu ya kuingia uwakala vyanzo vya mapato kwa

mawakala pamoja na kuzingatia taratibu za kuwapata mawakala wenye sifa.

- Waheshimiwa Mameya, Wenyekiti, Madiwani, na Watendaji wa Halmashauri wasiwe wenye kumiliki kampuni za kiuwakala na ambazo huchukua kazi za Uwakala au Ukandarasi katika Halmashauri husika ili waweze kufuatilia na kusimamia vyema utendaji wa mawakala au Wakandarasi hao.
- Halmashauri zifanye utafiti wa kina wa hali ya soko na kufanya upembuzi yakinifu kwa kila chanzo cha mapato kama msingi wa kuingia uwakala.
- Halmashauri zianze taratibu za kutumia mashine za kieletroniki (EFD) zitolewazo na TRA kwa ajili ya kutoa risiti za kukiri mapokezi ya fedha (hii itaondoa tatizo la upotevu wa vitabu vya risiti)
- Halmashauri kupitia Maofisa Mipango ziwe na mipango kabambe na endelevu ya kuibua vyanzo vipya vya mapato ikiwa ni pamoja na kodi za Majengo, mabango ya matangazo ya biashara, mirahaba na kodi za huduma.

3.2.8 Usiri katika utoaji wa taarifa kwa umma

Kamati ilipendekeza kuwa Halmashauri zitangaze taarifa za mapato na matumizi yake ya mwaka katika lugha ya Kiswahili. Taarifa hizo zitangazwe katika magazeti yanayopatikana eneo husika, na pia ziambatanishwe na mambo ya msisitizo *(Emphasis of matters)* kama inavyotakiwa katika kifungu cha 49 cha sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 na Agizo cha 31(9) la Memoranda ya fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 2009.

3.2.9. Udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI katika kuboresha mifumo ya udhibiti ya ndani, Kamati imebaini kuwepo kwa mapungufu mbalimbali katika mifumo hiyo na kupendekeza yafuatayo:-

a) Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kiimarishwe na kiwe kinajitengemea

b) Kamati ya Ukaguzi (*Audit committee*) ifanye shughuli zake ipasavyo na kwa ufanisi.

c) Mifumo ya kubaini viashiria vya wizi na ubadhilifu viimarishwe ikiwa ni pamoja na kuimarisha Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) Epicor 9.05, Lawson na Mfumo wa usimamizi wa Mapato (MRECOM).

3.2.10 Madeni ya Halmashauri

Kutokana na kuongezeka kwa madeni ya Halmashauri katika mwaka 2012/2013 yaliyofikia Sh.62,192,971,408 ikilinganishwa na madeni ya Sh.48,443,176,126 kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ilipendekezwa kuwa madai hayo yafanyiwe tathmini na yalipwe haraka iwezekanavyo, sambamba na kuongeza jitihada za kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa ili kuepusha Halmashauri zetu kuwa na kesi nyingi mahakamani, kwa mfano Halmashauri 18 kati ya 134 zilizokaguliwa zimegubikwa na wimbi zito la kesi zilizoko mahakamani zenye thamani ya sh.8.698,124,431.

SURA YA NNE

4.0 TATHMINI YA HALI YA FEDHA ZA HALMASHAURI

4.1 Ukaguzi wa Bajeti

Bajeti ni kitendo cha kuonesha kiasi cha fedha zitakazohitajika ili kukamilisha mipango iliyopangwa kabla ya kipindi cha utekelezaji wa mipango hiyo hakijafika. Bajeti hueleza ni kipi cha kufanya na kutenga rasilimali fedha na rasilimali nyingine ambazo zinahitajika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Bajeti inaonesha mpango sahihi wa fedha, kusimamia, kudhibiti na pia inatoa taarifa muhimu za kifedha kwa watoa maamuzi.

Kif. 43(1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) imeainisha kwamba, kila Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya mwanzo wa kila mwaka wa fedha, katika mkutano maalum utakaopitishwa, ipitishe bajeti ya makadirio ya kiasi: (a) inachotarajia kupokea na (b) inachotarajia kutolewa, na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika, na wakati wowote itakapohitajika, Mamlaka inaweza kupitisha bajeti ya ziada katika mwaka wa fedha husika.

Katika kipindi cha ukaguzi wa mwaka huu, mapungufu yafuatayo yalionekana katika ukaguzi wa bajeti:

4.2 Mwenendo wa Makusanyo ya mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

Mapato ya ndani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kiasi cha fedha ambacho kimekadiriwa na kukusanywa na Halmashauri husika kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vilivyoainishwa ikiwemo kodi za ndani, ada, tozo, adhabu, ada za mauzo ya leseni na mapato mengine katika mwaka husika.Kiasi hiki kinatumika katika Halmashauri pamoja na ruzuku inayotoka Serikali Kuu na wafadhili katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Halmashauri.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa 140 zilipanga kukusanya mapato kupitia vyanzo vyao vya ndani kwa kiasi cha Sh.310,707,485,716. Hata hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliweza kukusanya kiasi cha Sh.268,636,147,917, hii ikiwa ni chini ya bajeti kwa kiasi cha Sh.42,071,337,799 sawa na asilimia 13.5 ya makisio yaliyopangwa kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho (vii).**
Mchanganuo ufuatao unaonesha mwenendo wa bajeti iliyopitishwa kwa miaka mitano na makusanyo halisi kutoka kwenye vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Jedwali Na.8: Mwenendo unaoonesha bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya makusanyo halisi

Mwaka wa Fedha	Bajeti Iliyoidhinishwa (Sh.)	Mapato halisi (Sh.)	Tofauti (Sh)	Asilimia
2012/13	310,707,485,716	268,636,147,917	(42,071,337,799)	(13.5)
2011/12	297,383,435,946	236,716,345,736	(60,667,090,210)	(20.4)
2010/11	183,470,314,765	184,344,284,252	873,969,486	0.5
2009/10	136,673,109,767	137,416,106,722	742,996,955	0.5
2008/09	111,327,810,815	110,852,341,512	(475,469,303)	(0.4)

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba, katika mwaka wa fedha 2009/10 na 2010/11 kumekuwa na makusanyo zaidi ya bajeti kwa tofauti ya asilimia 0.5 kwa miaka yote miwili. Ingawa mwaka wa fedha 2008/2009, 2011/2012 na 2012/2013 makusanyo halisi yamekusanywa pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa kwa tofauti ya asilimia 0.4, 20.4 na 13.5 kwa mtiririko huo.

Zaidi ya hayo, mwenendo unaonesha ongezeko la bajeti na mapato halisi kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009 hadi 2012/2013. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2012/2013, bajeti iliyoidhinishwa imeongezeka kwa asilimia 4.5 na mapato halisi yameongezeka kwa asilimia 13.5.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuandaa bajeti yenye uhalisia na kuwa na mikakati imara katika ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato na hatimaye kuziwezesha Halmashauri kujiendesha kwa ufanisi zaidi. Pia, kuna vyanzo zaidi vya mapato ambavyo havijatambuliwa hivyo kupelekea kutokusanywa. Inapendekezwa kuwa Serikali za Mitaa zifanye upembuzi yakinifu ili kuweza kubaini na kuvitumia vyanzo vipya kuongeza mapato na kupunguza kiwango cha utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

4.3 Fedha zilizotolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa

4.3.1 Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizotolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa 40 zilipitishwa bajeti ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ya jumla ya Sh.819,461,698,489, ambapo kiasi cha Sh.897,430,294,282 kilipokelewa na hivyo kupelekea kiasi cha Sh.77,968,595,793 kutolewa zaidi ya bajeti ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa fedha zilizotolewa zaidi unaoneshwa kwenye **Kiambatisho (viii).**

Kukosekana kwa bajeti ya ziada ya kiasi kilichozidi kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha hizo. Inapendekezwa kwamba kibali kutoka mamlaka husika kipatikane kwanza ya kabla ya matumizi ya ziada kufanyika.

4.3.2 Fedha za ruzuku ya maendeleo zilizotolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa 22 ziliidhinishiwa bajeti ya fedha za ruzuku ya maendeleo ya Sh.72,797,438,713, ambapo kiasi cha Sh.86,265,649,139 zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo kupelekea kiasi cha Sh.13,468,210,426 kutolewa zaidi ya bajeti ya ruzuku ya maendeleo iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa fedha zilizotolewa zaidi unaoneshwa kwenye **Kiambatisho (ix).**

Hazina haikutoa fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge; kitendo hiki kinaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha za ziada ukizingatia kuwa fedha hizi hazina bajeti.

Inapendekezwa kwamba vibali kutoka mamlaka husika viwe vinapatikana na bajeti za ziada ziandaliwe kabla ya kufanyika kwa matumizi.

4.4 Fedha zilizotolewa pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti

4.4.1 Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizotolewa pungufu

Jumla ya Sh.2,102,969,648,522 zilipitishwa kwenye bajeti ya ruzuku ya matumizi ya kawaida kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 99. Lakini kiasi kilichopokelewa kwa mwaka unaokaguliwa ni Sh.1,827,566,402,405 kwa ajili ya utekelezaji wa matumizi ya kawaida, hivyo kupelekea upungufu wa Sh.275,403,246,117.

Utolewaji wa fedha pungufu za bajeti iliyoidhinishwa inapunguza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza shughuli zilizopangwa. Mchanganuo wa fedha zilizotolewa pungufu unaoneshwa kwenye **Kiambatisho (x).**

Jedwali hapo chini linaonesha mwenendo wa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida ambazo hazikupokelewa kwa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na.9: Mwenendo wa fedha ambazo hazikupokelewa

Mwaka wa fedha	Bajeti ya Ruzuku iliyoidhinishwa (Sh.)	Kiasi halisi kilichopokelewa (Sh.)	Kiasi kisichopokelewa (Sh.)	%	Idadi ya Halmashauri
2012/13	2,102,969,648,522	1,827,566,402,405	275,403,246,117	13	99
2011/12	1,618,877,128,175	1,447,482,142,661	171,394,985,514	11	87
2010/11	1,242,318,963,483	1,111,762,925,260	130,556,038,222	11	78
2009/10	1,248,760,338,699	1,104,588,746,584	144,171,592,119	12	87
2008/09	848,244,823,445	757,195,467,343	91,049,356,102	11	73

Jedwali hapo juu linaonesha ongezeko la bajeti kutoka Sh.848,244,823,445 mwaka wa fedha 2008/2009 hadi Sh.2,102,969,648,522 mwaka wa fedha 2012/2013 na pia kiasi halisi kilichopokelewa kimeongezeka kutoka Sh.757,195,467,343 katika mwaka 2008/09 hadi Sh.1,827,566,402,405 mwaka 2012/2013kwa mtirirko huo. Hata hivyo, kiasi kisichotolewa kimeongezeka kutoka Sh.91,162,719,876 mwaka 2008/2009 hadi Sh.275,403,246,117 mwaka wa fedha 2012/2013, hivyo kuna ongezeko dogo la asilimia 2 la kiasi kisichotolewa.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia OWM-TAMISEMI kuwasilisha athari za kutolewa fedha pungufu ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Zaidi ya hayo, ninazishauri Halmashauri husika kupanga matumizi kulingana na fedha iliyopokelewa.

4.4.2 Fedha za Ruzuku ya Maendeleo zilizotolewa pungufu

Katika mwaka huu wa fedha unaokaguliwa, jumla ya Sh.673,590,626,951 zilipitishwa kwenye bajeti ya ruzuku ya maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 114. Kiasi cha Sh.420,283,949,168 kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo, hivyo kupelekea upungufu wa kiasi cha Sh.253,306,677,783 ambazo hazijapokelewa.

Hii inamaanisha kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo haikutekelezwa kabisa na mingine imetekelezwa kwa

sehemu tu. Mchanganuo wa fedha zilizotolewa pungufu unaoneshwa kwenye **Kiambatisho (xi).**

Jedwali la hapo chini linaonesha mwenendo wa fedha za Ruzuku ya Maendeleo ambazo hazikupokelewa kwa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na.10: Mwenendo wa fedha za maendeleo ambazo hazikupokelewa

Mwaka wa fedha	Bajeti ya Ruzuku ya Maendeleo iliyoidhinishwa (Sh.)	Kiasi halisi kilichopokelewa (Sh.)	Kiasi kisichopokelewa (Sh.)	% ya kiasi kisichopokelewa	Idadi ya Halmashauri
2012/13	673,590,626,951	420,283,949,168	253,306,677,783	38	114
2011/12	595,064,422,505	345,568,067,477	249,496,355,027	42	113
2010/11	529,494,590,274	308,572,669,609	220,921,920,666	42	105
2009/10	395,038,612,520	246,475,254,935	148,563,337,585	38	86
2008/09	386,165,146,158	245,623,406,798	140,541,739,360	36	105

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba kuna ongezeko kubwa la bajeti ya ruzuku ya maendeleo. Pia, kuna ongezeko la fedha za ruzuku ya maendeleo zisizopokelewa kwa tofauti ya asilimia 2 kwa mwaka wa fedha 2009/2010, asilimia 4 kwa mwaka wa fedha 2010/2011, hakuna ongezeko kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 na kiasi kisichopokelewa kimepungua kwa asilimia 4 kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mamlaka za serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI inashauriwa kufuatilia suala hili katika Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kuwa fedha zilizopitishwa katika bajeti ya ruzuku ya maendeleo inapokelewa ili kutekeleza shughuli zilizopangwa. Vile vile, Halmashauri zinashauriwa kupanga utekelezaji wa miradi kulingana na umuhimu wa mradi husika na kujumuisha miradi isiyotekelezwa kwenye bajeti ya mwaka unaofuata.

4.5 Matumizi yaliyofanyika bila kuwepo katika bajeti

Katika mwaka wa fedha unaokaguliwa, jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 zimetumia kiasi cha Sh.741,163,865 kulipia madeni ya miaka iliyopita bila kuwepo kwenye orodha ya wadeni waliyoorodheshwa kwenye taarifa za fedha za mwaka wa fedha husika. Hii ni kinyume na Agizo 22(1) ya Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Zaidi ya hayo, taarifa za fedha za mwaka husika zitakuwa zimeadhirika kutokana na fedha za kulipa madeni hayo kutokuwa katika bajeti.

Hii inamaanisha kuwa shughuli zilizopangwa sawa na kiasi hicho cha fedha hazikutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha unaokaguliwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakumbushwa kuomba idhini ya kubadilisha matumizi kutoka mamlaka husika pale ambapo fedha za mwaka husika zinalipa madeni ya nyuma yasiyokuwa katika bajeti ya Halmshauri.

Matumizi yaliyofanywa na Halmashauri bila kuwepo kwenye bajeti yanaoneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na.11: Matumizi yaliyofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kuwepo kwenye bajeti

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi kilichotumika nje ya bajeti (Sh.)
1	H/W Mkuranga	28,435,500
2	H/W Mafia	3,844,500
3	H/W Rufiji	16,537,084
4	H/W Nzega	2,800,000
5	H/M Kigoma/Ujiji	2,917,000
6	H/W Arusha	18,045,187
7	H/W Ngorongoro	10,834,950
8	H/W Meru	19,775,000
9	H/W Longido	78,843,772
10	H/M Moshi	4,957,000
11	H/W Hai	36,410,000
12	H/W Mwanga	7,093,250
13	H/Jiji Tanga	17,993,000
14	H/W Korogwe	20,697,605
15	H/W Muheza	13,414,673
16	H/W Pangani	10,783,973
17	H/W Rorya	10,317,490
18	H/M Bukoba	9,411,200
19	H/W Biharamulo	2,805,000
20	H/W Muleba	8,473,800
21	H/W Magu	17,170,560
22	H/W Sengerema	17,929,000
23	H/W Geita	150,000,000
24	H/W Bukombe	30,615,000
25	H/W Bariadi	6,231,633
26	H/M Sumbawanga	18,248,120
27	H/W Sumbawanga	24,877,400
28	H/W Nkasi	7,042,140
29	H/W Njombe	2,760,613
30	H/Jiji Mbeya	37,409,926
31	H/W Ileje	1,801,458
32	H/W Mpanda	10,874,524
33	H/W Mbinga	41,296,694
34	H/W Chamwino	50,516,813
	Jumla	**741,163,865**

4.6 Mwenendo wa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri ikilinganishwa na matumizi ya kawaida

Ruzuku ya matumizi ya kawaida ni ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kuendesha shughuli za kila siku za Halmashauri kama vile mishahara, manunuzi ya vifaa na huduma ambazo zinapewa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh.268,948,851,548 kutoka vyanzo vyao vya ndani na kutumia jumla ya Sh.2,746,333,799,161 katika matumizi ya kawaida. Ulinganisho kati ya mapato na matumizi ya fedha umebaini kuwa Serikali za Mitaa, kwa kutumia mapato yake ya ndani zinaweza kugharamia matumizi ya shughuli za kawaida kwa asilimia 9.8 bila kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu na wafadhili. Mchanganuo kwa kila Halmashauri ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho (xii).**

Mwelekeo wa vyanzo vya mapato ya ndani vilivyokusanywa dhidi ya matumizi ya kawaida kwa miaka mitano ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini:

Jedwali Na.12: Mwelekeo wa mapato ya ndani dhidi ya matumizi ya kawaida

Mwaka Wa Fedha	Mapato toka vyanzo vya ndani (Sh.)	Matumizi ya Kawaida (Sh.)	%
2012/13	268,948,851,548	2,746,333,799,161	10
2011/12	236,716,345,736	2,277,035,217,362	11
2010/11	184,344,284,252	2,153,971,770,095	9
2009/10	137,416,106,722	1,823,788,009,947	8
2008/09	110,852,341,512	1,437,216,933,939	8

Inapendekezwa kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zijidhatiti katika kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa kuhakikisha kuwa vyanzo zaidi vinatambuliwa, udhibiti katika ukusanyaji wa mapato unaongezeka kwa kuzuia mianya ya upotevu na kutathmini upya mikakati ya ukusanyaji ili kutambua sehemu dhaifu na baadaye kuandaa mkakati wa kudhibiti udhaifu huu.

4.7 Ruzuku ya matumizi ya kawaida isiyotumika

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 140 zilitumia kiasi cha Sh.2,721,098,075,973 katika shughuli za kila siku ikilinganishwa na ruzuku kutoka Serikali Kuu ya jumla ya Sh.2,867,426,385,004, hivyo kupelekea bakaa ya Sh.146,328,309,031 sawa na asilimia 5 ya fedha za ruzuku za matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu. Mchanganuo umeoneshwa katika **Kiambatisho (xiii).**

Jedwali hapa chini linaonesha mwenendo wa ruzuku ya kawaida ambayo haikutumika kwa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na.13: Mwenendo wa ruzuku ya kawaida ambayo haikutumika kwa miaka mitano mfululizo

Mwaka wa Fedha	Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida iliyopokelewa (Sh.)	Matumizi halisi ya Kawaida (Sh.)	Ruzuku isiyotumika (Sh.)	% ya Ruzuku isiyotumika
2012/13	2,867,426,385,004	2,721,098,075,973	146,328,309,031	5.0
2011/12	2,311,080,861,836	2,186,486,605,144	124,594,256,692	5.4
2010/11	2,105,926,241,086	1,978,117,478,839	127,808,735,247	6.0
2009/10	1,521,937,206,309	1,373,576,272,098	148,360,934,211	9.7
2008/09	1,023,504,263,229	976,332,807,352	47,171,455,877	4.6

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba, ruzuku ya matumizi ya kawaida ambayo haijatumika imeongezeka kutoka asilimia 4.6 mwaka 2008/2009 hadi asilimia 9.7 mwaka

2009/2010 ya jumla ya ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa na mamlaka hizo. Hata hivyo, kiasi hicho kilipungua katika mwaka wa fedha 2010/2011 hadi asilimia 6 na ikaendelea kupungua hadi asilimia 5 katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha ruzuku ya matumizi ya kawaida ambacho hakijatumika inamaanisha kuwa , Serikali Kuu haikuwa na ufanisi katika kupeleka ruzuku kwa wakati au kulikuwa na ukiritimba wa utumiaji fedha katika Halmashauri. Hivyo, ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za kila siku katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unaathirika na hivyo kuzuia utekelezaji wa huduma zilizoainishwa kwa umma. Hii pia inaweza kusababisha kufanyika marekebisho ya bajeti ili kufidia athari za ongezeko la bei ya mali na vifaa zilizosababishwa na mfumuko wa bei.

Kwa hiyo, inapendekezwa kuwa ruzuku ya kawaida ni vyema ikatolewa kwa wakati. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuhakikisha kuwa,taratibu za ruzuku ya matumizi ya kawaida zinazingatiwa, kwa kuwezesha matumizi ya kawaida ambayo yanachochea kuongeza utoaji wa huduma bora.

4.8 Ruzuku ya miradi ya maendeleo isiyotumika

Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kujenga miundombinu au kufanya ukarabati wa miundombinu iliyopo kulingana na maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa lengo la kujenga uwezo katika jamii, kuboresha huduma na kupunguza umaskini. Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutumika katika maeneo yanayohusu kupunguza umaskini kama vile Afya, Elimu, Maji, Barabara na Kilimo.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha Sh.686,302,878,625 kilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za

Mitaa 138 ikiwa ni ruzuku ya fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Hata hivyo, hadi kufikia Juni 30, 2013 kiasi cha Sh.442,625,815,185 sawa na asilimia 64 kilitumika, na kubakia kiasi cha Sh. 243,677,063,440 sawa na asilimia 36 ya fedha zote zilizotolewa. Mchanganuo wa Halmashauri zilizokuwa na fedha za maendeleo ambazo zimebaki ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xiv)**

Mwenendo wa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo zisizotumika kwa miaka mitano mfululizo ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na.14: mwenendo wa fedha ambazo hazikutumika za miradi ya maendeleo

Mwaka wa Fedha	Ruzuku iliyotolewa (Sh.)	Kiasi kilichotumika (Sh.)	Kiasi kilichosalia (Sh.)	%	Idadi ya Halma-shauri
2012/13	686,302,878,625	442,625,815,185	243,677,063,440	36	138
2011/12	535,017,077,030	346,716,653,619	188,300,423,411	35	132
2010/11	542,339,143,645	367,778,247,642	174,560,896,003	32	130
2009/10	507,866,599,666	332,092,443,562	175,774,156,104	35	133
2008/09	328,203,178,845	239,482,549,650	88,720,629,195	27	118

Kuwepo kwa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo zisizotumika ni uthibitisho kwamba, miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa ruzuku hizi haikutekelezwa kikamilifu kama ilivyopangwa na hivyo huduma au faida zinazotokana na miradi hiyo kwa jamii husika hazijafikiwa. Hii pia inaweza ikasababisha mabadiliko ya bajeti ili kufidia athari zitakazotokana na mfumuko wa bei.

4.9 Fedha ambazo hazikutumika miaka iliyopita hazikujumuishwa kwenye bajeti ya mwaka huu (2012/2013) wa fedha

Kif. 43(1) (b) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) imeainisha kwamba, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya mwanzo wa kila

mwaka wa fedha, katika mkutano maalum utakaopitishwa, ipitishe bajeti ya makadirio ya kiasi (a) inachotarajia kupokea na (b) inachotarajia kutolewa, na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika, na wakati wowote itakapohitajika, Mamlaka inaweza kupitisha bajeti ya ziada katika mwaka wa fedha husika. Kinyume na kifungu hicho, jumla ya Sh.363,610,355,254 ikiwa ni fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa 128 zilizovuka mwaka 2011/2012 hazikujumuishwa kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013. Fedha hizi ni kwa ajili ya Maendeleo Sh.185,443,546,310 na fedha za matumizi ya kawaida Sh.178,166,808,944. Hii imepelekea kufanyika kwa matumizi zaidi ya bajeti. Mchanganuo wa fedha hizi unaoneshwa kwenye **Kiambatisho (xv)-a na (xv)-b**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kupata kibali cha matumizi ya fedha hizo na kukiwasilisha ukaguzi kwa ajili ya kuhakikiwa.

4.10 Makusanyo Pungufu katika vyanzo vikuu vya mapato ya ndani

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, vyanzo vikuu viwili yaani Kodi ya Majengo kwa Halmashauri za Manispaa na Majiji, na kwa upande mwingine ushuru wa mazao katika Halmashauri za Wilaya viliangaliwa na kuchanganuliwa. Yafuatayo ni maelezo ya kina:

4.10.1 Makusanyo pungufu ya Kodi ya Majengo

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 15 zilipanga kukusanya mapato ya kiasi cha Sh.16,990,245,305 kutokana na Kodi ya Majengo. Hata hivyo Mamlaka ya Serikali za Mitaa ziliweza kukusanya mapato ya Sh.10,283,099,573, hii inamaanisha kwamba Halmashauri zilikusanya pungufu ya bajeti kwa Sh.6,707,145,732 sawa na asilimia 39.5 ya bajeti.

Jedwali Na.15: Orodha ya Halmashauri ikionesha makusanyo pungufu ya Kodi ya Majengo

Na.	Halmashauri	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Mapato Halisi (Sh.)	Mapato Pungufu (Sh.)	% ya Mapato Pungufu
1	H/M Ilala	4,050,000,000	1,853,962,959	2,196,037,041	54.2
2	H/M Temeke	1,250,000,000	752,389,055	497,610,945	39.8
3	H/M Kinondoni	2,200,000,000	1,804,476,749	395,523,251	18.0
4	H/Jiji Dar es salaam	3,109,971,000	2,131,303,000	978,668,000	31.5
5	H/M Morogoro	520,000,000	294,926,715	225,073,285	0.4
6	H/Mji Kibaha	144,185,000	107,613,900	36,571,100	25.4
7	H/M Kigoma/Ujiji	152,000,000	42,137,899	109,862,101	72.3
8	H/Jiji Arusha	3,614,000,000	2,377,095,000	1,236,905,000	34.2
9	H/Mji Babati	11,250,000	6,132,000	5,118,000	45.5
10	H/Jiji Tanga	517,480,000	269,955,785	247,524,215	47.8
11	H/Mji Korogwe	35,700,000	7,289,590	28,410,410	79.6
12	H/M Bukoba	241,367,912	201,994,939	39,372,973	16.3
13	H/Mji Geita	2,776,000	910,000	1,866,000	67.2
14	H/Jiji Mwanza	962,749,393	367,637,658	595,111,735	61.8
15	H/M Tabora	178,766,000	65,274,324	113,491,676	63.5
	Jumla	**16,990,245,305**	**10,283,099,573**	**6,707,145,732**	**39.5**

Jedwali hapo juu linadhihirisha kwamba, Halmashauri tajwa hazikukusanya Kodi ya Majengo kama zilivyokasimiwa kwa wastani wa asilimia 39.5. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuandaa bajeti zenye uhalisia na vile vile kuwa na mikakati imara katika ukusanyaji wa Kodi za Majengo kwa lengo la kuongeza wigo wa mapato na hatimaye kuziwezesha Halmashauri husika kujiendesha zenyewe kwa ufanisi zaidi.

4.10.2 Makusanyo pungufu ya ushuru wa mazao

Ushuru wa Mazao ni moja ya chanzo kikuu cha mapato ya ndani kwa Halmashauri za Wilaya na hutozwa kwa mazao mbalimbali yanayopatikana ndani ya halmashauri husika. Hii inahusisha mazao yote ya biashara na chakula kama mahindi, pamba, nazi, na mawese.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa 93 zilikasimiwa kukusanya ushuru wa mazao kiasi cha Sh.62,291,702,831. Hata hivyo, hadi kufikia mwisho wa mwaka Juni 30, 2013, Mamlaka ya Serikali za

Mitaa hizo zilikusanya kiasi cha Sh.53,808,817,738 na kupelekea upungufu wa Sh.8,482,885,093 sawa na asilimia 14 ya kiasi kilichokasimiwa.

Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika na mapato yao yaliyokusanywa kutoka ushuru wa mazao ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xvi).**

Hazina haikutoa fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge, kitendo hiki kinaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha za ziada ukizingatia fedha hizi hazina bajeti.
Tunapendekeza kwamba vibali kutoka mamlaka husika vinapatikana na bajeti za ziada ziandaliwe kabla ya kufanyika kwa matumizi ya hizi.

SURA YA TANO

5.0 MASUALA MUHIMU YALIYOJIRI KATIKA UKAGUZI WA HESABU NA TATHMINI YA UDHIBITI WA NDANI

Utangulizi

Agizo la 11 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaitaka Menejimenti kuanzisha na kuuwezesha mfumo sahihi wa udhibiti wa ndani katika Halmashauri. Aidha Agizo Na.25(1) linazungumzia kuwa majukumu ya Menejimenti ya Halmashauri inatakiwa kuweka sawa hesabu za fedha, gharama, kumbukumbu za bohari na mifumo ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria zilizopo, kanuni na miongozo iliyotolewa na Waziri na Bodi ya Umoja wa Hesabu Kimataifa(IASB) zinazohusiana na Uhasibu wa Sekta za Umma.

5.1 Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na masuala ya utawala bora

Mfumo wa Udhibiti wa ndani unahusu namna zote ambazo rasilimali za Umma zinaelekezwa, zinasimamiwa na zinapimwa. Udhibiti wa ndani una jukumu muhimu katika kuzuia na kugundua ubadhirifu/matumizi mabaya na kulinda rasilimali za Umma, zinazoshikika na zisizoshikika. Utekelezaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani wenye ufanisi ni jukumu muhimu la Menejimenti ya Halmashauri.

Sehemu hii ya ripoti inaonesha matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na baadhi ya vipengele vya udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na; mifumo ya kihasibu, udhibiti wa mazingira ya utendaji kazi, tathmini za vihatarishi, udhibiti wa utendaji, teknolojia ya

habari na mawasiliano, ufuatiliaji wa udhibiti na kuzuia na kudhibiti udanganyifu.

Kwa ujumla inaeleweka wazi kuwa, wajibu wa kuanzisha mfumo wa udhibiti wa ndani ulio imara unabakia kuwa jukumu la Menejimenti ya Halmashauri husika. Hata hivyo, kwa sababu ya udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani katika Serikali za Mitaa, nimeainisha katika ripoti hii hoja za ukaguzi zinazotokana na udhaifu wa mifumo.

5.1.1 Mapungufu katika Mfumo wa Kiuhasibu-EPICOR toleo la 9.05

Katika mwaka huu wa Ukaguzi, shughuli za uhasibu katika Serikali za Mitaa zimeunganishwa kupitia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) kwa kutumia mfumo wa kiuhasibu wa EPICOR toleo la 9.05 chini ya usimamizi wa OWM-TAMISEMI. Kwa hali hii, kompyuta zimefungwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuingiza taarifa pamoja na kutoa idhini za malipo. Sehemu kubwa ya udhibiti wa ujumla wa mfumo ulikuwa unafanywa kupitia OWM-TAMISEMI ikiwa ni pamoja na udhibiti wa hifadhi za taarifa, udhibiti wa uingiaji katika mfumo, msaada wa kiufundi na mazingira ya usalama katika kihifadhi takwimu (server). Hivyo basi, Halmashauri walikuwa watumiaji wa mfumo tu.

Hata hivyo, mapitio ya mfumo katika Halmashauri 78 ilionesha kuwa kuna utendaji mdogo wa mfumo ambao unahitaji kuchukuliwa tahadhari kwa ajili ya kutoa taarifa za fedha za kuaminika kwa watumiaji.Yafuatayo hapa chini ni baadhi ya mapungufu yaliyoonekana:

- Uwezo wa chini wa Mtandao ambao ndiyo msingi wa shughuli zinazotakiwa kufanyika kila siku na hivyo kupelekea ucheleweshaji katika utoaji huduma na utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.
- Serikali za Mitaa hazikuweza kutumia moduli zote za mfumo ambapo ilipelekea kutumia nyaraka

mwongozo (manual documentation) kwa ajili ya baadhi ya udhibiti ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya wadaiwa, wadai, mali zisizo za kudumu na mali za kudumu. Kwa hali hii, taarifa za fedha haziwezi kuandaliwa kutoka kwenye mfumo.

- Halmashauri tano (5) hazikufungiwa mfumo wa Epicor toleo la 9.05 na kupelekea kutayarisha taarifa zake za fedha kwa kutumia utaratibu wa kawaida. Halmashauri hizo ni Halmashuri ya Mji wa Makambako, Halmashauri ya Wilaya ya Busokeli, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Mji wa Babati.

Mfumo wa uandishi wa hesabu kwa mkono huwa na makosa mengi ya kutoonyeshwa kwa baadhi ya tarakimu na kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kufanyika kwa mabadiliko ya hujuma kwa urahisi kama hakutakuwa na udhibiti wa kutosha na hivyo kupunguza kiwango cha taarifa kutoaminika Kutotumia mfumo pia kunaathiri umakini, upatikanaji wa taarifa kwa wakati na inasababisha utata wa utoaji taarifa za fedha katika ngazi zote.Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoonekana kuwa na mapungufu haya ni kama zilivyooneshwa katika **kiambatisho xvii.**

Kutokana masuala yaliyojitokeza hapo juu, ninasisitiza kwamba Halmashauri zote pamoja na OWM-TAMISEMI wanatakiwa kuwa makini kutumia kikamilifu mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha Epicor toleo la 9.05 kwa kutatua mapungufu yanayokabili mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha Epicor toleo la 9.05 kwa kudumisha miundo mbinu ya mawasiliano,kutoa mafunzo sahihi ya mfumo wa IFMS/Epicor kwa watumiaji na kuhakikisha kuwa moduli ambazo hazitumiki zinatumika.

5.1.2 Uandishi wa hesabu kwa mkono pamoja na kutumia mfumo wa Kompyuta EPICOR

Maelekezo yenye Kumb.Na.GB.174/389/01/34 ya kufunga akaunti zote za Halmashauri za zamani na kuanza kutumia akaunti mpya ambayo imetolewa na OWM-TAMISEMI ya tarehe 30/04/2012 inazitaka Halmashauri zote kuanza kutumia akaunti mpya kupitia mfumo wa Epicor ambao wataunganishwa pamoja. Aidha waraka Na.1 wa 1999/200 kutoka OWM-TAMISEMI ulihitaji mchakato wa shughuli zote za serikali ufanyike kwa kutumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS).

Hata hivyo, ilibainika kuwa Halmashauri ya Mji wa Kahama ilikuwa haitumii Mfumo wa Uhasibu wa Epicor badala yake ilikuwa inatumia mfumo unaoitwa "Quick use".

Uwepo wa Halmashauri zinazotumia mfumo wa Uhasibu tofauti na Mfumo wa Uhasibu wa Epicor ina maana kuwa ni vigumu kuzalisha taarifa za fedha ambazo zinalandana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma(IPSAS). Pia, ni vigumu kudhibiti matumizi dhidi ya bajeti kama inavyofanyika katika mfumo wa Uhasibu wa Epicor toleo la 9.05.

Kwa mtazamo huo hapo juu ninapendekeza kwamba, Halmashauri zote ziwekewe mfumo wa Epicor toleo la 9.05 ambao umeunganisha Halmashauri zote na kusimamiwa na OWM-TAMISEMI Dodoma ili kuwezesha mchakato wa shughuli za fedha pamoja kuzalisha ripoti ya fedha na ripoti nyingine kwa wakati.

5.1.3 Mapungufu katika utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ukaguzi wa ndani ni kichocheo cha kuboresha utawala, usimamizi wa vihatarishi na usimamizi wa udhibiti kwa

kutoa ufahamu na mapendekezo kulinganana uchambuzi na tathmini ya takwimu katika Halmashauri.

Pamoja na kujizatiti katika uadilifu na uwajibikaji, ukaguzi wa ndani huwa na manufaa kwa uongozi wa juu wa taasisi na viongozi waandamizi kama chanzo cha kutoa ushauri wa kujitegemea. Ukaguzi wa ndani husaidia taasisi kukamilisha malengo yake kwa kuleta utaratibu, mbinu nzuri ya kutathmini na kuboresha ufanisi wa mchakato wa usimamizi wa vihatarishi, kudhibiti na utawala bora.

Kifungu 45 (1) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa 2000) na Agizo la 13 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linamtaka Afisa Masuuli katika kila Halmashauri kuanzisha na kuendeleza kitengo imara cha ukaguzi wa ndani kama sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani.

Kinyume na mahitaji ya kisheria hapo juu, kutokana na tathmini za utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani, mapungufu yafuatayo yamebainika katika Halmashauri 102 kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xvii)**·

- Vitengo havina rasilimali za kutosha ikiwa ni pamoja na kutowezeshwa kifedha na rasilimali nyingine za vitendea kazi kama magari,kompyuta, mashine za kudurufu, “scanners” n.k.
- Vitengo bado vina upungufu wa watumishi, kwa Halmashauri 13 kwa kuwa na mtumishi mmoja au wawili. Kwa kuzingatia shughuli mbalimbali za Halmashauri, mkaguzi mmoja au wawili hawawezi kutosha kupitia maeneo yote yenye vihatarishi katika ukaguzi wao. Angalia jedwali 16 hapa chini.
- Wakaguzi wa ndani huwa hawatunzi mafaili ya nyaraka ambazo hutumika kurekodi ushahidi wote uliopatikana wakati wa ukaguzi. Nyaraka za ukaguzi

zinazoonesha taarifa ya maeneo yaliyokaguliwa na hutumika kusaidia kuonesha kazi ya ukaguzi iliyofanyika ili kutoa uhakika kwamba ukaguzi ulikuwa unafanyika kwa mujibu wa viwango husika vya ukaguzi.

Jedwali Na.16: Halmashauri zenye mkaguzi/wakaguzi mmoja au wawili

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Watumishi
1	H/W Bahi	1
2	H/W Ludewa	2
3	H/W Biharamulo	1
4	H/Mji Babati	2
5	H/W Serengeti	2
6	H/W Ileje	1
7	H/W Newala	1
8	H/W Geita	2
9	H/Mji Geita	2
10	H/W Namtumbo	2
11	H/W Iramba	2
12	H/W Singida	1
13	H/W Handeni	2

Kwa hali hii, wigo na mawanda ya Ukaguzi wa Ndani haukukidhi mahitaji kutokana na mapungufu yaliyotajwa hapo juu. Hivyo basi, udhibiti wa fedha na utendaji katika Mamlaka husika za Serikali za Mitaa haukufanyiwa tathmini kwa ufanisi.

Naendelea kusisitiza kwamba, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI na Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali chini ya Wizara ya Fedha zinashauriwa kuwa na umuhimu wa kuimarisha kazi za ukaguzi wa ndani kwa kuongeza rasilimali fedha na rasilimali watu. Aidha wakaguzi wa ndani

wanapaswa kupatiwa elimu na ujuzi ili waweze kuongeza wigo wa ukaguzi na kuboresha utendaji wao.

5.1.4 Mapungufu katika Kamati za Ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kamati ya Ukaguzi ni sehemu muhimu katika mfumo wa utawala iliyoundwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa Halmashauri. Kamati imara ya ukaguzi ina uwezo wa kuimarisha udhibiti wa mazingira na hivyo kusaidia Maafisa Masuuli kutimiza wajibu wao katika uongozi na majukumu ya udhibiti na pia kuwezesha ufanisi wa kazi za ukaguzi wa ndani na kuimarisha utoaji taarifa za fedha.

Kwa kuongezea, Kamati ya Ukaguzi wa hesabu inapaswa kutoa usimamizi unaojitegemea wa kazi na matokeo ya ukaguzi wa ndani na wa nje, kutathmini juu ya rasilimali zinazohitajika katika ukaguzi na kusuluhisha mahusiano kati ya wakaguzi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Katika kutathmini utendaji wa Kamati za Ukaguzi, ilibainika kuwa Halmashauri kama zilivyoonyeshwa kwenye **Kiambatisho (xvii**) hazikuwa na ufanisi kutokana na mapungufu yafuatayo:

- Hakukuwa na ushahidi kwamba, Kamati za Ukaguzi zilitoa usimamizi huru kwa mpango kazi wa ukaguzi wa ndani na matokeo, kufanya tathmini ya mahitaji ya rasilimali kwa ajili ya ukaguzi na upatanishi wa mahusiano ya wakaguzi na Serikali za Mitaa.
- Hakukuwa na nyaraka zinazoonesha kuwa Kamati za Ukaguzi zinahakikisha kwamba, matokeo ya ukaguzi yanafikishwa kwa menejimenti na maboresho yoyote yaliyopendekezwa au hatua za marekebisho zinatekelezwa.

- Hakuna ushahidi kwamba Kamati za Ukaguzi ziliweza kusimamia utendaji mzuri wa ukaguzi kwa kuhakikisha kuwa matokeo ya ukaguzi yanajadiliwa na maoni yaliyotolewa katika taarifa ya Mkaguzi wa Ndani yanafanyiwa kazi.
- Katika Halmashauri tatu ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Masasi na Urambo imebainika kuwa Kamati ya Ukaguzi imekutana mara moja tu katika mwaka mzima wa fedha. Kwa maana hiyo, Kamati ya ukaguzi imeshindwa kutimiza majukumu yake kisheria.

Utendaji usio wa ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi unaweza kusababisha udhaifu katika udhibiti wa mazingira ya utendaji kazi na utawala bora katika Halmashauri kwa ujumla. Ninapendekeza kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zifanye kazi kwa usahihi kwa kuhakikisha kunakuwepo muundo sahihi wa wajumbe, kuwepo hadidu za rejea sahihi, rasilimali na kuongeza ufanisi wa utendaji wa Kamati ya Ukaguzi. Kwa upande mwingine, Kamati inahitajika kujitathmini yenyewe kila mwaka ili kuweza kutambua fursa za kuboresha kwa kulinganisha utendaji wa Kamati dhidi ya muongozo wake wa Utendaji, miongozo yoyote iliyo rasmi na kanuni pamoja na njia bora za utendaji wa Kamati.

5.1.5 Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi

Tathmini ya vihatarishi ni utambuzi na uchambuzi wa vihatarishi husika kwa malengo ya kupata mafanikio na hivyo kutengeneza msingi wa jinsi ya kufanya usimamizi. Katika hili usimamizi wa vihatarishi ni sehemu ya asili ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa na mpango wa udhibiti wa kusimamia vihatarishi vya utendaji wa shughuli, kwani huwa inahusisha uelewa wa malengo ya taasisi, kutambua, kuchambua na kutathmini vihatarishi vinavyohusiana na kufikia hayo malengo na mara kwa mara kuendeleza na

kutekeleza mipango taratibu za kushughulikia vihatarishi vilivyotambuliwa.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinahitajika mara kwa mara kufuatilia na kuboresha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ili kujihakikishia kuwa, ni chombo imara kwa Halmashauri katika mchakato na utaratibu wa kutoa huduma kwa jamii.

- Licha ya mapendekezo yangu ya awali, ukaguzi uliofanyika katika sampuli ya Halmashauri 55 kama zinavyoonekana katika **Kiambatisho (xvii),** ilionesha kwamba, hakukuwa na kumbukumbu rasmi za Mfumo wa Usimamizi wa vihatarishi na haijafanyika tathmini ya hivi karibuni ya vihatarishi hivyo ili kutambua vihatarishi vilivyopo na vile vilivyoibuka ambavyo vingeweza kuathiri vibaya utoaji huduma.
- Hakuna kumbukumbu zinazoonesha mchakato wa tathmini ya vihatarishi ikiwa ni pamoja na kutunza rejesta ya vihatarishi ambayo hutumika kama sehemu kuu ya kutunzia taarifa za vihatarishi na pia kuruhusu taarifa zinazotoka kwenye mchakato wa usimamizi wa vihatarishi zimepangwa vizuri, kuweka kwenye viwango stahiki na kuhakikisha kuwa zimeunganishwa kwa ajili ya matumizi ya menejimenti.

Ukosefu wa nyaraka za Mfumo wa mipango imara wa usimamizi wa vihatarishi, Halmashauri husika hazitakuwa katika nafasi ya kukabiliana na vihatarishi ambavyo vinaweza kuleta madhara makubwa katika utendaji wa sasa na wa baadaye wa Halmashauri.

Napendekeza kwa Uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na OWM-TAMISEMI kubuni, kuanzisha utaratibu unaojitosheleza kutambua vihatarishi, kutathmini, kuchambua madhara ya vihatarishi, pamoja na udhibiti wa

utendaji katika ufuatiliaji na kukabiliana na vihatarishi husika kwa ajili ya utoaji ulio bora wa huduma kwa jamii.

5.1.6 Mazingira ya udhibiti wa Teknolojia ya Habari

Udhibiti wa Teknolojia ya Habari ni mifumo iliyoundwa kuhakikisha kuwa malengo ya taasisi husika yanafikiwa. Kimsingi, udhibiti wa Teknolojia ya Habari unahusiana na usiri, uaminifu, na upatikanaji wa takwimu pamoja na usimamizi wa jumla wa kazi za Teknolojia ya Habari ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Wakati wa kufanya tathmini katika mazingira ya udhibiti wa Teknolojia ya Habari, mapungufu yafuatayo yalibainika katika jumla ya Halmashauri 103 kama zinavyooneshwa katika **kiambatisho (xvii);**

- Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazina sera ya Teknolojia ya Habari, kitu ambacho kinaweza kuashiria udhaifu katika usimamizi na utumiaji wa vifaa vya teknolojia ya habari ikiwa ni pamoja na vifaa na programu za Teknolojia ya Habari.
- Kutokuwepo kwa mpango wa kujikinga na majanga na vipimo vya kujikinga na majanga havijawahi kufanyika. Kukosekana kwa mpango wa kujikinga na majanga kunasababisha ugumu katika kurejesha mfumo kwa wakati na kukosekana kwa vyanzo vya vipimo vya "data" kwa ajili ya kurejesha "data" husika na hakuna atakayehusika na urejeshwaji wa taarifa. Hii inasababisha hatari katika mpango endelevu wa Halmashauri husika.

Narudia mapendekezo yangu kuwa;

- OWM-TAMISEMI izisaidie Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuanzisha sera na taratibu za Teknolojia ya Habari ili kila mtumiaji aweze kuelewa majukumu na wajibu

wake katika kutunza vifaa na programu za Teknolojia ya Habari.

- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa ziwe na mpango wa kujikinga na majanga, hii ina maana ya kuandaa, kuandika, kujaribu na kutekeleza mpango wa kujikinga na majanga ambao unalenga mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) pamoja na mifumo mingine muhimu katika kila Halmashauri.

5.1.7 Kuzuia na kudhibiti udanganyifu

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 240 vinafafanua udanganyifu kama "kitendo cha makusudi kinachofanywa na mtu mmoja au zaidi ndani ya menejimenti, wale wanaohusika na utawala bora, wafanyakazi, au watu wa nje, wakishiriki kwa njia ya udanganyifu ili kupata faida kwa njia haramu au isiyo ya haki. Jukumu la msingi la kuzuia na kutambua udanganyifu ni la wale wanaohusika na utawala bora, watumishi wa Halmashauri na uongozi.

Tathmini zilizofanyika katika jumla ya Halmashauri 60 kama inavyoonekana katika **Kiambatanisho (xvii)** imebainisha kwamba**:**

- Uongozi wa Halmashauri husika haukuwa na kumbukumbu za kimaandishi zilizoidhinishwa za mipango ya kuzuia udanganyifu.
- Hakukuwa na mchakato uliowekwa na menejimenti za Halmashauri katika kubaini na kushughulikia vihatarishi vya ubadhirifu ndani ya Halmashauri.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina ushahidi wa kimaandishi na udhibiti mahsusi uliowekwa katika kukabiliana na vihatarishi ambao ulifanyika mara kwa mara katika mwaka husika.
- Kulikuwa na viashiria vya udanganyifu kama vile kukosekana kwa hati za malipo, matukio ya mapato kutopelekwa benki, hati za malipo kuwa na nyaraka

pungufu, kukosekana kwa stakabadhi za kukusanyia mapato na Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa ambazo zilibainisha kuwa kuna dalili za udanganyifu. Asili ya viashiria vya udanganyifu vilivyoainishwa hapo juu, vinaathiri udhibiti wa ndani na hivyo kuna hatari kubwa ya kuficha udanganyifu unaofanywa na menejimenti au watumishi katika ngazi tofauti.

Kwa kuwa wajibu wa kugundua na kuzuia udanganyifu ni wa menejimenti za Halmashauri husika, mianya iliyoainishwa inaweza kuwa ni chanzo cha udanganyifu na ni lazima izuiwe pamoja na kuandaa sera za kuzuia udanganyifu pamoja na mpango. Aidha, tahadhari inatolewa kwa uongozi wa Halmashauri ukishirikiana na OWM–TAMISEMI unatakiwa kubuni na kuweka kumbukumbu na kuidhinisha mipango ya kuzuia udanganyifu na kufanya tathimini za mara kwa mara za vihatarishi.

Udhibiti wa udanganyifu ni lazima uunganishwe na majukumu na mipango ya Halmashauri na ionekane kwamba ni jukumu la kila mtu katika Halmashauri. Mpango wa kudhibiti udanganyifu unapaswa kubainisha jukumu la pamoja la kubaini vihatarishi na kufanya kila liwezekanalo kuzuia na kugundua, kuepuka makosa yasitendeke na mafunzo ya ufahamu yatolewe kwa watumishi.

5.1.8 Utoaji wa huduma endelevu

Utoaji wa huduma endelevu unahusu utoaji wa huduma ambao unatosheleza mahitaji ya watu na kwa kiasi kikubwa unaboresha utendaji kijamii na kimazingira katika mzunguko wote wa maisha. Kimsingi, Mamlaka za Serikali za Mitaa ilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma kwa watu katika maeneo yao kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 113 na kifungu cha 60 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 na Serikali za Mitaa (Mamlaka za Mji), ya mwaka 1982 kwa mtiririko huo.

Wakati wa kupitia masuala yanayohusu utoaji wa huduma katika Serikali za Mitaa yafuatayo yalibainika: -

- Mamlaka ya Serikali za Mitaa zina kesi za kisheria zinazosubiri maamuzi ya mahakama zenye thamani ya jumla ya Sh.74,410,741,026 ambazo zinaweza kuathiri bajeti ya Halmashauri na utoaji wa huduma endapo hukumu ya kesi hizo itaonesha kuwa Halmashauri hizo zitakuwa zimeshindwa kama ilivyoonyeshwa kwenye **Kiambatisho (xviii).**
- Kuna mapungufu katika utoaji na kutotolewa kwa fedha ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa, hali inayopelekea kuwepo uhaba wa fedha katika kutekeleza shughuli zilizopangwa na hivyo kuathiri utoaji wa huduma. Aidha, Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazijakuwa na uwezo wa kukusanya mapato ya kutosha kutoka kwenye vyanzo vyake hata kwa ajili ya kuziwezesha kumudu gharama za matumizi ya kawaida. Rejea Aya 4.6.
- Kuwepo kwa madeni ya muda mrefu kunaharibu bajeti na muonekano wa Halmashauri kwa watoa huduma na watumishi ambao madai yao hayajalipwa kwa wakati. Hali hii ina athari kubwa kwa Halmashauri kwani wauzaji wa bidhaa na watoa huduma pamoja na watumishi hawatakuwa tayari kuendelea kutoa huduma kwa Halmashauri wasipohakikishiwa malipo yao kwa huduma walizotoa. Rejea Aya 5.7.7.

Ni muhimu kwa Halmashauri kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika utendaji wa shughuli za kila siku ili kupunguza uwezekano wa kutokea kesi za kisheria vinginevyo Halmashauri zinatakiwa kuimarisha vitengo vya sheria ili kupunguza hatari ya kupoteza kesi za kisheria. Aidha, Menejimenti za Halmashauri kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI na Hazina wanashauriwa kuongeza ufanisi

katika utoaji wa fedha zilizopo kwenye bajeti kwa ajili ya kukamilisha shughuli zilizopangwa.

5.1.9 Wakuu wa Idara Kutoweka kumbukumbu kwenye daftari la miadi na matumizi

Agizo la 9 (2)(e) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inawataka Wakuu wa Idara kutunza kumbukumbu sahihi za malipo,fedha na wadaiwa mbalimbali kwenye daftari la miadi na matumizi. Daftari la mihadi la matumizi ni daftari linalotumika katika kudhibiti matumizi ambapo hutoa taarifa za matumizi dhidi ya fedha zilizopokelewa na mihadi ili kuepuka kutumia zaidi.

Daftari la mihadi na matumizi ni muhimu kwa ajili ya kudhibiti matumizi hasa pale ambapo kuna mafungu mbalimbali ya fedha zilizoingizwa katika akaunti moja kama utaratibu ambao umeanzishwa mwaka huu wa fedha kwenye Halmashauri wa matumizi ya akaunti sita. Wakuu wa Idara kama watekelezaji wa shughuli za Halmashauri walipaswa kuwa na utaratibu madhubuti wa kudhibiti fedha zilizopo kwenye bajeti zao.

Katika ukaguzi uliyofanyika katika sampuli ya jumla ya Halmashauri 13 ilibainika kuwa Wakuu wa Idara hawatunzi kumbukumbu kwenye daftari la mihadi na matumizi kinyume na Agizo lililotajwa hapo juu. **Rejea Jedwali Na.17.**

Jedwali Na.17: Orodha ya Halmashauri ambazo hazijaweka kumbukumbu katika daftari la mihadi na matumizi

Na.	Halmashauri husika
1	H/W Chamwino
2	H/Mji Geita
3	H/W Hai

4	H/W Ileje
5	H/W Kilosa
6	H/W Longido
7	H/W Ludewa
8	H/W Mbarali
9	H/W Meatu
10	H/W Misungwi
11	H/Mji Mpanda
12	H/W Rungwe
13	H/M Shinyanga

Ninapendekeza kwa Halmashauri kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na OWM-TAMISEMI juu ya usimamizi wa akaunti sita kwa kuhakikisha udhibiti wa matumizi unaimarishwa na hii ni pamoja na matumizi bora ya daftari la mihadi na matumizi.

5.1.10 Masurufu yasiyorejeshwa Sh.283,837,962

Masurufu yanatafsiriwa kama ni kiasi cha fedha ambacho anapewa mtu kwa matumizi maalum. Agizo la 40 (2) na (3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaagiza kwamba Masurufu yanatakiwa yarejeshwe katika kipindi cha wiki mbili baada ya kukamilisha shughuli husika; vinginevyo masurufu yasiyorejeshwa yanatakiwa yakatwe kutoka katika mshahara wa mhusika katika kiwango kinachokubalika, Pia makato hayo yajumuishe na tozo kwa ajili ya kuchelewesha kurejesha masurufu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 (Iliyorekebishwa 2000). Vile vile Agizo la 40(4) na (5) linaeleza kuwa masurufu yalitolewe baada ya kufanya marejesho ya masurufu yaliyochukuliwa awali

Kinyume cha Sheria zilizotajwa hapo juu, kiasi cha masurufu yaliyofikia Sh.283,837,962 katika Halmashauri 23 hayakuwa

yamerejeshwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha na hakuna hatua iliyochukiliwa kulingana matakwa ya Sheria. Vile vile, masurufu yamelipiwa moja kwa moja katika vifungu vya matumizi na hayakuonyeshwa katika Mfumo wa Epicor ila yameonyeshwa katika Regista ya Masurufu iliyoandaliwa kwa mkono. Rejea Jedwali Na.18 hapa chini.

Jedwali Na.18: Orodha ya Halmashauri ambazo zina Masurufu yasiyorejeshwa

Na.	Halmashauri husika	Masurufu yasiyorejeshwa (Sh)
1	H/Jiji Arusha	964,300
2	H/W Arusha	14,289,670
3	H/Mji Geita	4,401,300
4	H/W Ileje	3,375,000
5	H/W Iramba	1,064,000
6	H/W Kahama	44,799,120
7	H/W Karatu	2,115,500
8	H/W Kibondo	41,175,862
9	H/W Kigoma	12,880,000
10	H/M Kigoma/Ujiji	4,450,000
11	H/W Longido	7,191,800
12	H/W Missenyi	9,915,700
13	H/W Misungwi	35,066,500
14	H/W Monduli	875,000
15	H/Mji Mpanda	7,083,470
16	H/Jiji Mwanza	52,963,000
17	H/W Njombe	2,850,000
18	H/Mji Njombe	5,310,000
19	H/W Rufiji/Utete	6,654,000
20	H/W Rungwe	4,100,000
21	H/W Songea	14,508,740
22	H/M Sumbawanga	3,014,000
23	H/W Ulanga	4,791,000
	Jumla	**283,837,962**

Inashauriwa kwamba utaratibu uliowekwa kwa ajili ya kutoa masurufu, kuweka kumbukumbu sahihi na kuhakikisha masurufu yanarejeshwa unatakiwa ufuatwe katika kudhibiti utoaji wa masurufu ili kupunguza kuwa na masurufu ya muda mrefu ambayo hayajarejeshwa.

5.2 Usimamizi wa Mapato

Usimamizi wa mapato ni mchakato ambao Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapanga, kuandaa bajeti, kutabiri, kutekeleza, kusimamia na kudhibiti makusanyo ya mapato na kutoa taarifa. Pia, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za jamii na kuinua kiwango cha mapato. Lengo la msingi la usimamizi wa mapato ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ili kutoa huduma inayotakiwa katika jamii sahihi kwa muda unaotakiwa na kwa kiasi kinachotakiwa.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/13, baadhi ya mapungufu yalibainika katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanayohusiana na usimamizi wa mapato kama ifuatavyo:

5.2.1 Vitabu 1,234 vya Makusanyo ya Mapato Kutowasilishwa kwa Ukaguzi

Agizo la 34 (6) na la 34 (7) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 limebainishwa kuwa, maafisa wote waliopewa vitabu vya makusanyo lazima wawasilishe taarifa ya vitabu vilivyotumika na vile ambavyo havijatumika kila mwisho wa mwezi na endapo kuna upotevu wowote wa vitabu, utolewe taarifa kwa Afisa Masuuli anayehusika mapema iwezekanavyo ambaye atatoa taarifa polisi. Kama upotevu umetokea nje ya makao makuu, afisa mhusika atoe taarifa polisi mapema iwezekanavyo na baadae Afisa Masuuli ajulishwe. Kinyume na maagizo haya, vitabu 1,234 vya makusanyo kutoka katika jumla ya Halmashauri 51 havikuwasilishwa kwa ukaguzi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xix).**

Kwa kuwa vitabu hivi vilikusudiwa kukusanya mapato ya Halmashauri, kiasi kilichokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo hakikuweza kujulikana. Hali hii inadhihirisha kuwa, kuna uwezekano mkubwa wa wizi wa mapato ya Halmashauri na kupotosha makisio ya mapato ya Halmashauri.

Hivyo inashauriwa kuwa, menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuweka mifumo imara ya udhibiti katika usimamizi wa vitabu vya makusanyo ili kuondoa uwezekano wa upotevu wa fedha za Halmashauri. Vilevile Halmashauri husika zinatakiwa kuwasilisha vitabu vilivyokosekana kwa ajili ya ukaguzi.

5.2.2 Maduhuli yaliyokusanywa na Mawakala lakini hayakuwasilishwa katika Halmashauri Sh.6,710,548,469

Katika mwaka wa fedha husika Halmashauri mbali mbali ziliingia mikataba na Mawakala wa kukusanya mapato kwa minajili ya kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri . Kinyume na Agizo la 37 (2) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 ambalo limeainisha kuwa, makusanyo yote ya Halmashauri yawasilishwe kwa watunza fedha wa Halmashauri husika kwa usalama. Hata hivyo, ilibainika wakati wa ukaguzi kuwa kiasi cha Sh.6,710,548,469 kilichokusanywa katika Halmashauri 58 hazikuwasilishwa kwa Watunza Fedha wa Halmashauri husika.

Inashauriwa kuwa, Menejimenti za Halmashauri ziimarishe udhibiti wa ndani katika makusanyo ya maduhuli yatokanayo na vyanzo vya ndani. Hii inajumuisha kuboresha taratibu za kuingia mikataba na kufuatilia marejesho kutoka kwa mawakala wa makusanyo.

Orodha ya Halmashauri kiasi kikichohusika ni kama zinavyooneshwa katika **Kiambatisho (xx).**

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ambayo hayakuwasilishwa na Mawakala katika Halmashauri kwa miaka mitano mfululizo unaonyeshwa pia katika Chati Mhimili kama ifuatavyo: -



Kutokana na jedwali hilo hapo juu, inaweza kubainika kuwa, kiasi cha makusanyo ya mapato ambayo hayakuwasilishwa katika Halmashauri na Mawakala kinaongezeka kutoka mwaka hadi mwaka. Hii ina maana kwamba kuna udhibiti dhaifu katika ukusanyaji wa mapato na kutokuwa makini katika kufuatilia utaratibu wa mikataba ya mapato. Ninapendekeza kwa Menejimenti za Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani wa ukusanyaji wa mapato

ikiwa ni pamoja na uimarishaji wa mifumo ya kuingia katika mikataba na mawakala wa kukusanya mapato na kufuatilia mapato ya fedha kutoka kwa mawakala hao.

5.2.3 Fedha zisizokusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani Sh.7,710,147,415

Kupanua wigo wa mapato ni moja ya mikakati ya kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani. Serikali za Mitaa zinatakiwa kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani ili kuongeza mapato kwa lengo la kuimarisha shughuli za Halmashauri kwa ufanisi zaidi na kupunguza utegemezi wa Serikali Kuu. Katika mwaka wa fedha 2012/13, Halmashauri zipatazo 54 hazikuweza kukusanya mapato kiasi cha Sh.7,710,147,415 kutoka kwa walipa kodi husika kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho (xxi).**

Hii inaashiria kwamba kuna udhaifu wa Halmashauri katika kusimamia ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani na pia inaonesha ni kwa jinsi gani zilivyoshindwa kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo ili kuziwezesha kupunguza utegemezi wa Serikali Kuu katika matumizi ya kawaida na yale ya miradi ya maendeleo.

Inashauriwa kwamba Serikali za Mitaa ziongeze juhudi zaidi na kuweka mikakati endelevu ili kuhakikisha kwamba mapato kutoka vyanzo vyote vya mapato yanakusanywa kwa ufanisi zaidi.

5.2.4 Kukosekana kwa sheria ndogo ndogo kwa baadhi ya vyanzo vya mapato

Ili kuongeza vyanzo vya makusanyo ya mapato, Halmashauri zinatakiwa kuchunguza vyanzo maalum vya mapato katika maeneo yao ya kijiografia na kutunga sheria ndogo ndogo kwa ajili ya makusanyo ya mapato hayo. Kuanzishwa kwa

mapato na sheria inatoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ndani ya mamlaka yao kisheria. Katika mwaka huu wa fedha, imebainika kwamba Halmashauri 18 hazikuweza kuanzisha vyanzo vya mapato na sheria ndogo zinazohusu vyanzo vyote walivyo na uwezo wa kukusanya mapato. Kwa mfano Halmashauri 18 hawakuwa na mapato na sheria juu ya minara ya mawasiliano, ushuru wa huduma na ada za mabango ya matangazo.

Kutokuwepo juhudi za kutosha za utekelezaji wa sheria ndogo za mapato kama chombo cha kuongeza makusanyo ya mapato ya Halmashauri kunamaanisha kwamba Halmashauri hazitumii kikamilifu vyanzo vyote vya mapato vilivyopo ndani ya mamlaka zao na hivyo kutofikia lengo la msingi la kutekeleza majukumu yake kwa kutumia mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani.

Ninapendekeza kwamba Serikali za Mitaa kufanya utafiti wa vyanzo vyote vya mapato na kutunga sheria juu ya vyanzo vyote vya mapato yaliyoko chini ya mamlaka zao kwa kuhakikisha kwamba kuna nguvu ya kisheria kwa ajili ya ukusanyaji na kuwabana wanaokiuka. Pia Serikali za Mitaa zinapaswa kuanzisha mikakati endelevu na kuongeza wigo wa kodi na hatimaye kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Jedwali Na. 19: Orodha ya Halmashuri ambazo hazijaanzisha sheria ndogo ndogo kwa baadhi ya vyanzo vya mapato

Na.	Halmashauri husika	Vyanzo vya mapato
1	H/W Bagamoyo	Ushuru wa huduma
2	H/W Bunda	Ada ya Hoteli za kitalii na sehemu za kuweka kambi
3	H/W Karatu	Ada ya Minara ya Mawasiliano
4	H/W Kilindi	Ushuru wa hudumma na Mrahaba
5	H/W Kilosa	Ada ya Mabango na Minara ya Mawasiliano

6	H/W Kongwa	Ada ya Minara ya Mawasiliano
7	H/W Longido	Ada ya Minara ya Mawasiliano
8	H/W Ludewa	Ushuru wa huduma
9	H/W Mafia	Ada ya Minara ya Mawasiliano
10	H/W Makete	Ushuru wa huduma
11	H/W Morogoro	Ada ya Minara ya Mawasiliano
12	H/W Mpanda	Ada ya Minara ya Mawasiliano
13	H/W Musoma	Ushuru wa huduma
14	H/W Nkasi	Ada ya Minara ya Mawasiliano
15	H/W Rufiji	Ada ya Minara ya Mawasiliano
16	H/W Rungwe	Ada ya Minara ya Mawasiliano
17	H/W Ulanga	Ushuru wa hoteli na nyumba za kulala wageni
18	H/Mji Mpanda	Kodi ya Vibanda Sokoni

5.2.5 Kutofanyika upembuzi yakinifu wa vyanzo vya mapato

Upembuzi yakinifu juu ya usimamizi wa mapato unahusisha tathmini na uchambuzi wa fursa za mapato zinazopatikana ndani ya mamlaka za Halmashauri. Kimsingi, huu ni uchunguzi wa kina na utafiti wa kufanikisha mchakato wa kufanya maamuzi. Madhumuni ya tathmini ni kutambua na kuamua faida chanya za kiuchumi kwenye fursa ili kuweza kupata chanzo kikuu cha mapato.

Katika kipindi cha mwaka 2012/13 imebainika kuwa Serikali za Mitaa hazijafanya utafiti juu ya uwezo na fursa mbalimbali za mapato katika maeneo yao ya mamlaka, hivyo kusababisha Halmashauri kushindwa kukusanya kiwango cha mapato yaliyopangwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Halmashauri iliingia mkataba na wakala kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato katika kituo cha mabasi na maegesho ya magari mjini Bukoba kwa kipindi cha miezi minane kwa kukusanya kiasi cha Sh.9,600,000 na 2,750,000 kwa mtiririko huo. Hata hivyo, ukaguzi wa vitabu vya stakabadhi vilivotumiwa na wakala umebaini kuwa wakala alikusanya jumla ya

Sh.224,425,000 kutoka katika vitabu vyote vilivyotolewa kwake kwa muda wote wa mkataba lakini aliwasilisha Sh.98,800,000 (44%) kwa mujibu wa mkataba hivyo kusababisha kiasi cha Sh.125,625,000 kubakia katika mikono ya wakala. Hii ina maana kwamba hakuna utafiti wa kina uliofanyika kabla ya maamuzi ya kuingia mkataba na wakala.

Aidha, hii ina maana kwamba Halmashauri hazina utamaduni wa kufanya mapitio mara kwa mara kuhusu uwezo wa mapato na mikakati ya kupata vyanzo zaidi vya mapato. Pia, Halmashauri kukosa kipaumbele kwa ajili ya kutumia fursa zilizopo juu ya vyanzo vya mapato hivyo kushindwa kupanga makadirio kwa usahihi ya kiasi cha mapato yatakayokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali.

Ninapendekeza kwamba Halmashauri zinapaswa kufanya mara kwa mara upembuzi yakinifu juu ya vyanzo vya mapato na fursa mbali mbali ili kubaini vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuweka mipango sahihi ili kuongeza makusanyo ya mapato na kuongeza mafanikio ya kufikia malengo yao.

5.2.6 Usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyokasimiwa

Maboresho ya makusanyo katika Serikali za Mitaa yamepelekea halmashauri kukasimu sehemu kubwa ya makusanyo ya mapato ya vyanzo vya ndani. Mikataba iliyoingiwa na Mawakala wa kukusanya mapato ilitakiwa iwe na usimamizi wa karibu ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zinanufaika kulingana na makubaliano yaliyoingiwa katika mkataba. Hata hivyo Halmashauri zinapitia matatizo mbalimbali katika usimamizi wa baadhi ya makusanyo yaliyokasimiwa. Matatizo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:

- Halmashauri hazikufanya utafiti au upembuzi yakinifu kuhusu ubora wa vyanzo vya mapato wala kufanya

utafiti wa awali kwa lengo la kuweka kizingiti cha kiasi cha kukusanywa kabla ya kuingia mkataba wa kukasimisha.

- Mikataba ya kukusanya mapato inayokasimiwa na Halmashauri ina rasimu duni, mikataba kukosa vifungu muhimu kama kiasi cha riba au adhabu kwa kuchelewesha makusanyo ya mapato, taarifa za fedha na za kiutendaji na wakati mwingine Mawakala wa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri bila ya kuwa na mikataba ya kisheria na Halmashauri.
- Mawakala wa kukusanya mapato hawawasilishi kiasi cha mapato kwa mujibu wa mikataba yao na mara nyingi hulipa pungufu ya mapato, na wakati mwingine kushindwa kulipa kiasi walichokubaliana kwa wakati. Hata hivyo, Halmashauri pia hazitozi adhabu ya kuchelewesha kuwasilisha makusanyo ya mapato kama ilivyokubaliwa katika mikataba.
- Halmashauri hazitathmini kuona kama utendaji wa mawakala umefanyika kwa ufanisi na wametekeleza majukumu yao ipasavyo bali huaangalia idadi ya vitabu vya makusanyo vilivyowasilishwa na mawakala kama kipimo cha ufanisi.
- Halmashauri hazina utaratibu wa ukaguzi wa mapato yaliyokasimiwa ili kutambua udhaifu na matatizo yanayowakabili mawakala ili kutafuta ufumbuzi. Pia hakuna taarifa za usuluhishi mara kwa mara kati ya vitabu vya mapato vya Mawakala wa mapato dhidi ya kiasi cha mapato kilichowasilishwa kwenye Halmashauri husika.

Hii ina maana kwamba Halmashauri hazijaweka udhibiti wa kutosha, ufuatiliaji na mikakati ya kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa mapato yaliyokasimiwa kwa mawakala unafanyika kwa ufanisi ili kuongeza makusanyo ya

Halmashauri. Kwa kufanya utafiti madhubuti wa vyanzo vya mapato, Halmashauri inaweza kuwa na uwezo wa kuunda msingi wa kuamua kiasi sahihi ambacho mawakala wanapaswa kuwasilisha kwa Halmashauri ili kuepuka kupoteza mapato na kupata faida ya ziada kwa Wakala isiyostahili. Ufuatiliaji utaziwezesha Halmashauri kufuatilia na kutambua udhaifu na matatizo yanayohusiana na ukusanyaji wa mapato ya mawakala kwa ajili ya hatua za marekebisho.

Nazishauri menejimenti za Halmashauri kufanya upembuzi yakinifu wa vyanzo vya mapato kabla ya kuingia mikataba na mawakala.Pia, Halmashauri waimarishe usimamizi wa mikataba ya ukusanyaji mapato yaliyokasimiwa kwa mawakala ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyopangwa yanafikiwa. Zaidi ya hayo Halmashauri ziwe na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ikiwemo kufanya tathmini ya utendaji wa Mawakala na ukaguzi wa mara kwa mara kupitia taarifa za fedha na zile za utendaji.

5.2.7 Maduhuli yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa Benki wala katika Halmashuri husika Sh.585,502,820

Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 inahitaji fedha zote ambazo zimekuwa zikipokelewa katika Serikali za Mitaa kulipwa katika akaunti za benki za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kila siku au siku ya kazi inayofuata. Pia Agizo la 37 (2) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2009 linahitaji fedha zote ambazo zimekuwa zikikusanywa na Maafisa wateule katika Serikali za Mitaa kuwa zinawasilishwa kwa Mtunza Fedha kwa ajili ya usalama kabla ya muda wa kazi kuisha kila siku au siku ya kazi inayofuata. Katika mwaka 2012/2013, ilibainika kuwa makusanyo kutoka vyanzo vya mapato ya kiasi cha Sh.585,502,820 kutokana na ushuru mbalimbali wa mapato hayakudhibitishwa kupelekwa benki wala katika

Halmashauri husika ikiwa ni kinyume na matakwa ya Sheria kama ilivyoainishwa katika **Kiambatanisho(xxii)**

Kwa kushindwa kuwasilisha mapato yaliyotokana na maduhuli pamoja na kupelekwa benki kunaongeza hatari ya wizi na mapato yanaweza kutumika bila Halmshauri husika kujua. Kwa kutowasilisha makusanyo ya mapato benki , uhalali na usahihi wa makusanyo ya ndani yaliyopatikana haukuweza kuthibitika.

Napendekeza kwamba Uongozi wa Halmashauri zihakikishe kwamba,makusanyo ya maduhuli yanawasilishwa na hukabidhiwa katika Halmashauri nakupelekwa benki mara moja baada ya kuwa yamekusanywa .

5.3 Usimamizi wa Fedha

Usimamizi wa fedha unahusu mchakato wa kukusanya, utunzaji na kugawa fedha za umma kwa lengo la msingi na kuhakikisha kuwa fedha zinatosha kukidhi mahitaji ya kila siku ya Halmashauri. Usimamizi wa fedha ni muhimu kwa vile fedha zinaweza kuwa kwenye hatari zaidi kama tahadhari hazitachukuliwa. Kuendeleza udhibiti imara wa ndani juu ya fedha kunaweza kukuza usahihi, kuzuia wizi, na kuhakikisha Halmashauri zina fedha za kutosha kulipa madeni yao. Hii ni pamoja na kuendeleza udhibiti wa ndani wa stakabadhi za fedha na utoaji wa fedha, kuanzisha taratibu za kuboresha makusanyo ya mapato yaliyolengwa, na kuanzisha utaratibu mzuri wa mawasiliano kati ya Mweka Hazina na Wakuu wa Idara ili kuhakikisha kwamba fedha zilizopo hazitumiki vibaya.
Ukaguzi wa usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa, umebainisha masuala mbalimbali kama yalivyoainishwa hapa chini:

5.3.1 Bakaa katika taarifa ya usuluhisho wa Benki

Agizo 29 (2) la Memoranda ya Serikali za Mitaa, 2009 linahitaji la Mweka Hazina kuhakikisha kwamba, usuluhisho unafanyika, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa akaunti mbali mbali sanjari na kufanya usuluhishi kati ya daftari la fedha na taarifa za benki kila mwezi na kufanya masahihisho ipasavyo. Kinyume na Agizo hili, Halmashauri 43 zimeonesha taarifa ambazo zina bakaa ya masuala ambayo hayajafanyiwa usuluhisho wa kibenki.

Aidha, hakuna ushahidi uliotolewa kwa timu za ukaguzi kama taarifa za usuluhisho wa benki zimepitiwa na maofisa waandamizi wa Halmashauri. Muhtasari wa masuala ambayo hayajasuluhishwa katika taarifa za benki kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2013 ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho (**xxiii).**

- Jumla ya makusanyo ya Sh.5,864,183,413 kutoka Halmashauri mbalimbali yalionyeshwa katika vitabu vya Halmashauri lakini kiasi hicho cha fedha hakikuonekana katika taarifa za benki.
- Kiasi cha Sh.16,842,008,917 kililipwa kwa watu mbali mbali kwa kutumia hundi lakini hazikuweza kuwasilishwa benki kwa ajili ya malipo hadi wakati wa ukaguzi.
- Hundi ambazo zimechacha zenye thamani ya Sh.107,345,185 hazikufutwa katika vitabu vya fedha husika ili kuhakikisha usahihi wa bakaa ya fedha katika taarifa ya mwisho wa mwaka.

Jedwali Na.20 hapa chini linaonesha ulinganifu wa masuala ambayo hayakusuluishwa katika taarifa ya benki kwa miaka mitano (5) kutoka mwaka 2007/08 hadi 2012/13.

Jedwali Na.20: Ulinganifu wa masuala ambayo hayakusuluishwa

Mwaka wa fedha	Mapato kwenye daftari la fedha lakini hayapo kwenye taarifa za Benki (Sh.)	Hundi ambazo hazijawasilishwa Benki (Sh.)
2012/13	5,864,183,413	16,842,008,917
2011/12	3,872,146,712	18,368,780,081
2010/11	5,088,963,792	10,897,078,986
2009/10	10,418,079,556	28,792,732,991
2008/09	3,511,801,077	10,895,917,505

Kutokana na Jedwali hilo hapo juu, inaonesha kuwa mapato yameingizwa katika daftari la fedha lakini hayakuonyeshwa katika taarifa za benki yameongezeka kwa Sh.1,992,036,701 kutoka mwaka wa fedha 2011/12 hadi mwaka wa fedha 2012/13 sawa na 34%.

Hundi ambazo zililipwa kwa walipwaji mbali mbali na hazikuwasilishwa benki zimeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa Sh.7,471,701,095 kutoka mwaka wa fedha 2010/11 hadi mwaka wa fedha 2011/12 na kuweza kupungua kwa Sh.1,526,771,164 sawa na 9% kwa mwaka 2012/2013.

Makosa na matumizi mabaya ya fedha za umma kutokana na masuala ambayo hayajafanyiwa usuluhisho wa kibenki yanaweza yakachukua muda mrefu bila kubainishwa na Uongozi wa Halmashauri na kuweza kusababisha hasara ambayo ingeweza kuepukwa na kwa Halmashauri na vinginevyo inaweza kuwa chanzo cha udanganyifu.

Inapendekezwa kwamba, Menejimenti za Halmashauri zihakikishe kwamba, taarifa za usuluhisho wa kibenki zinatayarishwa kila mwezi na kupitishwa na maofisa waandamizi wa Halmashauri. Pia marekebisho yote muhimu

ikiwa ni pamoja na kufuta hundi zilizochacha yanatakiwa kufanyika katika daftari za fedha ili kuonesha bakaa ya fedha ambayo ni sahihi mwishoni mwa mwaka.

5.3.2 Ukaguzi wa kushtukiza wa fedha taslimu

(i) Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka akaunti ya zamani kwenda akaunti mpya Sh.498,497,315

Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ilitoa maelekezo kwa barua yenye kumbukumbu GB.174/389/01/34 ya 30/04/2012, kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote zilitakiwa kufunga akaunti za benki za zamani ifikapo tarehe 1 Julai 2012 na kufungua akaunti mpya sita za benki. Maelekezo yalizitaka Halmashauri zote kufanya usuluisho wa masuala yote katika benki na baadaye bakaa ya fedha zihamishiwe kwenye Akaunti mpya isipokuwa fedha zinazohusisha hundi ambazo hazijalipwa hadi tarehe na 30 Juni, 2012. Baada ya uhamisho wa fedha kwenye akaunti mpya menejimenti za Halmashauri zilitakiwa kutayarisha taarifa na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na hatimaye taarifa hizo ziweze kuwasilishwa kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali -Hazina Dar-es Salaam kwa ajili ya uhakiki. Ilikatazwa kabisa kufanya malipo yoyote mapya kutoka akaunti ya zamani katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Hata hivyo wakati wa kupitia miamala ya kibenki katika Halmashauri mbali mbali imebainika kwamba Halmashauri 12 hazikuwa zimehamisha fedha jumla ya Sh.498,497,315 kutoka akaunti za zamani kwenda akaunti mpya na kwa kuzingatia uwajibikaji, Halmashauri ziliendelea kutumia akaunti za zamani katika kufanya malipo ikiwa ni kinyume na maelekezo ya OWM-TAMISEMI. Halmashauri ambazo zimehusika ni kama zinavyoonekana katika jedwali Na.21 hapa chini:

Jedwali Na.21-Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya zamani kwenda Akaunti mpya

Na.	Halmashauri husika	Kiasi (Sh.)
1	H/W Kasulu	171,621,807.00
2	H/W Hanang	85,933,986.00
3	H/M Bukoba	75,684,729.00
4	H/W Chamwino	54,066,233.00
5	H/W Kasulu	31,725,700.00
6	H/W Sengerema	29,070,667.00
7	H/W Iramba	14,810,205.00
8	H/W Sumbawanga	11,336,560.00
9	H/W Mbinga	10,652,547.00
10	H/W Kibondo	9,675,301.00
11	H/W Mpanda	2,897,732.55
12	H/Jiji Tanga	1,021,847.52
Jumla		**498,497,315**

Kuchelewa katika kufunga akaunti za benki ambazo hazitumiki tena inaweza kupelekea ushawishi wa kugushi taarifa za akaunti na ongezeko la gharama za kibenki ambazo zingeweza kuepukika. Pia kuna uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali na kwa kutoa taarifa ambazo siyo sahihi za salio la fedha benki katika taarifa za fedha.

Ninapendekeza kwamba, Halmashauri zifanye uchunguzi na kufanya usuluisho wa benki na menejimenti za benki kwa ajili ya kuhakikisha kwamba fedha ambazo bado zipo katika akaunti ya zamani zinahamishiwa kwenye akaunti mpya ili kukamilisha shughuli zilizopangwa.

(ii) Ukaguzi wa kushitukiza wa fedha taslim haukufanyika katika Halmashauri

Agizo la 46 (1) la Memoranda ya Serikali za Mitaa, 2009 linahitaji Afisa Masuuli au mwakilishi wake katika vipindi maalum kupanga utaribu wa kufanya ukaguzi wa mshitukizo kwa ajili fedha taslim. Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa katika Halmashauri zilizochaguliwa umebaini kwamba Halmashauri 31 hazikuwa na utaribu wa kufanya ukaguzi wa mshitukizo kwa fedha taslim na Afisa Masuuli au Mwakilishi wake. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuwa zimefanya ukaguzi wa mshitukizo wa fedha taslim ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xxiv).**

Hii ina maana kwamba Halmashauri hazikuweka udhibiti na utaratibu wa usimamizi wa fedha. Kwa kutokufanya ukaguzi wa mshitukizo wa fedha taslim, fedha zinaweza kutumiwa vibaya au kupotea bila Uongozi wa Halmashauri kuwa na taarifa.

Ninapendekeza kwamba Uongozi wa Halmashauri uanzishe utaratibu madhubuti wa usimamizi wa fedha ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mshitukizo wa fedha taslim mara kwa mara ili kuimarisha uwajibikaji wa usimamizi wa fedha.

(iii) Kiasi cha fedha taslim ambacho kinatakiwa kuwepo katika Halmashauri

Agizo la 99 (1) la Memoranda ya Serikali za Mitaa, 2009 linaelekeza kwamba, Kiwango cha juu cha fedha taslimu ambacho kinatakiwa kiwepo katika ofisi kikubalike na Halmashuri husika na kisizidi bila kibali". Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika wa fedha taslimu katika Halmashauri mbalimbali ulibaini kuwa, Halmashauri 24 hazikuwa zimeweka viwango vya juu vya fedha taslimu ambavyo

vimeidhinishwa na Kamati ya Fedha kama sheria inavyotaka. Halmashauri husika ni kama zinavyoonekana katika **Kiambatisho (xxiv).**

Kuweka fedha katika Ofisi za Halmashauri bila ya kuwa na kiwango cha juu cha kikomo kilichoaidhinishwa inaongeza hatari ya upotevu wa fedha kwa njia ya wizi na matumizi yasiyotarajiwa hivyo Halmashauri inaweza kuwa na kiasi kikubwa cha fedha bila sababu yoyote ya kuridhisha.

Ninapendekeza kwamba Halmashauri zianzishe utaratibu wa kuweka kiwango cha juu cha fedha ambazo Halmashauri inapaswa kuwa nazo katika majengo kwa ajili ya udhibiti.

5.4 Usimamizi wa Rasilimali watu

Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni moja ya shughuli inayolenga kuajiri, kusimamia na kutoa maelekezo kwa watu wanaofanya kazi katika Halmashauri inayohusika na masuala ya watumishi kama vile fidia, upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi (OPRAS), motisha na maendeleo ya watumishi ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

Wakati wa ukaguzi wa 2012/2013, tathmini zilifanyika ili kujua ufanisi katika usimamizi wa rasilimaliwatu na mishahara kwa mwaka ulioisha 30 Juni, 2013 katika serikali za mitaa. Mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:

5.4.1 Mapungufu katika upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi (OPRAS)

Kwa kutumia sampuli ya Halmashauri 16 ilibainika kwamba, Halmashauri hazifanyi upimaji wa utendaji kazi wa kutosha kwa watumishi wake kinyume na kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma Aya D(62-63) ya mwaka 2009. Hivyo, upimaji wa utendaji kazi umekuwa ukifanyika kwa watumishi husika ukifika wakati wa kupandishwa vyeo.

Kutokuwepo au upungufu katika upimaji wa utendaji kazi kunapelekea ugumu katika ufuatiliaji wa utekelezaji. Aidha, watumishi hawapati mafunzo ya kutosha katika ujazaji wa fomu za upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi (OPRAS). Hivyo inakuwa vigumu kujua utendaji kazi wa watumishi kama fomu zinajazwa kwa lengo la kupandishwa vyeo tu.

Orodha ya Halmashauri zenye mapungufu katika upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi (OPRAS) ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na.22: Orodha ya Halmashauri zenye mapungufu katika upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi (OPRAS).

Na.	Halmashauri husika
1	H/W Chamwino
2	H/W Geita
3	H/W Hanang’
4	H/W Igunga
5	H/W Ileje
6	H/M Ilemela
7	H/W Kondoa
8	H/Mji Korogwe
9	H/W Mbeya
10	H/W Mbinga

11	H/W Mbozi
12	H/M Mtwara
13	H/W Nzega
14	H/W Siha
15	H/W Sikonge
16	H/M Sumbawanga

Ninapendekeza kuwa Menejimenti za Halmashauri husika zihakikishe kwamba watumishi wanapata mafunzo juu ya utekelezaji wenye tija wa tathmini ya utendaji. Aidha, ufuatiliaji na utaratibu wa tathmini ni lazima uwepo ili kuwa na uwezekano wa kutambua, kutathmini na kuainisha maeneo muhimu na mapungufu katika upimaji wa utendaji wa kazi wa watumishi ili kuwezesha hatua kuchukuliwa kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

5.4.2 Kutokuwepo na kutoboresha Rejesta za Watumishi

Agizo la 79(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linamtaka Mkuu wa Idara ya Rasilimaliwatu kutunza na kuboresha rejesta yenye orodha na kumbukumbu za watumishi wote. Pia, Agizo la 79(5) la Memoranda hiyo hiyo, linaagiza kuwa kumbukumbu za mishahara isiyolipwa zitunzwe na kuingizwa kwenye rejesta ya mishahara isiyolipwa. Kumbukumbu hizo zinatakiwa ziwe na mambo yafuatayo:

(a) Kumbukumbu za ajira, kujiuzulu, kuachishwa kazi, kusimamishwa kazi, kuazimwa kwenda sehemu nyingine kikazi na uhamisho.
(b) Mbadiliko ya mshahara mbali na ongezeko la kawaida la mshahara la kila mwaka na malipo mengine ambayo hayapo katika mkataba ulioingiwa kati ya mwajiri na mwajiriwa.

(c) Kutokuwepo kwenye kituo cha kazi kwa sababu ya kuumwa au sababu nyingine mbali na likizo iliyoidhinishwa.

(d) Taarifa muhimu zinazohitajika kutunza kumbukumbu za huduma kwa ajili ya kodi ya mapato na michango mbalimbali katika mifuko ya hifadhi za jamii.

Katika kupitia rejista za watumishi katika Halmashauri 11 ilibainika kuwa Halmashauri hizo hazifuati maagizo yaliyopo kwenye Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 kama ifuatavyo:

- Rejesta za mishahara isiyolipwa hazitunzwi vizuri na mara nyingi taarifa za namba za mishahara na sababu za kutokulipwa mishahara havionyeshwi katika rejesta hizo.
- Kitengo cha mishahara hakirekebishi taarifa za watumishi, hali inayopelekea malipo ya mishahara kufanyika kwa watumishi ambao wamemaliza muda wao wa kazi kutokana na kustaafu, kuachishwa kazi, kutoroka na kifo.

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kurekebisha taarifa za Watumishi wake mara kwa mara ili kuepuka uwezekano wa kulipa watumishi hewa.

Jedwali Na.23: Idadi ya Halmashauri ambazo hazitunzi/kuboresha rejesta za watumishi

Na.	Jina la Halmashauri	Kutokuwepo/kuboresha rejesta za watumishi
1	H/W Bariadi	√
2	H/M Dodoma	√
3	H/W Ileje	√
4	H/W Iramba	√
5	H/W Karatu	√
6	H/M Kigoma/Ujiji	√
7	H/Jiji Mbeya	√
8	H/W Mbozi	√
9	H/W Mkinga	√
10	H/M Shinyanga	Regista haipo kabisa
11	H/W Tabora	√

Vile vile, Idara za Rasilimaliwatu zinatakiwa kuanzisha na kuboresha rejesta za watumishi ili kuweza kusimamia masuala yote yanayohusu watumishi ikiwemo mishahara na stahili zao nyingine. Aidha, kunatakiwa kuwepo uboreshwaji wa rejesta za mishahara isiyolipwa.

5.4.3 Mishahara isiyolipwa ambayo haikurejeshwa Hazina Sh.708,377,328 na ucheleweshwaji wa kurejesha Sh.971,162,783

Agizo la 79(5) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linaagiza kwamba, mishahara isiyolipwa inatakiwa ipelekwe benki ndani ya siku kumi (10) za kazi. Pia maelekezo kutoka Wizara ya Fedha ambayo yalitolewa kwa barua yenye Kumb. Na.EB/AG/5/03/01/Vol.VI/136 ya tarehe 31 Agosti, 2007 ambayo inaelekeza kwamba mishahara yote isiyolipwa inatakiwa kurejeshwa Hazina kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

Kinyume na matakwa hayo, ukaguzi wa mishahara umebaini kwamba, kuna mishahara isiyolipwa ya kiasi cha Sh.708,377,338 katika Halmashauri 16 ambayo haikurejeshwa Hazina.Hali hii inaweza ikawa imesababishwa na ukosefu wa uwajibikaji katika mishahara isiyolipwa ambayo inaweza kusababisha hasara ya fedha za serikali.

Pia,Halmashauri 18 zilirejesha fedha Hazina kiasi cha Sh.971,162,783 ikiwa ni mishahara isiyolipwa kwa watumishi waliofariki, waliostaafu na walioachishwa kazi baada ya muda wa wiki mbili kupita ikiwa ni kinyume na Agizo la 79(6) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009. Halmashauri 34 zilizohusika zinaonyeshwa katika **kiambatisho(xxv).**

Ninapendekeza kwa Halmashauri husika kufuata matakwa kwa kurejesha mishahara isiyolipwa kwa wakati Wizara ya Fedha na kufuatilia stakabadhi za kikiri mapokezi kwa marejesho yaliyofanyika.

5.4.4 Mishahara Iliyolipwa kwa watumishi waliotoroka, waliostaafu na walioachishwa kazi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha Sh.832,448,998 za mishahara katika Halmashauri zililipwa kwa watumishi waliotoroka,waliofariki,waliostaafu na walioachishwa kazi.Hili ni ongezeko la Sh.139,316,226 (20%) ukilinganisha na Sh.693,132,772 kwa Halmashauri 43 zilizooneshwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Rejea **Kiambatisho(xxvi**)

Aidha, jumla ya Sh.482,405,746 ikiwa ni makato kutoka katika mishahara ya Watumishi hao zililipwa kwa taasisi mbalimbali kama vile Mifuko ya Hifadhi za jamii,Taasisi za fedha, Bima ya Afya (NHIF) na Mamlaka ya Mapato (TRA). Kufanyika kwa malipo kwa watumishi ambao hawapo katika

utumishi kunasababisha hasara ya fedha za umma hali ambayo inaitaka Menejimenti kuchukua hatua za haraka kukabiliana nayo.

Chati iliyopo hapa chini inalinganisha mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao hawapo katika utumishi kwa miaka minne mfululizo.

Mlinganisho wa mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliotoroka, waliostaafu na waliofariki kwa miaka minne kuanzia 2009/2010 na 2012/2013



Kutokana na chati hapo juu inaweza inadhihirika kwamba, malipo ya mishahara kwa watumishi hewa yanaonekana kuwa na udhibiti hafifu wa mfumo wa ndani hali inayoweza kupelekea upotevu mkubwa wa fedha za serikali kwa kuwalipa watumishi ambao hawapo katika utumishi. Pia hali

hii imesababishwa na kukosekana kwa ukaguzi wa mara kwa mara ambao ulitakiwa ufanywe na maafisa wa usimamizi wa rasilimali watu kwa kushirikiana na wakuu wa idara na wakaguzi wa ndani katika kuhalalisha maingizo yote ya mishahara na kuhakikisha taarifa zote za watumishi zinaboreshwa.

Ninatoa ushauri kwa hizi Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kuboresha taarifa za watumishi katika rejesta ili kuachishwa kazi kwa aina yoyote kuweze kujulikana mapema kabla mishahara haijalipwa. Pia, ninapendekeza kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa/ OWM-TAMISEMI, Ofisi ya Rais inayosimamia Utumishi wa Umma na Hazina kuanzisha mahusiano ya karibu ya kikazi ili kutoa maamuzi kwa wakati kwa masuala yanayohusiana na watumishi walioachishwa kazi na mishahara yao inaendelea kulipwa.

5.4.5 Watumishi waliokopa zaidi

Waraka wa utumishi wa Umma Na. CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2010 unaelekeza kwamba, makato katika mishahara ya watumishi yanatakiwa yasizidi theluthi mbili (2/3) ya mishahara yao.

Licha ya kuripoti miaka iliyopita, bado kuna mwendelezo wa watumishi wa Halmashauri ambao mishahara yao inakatwa zaidi ya 2/3 ya mishahara yao. Pia kuna baadhi ya watumishi wamekuwa wakikatwa mshahara wote. Katika jumla ya Halmashauri 34 zilizokaguliwa, imebainika kuwepo kwa jumla ya watumishi 3,650 ambao wanapokea chini ya 1/3 ya mishahara yao. Hali hii inaonesha kuwa kumekuwepo maboresho katika udhibiti wa mikopo inayozidi kiwango kilichoidhinishwa ukilinganisha na idadi hiyo hiyo ya Halmashauri zilizooneshwa kukopesha zaidi ya kiwango katika mwaka uliopita kama inavyoonekana hapa chini kwenye kiambatisho (**xxvii).**

Mikopo isiyodhibitiwa inaweza kuleta madhara makubwa kwa watumishi husika katika ufanisi wa kazi na katika Halmashauri husika. Matatizo hayo ya mishahara yanachangiwa na uongozi wa Halmashauri husika kutokuwa makini katika kuhakikisha kuwa maslahi ya wafanyakazi yanalindwa.

Ninapendekeza kwamba Halmashauri zinatakiwa kuweka udhibiti wa taratibu za kukopa kwa lengo la kutokuwa na mapungufu yoyote ya kutokufuata miongozo ambayo ni muhimu katika kupunguza athari hasi za utendaji wa watumishi.

Serikali kupitia Wizara ya Fedha inashauriwa kufuatilia kwa karibu maelekezo na sheria zilizotolewa kwa taasisi zote za fedha katika kusimamia kiwango cha mikopo ya watumishi.

5.4.6 Tofauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa na mishahara iliyolipwa Sh.184,174,087

Ukaguzi ulibaini Hazina kupeleka kwa fedha za mishahara zaidi kwa kiasi cha Sh.184,174,087 kwenda katika Halmashauri.Haya ni matokeo ulinganisho uliofanywa kati ya mishahara halisi iliyolipwa na fedha za mishahara zilizopokelewa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Halmashauri 12 zilizochukuliwa kama sampuli. Maelezo ya kina kwa Halmashauri yanaonyeshwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na.24: Halmashauri zilizolipa mishahara zaidi ya fedha walizopokea

Na.	Jina la Halmashauri	Ruzuku za Mishahara iliyopokelewa (Sh.)	Mishahara iliyolipwa (Sh.)	Tofauti (Sh.)
1	H/W Bariadi	13,112,081,333	12,950,639,003	161,442,330
2	H/W Bunda	10,415,191,563	10,412,732,991	2,458,572
3	H/Jiji Dar es Salaam	890,029,952	1,086,090,429	-196,060,477
4	H/W Iramba	10,414,880,422	10,385,918,311	28,962,111
5	H/W Kyela	7,620,415,290	7,644,153,353	-23,738,062
6	H/W Manyoni	574,076,397	570,203,098	3,873,299
7	H/W Mbozi	17,887,503,370	17,889,575,177	-2,071,807
8	H/W Moshi	45,286,724,498	45,059,844,851	226,879,647
9	H/M Moshi	9,840,755,071	9,836,289,273	4,465,798
10	H/W Mvomero	10,739,909,635	10,736,746,574	3,163,061
11	H/W Same	21,010,310,792	21,040,818,213	-30,507,421
12	H/M Singida	6,578,266,131	6,572,959,094	5,307,037
Jumla		**154,370,144,454**	**154,185,970,367**	**184,174,087**

Ninarudia pendekezo langu lililopita kwamba, menejimenti za Halmashauri zisuluhishe kumbukumbu za fedha za mishahara zinazopokelewa kupitia taarifa ya kutolea fedha kutoka Hazina (exchequer issue notification) kwenda kwa Maafisa Masuuli na kuwasiliana na Hazina ili kurejesha kiasi cha mishahara kilichozidi.

5.4.7 Kutokuwepo kwa usahihi wa tarehe ya kuzaliwa kwa Watumishi katika Orodha kuu ya kulipia mishahara kutoka Hazina

Serikali ina mfumo wake wa mishahara ambao umeunganisha mishahara ya watumishi wote wa Umma katika Mfumo wa habari wa Rasilimali watu ambapo taarifa muhimu za mtumishi huingizwa na kufanyiwa marekebisho mara kwa mara. Taarifa hizo ni kama vile tarehe za

kuzaliwa, viwango vya mishahara, kupandishwa vyeo n.k.Taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya matumizi tofauti ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa malipo ya mishahara na hivyo ni muhimu kuwa na taarifa sahihi kwenye mfumo.

Hata hivyo, katika Halmashauri 15 zilizokaguliwa ilibainika kwamba,tarehe za kuzaliwa za watumishi 2,345 katika orodha kuu ya mishahara ya serikali ilikuwa sio sahihi kwani zilikuwa zinatokea kama 1/1/1700,1/1/1900 na 1/1/2012. Suala kama hili lilioneshwa katika miaka iliyopita ambapo katika Halmashauri 15 zilizochaguliwa watumishi 1,531 walikuwa na tarehe za kuzaliwa zisizo sahihi.

Jedwali Na.25 : Idadi ya Halmashauri zinazoonesha watumishi wenye tarehe za kuzaliwa zisizo sahihi katika orodha kuu ya mishahara Hazina

Na.	Jina la Halmashauri	Na. ya watumishi wenye tarehe zisizo sahihi katika Orodha ya Mishahara
1	H/W Arusha	75
2	H/W Bukombe	12
3	H/W Igunga	14
4	H/W Ileje	2,100
5	H/W Karatu	14
6	H/W Kilombero	4
7	H/M Kinondoni	4
8	H/W Mbeya	6
9	H/W Meatu	19
10	H/W Mtwara	6
11	H/Manispaa Mtwara	10
12	H/W	19

	Ngorongoro	
13	H/W Pangani	4
14	H/W Same	50
15	H/W Urambo	8
	Jumla	**2,345**

Hii ina maana kwamba, Maafisa Rasilimali watu hawajaboresha taarifa katika mfumo wa LAWSON ili kuwezesha mabadiliko kufanyika katika Orodha kuu ya Mishahara. Tarehe za kustaafu za watumishi haziwezi kujulikana kwa urahisi na Hazina kwa kuwa kumbukumbu za watumishi zitakuwa zimetunzwa kwenye mafaili ya watumishi husika yasiyo ya kielektroniki.

Uongozi wa Halmashauri husika unashauriwa kuwa, taarifa za watumishi na taarifa katika Orodha kuu ya kulipia mishahara kutoka Hazina zisuluhishwe na kwamba terehe za kuzaliwa zisahihishwe ipasavyo.

5.4.8 Makato ya Kisheria ambayo hayakuwasilishwa katika Taasisi husika Sh.83,619,613

Mshahara wa mtumishi unapunguzwa na makato ya kisheria ambayo yanahusisha michango katika mifuko ya hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato. Malipo ya kisheria mara nyingi huwa yanafanyika Hazina na huwa taarifa inatumwa kwenye Halmashauri. Hata hivyo, kuna watumishi ambao makato yanatakiwa kufanywa na Halmashauri kisha yanawasilishwa kwa Taasisi husika.

Mapitio ya nyaraka mbalimbali za mishahara na makato katika halmashauri saba (7) yalibaini kwamba makato ya kiasi cha Sh.83,619,613 hayajawasilishwa kwenye taasisi husika kama vile LAPF, PSPF, NSSF, PPF na TRA kama yalivyoonyeshwa kwenye jedwali 26 hapa chini:

Jedwali Na.26:Muhtasari wa makato yasiyowasilishwa katika taasisi husika

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi cha makato yasiyowasilishwa katika taasisi husika (Sh.)
1	H/W Geita	2,476,800
2	H/W Igunga	4,956,626
3	H/W Kondoa	12,548,329
4	H/M Lindi	2,596,644
5	H/W Manyoni	7,871,152
6	H/Mji Mpanda	5,144,064
7	H/W Mvomero	48,025,998
	Jumla	**83,619,613**

Kuwasilisha makato yanayofanyika katika ngazi ya halmashauri ni lazima, Kinyume na hapo, Halmashauri zinaweza kutumia makato yasiyowasilishwa katika shughuli nyingine na hivyo kusababisha madeni ambayo itakuwa ngumu kuyalipa kwa miaka inayofuata. Hata hivyo yanaweza yakaongeza gharama kutokana na faini ya kuchelewa kuwasilisha michango. Kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama LAPF, PSPF, NSSF na PPF kutokuwasilisha michango kunaathiri ulipaji wa mafao ya kustaafu.

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuimarisha taratibu za ufuatiliaji wa makato ya mishahara ya watumshi kwa kuhakikisha kuwa makato hayo yanawasilishwa mara baada ya usuluhisho kufanyika. Pia ninazisihi Halmashauri kuhakikisha kwamba makato ambayo hayajawasilishwa yanalipwa kwa taasisi husika na makato ambayo hayajalipwa yaoneshwe kama madeni katika taarifa za fedha.

5.4.9 Kutowasilishwa kwa Stakabadhi za kupokelea mishahara isiyolipwa na makato ya Kisheria yaliyolipwa Sh. 685,034,393

Kiasi cha Sh.685,034,393 ikiwa ni mishahara iliyorudishwa Hazina kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na makato ya kisheria yaliyolipwa katika taasisi mbalimbali kutoka Halmashauri kumi (10) hazikuweza kuthibitika kama kimepokelewa na taasisi husika kwa vile stakabadhi za kukiri mapokezi hazikuwasilishwa kuthibitisha kupokelewa kwa kiasi cha fedha kilicholipwa, hii ikiwa ni kinyume na Agizo la 8 (2) (c) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Halmashauri zilizokaguliwa katika eneo hili ni kama zinavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 27: Stakabadhi zisizowasilishwa za kupokelea mishahara isiyolipwa na makato ya Kisheria yaliyolipwa

Na.	Jina la Halmashauri	Stakabadhi ambazo hazikuwasilishwa kutoka kwa taasisi (Sh.)	Mishahara isiyolipwa na kuwasilishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa lakini hakuna stakabadhi ya kukiri mapokezi (Sh.)
1	H/W Bukombe	8,147,083	-
2	H/W Bariadi	-	41,710,089
3	H/M Dodoma	23,645,800	22,459,312
4	H/WGeita	150,000,000	102,170,117
5	H/W Ludewa	-	27,655,410
6	H/W Ngara	136,546,560	-
7	H/W Njombe	-	128,497,509
8.	H/Mji Njombe	-	44,202,513
	Jumla ndogo	**318,339,443**	**366,694,950**
Jumla kuu			**685,034,393**

Kukosekana kwa stakabadhi za kupokea malipo hayo kutoka kwa walipwaji ina maana kwamba, kuna uwezekano wa malipo hayo kufanyika kimakosa kwa walipwaji wasiohusika. Menejimenti za Halmashauri husika zinashauriwa kufuatilia kwa walipwaji mara tu malipo yanapokuwa yamefanyika ili kuhakikisha kuwa malipo yamepokelewana walipwaji sahihi.

5.4.10 Karadha za mishahara zisizorejeshwa Sh.520,484,151

Agizo la 41(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linatoa maelekezo jinsi karadha za mishahara zinavyofanyika kwa mtumishi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na mtumishi anayeajiriwa kwa mara kwanza au anayehamishwa, malipo ya ada ya shule ya Mtumishi au watoto wake, malipo kwa ajili ya matibabu ya haraka au kifaa kwa ajili ya mtumishi au familia yake, ununuzi wa vifaa muhimu kutokana na moto

au wizi katika makazi ya mtumishi na mwisho kwa ajili ya kumudu gharama za mazishi kwa mtu wa karibu wa familia ya mtumishi. Masharti ya kurejesha karadha ya mishahara inaelezewa kuwa si zaidi ya miezi kumi na mbili(12).

Wakati wa Ukaguzi wa mwaka huu, ilibainika kuwa Halmashauri 25 zimetoa karadha kwa watumishi zenye jumla ya Sh.520,484,151 ikilinganishwa na karadha za Sh.312,089,918 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2011/2012 na Halmashauri 10 ambazo hazijarejeshwa. Hii ni kinyume na Agizo lililotajwa hapo juu. Orodha ya Halmashauri zenye karadha za mishahara zisizorejeshwa inaonyeshwa kwenye jedwali Na.28 hapa chini:

Jedwali Na.28: Karadha za mishahara zisizorejeshwa

Na.	Jina la Halmashauri	Karadha za mishahara/Mikopo ya watumishiisiyorejeshwa (Sh.)
1	H/W Arusha	1,759,210
2	H/W Babati	16,822,113
3	H/Mji Babati	9,208,887
4	H/W Bariadi	6,750,000
5	H/Mji Bariadi	3,800,000
6	H/W Chunya	39,925,364
7	H/M Ilemela	2,772,650
8	H/W Kahama	71,801,236
9	H/W Karatu	840,078
10	H/W Kongwa	15,604,775
11	H/W Longido	9,333,000
12	H/Mji Masasi	2,754,000
13	H/W Mbarali	5,100,000
14	H/Jiji Mbeya	31,513,495
15	H/W Mbeya	107,210,030
16	H/W Mbinga	74,861,400
17	H/W Meatu	1,470,000
18	H/W Misungwi	22,100,000
19	H/W Moshi	19,226,912
20	H/W Mpanda	11,880,000

21	H/M Mtwara	40,148,361
22	H/W Siha	5,069,320
23	H/W Sikonge	9,783,320
24	H/W Songea	6,300,000
25	H/W Urambo	4,450,000
	Jumla	**520,484,151**

Kutokurejeshwa kwa karadha za mishahara kwa muda kunaathiri utekelezaji wa shughuli nyingine zilizopangwa na inaweza kuwa chanzo cha madeni yasiyolipika kwa watumishi.

Menejimenti za Halmashauri inatakiwa kuzingatia Agizo la 41 (1) kwa kuhakikisha kuwa karadha za mishahara kwa watumishi zinarejeshwa ndani ya muda uliopangwa.

5.4.11 Watumishi ambao hawapo tena kwenye utumishi wa Umma lakini wanaendelea kuonekana katika Orodha ya Mishahara ya Hazina

Agizo la 79 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, 2009 inaelekeza kuwa wakuu wa idara wanatakiwa kutunza rejista hai ya watumishi wote ikiwa na maelezo yao ambayo itampa mweka hazina taarifa juu ya mambo yote yanayohusu ajira, kuacha kazi, kuachishwa kazi, kusimamishwa kazi, uhamisho na taarifa yoyote muhimu kwa utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kwa ajili ya kodi ya mapato, mifuko ya hifadhi ya jamii n.k. Pia kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kinatamka kwamba, “pale ambapo mtumishi wa umma atakuwa hayupo kazini kwa siku tano (5) bila sababu na wala si likizo mtumishi huyo atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwa nje ya kituo cha kazi na ataachishwa kazi”.

Kinyume na Agizo hili, katika kupitia orodha ya mishahara ya watumishi na taarifa zao kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 imebainika kuwa watumishi 510 kutoka katika Halmashauri sita (6) ambao ni waliostaafu, waliofariki, walioacha na kuachishwa kazi waliendelea kuonekana kwenye orodha ya mishahara ya Hazina. Halmashauri husika na idadi ya watumishi wanaoendelea kuonekana katika orodha ya mishahara ni kama inavyooneshwa katika jedwali Na.29 hapa chini:

Jedwali Na.29: Halmashauri ambazo zina watumishi ambao hawapo kwenye utumishi na hawajafutwa kwenye orodha ya mishahara ya Hazina

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya waliokuwa watumsihi
1	H/W Kahama	51
2	H/W Kilombero	41
3	H/W Mbozi	17
4	H/W Moshi	8
5	H/W Nanyumbu	368
6	H/W Tandahimba	25
		510

Kuchelewa kufuta majina ya watumishi wastaafu, waliokufa, waliofukuzwa au kuacha kazi kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama ya mishahara na upotevu wa fedha za umma zinazolipwa kwa watumishi hewa.

Ninashauri Menejimenti za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba watumishi waliostaafu, waliokufa, walioacha au kuachishwa kazi, taarifa zao zinatakiwa zitolewe haraka kwa ajili ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha

kuwa majina yao yanafutwa mara moja katika orodha ya mishahara ya Hazina.

5.4.12 Uhaba wa Rasilimali Watu

Utendaji na ufanisi wa Taasisi yoyote unategemea upatikanaji wa rasilimali watu ambayo ni moja ya rasilimali muhimu. Katika mwaka 2012/2013, Halmashauri 73 zilichaguliwa kama sampuli wakilishi ambapo ilionekana kwamba Ikama zilionesha mahitaji ya watumishi 183,095 lakini idadi halisi iliyopo ilikuwani 143,111 tu na kusababisha upungufu wa watumishi 39,984 ambao ni sawa 22% ya idadi inayotakiwa. Upungufu huo una madhara katika utendaji kwa jumla katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, kuzidiwa kwa kazi na kupungua kwa ari ya kazi kwa watumishi wa umma waliopo. Sekta ambazo zimeathiriwa zaidi ni sekta za Afya, Kilimo na Elimu. Rejea **Kiambatisho(xxviii)**

Ninajua kwamba serikali imefanya jitihada ya kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta mbalimbali. Hata hivyo, kiwango cha uhaba wa watumishi cha kiwango cha 22% bado ni kikubwa ukilinganisha na mahitaji. Kwa hali hiyo, ninarudia mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwamba:

- Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI iweke mkakati utakao punguza wimbi la wafanyakazi kuacha kazi
- Kuwe na utoaji wa motisha maalum kwa madhumuni ya kuwahamasisha wafanyakazi kufanya kazi katika Halmashauri za pembezoni. Mapengo mengi ya ajira yaliyothibitishwa katika Halmashauri yapo katika maeneo ya pembezoni ikilinganishwa na maeneo ya mijini.

5.4.13 Kuajiri wafanyakazi wa muda katika kazi za kutoa huduma

Katika kipindi cha mwaka husika, ilibainika kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Halmashauri ya Mji wa Geita zilikuwa zimeajiri wafanyakazi wa muda 66 na 72 kwa mtiririko huo kwa kuingia nao mikataba kinyume na Aya ya D.30 Aya ndogo ya 2 ya Kanuni za Kudumu kwa Utumishi wa Umma (2009) ambayo inakataza kuajiri kwa mikataba ya muda kwa nafasi zote za kazi za kutoa huduma.

Ilibainika zaidi pia kwamba, ajira ya vibarua ilikuwa na baadhi ya mapungufu yafuatayo:

- Halmashauri hazikuomba kibali cha ajira kutoka katika Bodi ya Ajira ikiwa ni kinyume na Aya A.1 (27) ya Kanuni za Kudumu kwa Utumishi wa Umma za mwaka 2009 , toleo la tatu .
- Wafanyakazi vibarua waliajiriwa katika Halmashauri bila kutangaza nafasi hizo kinyume na Kanuni za Kudumu D.9 (1) - (2).

Kuajiri idadi kubwa ya wafanyakazi wa muda ni kinyume na maagizo na ina athari katika shughuli za Halmashauri kwani kuna uwezekano wa kubakiza wafanyakazi ambao hawana uwezo na kuwa mzigo mkubwa kwa Halmashauri kwani mishahara yao haikuwa kwenye bajeti iliyopitishwa mwaka uliopita.

Napendekeza kwa menejimenti za Halmashauri kuhakikisha kwamba maagizo, taratibu, kanuni na Sheria zinafuatwa kwa watumishi wanaoajiriwa kwa mikataba .

5.4.14 Nafasi za Wakuu wa Idara ambazo zinakaimiwa kwa zaidi ya miezi sita

Aya D24 (3) ya Kanuni za Kudumu kwa Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa, ikiwezekana, mtumishi wa umma hatakiwi kukaimu nafasi iliyo wazi kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita. Mamlaka ya uteuzi inatakiwa kuhakikisha kuwa mchakato kwa kumteua mtumishi ambaye atashika nafasi iliyo wazi unakamilika ndani ya kipindi cha miezi sita. Sampuli ya Halmashauri 31 zilizokaguliwa, imebainika kwamba, wafanyakazi 166 walikuwa wanakaimu nafasi za Wakuu wa Idara au hata Maafisa Masuuli kwa zaidi ya miezi sita ikiwa ni kinyume na maelekezo katika Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma. Orodha ya sampuli za Halmashauri zilizokaguliwa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na.30: Idadi ya Watumishi wanaokaimu nafasi za Wakuu wa Idara kwa muda zaidi ya miezi sita katika Halmashauri mbali mbali

Na	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi wanaokaimu	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi wanaokaimu
1	H/W Babati	4	17	H/W Meatu	6
2	H/W Bagamoyo	3	18	H/W Mkinga	10
3	H/Mji Bariadi	7	19	H/W Moshi	2
4	H/W Bunda	4	20	H/M Moshi	2
5	H/W Chunya	11	21	H/W Rombo	5
6	H/M Dodoma	4	22	H/W Rorya	7
7	H/W Hai	2	23	H/W Rorya	7
8	H/W Ileje	5	24	H/W Same	6
9	H/M Ilemela	7	25	H/W Serengeti	2
10	H/W Kahama	2	26	H/W Shinyanga	5
11	H/W Karagwe	7	27	H/W Siha	5
12	H/W Kilwa	5	28	H/W Sikonge	6
13	H/M Lindi	1	29	H/W Simanjiro	6
14	H/W Magu	4	30	H/W Sumbawanga	9
15	H/W Manyoni	4	31	H/W Tarime	12
16	H/W Mbozi	6		**Jumla**	**166**

Kushindwa kuwa

kuthibitisha watumishi wanaokaimu inaweza kuisababishia Halmashuri husika madeni yatakayotokana na posho ya kukaimu. Aidha, kukaimu kwa muda mrefu kunapunguza ari ya utendaji kazi kwa maafisa wanaokaimu katika kufanya vizuri katika nafasi zao na kutoa huduma kwa ufanisi.

Kwa hiyo ninapendekeza kwamba Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menegimenti ya Utumishi wa Umma kuwateua watumishi waliokaimu au kuteua Watumishi wapya wenye sifa ili kushika nafasi hizo.

5.4.15 Watumishi ambao wana namba za mshahara zaidi ya moja

Namba ya mshahara ni utambulisho wa kipekee wa ajira ambayo inatofautisha kati mtumishi mmoja na mwingine. Kwa maana hiyo hainatarajiwi kwa mtumishi kuwa na namba za mshahara zaidi ya moja na kwa wakati mmoja.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa katika mfumo wa malipo tumebaini kuwa Halmshauri sita zimebainika kuwa na wafanyakazi 25 ambao walikuwa na namba mbili tofauti za mshahara kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na.31: Wafanyakazi na zaidi ya moja namba ya hundi

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi wenye zaidi ya namba moja ya mshahara
1	H/W Mbozi	3
2	H/W Nanyumbu	2
3	H/W Rufiji/Utete	3
4	H/W Sumbawanga	7
5	H/M Temeke	5
6	H/W Tunduru	5
Jumla		**25**

Wafanyakazi ambao wana namba za mshahara zaidi ya moja wana uwezo wa kupata mshahara zaidi ya mwezi mmoja. Kulipwa kwa mshahara miwili kwa mfanyakazi mmoja kunapelekea kuwa na matumizi mabaya ya fedha za Serikali na kuathiri shughuli nyingine za umma ambazo zingefanyika kwa kutumia fedha hizo. Hii ni ishara ya kutokuwa na udhibiti wa kutosha wa mishahara ya watumishi na kutofanyika kwa usuluhisho baina watumishi waliopo.

Halmashauri zinashauriwa kuhakiki kumbukumbu za watumishi kwa wakati na kukagua orodha za mishahara kabla ya kufanya malipo ili kubaini watumishi ambao wana namba za mishahara zaidi ya moja na kuchukua hatua za haraka ili kurekebisha hali hiyo.

5.5 Usimamizi wa Mali

Ukaguzi wa usimamizi wa mali katika Serikali za Mitaa, umebainisha masuala mbalimbali kama yalivyoainishwa hapa chini:

5.5.1 Mali kutokuwa na namba za utambulisho na utunzaji wa regista ya mali za kudumu

Ukaguzi wa mali za kudumu za Halmashauri ulibainisha kuwa Halmashauri 18 hazikuwa zimeboresha Regista za mali za kudumu ili kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu zinaingizwa katika Regista. Kwa mfano, kumbukumbu muhimu kama nyongeza ya mali ikiwa ni pamoja na tarehe, gharama na chanzo cha fedha , namba ya utambulisho ya mali, eneo mali zilipo, maelezo ya kuuza mali ikiwa ni pamoja na tarehe, bei na njia iliyotumika kuuza mali; hivyo vyote havikuainishwa kwenye regista za mali za kudumu ikiwa ni kinyume na Agizo la 103 (1) na (2) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka, 2009 ambalo linahitaji Halmashauri kuwa daftari la mali za kudumu ambalo linamilikiwa na kuweka taarifa zote muhimu.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba mali za kudumu katika Halmashauri 15 hazikuwa na namba za utambulisho ikiwa ni kinyume na Agizo la 63 (5) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 ambalo linahitaji mali zote za kudumu kuwa na alama ya namba ya utambulisho na kuingizwa katika regista ya mali za kudumu.

Kwa kutokuwa na namba za utambulisho na regista iliyoboreshwa ya mali za kudumu, mali za Halmashauri zinaweza kutumika vibaya au kupotea bila menejimenti ya Halmashauri kufahamu. Pia itakuwa vigumu kwa Halmashauri kufahamu idadi sahihi ya mali inayomilikiwa hivyo mali inaweza kuonyeshwa pungufu katika taarifa za fedha. **Rejea Kiambatanisho (xxix).**

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuhakikisha kwamba rejista za mali za kudumu zinaandaliwa vizuri na kuboreshwa kwa kuingiza taarifa zote muhimu kwa ajili ya udhibiti mzuri wa mali. Pia Halmashauri kwa kushirikiana na Wakuu wa Idara wanatakiwa kuhakikisha kwamba mali zilizopo katika Idara zao zinawekwa namba za utambulisho na kuingizwa katika Regista ya mali za kudumu kwa ajili ya kuzitambua kwa urahisi kama ni mali ya Halmashauri.

5.5.2 Magari yaliyotelekezwa kwa muda mrefu na yasiyofanyiwa matengenezo

Halmashauri ina jukumu la kusimamia na kudhibiti mali zote chini ya utawala wake na kuhakikisha kwamba mali zote zinafanya kazi vizuri kwa faida ya Halmashauri kwa ujumla. Moja ya udhibiti wa mifumo ya ndani ni kuhakikisha kwamba, magari yote, mitambo na pikipiki zinafanya kazi kwa gharama ndogo ya matengenezo.

Agizo la 45 (1) la Memoranda ya Fedha Serikali za Mitaa, 2009 linasema kwamba, " mali zote ambazo hazihitajiki,

mali ambazo ni vigumu kuzifanyia matengenezo, mali ambazo zimepitwa na wakati au chakavu zinatakiwa kutambuliwa na kutolewa katika kumbu kumbu za Hjalmashauri na baadaye taarifa iandaliwe kwa ajili ya kupitishwa na Kamati ya Fedha na hatimaye Baraza na Madiwani." Pia, Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma Na.21 Aya ya 26 vinasema kwamba, " Taasisi inatakiwa kufanya tathmini kila inapoandaa taarifa kwa kuangalia kama kuna dalili za mali ambazo zimepungua utendaji kazi wake. Kama kuna dalili yoyote, Taasisi husika inatakiwa kuthaminisha mali hizo ili kujua kiasi kinachoweza kupatikana kama mali itauzwa."

Ukaguzi uliofanywa katika Regista ya mali za kudumu pamoja viambatanisho vilivyowasilishwa pamoja na taarifa za fedha imebainika kwamba kuna mali za kudumu ambazo hazitumiki na zimetelekezwa kwa muda mrefu na siyo rahisi kufanyiwa matengenezo. Menejimenti husika haikuchukua hatua yoyote ama kwa kuthaminisha uwezo wa mali hizo kufanya kazi na kufahamu ni kwa kisi gani Halmashauri haiwezi kufaidika nazo, kufanya utaratibu wa kuziuza au kuzifanyia matengenezo makubwa. Maelezo ya mali hizo kwa kila Halmashauri yameonyeshwa katika **Kiambatanisho (xxx).**

Kuendelea kuwa na mali nyingi ambazo hazitumiki kunaweza kuongeza gharama za matengenezo na kusababisha utendaji wake kuzorota zaidi kutokana na uchakavu na hivyo kupunguza kiasi cha mapato ambacho kingepatikana kama mali zingekuwa zimeuzwa mapema. Ninapendekeza kwamba Halmashauri zinapaswa kutambua na kutathmini utendeaji kazi wa mali zilizopo ili ziweze kuuzwa au kufanyiwa matendenezo kama gharama ya matengenezo siyo kubwa ili kuzipatia faida za kiuchumi Halmashauri husika .

5.5.3 Mitambo, Mali na Vifaa ambavyo havikuthaminishwa

Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma Na.17 Aya ya 42 inasema kwamba, Taasisi inatakiwa kufanya tathmini ya thamani ya Mali zake kwa kutumia gharama ya kununulia *("cost model")* ambayo imeainishwa katika Aya ya 43 au kuthaminisha ("*revaluation module*") ambayo imeainishwa katika Aya ya 44 pamoja na sera yake ya uhasibu na anatakiwa kutumia sera yake ya uhasibu kwa mali, mitambo na Vifaa vyote. Pia, aya 44 inasema kwamba "baada ya kutambua mitambo, mali na vifaa ambavyo thamani yake inaweza kufahamika, Taasisi inaweza kuonesha kiasi kilichothaminishwa ikiwa ni thamani halisi kwa tarehe iliyothaminishwa, kutoa gharama ya uchakavu na gharama ambayo ni sawa na hasara inayotokana na kupungua utendaji wa Mali husika.

Katika kupitia taarifa za fedha nimebaini kuwa Halmashauri 16 zimetunza taarifa za kuwepo kwa Mali ,Vifaa na Mitambo ambavyo havikuwa na thamani na Mali zingine zilionekana zimekwisha tolewa uchakafu hadi kubaki bila thamani ingawaje zilikuwa zinatumika na Halmashauri kwa shughuli za kila siku.

Hata hivyo, Halmashauri hazikuwa na mpango ama wa kuthaminisha Mali zake au kuangalia upya muda wa kutumika kwa mali hizo ili waweze kujua thamani halisi ya mali hizo. Maelezo ni kama yanavyoonekana katika jedwali Na.30 hapa chini:

Jedwali Na.32: Orodha ya Halmashauri ambao zina Mali, Vifaa na Mitambo lakini hazikufanyiwa tathminini.

Na.	**Halmashauri**	**Aina ya Mali za kudumu**
1	H/M Dodoma	Majengo, Magari na Vifaa vya Ofisini.

2	H/W Kasulu	Majengo
3	H/W Mkuranga	Magari
4	H/W Ngorongoro	Majengo na Magari
5	H/M Iringa	Majengo na Vifaa vya Ofisini
6	H/Mji Bariadi	Majengo, Magari na Vifaa vya Ofisini ambavyo vimehamishiwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi.
7	H/W Rorya	Majengo, Magari na Vifaa vya Ofisini.
8	H/W Serengeti	Majengo na Vifaa vya Ofisini
9	H/M Shinyanga	Majengo na Magari
10	H/W Hanang	Piki piki
11	H/W Bariadi	Magari
12	H/W Kiteto	Magari
13	H/W Manyoni	Majengo, Magari na Vifaa vya Ofisini.
14	H/W Sikonge	Majengo
15	H/W Urambo	Majengo, Magari na Vifaa vya Ofisini.
16	H/M Ilemela	Ardhi na Majengo

Hii ina maana kwamba taarifa ya thamani ya Mali, Vifaa na Mitambo iliyoonyeshwa katika taarifa za fedha na viambatanisho vyake siyo sahihi na kuna uwezekano ikatolewa taarifa ambayo ni sahihi ya mali za Halmashauri ili kupata faida za kiuchumi. Kwa hali hii thamani ya Mali, Vifaa na Mitambo katika taarifa za fedha inaweza kuwa imepunguzwa kuliko ambavyo hali halisi ingepaswa kuwa.

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuweka makadirio kwa ajili ya kuthaminisha Mali au kuongeza muda wa matumizi wa Mali zake katika mchakato wa kuandaa bajeti

ili kuwa na uhakika kwamba taarifa ya Mali, Vifaa na Mitambo inayoonyeshwa katika taarifa za fedha ni sahihi.

5.5.4 Mitambo, Mali na Vifaa ambazo hazina nyaraka za umiliki

Agizo la 52 (4) na (5) la Memoranda ya Fedha ya Serikali, 2009 inaelekeza kwamba uwekezaji ambao ni wa fedha taslim ambao unafanyika kwa kipindi kifupi kama vile uwekezaji wa kiuchumi kwa kununua hisa au kuchangia mtaji (ikiwa ni pamoja na kwa njia ya ubia) utafanyika baada ya maazimio ya uongozi wa Halmashauri na utajumuishwa katika bajeti ya maendeleo au bajeti ya matumizi ya kawaida. Uwekezaji kama huo utathibitishwa kwa kuwa na hati ya dhamana au mkataba ambao utaingizwa katika rejista na kutunzwa kwa usalama na Afisa Masuuli".

Kinyume na utaratibu uliotajwa hapo juu, Ukaguzi umebaini kuwa mali zimeonyeshwa katika taarifa za fedha za Halmashauri 20 zinazohusiana na Mali, Mitambo na mali nyinginezo za kifedha ambazo zimekosa ushahidi wa maandishi kuthibitisha umiliki wake.

Ninapendekeza kwamba, Serikali za Mitaa lazima kupata haki za umiliki na udhibiti wa mali zake kama vile kadi za usajili wa magari na hati miliki za majengo yaliyoko katika himaya ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Orodha ya Halmashauri ambazo zilikuwa na mali bila ushahidi wa maandishi ya umiliki ni kama inavyooekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na.33: Orodha ya Halmashauri ambazo zina mali ambazo hazina Hati miliki

Na.	Halmashauri husika	Mali ambazo hazina Hati miliki	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Nanyumbu	Majengo	8,545,334
2.	H/W Kiteto	Ardhi na Majengo	16,556,300
3.	H/W Bukombe	Piki piki	24,242,203
4.	H/W Chunya	Mali zilizowekezwa	50,988,180
5.	H/W Masasi	Majengo na Magari	569,990,221
6.	H/W Mkuranga	Ardhi, Majengo na Magari	5,644,531,373
7.	H/W Masasi	Majengo	Taarifa haikutolewa
8.	H/W Newala	Majengo ,Magari na Pikipiki	Taarifa haikutolewa
9.	H/Mji Geita	Magari na Pikipiki	Taarifa haikutolewa
10.	H/W Pangani	Majengo	Taarifa haikutolewa
11.	H/W Handeni	Majengo	Taarifa haikutolewa
12.	H/M Shinyanga	Magari	329,787,558.26
13.	H/W Kilindi	Majengo	Taarifa haikutolewa
14.	H/W Mpanda	Mali zilizowekezwa	14,479,000
15.	H/W Masasi	Ardhi na Majengo	Taarifa haikutolewa
16.	H/W Songea	Ardhi na Majengo	5,300,639,334
17.	H/W Mbarali	Majengo na Magari	6,320,086,924
18.	H/M Songea	Ardhi na Majengo	3,045,587,251
19.	H/W Mbulu	Mali zilizowekezwa	5,000,000
20	H/W Mbinga	Mali zilizowekezwa katika Taasisi za Fedha	12,000,000

5.5.5 Thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa ambayo haikuonyeshwa katika taarifa za fedha ama kwa bei ya kununulia au kwa bei ya soko Sh.8,881,529,919

Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma Na.17 vinasema kwamba kila Taasisi inahitaji kufuata kanuni ili kutambua gharama za mali zote kwa ujumla ambazo ni Mali, Mitambo na Vifaa mitambo na vifaa wakati wanavinunua , ikiwa ni pamoja na gharama za awali na matumizi ya baadaye.

Pia Aya ya 14 inaeleza kwamba gharama ya Mali, Mitambo na Vifaa zinatakiwa kutambuliwa ikiwezekana kwa faida ya baadaye ya kiuchumi au uwezekano wa huduma zinazotokana na Mali hizo kwa Taasisi ama kwa bei iliyonunulia mali hizo au thamani ya Mali kwa wakati huo inayoendana na bei katika soko.

Mapitio ya taarifa za fedha pamoja na viambatanisho vyake yalibainisha kuwa Halmashauri 11 zilionesha thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa ya chini kwa Sh.359,637,943 na thamani ya Mali Sh.8,521,891,976 ilionyeshwa zaidi katika Taarifa za fedha kama inavyoonekana katika jedwali Na.34 hapa chini:

Jedwali Na.34: Orodha ya Halmashauri ambazo thamani ya Mali, Vifaa na Mitambo zimeonyeshwa pungufu au zaidi katika taarifa za fedha

Na.	Halmashuri husika	Kiasi cha Mali kilichoonyeshwa pungufu (Sh.)	Kiasi cha Mali kilichoonyeshwa zaidi (Sh.)
1	H/W Mkuranga	33,094,830	0
2	H/W Kishapu	112,063,713	0
3	H/W Ukerewe	0	3,298,355,446.21
4	H/M Ilemela	0	2,384,693,376
5	H/Jiji Mwanza	0	2,110,695,766.00
6	H/W Misungwi	0	172,247,989

7	H/W Kwimba	0	149,444,041.00
8	H/W Sengerama	0	10,492,213
9	H/W Kasulu	101,942,800	0
10	H/W Bukombe	0	723,758,770.60
11	H/Jiji Dar es salaam	112,536,600	0
12	H/Mji Korogwe	0	395,963,145
Jumla		**359,637,943**	**8,521,891,976**

Hii ina maana kwamba taarifa iliyotolewa ya Mali, Vifaa na Mitambo vya Halmashauri haikuonesha uhalisia wa Mali za Halmashauri na kwa maana hiyo, thamani ya Mali za Halmashuri kwa mwaka unaokaguliwa zimeonyeshwa pungufu katika taarifa za fedha.

Menejimenti za Halmashuri husika zinatakiwa kuhakikisha kuwa Mali, Vifaa na Mitambo vinatambuliwa na kuingizwa katika taarifa za fedha ili kuonesha taarifa ya mali zinazomilikiwa na Halmashauri ambayo ni sahihi.

5.6 Mapitio ya usimamizi wa Matumizi

5.6.1 Malipo yenye Nyaraka Pungufu Sh.3,514,703,776

Agizo la 8(2)(c) na 104 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linaagiza kuwa malipo yote yanayofanywa na Halmashauri yaambatishwe na nyaraka sahihi.

Wakati wa ukaguzi wa kumbukumbu za matumizi katika sampuli ya Halmashauri 67 zilizochaguliwa, ilibainika kuwa matumizi ya jumla ya Sh.3,514,703,776 yalifanywa bila kuwepo nyaraka sahihi. Malipo yaliyofanyika bila viambatisho vya kutosha yanakwaza mawanda ya ukaguzi katika kuhakiki uhalali wa malipo husika. Orodha ya Halmashauri husika na kiasi kwa kila halmashauri umeoneshwa katika **Kiambatisho (xxxi).**

Hali hii itakuwa imechangiwa na udhibiti dhaifu uliopo wa utunzaji wa nyaraka na viambatisho vingine vya malipo.

Ninapendekeza kwamba, Halmashauri ziweke utaratibu wa udhibiti wa malipo kwa kuwa na ukaguzi wa awali utakaopitia kwa ufanisi malipo yote kabla hayajafanyika. Aidha, utaratibu wa utunzaji wa viambatisho vinavyothibitisha uhalali wa malipo uandaliwe vizuri na udhibitiwe kwa kuanzishwa kwa rejista ambayo itasaidia kufuatilia nyaraka zinapotoka sehemu moja hadi nyingine ili kujua mahali nyaraka zilipo.

5.6.2 Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo Sh.8,063,469,984

Agizo la 34(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inamtaka Mweka Hazina wa Halmashauri kuweka mfumo bora wa uhasibu na kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazotakiwa kuambatanishwa zinakuwa salama.

Aidha, Agizo la 104 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, ambayo kwa pamoja yanaelekeza kuwa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake vinatakiwa kuwekwa vizuri na kutunzwa kwa muda usiopungua miaka mitano (5).

Wakati wa ukaguzi wa 2012/2013 ilibainika kwamba matumizi yenye jumla ya Sh.8,063,469,984 yaliyofanyika katika Halmashauri 19 lakini hati za malipo pamoja na viambatanisho vya matumizi hayo havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo, uhalali wa matumizi haya haukuweza kuthibitishwa kutokana na kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi. Halmashauri husika ni kama zinavyoonyeshwa katika Jedwali hapa chini:

Jedwali Na.35: Orodha ya Halmashauri zenye matumizi yasiyo na Hati za malipo

Na	Halmashauri husika	Kiasi cha fedha kilicholipwa kwa Hati za Malipo zilizokosekana (Sh.)
1	H/W Arusha	4,100,000
2	H/W Bariadi	5,381,170,011
3	H/W Chamwino	18,734,100
4	H/Jiji Dar es Salaam	5,982,940
5	H/W Karatu	4,073,688
6	H/W Kasulu	58,906,246
7	H/W Kwimba	67,500,153
8	H/W Longido	70,655,227
9	H/W Mafia	8,539,000
10	H/W Masasi	12,501,600
11	H/Mji Masasi	7,760,000
12	H/W Maswa	29,300,000
13	H/W Mbeya	26,562,016
14	H/W Misungwi	112,362,500
15	H/Jiji Mwanza	2,192,601,169
16	H/W Rorya	15,590,232
17	H/W Rungwe	6,019,000
18	H/W Sengerema	39,369,702
19	H/W Shinyanga	1,742,400
	Jumla	**8,063,469,984**

Kwa kuwa tatizo hili linajitokeza katika idadi kubwa ya Halmashauri, ningependa kuwakumbusha Maafisa Masuuli kuhusu wajibu wao wa msingi wa kuhakikisha kwamba, nyaraka zote muhimu zinatunza vizuri ikiwa ni pamoja na Hati za malipo .

5.6.3 Kukosekana kwa stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji Sh.292,058,967

Jumla ya Sh.292,058,967 ambazo zinahusisha Halmashauri tisa (9) ni malipo ambayo ama yalilipwa moja kwa moja na Hazina ikiwa ni makato ya kisheria, au yalilipwa na Halmashauri hizo kwenda kwenye Taasisi mbalimbali kwa ajili ya huduma mbalimbali zilizotolewa na taasisi hizo, lakini malipo hayo hayakuweza kuthibitika kama yamepokelewa na Taasisi husika kwa kuwa stakabadhi/risiti ya kukiri kupokea kiasi hicho cha fedha hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hii inapingana na Agizo la 8(2)(c) na 104 la Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 2009. Sampuli ya Halmashauri ni kama inavyoonekana katika orodha hapa chini:

Jedwali Na36: Orodha ya Halmashauri ambazo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji zilikosekana

Na.	Halmashauri husika	Kiasi (Sh.)
1	H/W Bagamoyo	8,140,000
2	H/W Bukoba	8,518,427
3	H/W Karatu	4,591,000
4	H/Mji Kibaha	3,153,200
5	H/Mji Korogwe	4,584,422
6	H/W Longido	145,026,786
7	H/W Mufindi	31,026,367
8	H/Jiji Mwanza	22,278,400
9	H/W Tabora	1,905,465
10	H/M Tabora	62,834,900
	Jumla	**292,058,967**

Kukosekana kwa stakabadhi ya kukiri mapokezi kutoka kwa mlipwaji kunamzuaia mkaguzi kuhakiki matumizi yaliyofanyika katika kifungu husika.

Tatizo hili limekuwa likijirudia mara kwa mara katika halmashauri nyingi licha ya kutoa maoni yangu mara nyingi juu ya suala hilo, Hivyo, napenda kuzikumbusha kwa mara nyingine, Menejimenti za Halmashuri kuhusu wajibu wao katika kuhakikisha kwamba, kila Halmashauri inatunza, inalinda nyaraka vizuri na kwamba nyaraka hizo ni lazima zitolewe kwa ajili ya ukaguzi pindi zinapohitajika.

5.6.4 Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika Sh.2,061,468,497

Agizo la 23(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inaagiza uwa kila malipo ya matumizi yalipwe kulingana na kifungu cha mapato sahihi na kwa mujibu wa maelezo ya bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopangwa zitumike tu kwa malengo yaliyokusudiwa.

Wakati wa ukaguzi wa 2012/2013, ilibainika kuwa katika Halmashauri 45 kulikuwa na matumizi ya jumla ya Sh.2,061,468,497 yaliyobainika kuwa yamefanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika bila kibali cha Kamati ya fedha kuidhinisha ili fedha zihamishwe kwenda vifungu vingine. Hii pia ni kinyume na Kifungu 43(5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa,1982 (Iliyorekebishwa 2000).Halmashauri zilizobainika kuwa na matumizi yaliyofanyika kwa kutumia vifungu visivyohusika ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambanisho (xxxii).**

Kufanya matumizi kwa kutumia vifungu visivyohusika haimaanishi tu kuwa ni kinyume cha udhibiti wa bajeti na maagizo bali pia huongeza matumizi katika vifungu husika ambavyo matumizi yamefanyika. Hali hii inakuwa na athari za kufanya makosa katika kifungu kimoja kimoja kwa kuonesha matumizi zaidi au kidogo katika taarifa za fedha.

Bado ninasisitiza kwa Halmashauri husika juu ya umuhimu wa kufuata maagizo na udhibiti wa bajeti kwa kuwa jambo hili limekuwa likijirudia mara kwa mara na bado udhibiti haujaimarishwa ili kupunguza kasoro hizo.

5.6.5 Uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambayo haijarejeshwa Sh.2,058,258,530

Ukaguzi wa malipo na nyaraka mbali mbali katika sampuli ya Halmashauri 18 umebaini kuwa ulifanyika uhamisho wa ndani wa fedha kiasi cha Sh.2,058,258,530 kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ndani ya Halmashauri hizo ambazo hazikurejeshwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2012/2013 kinyume na Agizo la 23 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Halmashauri zilizohusika ni kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na.37: Orodha ya halmashauri zilizofanya uhamisho wa ndani wa fedha kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ambazo hazijarejesha

Na	Jina la Halmashauri	Kiasi mkopo ambacho hakijarejeshwa (Sh.)
1	H/W Bahi	41,331,700
2	H/W Bariadi	6,996,000
3	H/Mji Bariadi	11,439,000
4	H/M Ilemela	543,442,629
5	H/W Karagwe	8,033,000
6	H/W Kilwa	715,771,262
7	H/W Longido	68,023,837
8	H/W Ludewa	19,000,000
9	H/W Meru	52,035,472
10	H/W Missenyi	8,435,000
11	H/W Misungwi	9,400,000
12	H/W Morogoro	135,346,000
13	H/Mji Mpanda	100,000,000
14	H/Jiji Mwanza	301,487,630
15	H/W Pangani	7,000,000
16	H/W Same	6,640,000
17	H/W Sengerema	19,127,000
18	H/W Sikonge	4,750,000
	Jumla	**2,058,258,530**

Mwenendo wa uhamishaji wa fedha ndani ya Halmashauri kwa kipindi cha miaka mitatu (3) ambazo hazikurejeshwa ni kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali Na.38: Mwenendo wa fedha zilizohamishwa ndani ya Halmashuri bila kurejeshwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3)

Mwaka wa fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zilizohusika
2012/2013	2,058,258,530	18
2011/2012	2,673,964,170	45
2010/2011	750,621,650	20

Fedha zilizopokelewa katika kila mwaka wa fedha zinatarajiwa kutumika kutekeleza shughuli zilizopo kwenye bajeti iliyoidhinishwa. Kwa kuhamisha fedha kwa njia ya mkopo kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine ni matumizi ambayo ni kinyume na bajeti iliyoidhinishwa. Pia, hali hiyo itasababisha kushindwa kutekelezwa kwa shughuli zilizoidhinishwa katika mwaka husika.

Ninapendekeza kwamba, kabla Halmashauri hazijafanya uhamisho wa ndani kutoka akaunti moja kwenda nyingine kwa njia ya mikopo ihakikishe kuwa taratibu na kanuni zinafuatwa. Aidha, marejesho ya mikopo yafanyike ndani ya mwaka husika ili shughuli ambazo zilikasimiwa fedha hizo ziweze kutekelezwa.

5.6.6 Posho za wito zilizopokelewa lakini hazijalipwa Sh.348,094,400

Aya L.19 (1) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inaelezea kuwa posho za wito kama posho maalum inayolipwa kwa mtumishi wa kada ya afya ambaye anaweza akahitajika kutoa huduma ya dharura wakati zamu yake ya kawaida inakuwa imeshapita. Aidha, tarehe 21/02/2012 Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitoa maelekezo kupitia barua yenye Kumb. Na.CAC.17/45/A1/F/73 inayoelezea viwango vya posho za

wito zinazotakiwa kulipwa katika kada mbalimbali zinazotoa huduma za afya.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2012/2013, mapitio yalifanyika katika sampuli ya Halmashauri 14 ambapo ilibainika kwamba jumla ya Sh.933,495,000 zilipokelewa ili ziweze kutumika kulipia posho za wito wa dharura. Hata hivyo, Sh.585,400,600 (63%) zililipwa kwa watumishi mbalimbali wa sekta ya afya na kuacha bakaa ya jumla ya Sh.348,094,400 (37%). Rejea jedwali 39 hapa chini.

Kwa nyongeza, mambo yafuatayo yalibainika kuhusiana na kiasi cha fedha kilicholipwa:

- Halmashauri zilichelewa kutambua mapato yanayohusiana na posho za wito wa dharura kwa kipindi kinachofikia hadi miezi sita. Hali hii, imesababisha malipo kutokufanyika kwa wakati na kusababisha kuwepo kwa Halmashauri ambazo hazijalipa posho zote kwa wakati kwa mwaka husika.
- Kiasi cha Sh.38,610,000 kati ya bakaa ya Sh.39,510,000 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto zilitumika kwa ajili ya shughuli nyingine tofauti na posho za wito wa dharura ambapo hali hii ni kinyume na lengo la fedha iliyopokelewa na kubaki.

Watumishi ambao wana haki ya kulipwa posho za wito wa dharura wasipolipwa kwa wakati inawapunguza ari katika utendaji wao wa kazi, hali ambayo kwa ujumla inaharibu utoaji wa huduma bora kwa jamii. Hata hivyo, kubakiza posho za wito wa dharura ambazo zimepokelewa kwa muda mrefu bila ya kuwalipa walengwa inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo na hatimaye kuisababishia Halmashauri kuwa na watumishi wenye madai yasiyolipwa.

Jedwali 39: Kiasi cha posho za wito wa dharura ambazo hazijatumika katika mwaka wa fedha 2012/13

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi kilochopokelewa (Sh.)	Kiasi kilicholipwa (Sh.)	Bakaa/Kiasi kilichotumika zaidi (Sh.)
1	H/W Karatu	100,800,000	47,583,000	53,217,000
2	H/W Kilindi	7,200,000	4,240,000	2,960,000
3	H/W Kiteto	57,600,000	18,090,000	39,510,000
4	H/W Longido	66,000,000	38,080,000	27,920,000
5	H/WLushoto	85,800,000	52,054,000	33,746,000
6	H/W Mkinga	79,200,000	65,670,000	13,530,000
7	H/M Moshi	86,400,000	53,470,000	32,930,000
8	H/W Mtwara	15,495,000	6,520,000	8,975,000
9	H/W Nanyumbu	79,200,000	85,300,000	-6,100,000
10	*H/W Newala*	72,000,000	63,990,000	8,010,000
11	H/W Ngorongoro	86,400,000	79,200,000	7,200,000
12	H/W Pangani	64,800,000	10,962,000	53,838,000
13	H/W Simanjiro	72,600,000	20,286,600	52,313,400
14	H/W Tandahimba	60,000,000	39,955,000	20,045,000
		933,495,000	**585,400,600**	**348,094,400**

Ninapendekeza kwa Halmashauri husika (a) kufuata maelekezo yaliyotolewa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, (b) kukiri mapokezi ya fedha za posho za wito wa dharura kwa wakati ili kuwezesha malipo kufanyika kwa wakati; na (c) kuhakikisha kuwa fedha zilizopokelewa zinalipwa tu kwa lengo la kutolewa kwake na ikitokea kuwa fedha hizo zimetumika kwa kazi nyingine, inabidi juhudi zifanyike kuhakikisha fedha hizo zinarudishwa mapema iwezekanavyo bila kuathiri huduma za jamii.

5.6.7 Malipo ambayo hayakufanyiwa ukaguzi wa awali Sh.1,205,767,982 na yasiyoidhinishwa Sh.1,122,360,501

Waraka Na. 1(6 vi) wa mwaka 2013 wa Utumishi wa Umma wenye Kumb.Na.CAB.157/547/01/B/144 uliyotolewa tarehe 01/04/2013 unazitaka Halmashauri kuanzisha mifumo bora ya udhibiti wa ndani ikiwemo kufanya ukaguzi wa awali kwa

lengo la kuhakikisha kwamba hati zote za malipo zimeambatishwa na nyaraka husika kabla ya malipo hayo kufanyika. Aidha, Aya 2.4.2 ya Kitabu cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 inamtaka Mkuu wa Idara kuhakiki kazi ya karani na kabla kuidhinisha malipo. Hati za malipo na nyaraka halisi hatimaye zinapitishwa Idara ya fedha ambako ukaguzi wa awali utafanyika kuangalia usahihi na uhalali wa tarakimu kwenye hati ya malipo.

Hata hivyo, mapitio ya malipo yaliyofanyika katika mwaka husika ilibainika kwamba jumla ya Sh.1,122,360,501 zinazohusiana na Halmashauri tisa(9) yalilipwa bila ya idhini sahihi ya maafisa wa Uhasibu au Wakuu wa Idara wakati kwa upande mwingine jumla ya malipo ya Sh.1,205,767,982 yanayohusiana na Halmashauri 14 yalipitishwa kabla ya kupita ukaguzi wa awali. Muhtasari wa Halmashauri kwa mazingira yaliyotajwa hapo juu ni kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Jedwali Na.40: Orodha ya Halmashauri na kiasi kilicholipwa kabla kufanyiwa ukaguzi wa awali na kukosa idhini sahihi ya kufanya malipo

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi ambacho hakikufanyiwa ukaguzi wa awali (Sh.)	Kiasi kilichokosa idhini ya malipo (Sh.)
1	H/W Arusha	414,450,388	318,177,288
2	H/W Bariadi	132,108,000	-
3	H/W Chunya	-	12,619,500
4	H/W Ileje	-	2,165,000
5	H/W Kishapu	25,990,986	-
6	H/W Kiteto	57,880,709	-
7	H/W Kwimba	-	628,421,435
8	H/W Lindi	10,114,400	-
9	H/W Ludewa	20,802,800	-
10	H/W Mafia	48,183,441	-
11	H/W Magu	68,037,341	-
12	H/W Mbeya	13,613,600	-
13	H/W Mbozi	242,726,832	91,984,498
14	H/W Mbulu	8,060,400	-
15	H/W Mpanda	68,505,000	-
16	H/W Mwanga	16,782,000	-
17	H/Jiji Mwanza	-	28,670,000
18	H/W Namtumbo	-	34,816,780
19	H/M Songea	-	2,506,000
20	H/M Sumbawanga	78,512,085	-
21	H/W Tunduru	-	3,000,000
	Jumla	**1,205,767,982**	**1,122,360,501**

Malipo yaliyofanyika bila kupitia ukaguzi wa awali yanabeba hatari ya kutokuwa na viambatisho vya kutosha na idhini isiyofaa. Kwa hali hii, mapungufu katika malipo yanaweza yakapitishwa bila kujua na matokeo yake ni kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Kwa hiyo, inasisitizwa kwa Halmashauri kufuata maelekezo na miongozo katika kuimarisha uangalizi wa ndani ikiwa ni

pamoja na kupitisha kila malipo katika ukaguzi wa awali na kuhakikisha kwamba kila malipo yanaidhinishwa kwa usahihi katika ngazi zote zinazohusika kulingana na mgawanyo wa kazi. Hii ni muhimu katika usimamizi wenye ufanisi wa rasilimali ambazo zimekabidhiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kutoa huduma bora.

5.7 Masuala Mengine

5.7.1 20% fidia ya vyanzo vya ndani vya mapato hazikupelekwa Vijijini Sh.2,445,264,248

Katika mwaka 2004 Serikali ilifuta baadhi ya vyanzo vya mapato ya ndani (baadhi ya kodi) na iliamua kutoa fidia kwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kodi zilizofutwa. Serikali za Mitaa ziliagizwa kuhamisha 20% ikiwa ni fidia ya vyanzo vya ndani vilivyofutwa kutokana na ruzuku zinazotolewa na Serikali Kuu na kupeleka ngazi ya chini kwa ajili kufidia pengo la vyanzo vya mapato vilivyofutwa.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri 50 hazikuwa zimehamisha jumla ya Sh.2,445,264,248 kwenda vijijini kuziba pengo la mapato ya kodi yaliyofutwa. Hii ina maana kwamba shughuli za maendeleo zilizopangwa kutekelezwa katika ngazi ya vijiji hazikuweza kukamilika hivyo imepelekea ucheleweshaji wa kutoa huduma bora kwa jamii iliyokusudiwa. Orodha ya Halmashauri na kiasi kilichohamishwa ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho xxxiii.**

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kuanzisha udhibiti ambao utahakikisha kwamba 20% ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu inahamishwa mara moja kwenda katika ngazi ya Vijiji ili kukamilisha shughuli za maendeleo zilizopangwa.

5.7.2 Ruzuku ya fedha za Mpango wa Maendeleo wa Elimu iliyopokelewa lakini haikuhamishiwa katika Shule husika Sh. 1,356,500,282

Katika kila mwaka, Halmashauri zinapata fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kuzihamisha kwenda katika shule mbalimbali za msingi na sekondari kwa kufuata uwiano ulio sawa. Halmashauri zinatakiwa kupeleka ruzuku katika mashule kulingana na idadi ya wanafunzi ili kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo zilizo katika bajeti ya ruzuku hiyo na masuala mengine ya kiutendaji kama vile ununuzi wa vitabu na vifaa vya kufundishia.

Mapitio ya fedha za ruzuku zilizopokelewa katika mwaka husika, imebainika kuwa Halmashauri 17 zilipata ruzuku yenye jumla ya Sh.1,356,500,282 lakini hazikuweza kuhamisha fedha hizo katika shule husika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi maendeleo na shughuli za uendeshaji. Hivyo hali hiyo imesaababisha fedha hizo kutumika na kuchelewa katika kutoa huduma iliyotarajiwa kwa maendeleo ya shule husika. Pia, ilibainika kuwa katika Halmashauri 7 ruzuku ya kiasi cha Sh.485,135,750 zilitumika katika matumizi ambayo siyo ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu kama vile kulipa posho. **Rejea Kiambatisho xxxiv.**

Menejimenti za Halmashuri husika zinashauriwa kuwa mara zinapopata ruzuku ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu kutoka Hazina, zinatakiwa zipelekewe fedha hizo mashuleni mara moja ili zikatumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

5.7.3 Uhaba wa walimu na miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari

Tangu kuanzishwa kwa shule za sekondari za Kata uandikishaji wa wanafunzi katika Shule za msingi na sekondari umeongezeka. Ongezeko hilo limekuja na mahitaji makubwa ya kuongezeka kwa idadi ya walimu na miundombinu ya shule kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko

la wanafunzi kama vile madarasa, nyumba za walimu , maktaba, zahanati, vyoo, Ofisi za utawala, mabweni, madawati, viti, meza, na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunza. Kutokuwa na idadi ya walimu wa kutosha katika shule pamoja na miundombinu mingine kunaathiri kwa kiasi kikubwa shule mafanikio ya wanafunzi na utendaji bora katika shule za umma.

Mapitio ya utendaji wa elimu katika shule za msingi na sekondari yamebainisha kuwa Halmashauri 54 hazikuwa na miundombinu ya kutosha katika shule za msingi na sekondari. Pia, ukaguzi ulibainisha kuwa shule za msingi na sekondari zina upungufu wa walimu hali ambayo huathiri sana ubora wa elimu. Tatizo hili limesababisha na kushindwa kufikia lengo la kitaifa la uwiano wa 1:45 (wanafunzi 45 kwa mwalimu). Mwenendo unaonesha kwamba wengi wa walimu hawafiki katika vituo vyao vya kazi wanapoajiriwa haswa wanaopangwa katika vijiji kutokana na miundombinu duni iliyopo katika vijiji. **Rejea Kiambatanisho (xxxv).**

Zaidi ya hayo, nimebaini kuwa utendaji wa wanafunzi katika Shule za Sekondari za Serikali unapungua mwaka hadi mwaka. Ukaguzi umebainisha kuwa uwezo wa wanafunzi kufaulu au kufanya vizuri kwenye mitihani yao kumaliza kidato cha nne na sita unapungua kila mwaka.

Hii ina maana kwamba uhaba wa vifaa vya shule na walimu ni changamoto kubwa inayoikabili sekta ya elimu katika Halmashauri. Ukosefu wa miundombinu katika shule unaweza kuendelea kuathiri utendaji wa elimu katika shule za msingi na sekondari.

Ninapendekeza kwamba, Menejimenti za Halmashauri zianzishe mikakati ya kuboresha miundombinu ya shule kwa kuongeza na kuimarisha ubora wa elimu. Pia, kutenga fedha zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya shule na kufanya usimamizi wa karibu ambao utawezesha wanafunzi kufanya vizuri zaidi.

5.7.4 Wadaiwa wa Halmashauri na Malipo yaliyolipwa kabla ya huduma kutolewa na Wadai wa Halmashauri

Sehemu kubwa ya wadaiwa katika Halmashauri ni pamoja na; malipo mbalimbali kabla ya huduma kutolewa, madai kutoka kwa mawakala wa kukusanya mapato, madurufu na masurufu kwa watumishi pamoja mikopo kwa Wanawake na Vijana.

Ni muhimu kudumisha sifa nzuri na maelewano kati ya Halmashauri na wazabuni kwa kulipa madai yao kwa wakati ili kujenga imani kwa jamii inazozihudumia.

Mapitio ya taarifa za fedha pamoja na viambatanisho vyake katika mwaka 2012/2013 yamebaini kwamba kuna wadaiwa na wadai katika Halmashauri 140 ya kiasi cha Sh.72,267,554,838 na Sh.104,282,263,060 ambao walikuwa bado kulipa madeni yao kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho xxxvi.**

Halmashauri ambazo zina kiasi kikubwa cha madeni ni Halmashauri ya Ilala ambayo inadaiwa Sh.9,209,068,088, Halmashauri ya Temeke inadaiwa Sh.4,019,008,196, Halmashauri ya Jiji la Mwanza inadaiwa Sh.3,601,987,028 na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inadaiwa Sh.2,588,802,730.

Mwenendo wa Wadaiwa na Wadai kwa miaka ya fedha 2007/2008 hadi 2012/2013 ni kama inavyoonekana katika Chati muhimili hapa chini :



Mwenendo huo hapo juu unaonesha kwamba, wadaiwa wamepungua kutoka mwaka wa fedha 2009/10 hadi mwaka 2010/11 kwa kiasi cha Sh.6,263,356,678 sawa na 16% na kisha kuongezeka kwa Sh.10,647,428,766 na Sh.23,824,135,208 katika mwaka 2011/12 na 2012/13 kwa mtiririko huo. Wadaiwa huathiri kiwango cha mtaji wa Halmashauri na hatimaye kudhoofisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika wakati uliopangwa kutokana na matatizo ya ukwasi.

Pia kuna ongezeko kubwa la kiasi cha wadai kwa Sh.42,089,291,652 sawa na 40% kutoka mwaka 2011/2012 hadi 2012/13.

Ninapendekeza kwa Halmashauri husika kulipa wadai wao mara moja wakati wa kulipa ukifika, kuweka udhibiti wa kutosha, sera na taratibu ili kuhakikisha kwamba, Menejimenti ya Halmashauri zinawajibika kwa ajili ya ahadi yoyote iliyoiweka.

SURA YA SITA

6.0 Ukaguzi wa Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo (LGDG)

Serikali za Mitaa hutekeleza miradi yake kwa fedha za ruzuku ya miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu na wahisani pamoja na fedha zitokanazo na mapato ya ndani.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, nilifanya tathmini ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya LGDG ambapo jumla ya Sh.137,113,787,841 zilipokelewa. Miradi mingine iliyofadhiliwa ni NMSF, CHF, CDCF, MMEM, MMES EGPAF, TSCP na PFM. Aidha, Serikali za mitaa hupokea pia ruzuku kwa ajili ya uboreshaji wa huduma na miradi ya kijamii kupitia Mfuko wa Jamii (TASAF), Mfuko wa Pamoja wa Afya (HBF), Program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) na Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP). Matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo yametolewa ripoti kwa kila Halmashauri na katika Ripoti Kuu ya Miradi. Yafuatayo ni maelezo kwa undani juu ya miradi hiyo:

6.1 Ruzuku ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa hufadhiliwa na Serikali ya Tanzania pamoja na nchi wahisani ambao ni Ujerumani KFW, Uholanzi, na Cooperation Tech Belgium kupitia Benki Kuu ya Tanzania Holding Akaunti Na.9931206651.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, programu hii ya LGDG ilikuwa na jumla ya Dola za Kimarekani (USD) 19,750,976 ikiwa ni sawa na Sh.32,271,370,132 ikihusisha salio anzia la Dola za Kimarekani 139,042.49 sawa na Sh.227,183,290 ambazo zilichangiwa na Washirika wa Maendeleo. Aidha, kulikuwa na mchango wa Serikali ya Tanzania wa kiasi cha Sh.107,069,897,000 ambayo ilifanya jumla kuu kuwa Sh.139,341,267,132 kwa ajili ya utekelezaji

wa shughuli za LGDG zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2012/13. Katika mwaka huu wa ukaguzi, jumla ya Dola za Kimarekani 19,743,797 sawa na Sh.32,259,640,338 zilihamishwa kupelekwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Uchambuzi wa fedha zilizokuwepo kwa kipindi cha mwaka kutoka kwa washirika wa maendeleo umeoneshwa katika jedwa Na.41.

Jedwali Na. 41: Orodha ya Wahisani wa Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Na.	Mshirika wa Maendeleo	Kiasi (USD)	Kiasi (Sh.)
Salio anzia 1 Julai, 2012		139,043.49	227,183,290
1	KFW	6,621,779.00	10,819,408,804.69
2	Netherlands	3,926,551.80	6,415,641,219.32
3	Cooperation Tech. Belgium	9,063,603.47	14,809,136,817.40
	Jumla	**19,750,976.76**	**32,271,370,131.41**

Aidha, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kama dirisha dogo chini ya mfumo wa LGDG ulipokea jumla ya Sh.10,182,000,000 kutoka Serikali ya Tanzania na Sh.15,047,000,000 ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo katika miradi ya MMAM.

6.1.1 Kutokutolewa kwa fedha za LGDG Sh.100,664,000,000

Mapitio ya fedha za LGDG yalionesha kutokutolewa kwa fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya LGDG kama ilivyokuwa imekasimiwa.

Jedwali Na.42: Mapokezi ya fedha za LGDG katika Serikali za Mitaa

Na.	Chanzo cha fedha	Kiwango kilichotengwa (Sh.)	Jumla ya fedha zilizotolewa (Sh.)	Kiasi kisichotolewa (Sh.)	% ya matoleo pungufu
1	CDG	200,202,000,000	138,289,000,000	61,913,000,000	30.93
2	CBG	5,544,000,000	0	5,544,000,000	100
3	RWSSP	40,900,000,000	38,997,000,000	1,903,000,000	4.65
4	ASDP	39,278,000,000	19,745,000,000	19,533,000,000	49.73
5	MMAM	37,000,000,000	25,229,000,000	11,771,000,000	31.81
	Jumla	**322,924,000,000**	**222,260,000,000**	**100,664,000,000**	**31.17**

Kutokutolewa kwa Sh.100,664,000,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kunamaanisha kutokutekelezwa kwa shughuli zenye kiwango hicho zilizoidhinishwa chini ya mpango wa LGDG na hivyo jamii ilishinda kupata manufaa yatokanayo miradi hiyo.

6.1.2 Fedha zisizotumika mwishoni mwa mwaka Sh.38,615,006,253

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, OWM-TAMISEMI kupitia Wizara ya Fedha ilipeleka jumla ya Sh.138,289,000,000 kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Hata hivyo, ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo katika Halmashauri 99 ulibaini kubaki kwa kiasi cha Sh.38,615,006,253 za LGDG ambazo hazikutumika hadi ilipofika tarehe 30 Juni, 2013 kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xxxvii).**

Hii inamaanisha kuwa shughuli zilizoidhinishwa kutekelezwa hazikukamilika kama ilivyopangwa na hivyo kupelekea kutofikiwa kwa malengo yaliyotarajiwa.

Jedwali Na.43: Mwenendo wa fedha zisizotumika kwa miaka miwili.

Mwaka	Fedha isiyotumika (Sh.)	Idadi ya halmashauri	Wastani wa bakaa kwa Halmashauri (Sh.)
2012/2013	38,615,006,253	99	390,050,568
2011/2012	14,295,289,503	74	193,179,588

Jedwali Na.43 linaonesha kupanda kwa wastani wa bakaa ya kiasi cha Sh.196,870,980 sawa na 102% kutoka mwaka 2011/12 kwenda 2012/13.

Kuwepo kwa kiasi kikubwa kisichotumika cha Sh.38,615,006,253 inamaanisha kuwa shughuli zilizoidhinishwa hazikutekelezwa kwa ukamilifu hivyo jamii iliyolengwa kukosa huduma zilizotarajiwa kwa wakati.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuongeza juhudi katika kutumia fedha zinazopokelewa kutoka Hazina ili kutekeleza shughuli zilizopangwa katika Halmashauri kwa wakati.

6.1.3 Halmashauri kutochangia asilimia 5% ya fedha ya ruzuku kutoka mapato ya ndani kwenye miradi ya LGCDG Sh.756,375,388

Mwongozo wa matumizi na uendeshaji wa Fedha za Ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa aya ya 3.3 (ukurasa wa 17) toleo la 1 Julai 2005 unazitaka Halmashauri kuchangia si chini ya asilimia tano ya fedha za ruzuku zilizopokelewa. Utaratibu huu ulianzishwa kwa sababu zifuatazo:

- Kuzijengea Halmashauri uwezo katika umiliki na uwekezaji katika miradi.

- Kuweza kuoanisha matumizi na faida itokanayo na matumizi hayo katika huduma zitolewazo na Halmashauri.
- Kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakuwa endelevu.
- Kuboresha motisha katika kuongeza makusanyo ya maduhuli kutoka vyanzo vya ndani.
- Kuwezesha Halmashauri kuwa makini katika uwekezaji na utekelezaji wa miradi.

Hata hivyo, Halmashauri zifuatazo hazikuweza kukidhi masharti ya kuchangia fedha kama ifuatavyo:

Jedwali Na.44: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuchangia 5% ya fedha za ruzuku toka na mapato ya ndani

Na.	Halmashauri	Fedha ambazo hazikulipwa (Sh.)
1	H/W Kibondo	87,589,225
2	H/W Iramba	99,333,375
3	H/W Kigoma	57,397,083
4	H/W Korogwe	48,623,785
5	H/W Pangani	9,011,570
6	H/M Bukoba	112,233,025
7	H/Jiji Mwanza	342,187,325
	Jumla	**756,375,388**

Hali hii ya kutochangia asilima tano inakwamisha utekelezaji wa miradi katika ngazi za chini za serikali.

Halmashauri zinashauriwa kuwa zinachangia asilimia tano ya ruzuku iliyopokelewa ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

6.1.4 Malipo yasiyo na viambatanisho Sh.700,562,352

Ukaguzi wa hati za malipo unaohusu fedha za LGCDG katika Halmashauri 11 ulionesha kuwa, matumizi ya jumla ya Sh.700,562,352 yalifanyika bila kuwa na viambatanisho vya kutosha kinyume na Agizo la 8 (2) (a) la LGFM ya mwaka 2009. Kukosekana kwa viambatanisho katika malipo kunasababisha ukaguzi kushindwa kuhakiki uhalali wa malipo yaliyofanywa. Jedwali Na.45 linaonesha orodha ya Halmashauri na kiasi kilisichokuwa na viambatanisho:

Jedwali Na.45: Malipo yasiyo na viambatanisho Sh.700,562,352

Na.	Jina la Halmashauri	Chanzo cha fedha	Kiasi kisicho na viambatanisho (Sh.)
1.	H/W Meru	CHF	9,000,000
2.	H/W Njombe	PFM	2,850,000
		NMSF	37,600,000
3.	H/W Rufiji	NMSF	1,037,000
4.	H/Jiji Tanga	TSCP	7,900,000
6.	H/Jiji Bukombe	CDG	256,094,860
		PEDP	76,585,157
7.	H/W Geita	CDG	14,890,000
8.	H/W Musoma	PEDP	9,585,314
		NMSF	78,308,000
9.	H/W Kwimba	PEDP	11,363,634
		SEDP	178,286,387
10.	H/W Magu	CDG	5,070,000
11.	H/W Ukerewe	NMSF	11,992,000
Jumla			**700,562,352**

Aidha, Kanuni ya 68(4) ya Kanuni za Manunuzi za mwaka 2005 zinataka kuwepo kwa walau nukuu za bei tatu kutoka kwa wazabuni. Hata hivyo, kinyume na kanuni hii Halmashauri 3 zilinunua bidhaa zenye thamani ya

Sh.42,521,680 bila kuwa nukuu za bei kama ivyoonekana hapo chini.

Jedwali Na.46: Manunuzi ya bidhaa bila kuwa na nukuu za bei

S/N	Jina la Halmashauri	Chanzo cha fedha	Thamani ya bidhaa (Sh.)
1	H/W Lushoto	MMAM	3,522,680
2	H/W Tarime	CDCF	20,000,000
3	H/Mji Njombe	CDG	18,999,000
Jumla			**42,521,680**

Halmashauri zinatakiwa kuboresha mfumo wa utunzaji kumbukumbu kwa kuhakikisha kuwa nyaraka za malipo zimehakikiwa vizuri kabla malipo hayajafanyika na kisha kumbukumbu hizo zitunzwe vizuri. Pia, katika kila mchakato wa manunuzi ya bidhaa nukuu za bei zinapaswa kupatikana kutoka kwa wazabuni ili kupata bei nafuu ya bidhaa zinazonunuliwa.

6.1.5 Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM)

Lengo la mpango huu ni kuharakisha utoaji wa huduma bora ya Afya ya Msingi, kuimarisha mifumo ya afya, ukarabati wa miundo mbinu, kuendeleza rasilimali watu, kuimarisha mifumo ya rufaa, kuongeza uwezo kifedha na kuboresha utoaji wa dawa na vifaa tiba.

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2013 jumla ya Sh.25,229,000,000 zilipelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Yafuatayo yalikuwa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi:

6.1.5.1 Fedha ambazo hazikutumika Sh.10,975,907,846

Katika ukaguzi wa mwaka 2012/13 wa mapokezi na matumizi ya fedha ya MMAM, ilibainika kuwa jumla ya

Sh.10,975,907,846 katika Halmashauri 81 zilibaki bila kutumika mwishoni mwa mwaka wa fedha kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xxxviii).** Jedwali Na.47 hapo chini linaonesha wastani wa fedha ambazo hazikutumika kwa miaka mitatu mfululizo.

Jedwali Na.47: Mwenendo wa fedha zisizotumika kwa miaka mitatu

Mwaka	Kiasi cha fedha kisichotumika (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zilizohusika	Wastani wa bakaa kwa Halmashauri (Sh.)
2012/2013	10,975,907,846	81	135,505,035
2011/2012	2,586,057,984	32	80,814,312
2010/2011	5,848,929,864	48	121,852,706

Jedwali hilo hapo juu linaonesha kupungua kwa wastani wa fedha zilizobaki mwishoni mwa mwaka 2010/11 kwa Sh.41,038,394 sawa na 34% na kuongezeka kwa Sh.54,690,723 sawa na 68% ikimaanisha hali haijaboreshwa katika kutumia fedha zinazotolewa katika mwaka husika.

Kubaki kwa kiasi cha Sh.10,975,907,846 ambacho ni kikubwa katika mwaka wa fedha ina maanisha kuwa miradi iliyoidhinishwa kutekelezwa katika mwaka husika haikukamilika na hivyo kusababisha jamii kutofaidika kikamilifu.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuongeza uwezo wa kutumia fedha zilizopokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii.

6.2 Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo Na. 16 ya mwaka 2009 kwa ajili ya miradi ya mandeleo katika majimbo.Yafuatayo ni masuala yaliyoonekana kupitia ukaguzi juu ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za mfuko wa Jimbo:

6.2.1 Fedha za Mfuko wa Jimbo ambazo hazikutumika Sh.2,591,012,939

Mapitio ya taarifa za benki na ripoti ya usuluhisho wa benki kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013 ilionekana kuwepo kwa kiasi cha Sh.2,591,012,939 katika Halmashauri 66 za Mfuko wa Jimbo ambazo zilikuwa bado kutumika. Hii imesababishwa na usimamizi hafifu wa Kamati za Mfuko wa Jimbo.

Kushindwa kutumia fedha zinazopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa wakati inapelekea jamii kukosa kunufaika na Mfuko huo na hivyo malengo yaliyokusudiwa hayakutimia. Kwa orodha ya Halmashauri na viwango vilivyobaki angalia **Kiambatisho (xxxix)**

Jedwali Na.48: Mwenendo wa fedha za CDCF ambazo hazikutumika

Mwaka	Fedha ambayo haikutumika (Sh.)	Idadi ya Halmashauri	Wastani wa bakaa kwa Halmashauri (Sh.)
2012/2013	2,591,012,939	66	39,257,772
2011/2012	2,561,822,820	69	37,127,867
2010/2011	2,683,368,422	51	52,615,067

Jedwali hilo hapo juu linaonesha kupungua kwa wastani wa bakaa ya Sh.15,487,200 sawa na 29% kutoka mwaka 2010/11 na 2011/12 na kupanda kwa Sh.2,129,905 sawa na 6% kwa mwaka 2011/12 na 2012/2013.

Kiwango cha Sh.2,591,012,939 kilichobaki mwishoni mwa mwaka ni kiwango kikubwa kinachomaanisha kuwa miradi mingi inayofadhiliwa na Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo haikutekelezwa kwa wakati na hivyo kuinyima jamii faida ya miradi hiyo.

Halmashauri zinashauriwa kuongeza uwezo wa kutumia fedha zote katika mwaka husika ili kuwezesha utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

6.2.2 Kutoandaliwa kwa taarifa za CDCF na kuziwasilisha OWM-TAMISEMI

Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuandaa taarifa na kuziwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kinyume na matakwa ya kifungu 7(3) ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009.

Inashauriwa kwamba, OWM-TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya mwaka unaofuata hazitolewi kama Halmsahauri husika haijawasilisha taarifa ya mapato na matumizi kama inavyotakiwa na sheria. Katika mwaka huu wa fedha inaonekana kuwa Halmashauri 12 hazikuandaa taarifa na kuziwasilisha OWM-TAMISEMI kama ifuatavyo:

Jedwali Na.49: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuandaa taarifa na kuziwasilisha OWM-TAMISEMI

Na.	Jina la Halmashauri
1	H/W Kahama
2	H/W Ileje
3	H/W Ludewa

4	H/W Pangani
5	H/W Handeni
6	H/W Sikonge
7	H/W Karagwe
8	H/W Tabora
9	H/W Kibondo
10	H/W Mbozi
11	H/W Iringa
12	H/M Ilemela

6.2.3 Miradi ya CDCF ambayo haikuibuliwa na Wananchi Sh.195,599,000

Kifungu cha 12 cha sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 kinaeleza kuwa, orodha ya miradi inayoweza kutekelezwa na Mfuko inatakiwa kuibuliwa na wananchi wanaoishi katika Jimbo husika. Pia, kifungu cha 10(4) kinaitaka kila Kata kuja na miradi inayopewa kipaumbele na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kuidhinisha au kutoidhinisha miradi hiyo:

Tofauti na matakwa ya vifungu hivyo, miradi yenye thamani ya Sh.195,599,000 iliyotekelezwa katika Halmashauri 50 zilizoorodheshwa hapa chini haikuwa na ushahidi kwamba wananchi walihusika katika kuiibua.

Jedwali Na.50: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuibua Miradi ya CDCF

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Iramba	62,250,000
2	H/W Chato	21,600,000
3	H/W Handeni	32,715,000
4	H/W Sengerema	12,834,000
5	H/W Lushoto	9,200,000
6	H/W Tabora	57,000,000
	Jumla	**195,599,000**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo inatakiwa kuidhinisha na kupeleka fedha kwenye miradi iliyoibuliwa na wananchi tu.

Pia, kifungu cha 19 (2) cha sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 kinaeleza kuwa, miradi yote itakuwa ya Maendeleo na inaweza kuhusisha gharama za masomo, mipango na ubunifu au nyenzo zozote za kiufundi kwa ajili ya miradi lakini haihusishi gharama za matumizi ya kawaida ya mradi.

Lakini kinyume na matwaka ya sheria hiyo, Halmashauri za Wilaya tatu zilitumia jumla ya Sh.19,994,660 kugharimia posho za kujikimu nje ya kituo cha kazi na posho za vikao na gharama za kusafiri (nauli) kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na.51: Orodha ya Halmashauri zilizotumia fedha za CDCF kwa matumizi ya kawaida

Na.	Jina la Halmashauri	Malipo yaliyofanywa	Kiasi kilicholipwa (Sh.)
1	H/W Ludewa	Ununuzi wa mafuta kwa magari binafisi	3,421,660
2	H/W Urambo	Posho za safari kwa ajili ya usimamizi wa miradi na posho za vikao.	12,845,000
3	H/W Kondoa	Posho za vikao, nauli, chakula na vinywaji wakati wa mikutano ya kamati za CDCF.	3,728,000
Jumla			**19,994,660**

Nashauri kamati za Mfuko wa Jimbo kuzingatia matakwa ya sheria ya Mfuko huo.

6.3 Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuthibiti UKIMWI (NMSF) 2008-2012 (NMSF)/TACAIDS

Tarehe 1 Desemba 2000 Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza kuundwa kwa Tume ya Kuthibiti Ukimwi. Aidha, Bunge nalo lilitunga sheria Na.22 ya 2001 kwa ajili ya kuipa Tume nguvu ya kisheria, kutoa uongozi wa kimkakati, kuratibu na kuimarisha juhudi za wadau wote wanaojihusisha na kupambana na UKIMWI.

Katika ukaguzi huu mapungufu yafuatayo yalionekana:

6.3.1 Fedha za UKIMWI ambazo hazikutumika Sh.2,333,558,283

Katika mwaka huu wa ukaguzi, TACAIDS kupitia Wizara ya Fedha walipeleka fedha kwenye Halmashauri kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuthibiti UKIMWI (NMSF) 2008-2012 ambao wafadhili wake wakuu ni Serikali ya Marekani kupitia USAID, PEPFAR, Wafadhili mbalimbali na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia MTEF. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika wa matumizi ya fedha zilizopokelewa katika Halmashauri 58 zilizochaguliwa ulibaini kuwepo kwa fedha mwishoni mwa mwaka ambazo zilikuwa hazijatumika kiasi cha Sh.2,333,558,283.

Kuwepo kwa kiasi kikubwa kisichotumika mwishoni mwa mwaka kinazuia kutekelezwa kwa shughuli za afya katika Halmashauri husika. Orodha ya Halmashauri na viwango vya fedha ziliyobaki vimeoneshwa katika **kiambatisho (xl)**.

Jedwali lifuatalo hapa chini linaonesha mwenendo wa fedha zinazobaki bila kutumika kwa miaka mitatu mfululizo.

Jedwali Na.52: Mlinganisho wa wastani wa bakaa za fedha za NMSF kwa miaka mitatu

Mwaka	Kiasi kilichobaki (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zilizohusika	Wastani wa kiasi kilichobaki kwa Halmashauri (Sh.)
2012/13	2,333,558,283	58	40,233,764
2011/12	1,545,629,527	59	26,197,111
2010/11	1,104,364,692	41	26,935,724

Jedwali hilo hapo juu linaonesha kupungua kwa wastani wa kiwango cha fedha zilizobaki mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/12 ukilinganisha na mwaka 2010/11 kwa Sh.738,614 ikiwa ni sawa na 3% wakati kuna wastani wa ongezeko la Sh.14,036,653 ikiwa ni sawa na 54% katika mwaka 2012/2013. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuongeza uwezo wa kutumia fedha zote zinazopokelewa kwa ajili ya utekelezeji wa shughuli za UKIMWI katika mwaka husika.

6.4.0 Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF)

Mfuko wa Afya wa Jamii CHF) ulianzishwa mwaka 1997 ikiwa ni kati ya vyanzo vilivotambuliwa na Serikali kwa kuhamasisha jamii kuchangia huduma katika Sekta ya afya Tanzania.

Ukusanyaji na matumizi ya fedha za mfuko huu imeelezwa vizuri katika waraka Na.2 wa 1997 uliotolewa na Wizara ya Afya ambao ulitoa mwongozo kuwa fedha hizo zitatumika kwa shughuli zilizoidhinishwa ikiwa ni pamoja na gharama za madawa, vifaa tiba, ukarabati mdogo wa majengo, mafuta na posho za kujikimu kwa watoa huduma ya afya. Waraka huo unataka manunuzi ya madawa na vifaa tiba kufanywa kutoka wa wazabuni walioidhinishwa.

Wakati wa ukaguzi yafuatayo yalionekana:-

6.4.1 Bakaa ya fedha za CHF isiyotumika Sh.2,070,366,726

Kupitia taarifa za benki na vitabu vya Halmashauri 46 ilionekana kuwa kiasi cha fedha zilizokusanywa kwa mwaka cha Sh.2,070,366,726 hazikutumika kwa kutekeleza shughuli zilizoidhinishwa chini ya Mfuko wa Afya wa Jamii.

Kiasi hiki cha Sh.2,070,366,726 kilichobaki ni kikubwa mno na kinakwamisha huduma za afya ziliyotarajiwa kupatikana kutokana na matumizi ya fedha hiyo. Taarifa nyingine zaidi zimeoneshwa katika **Kiambatisho xli.**

Jedwali Na.53: Mwenendo wa bakaa za fedha za CHF kwa miaka mitatu mfululizo

Mwaka wa fedha	Bakaa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zilizohusika	Wastani wa bakaa kwa Halmashauri
2012/2013	2,070,366,726	46	45,007,972
2011/2012	1,709,747,559	38	44,993,357
2010/2011	2,963,900,725	33	89,815,173

Jedwali hilo hapo juu linaonesha kupungua kwa wastani wa fedha zinazobaki bila kutumika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kiasi cha Sh.44,821,817 sawa na 50% kutoka mwaka 2010/2011 mpaka 2011/2012 na ongezeko la Sh.14,615 sawa na 0.03% kutoka mwaka 2011/2012 mpaka 2012/2013. Hii inamaanisha kuwa Halmashauri hazijaimarisha utumiaji wa fedha zinazokusanywa kwa shughuli za CHF.

Halmashauri zinatakiwa kuongeza juhudi zaidi katika katika kuhakikisha kuwa fedha zinazokusanywa katika mwaka husika zinatumika ili kuwezesha utoaji wa huduma bora ya afya katika Halmashauri.

6.4.2 Matumizi yaliyofanyika kinyume na Miongozo ya Mfuko wa Afya wa Jamii CHF ya kiasi cha Sh.149,411,700

Mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) wa Juni, 1999 unaelezea kuwa fedha za CHF zitatumika kwa matumizi yanayohusiana na shughuli za afya. Matumizi kwa huduma na bidhaa zinazohusiana na afya zinazoruhusiwa katika mpango huu ni pamoja na ununuzi wa madawa, vifaa tiba, ukarabati wa miundombinu ya afya, ununuzi wa thamani za vituo vya huduma vya afya na bidhaa nyingine zinazotumika katika vituo hivyo, sare za wauguzi, posho kwa wataalam na watoa huduma wanapokuwa zamu, posho za safari kwa wataalam wa afya wanapokuwa katika shughuli za afya kama zilivyopangwa katika mpango wa afya wa Kata.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi ilionekana kuwa, kiasi cha Sh.149,411,700 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa saba (7) zilitumika kinyume na mwongozo wa Mfuko huu. Matumizi hayo yalikuwa kwa ajili ya kulipa mishahara, posho, ununuzi wa madawati ya shule za msingi na matumizi mengine ya kiutawala. Hadi wakati wa ukaguzi, fedha hizi zilikuwa bado hazijarejeshwa katika Mfuko wa Afya wa Jamii.

Jedwali 54: Malipo yaliyofanya kinyume na miongozo ya CHF

Na.	Jina la Halmashauri	Maelezo ya Malipo	Kiasi (Sh.)
1	H/W Meru	Malipo yalifanywa kugharimia shughuli za utawala.	9,000,000
2	H/W Mbozi	Ununuzi wa madawati ya shule za misingi.	6,000,000
3	H/W Mwanga	Posho ya walinzi	17,430,000
4	H/W Pangani	Malipo yaliyofanywa kwa shughuli za mfuko wa pamoja wa afya na UKIMWI.	21,416,300

5	H/W Bariadi	Ununuzi wa jokofu la chumba cha kuhifadhia maiti.	44,000,000
6	H/W Lushoto	Malipo yaliyofanywa kwa shughuli za mfuko wa pamoja wa afya.	33,980,000
7	H/Jiji Mwanza	Malipo yaliyofanyika kwa mtu asiyejulikana.	17,585,400
		Jumla	**149,411,700**

Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha kuwa zinatumia fedha za mfuko wa CHF kwa shughuli zilizoidhinishwa na mwongozo Na.2 wa mwaka 1997 uliotolewa na Wizara ya Afya.

6.4.3 Madai ambayo hayajalipwa na Bima ya Afya Sh.198,356,656

Ukaguzi uliofanyika kuangalia uendeshaji na uzingatiaji wa miongozo ya Mfuko wa Afya ya Jamii, ulionesha kuwa kiasi cha Sh.198,356,656 kiliombwa kutoka Bima ya Afya kama marejesho kwa ajili ya huduma za afya zilizotolewa kwa wanachama wa Mfuko ambao pia ni wanachama wa Bima ya Afya.

Bima ya Afya kutorejesha fedha kwa Halmashauri kunazuia juhudi za Serikali kuimarisha huduma endelevu za afya katika Halmashauri.

Jedwali Na. 55: Orodha ya Halmashauri zilizokuwa zinaidai Bima ya Afya

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Serengeti	14,230,454
2	H/W Bunda	14,940,000
3	H/W Singida	10,171,000
4	H/W Manyoni	6,750,655
5	H/W Kilosa	61,180,300
6	H/W Korogwe	19,630,000
7	H/W Mbarali	45,875,000
8	H/W Mpanda	23,560,405
9	H/M Shinyanga	2,018,842
Jumla		**198,356,656**

Zaidi ya hayo, kwa mwaka 2012/2013 inaonesha kuwa katika Halmashauri tatu (3) jumla ya Sh.41,297,424 zilikusanywa kwa ajili ya shughuli za CHF, lakini Halmashauri hazikuandaa taarifa na kuzituma NHIF kwa ajili ya kupewa kiasi sawa na walichokusanya na hivyo kupelekea hasara ya Sh.41,297,424 kama inavyooneshwa hapa chini:-

Jedwali Na.55: Fedha ambazo hazikuombwa toka NHIF

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Manyoni	10,375,000
2	H/W Kisarawe	10,231,305
3	H/W Morogoro	20,691,119
Jumla		**41,297,424**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa madeni yaliyoko Bima ya Afya.

6.5 Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana

Katika mwaka 1993 Serikali ya Tanzania ilianzisha Mfuko wa Wanawake kwa Azimio la Bunge kwa mujibu wa "Exchequer and Audit Ordinance" ya mwaka 1961. Lengo la mfuko huu ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wenye kipato cha chini ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na hivyo kuboresha kiwango cha maisha ya familia zao. Yafuatayo yalijitokeza katika ukaguzi wa mfuko huu.

6.5.1 Fedha ambazo hazikupelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana Sh.10,905,858,533

Wakati wa ukaguzi wa utendaji kazi wa Mfuko wa Wanawake na Vijana ilionekana kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 68 kwa kushirikiana na Serikali Kuu hazikupeleka kiasi cha Sh.10,905,858 na hivyo kukwamisha malengo ya mfuko huo. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikuchangia katika mfuko huo zimeoneshwa katika **Kiambatisho (xlii).**

Jedwali Na.57: linaonesha jumla ya fedha ambazo hazikupelekwa kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa miaka mitatu mfululizo na wastani kwa kila Halmashauri.

Jedwali Na.57: Mwenendo wa fedha zisizopelekwa kwenye mfuko wa Wanawake na Vijana

Mwaka	Kiasi kisichopelekwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri	Wastani wa fedha zisizopelekwa kwa kila Halmashauri (Sh.)
2012/2013	10,905,858,533	68	160,380,273
2011/2012	511,761,787	31	16,508,445
2010/2011	1,587,780,350	23	69,033,928

Wastani wa fedha kutopelekwa katika Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa Halmashauri umeongezeka kwa Sh.143,871,828 sawa na asilimia 87.2% ukilinganisha na

mwaka uliopita. Kwa hiyo, inaonesha kuwa Halmashauri hazipeleki fedha kuchangia Mfuko wa Wanawake na Vijana na hivyo kupelekea malengo ya uanzishwaji wa Mfuko huo kutofanikiwa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweke mpango mkakati wa kupeleka fedha ambazo zilikuwa hazijapelekwa kwenye vikundi vya wanawake na vijana ili kuviwezesha kujiendesha na kumudu maisha na kutekeleza madhumuni ya kuanzishwa kwa mifuko hiyo.

6.5.2 Mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya kinamama na vijana bado kurejeshwa Sh.1,389,192,866

Ukaguzi wa mikataba ya mikopo na nyaraka za urejeshaji mikopo katika Halmashauri 58, ulionesha kuwa na kiasi cha Sh.1,389,192,866 ikiwa ni mikopo iliyotolewa kwa vikundi mbalimbali vikiwa bado hakijarejeshwa ingawa muda wa marejesho ulikuwa tayari umeshapita. Orodha ya Halmashauri ambazo mikopo haijarejeshwa zimeoneshwa katika **kiambatisho (xliii).**

Hii inaonesha na usimamizi usioridhisha katika ukusanyaji madeni hivyo kupelekea Halmashauri kutokuwa na uwezo wa kuendelea kutoa mikopo zaidi kwa watu au vikundi vingine.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kujipanga zaidi katika kukusanaya madeni hayo kutoka kwa vikundi vya akina mama na vijana ili fedha za Mfuko huo ziweze kunufaisha makundi mengine.

6.6 Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)

Serikali ya Tazanzania ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi mwaka 2001 ili kutoa elimu bure na bora kwa shule za Msingi. Msisitizo hapa ilikuwa ni kuongeza ubora wa elimu katika maeneo yafuatayo: kuongeza idadi ya

watoto wanaodahiliwa katika shule za Msingi, kujenga uwezo na kujipanga kitaasisi. MMEM ni moja ya matokeo ya Programu ya Mafanikio ya Maendeleo ya Elimu Tanzania. Wakati wa ukaguzi yafuatayo yaonekana:-

6.6.1 Bakaa ya Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) Sh.1,138,230,899

Ukaguzi wa mapato na matumizi ya Fedha za MMEM zilizopokelewa na Halmashauri kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa elimu na kuhakikisha wanafunzi hawaachi shule, inaonesha kuwa Halmashauri 13 zilibaki na bakaa ya Sh.1,138,230,899 kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:

Jedwali Na.58: Orodha ya Halmashauri zenye fedha za MMEM ambazo hazikutumika

Na.	Halmashauri	Fedha iliyopo (Sh.)	Fedha iliyotumika (Sh.)	Bakaa (Sh.)	% ya bakaa
1	H/W Monduli	11,363,636	-	11,363,636	100
2	H/W Kibaha	52,200,646	31,147,366	21,053,280	40
3	H/Mji Kibaha	104,683,553	101,493,636	3,189,917	3
4	H/W Mkuranga	411,505,805	379,395,087	32,110,718	8
5	H/W Karagwe	284,882,973	78,182,000	206,700,973	73
6	H/W Kilwa	722,423,844	438,789,478	283,634,366	39
7	H/W Nachingwea	268,000,219	249,269,699	18,730,520	7
8	H/W Rungwe	607,093,722	597,331,000	9,762,722	2
9	H/W Morogoro	11,363,636	8,086,136	3,277,500	29
10	H/W Misungwi	199,618,723	-	199,618,723	100
11	H/W Korogwe	1,104,808,070	808,700,777	296,107,293	27
12	H/W Kilindi	287,906,901	270,953,500	16,953,401	6
13	H/W Biharamulo	381,423,758	345,695,906	35,727,852	9
Jumla		**4,447,275,484**	**3,309,044,586**	**1,138,230,899**	**26**

Jedwali lifuatalo hapa chini linalinganisha bakaa ya Mwaka 2011/12 na ya mwaka 2012/13.

Jedwali Na.59: Mwenendo wa fedha za MMEM ambazo hazijatumika

Mwaka	Bakaa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri	Wastani wa bakaa kwa halmashauri (Sh.)
2012/13	1,138,230,899	26	87,556,223
2011/12	305,361,658	13	61,072,332

Kutokana na jedwali hilo hapo juu, inaonesha kupanda kwa wastani wa fedha zilizobaki kwa Sh.26,483,891 sawa na 43% ukilinganisha na mwaka uliopita 2011/12 na hii inamaanisha kuwa Halmashauri hazikuwa na uwezo wa kutumia fedha zote za MMEM katika mwaka husika.

Hivyo Halmashauri zinashauriwa kuongeza nguvu zaidi katika matumizi ya fedha zilizopangwa katika kipindi husika ili kutimiza malengo ya fedha hizo.

6.7 Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM)

Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) ulianzishwa kwa sheria ya Misitu ya 2002, ambayo inatoa msingi wa kisheria kwa jamii, vikundi au watu binafsi popote Tanzania Bara kumiliki, kusimamia au kushiriki usimamizi wa misitu kwa masharti mbalimbali. Yafuatayo yalionekana katika ukaguzi wa miradi ya PFM.

6.7.1 Bakaa ya fedha za Usimamizi Shirikishi wa Misitu Sh.119,054,705

Ukaguzi wa mapato na matumizi wa mradi shirikishi wa usimamizi wa misitu kwa mwaka wa fedha 2011/12 umeonesha kuwepo kwa kiasi kisichotumika kinachofikia Sh.119,054,705 katika Halmashauri nane kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi shirikishi wa misitu.

Orodha ya Halmashauri 8 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na.60: Orodha ya Halmashauri zenye bakaa ya fedha za PFM

Na.	Halmashauri	Kiasi kilichopo (Sh.)	Kiasi kilichotumika (Sh.)	Bakaa (Sh.)	% ya bakaa
1	H/W Bagamoyo	48,751,290	26,494,181	22,257,109	46
2	H/W Iringa	63,533,600	51,307,350	12,226,250	19
3	H/W Kilolo	46,040,000	35,330,950	10,709,050	23
4	H/W Chunya	114,906,000	95,957,710	18,948,290	16
5	H/W Mbeya	47,182,000	45,630,500	1,551,500	3
6	H/W Mbozi	57,702,000	54,364,672	3,337,328	6
7	H/W Kilosa	68,127,818	52,908,238	15,219,580	22
8	H/W Morogoro	60,921,523	26,115,925	34,805,598	57
Jumla		**507,164,231**	**388,109,526**	**119,054,705**	**23**

Jedwali hapa chini linalinganisha fedha zilizobaki kwa miaka mitatu mfululizo.

Jedwali Na.61: Mwelekeo wa Halmashauri ambazo hazikutumia fedha za PFM

Mwaka wa fedha	Bakaa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri	Wastani wa bakaa kwa Halmashauri (Sh.)
2012/2013	119,054,705	8	14,881,838
2011/2012	32,366,811	9	3,596,312
2010/2011	178,826,876	11	16,256,989

Jedwali hapo juu linaonesha kupungua kwa wastani wa Sh.12,660,676 ikiwa ni sawa na 78% ya fedha zilizobaki bila kutumika kati ya mwaka 2010/11 na 2011/12 wakati kuna ongezeko la Sh.11,285,525 sawa na 31.4% ya fedha zilizobaki mwaka 2012/13.

Uongozi wa Halmashauri uongeze juhudi za kutumia fedha za PFM katika muda uliopangwa.

6.8 Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II) ni mwendelezo wa (MMES I) ambao ulitekelezwa kati ya mwaka 2004 na 2009, mpango ukiwa umejengwa kwenye malengo ya taifa ya utoaji wa elimu ya sekondari. Malengo ya jumla ya MMES I yalikuwa kuboresha upatikanaji wa elimu kwa usawa, usimamizi na utoaji elimu Tanzania. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa kulikuwa na mapungufu yafuatayo:-

6.8.1 Bakaa ya fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) Sh.10,661,451,772

Wizara ya fedha ilipeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya shughuli za MMES, lengo ikiwa ni kuboresha elimu ya sekondari na kuongeza idadi ya wanafunzi.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa mapato na matumizi ilibainika kuwa Halmashauri 60 zilipokea jumla ya Sh.21,869,260,499 na kati ya hizo, kiasi cha Sh.11,207,808,727 zilitumika na kuacha bakaa ya Sh.10,661,451,772 ambayo ni sawa na asilimia 49% ya fedha iliyokuwepo kama inavyoonekana katika **Kiambatisho (xliv).**

Jedwali lililopo hapa chini linalinganisha wastani wa fedha zinazobaki kwa Halmashauri kwa miaka mitatu.

Jedwali 62: Mlinganisho wa bakaa ya fedha za MMES kwa miaka mitatu

Mwaka wa Fedha	Bakaa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri	Wastani wa bakaa kwa halmashauri (Sh.)
2012/2013	10,661,451,772	60	177,690,863
2011/2012	1,075,614,880	12	89,634,573
2010/2011	724,673,833	11	65,879,439

Kutokana na jedwali hapo juu yaonesha kuwa wastani wa bakaa kwa Halmashauri uliongezeka kwa Sh.23,755,134 sawa na 36% kwa mwaka 2010/11 na 2011/12 wakati wastani huo ulipanda mpaka Sh.88,056,290 sawa na 98% kwa mwaka 2011/12 na 2012/13.

Menejimenti za Halmashauri husika ziongeze juhudi katika kutekeleza na kukamilisha miradi yote iliyopangwa.

6.9 Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF)

The Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Foundation ni asasi isiyokuwa ya kiserikali ambayo inatoa huduma za kuzuia na kuondoa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa watoto kupitia tafiti, kutetea watoto, kinga na tiba. Katika kipindi cha mwaka huu wa ukauguzi, mapungufu yafuatayo yalionekana:-

6.9.1 Bakaa ya fedha za EGPAF ya Sh.193,383,312

Mapitio ya taarifa za benki, vitabu na nyaraka nyingine kwa Halmashauri 12 ilionekana kuwa, kulikuwa na bakaa ya Sh.193,383,312 zisizotumika mpaka mwishoni mwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zinazofadhiliwa na asasi hiyo.

Jedwali Na.63: Bakaa ya fedha za EGPAF

Na.	Halmashauri	Kiasi kilichokuwepo (Sh.)	Kiasi kilichotumika (Sh.)	Bakaa (Sh.)	% ya bakaa
1	H/W Karatu	128,672,490	126,642,060	2,030,430	2
2	H/W Monduli	115,365,352	91,834,653	23,530,699	20
3	H/W Ngorongoro	109,024,893	108,563,522	461,371	0.4
4	H/W Longido	128,174,290	106,142,830	22,031,460	17
5	H/W Arusha	45,976,796	33,875,783	12,101,013	26
6	H/W Siha	60,577,627	51,441,892	9,135,735	15
7	H/W Rombo	134,782,350	132,119,700	2,662,650	2
8	H/W Same	118,274,869	117,212,600	1,062,269	1
9	H/W Kahama	236,132,667	192,086,690	44,045,977	19
10	H/W Bariadi	230,103,846	190,503,820	39,600,026	17
11	H/W Maswa	189,994,422	156,619,807	33,374,615	18
12	H/M Tabora	113,960,174	110,613,106	3,347,068	3
	Jumla	**1,611,039,775**	**1,417,656,464**	**193,383,312**	**12**

Kiasi cha Sh.193,383,312 kilichobaki kinainyima jamii kupata huduma iliyotegemewa kwa wakati.

Halmashauri zinatakiwa kuongeza juhudi katika kutumia fedha zilizotolewa katika mwaka ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya asasi.

6.10 Mpango mkakati wa Miji Tanzania (TSCP)

Lengo la mradi wa kuendeleza Miji Tanzania ni kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za msingi za miji kwa kuzihusisha Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ni kama yalivyooneshwa hapa chini:

6.10.1 Fedha zisizotumika za Mpango Mkakati wa Miji Tanzania (TSCP) mwishoni mwa mwaka Sh.4,765,494,942

Mapitio ya taarifa za benki zikilinganishwa na taarifa katika vitabu vya mapato na matumizi na kumbukumbu nyingine katika Halmashauri nne (4) zilionesha kuwa kiasi cha Sh.4,765,494,942 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kuendeleza Miji Tanzania hazikutumika kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini:

Jedwali 64: Fedha ya TSCP ambayo haikutumika mpaka mwishoni mwa mwaka.

Na.	Halmashauri	Kiasi kilichokuwepo (Sh.)	Kiasi kilichotumika (Sh.)	Kiasi kisichotumika (Sh.)	% ya bakaa
1	H/Jiji Arusha	3,676,195,865	3,043,792,525	632,403,340	17
2	H/M Dodoma	5,490,402,103	4,527,680,209	962,721,894	18
3	H/Jiji Mbeya	3,378,842,028	2,368,971,181	1,009,870,847	30
4	H/Jiji Tanga	15,222,189,780	13,061,690,919	2,160,498,861	14
	Jumla	**27,767,629,776**	**23,002,134,834**	**4,765,494,942**	17

Kiasi kikubwa kilichobaki cha Sh.4,765,494,942 mwishoni mwa mwaka kilipelekea kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa na hivyo kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

Halmashauri zenye miradi hiyo zinatakiwa kuongeza juhudi zaidi katika utekelezaji wa miradi ili kuweza kuikamilisha katika mwaka husika.

6.11 Fedha za Miradi ambazo hazikutolewa

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Halmashauri nane (8) zilipanga kutumia kiasi cha Sh.37,788,892,722 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013, kiasi cha Sh.17,127,313,909 zilikuwa zimepokelewa, na kupelekea

Sh.20,661,578,813 sawa na 55% ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti kutopokelewa kama ilivyooneshwa katika jedwali Na.65.

Jedwali Na.65: Fedha za Miradi ambazo hazikutolewa

S/N	Jina la Halmashauri	Chanzo cha Fedha	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Kiasi kilichopokelewa (Sh.)	Kiasi kisichotolewa (Sh.)	% ya matoleo pungufu
1	H/W Serengeti	MMES	410,944,029	359,571,823	51,372,206	13
		PFM	150,000,000	0	150,000,000	100
2	H/W Kyela	MMEM	532,260,000	391,927,000	140,333,000	26
3	H/W Ludewa	MMEM	285,782,000	266,582,660	19,199,340	7
		MMES	150,367,000	124,416,279	25,950,721	17
4	H/W Morogoro	Global	86,683,670	10,593,200	76,090,470	88
5	H/W Rungwe	MMES	293,416,767	269,496,767	23,920,000	8
		MMEM	675,978,471	627,200,789	48,777,682	7
6	H/M Kigoma/Ujiji	TSCP	15,337,385,560	5,886,041,325	9,451,344,235	62
		MMEM	469,000,000	8,501,276	460,498,724	98
		MMES	762,427,000	306,874,636	455,552,364	60
7	H/Jiji Mbeya	TSCP	17,966,748,225	8,399,971,154	9,566,777,071	53
		MMEM	667,900,000	476,137,000	191,763,000	29
		Jumla	**37,788,892,722**	**17,127,313,909**	**20,661,578,813**	**55**

Miradi ya kiasi cha Sh.20,661,578,813 iliyopangwa haikufanyika na hivyo kusababisha malengo yaliyopangwa kutotekelezwa.

Halmashauri zinatakiwa kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti zinatolewa. Pia, Halmashauri zinashauriwa kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa miradi hiyo.

6.12 Miradi ambayo haijatekelezwa

Wakati wa ukaguzi, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipeleka fedha katika vijiji, Kata na Shule kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hata hivyo, katika Halmashauri 29 zilizochaguliwa, ilibainika kuwa miradi yenye thamani ya

Sh.3,794,503,704 ilikuwa haijaanza kutekelezwa ingawa fedha zilikuwa zimepokelewa. Kuchelewa kutekeleza miradi hiyo hupelekea kupanda kwa gharama za miradi hiyo na faida yake kuchelewa kupatikana. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho (xlv).**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuchukua hatua kuhakikisha miradi yote imetekelezwa na malengo yaliyopangwa yanapatikana. Aidha, Halmashauri zinashauriwa kuimarisha usimamizi wa miradi inayotekelezwa katika ngazi za chini.

6.13 Miradi iliyokamilika lakini haitumiki

Wizara ya Fedha hutoa fedha kwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Lengo hapa ni kuboresha utoaji huduma katika ngazi za Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri 24 zilikuwa na miradi yenye thamani ya Sh.2,887,405,130 iliyokuwa imekamilika lakini bila kutumika kama ilivyotegemewa. Kwa sababu hiyo manufaa yatokanayo na kuitumia miradi hiyo hayakupatikana kwa muda muafaka. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho (xlvi).**

Halmashauri zinashauriwa kuchukua hatua madhubuti kwa kuhakikisha kuwa miradi yote iliyokamilika inatumika ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa miradi hiyo na kupata thamani ya fedha.

6.14 Miradi ambayo haijakamilika

Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Halmashauri zilipokea fedha kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Ziara za ukaguzi zilizofanyika wakati wa ukaguzi katika Halmashauri 22 iligundulika kuwa miradi yenye thamani ya Sh.3,031,139,556 ilikuwa haijakamilika

ingawa tarehe za mikataba hiyo zilikuwa tayari zimeshapita. Kuchelewa kukamilika kwa miradi kunapelekea miradi hiyo kuongezeka gharama za kukamilisha miradi hiyo. Maelezo zaidi yametolewa katika **Kiambatisho (xlvii).**

Zaidi ya hayo, miradi yenye thamani ya Sh.193,420,343 katika Halmashauri 5 ilikuwa imekamilika lakini katika viwango hafifu na hakuna hatua zilizokuwa zimechukuliwa dhidi ya wakandarasi waliopewa miradi hiyo. Maelezo zaidi yametolewa katika Jedwali Na.66.

Jedwali 66: Miradi iliyokamilika na viwango hafifu

Na.	Halmashauri	Jina la Mradi	Chanzo cha fedha	Thamani ya Mradi (Sh.)
1	H/W Meru	Ujenzi wa madarasa katika shule ya Msingi Mareu yenye Sh.10,000,0000 na ujenzi wa Zahanati - Mikungani Sh.20,000,000.	CDG	30,000,000
2	H/W Ngorongoro	Ujenzi wa Wodi ya Wagonjwa wa kifua kikuu WASSO awamu ya kwanza.	CDG	19,908,343
3	H/W Monduli	Ujenzi wa Bwalo na Maabara - Kipok	CDG	110,000,000
4	H/W Handeni	Uchimbaji wa visima virefu – kata ya Kabuku nje na Kabuku ndani @ Sh.8,000,000	CDCF	16,000,000
5	H/W Meatu	Ujenzi wa ofisi ya Kata Mwanhuzi	CDG	17,512,000
			Jumla	**193,420,343**

Halmashauri zinatakiwa kuchua hatua madhubuti kwa kuhakikisha kuwa miradi yote ambayo ilikuwa imekamilika inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Lakini pia, Halmashauri zinashauriwa kuimarisha usimamizi wa miradi inayotekelezwa katika ngazi za chini na kampuni zote zilizofanya kazi hafifu zitolewe taarifa kwenye Bodi ya Usajili wa Makampuni.

SURA YA SABA

7.0 Usimamizi wa mikataba na manunuzi

Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 kifungu cha 3(1) kimefafanua manunuzi kama mchakato wa kununua, kukodisha, au vinginevyo kupata bidhaa na huduma yoyote au kazi za ujenzi unaofanywa na taasisi inayonunua kwa kutumia fedha za umma na mchakato huo unahusisha kazi zote za kutoa maelezo ya mahitaji, maandalizi ya zabuni, kufanya uteuzi wa mzabuni au mkandarasi na hatimaye kuandaa na kutoa mkataba. Kutokana na ukweli kwamba kiasi kikubwa cha rasilimali za Serikali huelekezwa katika ununuzi wa bidhaa na huduma, kuna haja ya kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha na uwazi katika ngazi zote za mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kupata thamani ya matumizi ya fedha za umma.

7.1 Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za manunuzi

Kifungu cha 44(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 na kanuni ya 31 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Vifaa, ujenzi na huduma zisizo za ushauri, kuuza mali za umma kwa zabuni) za mwaka 2005 zinanitaka kueleza katika ripoti yangu ya mwaka kama taasisi niliyoikagua imezingatia sheria na kanuni za manunuzi. Kwa kuzingatia jukumu hili katika taasisi za manunuzi ikiwa ni pamoja na Halmashauri, ninaweza kusema kwa ujumla kuwa hali ya uzingatiaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake bado si ya kuridhisha.

7.2 Ufanisi wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU)

Kifungu cha 34 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na kanuni ya 22 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni kwa Serikali za Mitaa ya 2007, inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi zianzishe kitengo cha usimamizi wa manunuzi kilicho na wajumbe wa kutosha. Kitengo hiki kinatakiwa kuwa na wataalam wa manunuzi na wataalam wenye fani mbalimbali wakisaidiwa na watumishi wa utawala.

Mapitio ya ufanisi wa utendaji kazi wa vitengo vya manunuzi kwa mwaka huu katika Halmashauri mbalimbali vimeonesha kutoimarika ikilinganishwa na miaka iliyotangulia. Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 63 zilibainika kuwa na vitengo vya manunuzi visivyo na ufanisi wa kuridhisha hii ikiwa ni sawa na Halmashauri 63 zilizooneshwa katika mwaka wa fedha uliopita. Mapungufu yaliobainika ni pamoja na manunuzi ya bidhaa kupitia masurufu kinyume na Agizo la 69(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009; manunuzi ambayo hayakuwa kwenye mpango wa manunuzi kinyume na kifungu 45(b) cha sheria za manunuzi (2004) na kanuni 46(9) ya kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2005. Mengine ni kwenye manunuzi ya huduma na bidhaa ambayo yamefanyika kabla ya kuidhinishwa hati ya manunuzi/mikataba midogo (LPO) kinyume na Agizo la 69 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009; Wazabuni kupewa kazi za manunuzi bila umma kutangaziwa zabuni husika kinyume na kanuni ya 80(5) na ya 97(12) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma; kuongeza kazi katika mikataba kusikoidhinishwa na bodi ya zabuni kinyume na kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Manunuzi ya 2005,na kutowasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali nakala za mikataba mbalimbali ya manunuzi ya bidhaa, kazi na huduma ambayo Halmashauri zimeingia kinyume na kanuni ya 116 ya Kanuni za Manunuzi

ya Umma 2005 (Bidhaa, kazi na huduma zisizo za kishauri) **Kiambatisho (xlviii).**

Kutokuanzishwa kwa vitengo vya usimamizi wa manunuzi ni kutozingatiwa kwa sheria ya manunuzi ya (2004) na kanuni zake za mwaka 2005 pamoja na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aidha vitengo vya usimamizi wa manunuzi ama vilivyopo havina idadi ya kutosha ya watumishi au watumishi waliopo hawana sifa stahiki zinazohusiana na manunuzi.

7.3 Tathmini ya usimamizi wa mikataba na ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi, na huduma katika Serikali za Mitaa

Aya hii inafafanua kwa ujumla masuala ya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005, pia Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aya hii inahusika pia na usimamizi wa mikataba na masuala ya uzingatiwaji wa sheria ya manunuzi ya umma ambayo yalionekana kuwa ya msingi na muhimu kuoneshwa katika taarifa hii na taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa kila Halmashauri husika katika mwaka wa fedha 2012/2013. Tathmini yangu kwa ujumla juu ya uzingatiaji sheria zilizotajwa hapo juu ilibainisha mapungufu yafuatayo:

7.3.1 Ununuzi wa bidhaa na huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni Sh.344,129,357

Kifungu cha 7 cha sheria za Bodi za Zabuni ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kanuni GN Na. 177 iliyochapishwa tarehe 03/08/2007 na kifungu cha 34 cha Sheria za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 inazitaka Halmashuri kuwa na Bodi za Zabuni. Kinyume na sheria zilizotajwa hapo juu, katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2012/13 ilibainika kuwa

Halmashauri 16 zilifanya manunuzi ya jumla ya Sh.344,129,357 bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Orodha ya Halmashauri hizo na kiasi husika vimeoneshwa hapo chini:

Jedwali Na.67 : Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Meru	8,307,200
2	H/W Kisarawe	4,320,000
3	H/W Mpwapwa	44,800,000
4	H/W Kilolo	28,538,670
5	H/W Kigoma	12,234,000
6	H/M Bukoba	6,665,000
7	H/JIJI Mbeya	35,450,900
8	H/W Mbozi	14,058,500
9	H/W Magu	77,563,000
10	H/M Sumbawanga	17,411,600
11	H/Mji Mpanda	10,283,640
12	H/W Mbinga	19,552,000
13	H/W Songea	24,366,850
14	H/W Namtumbo	23,837,000
15	H/W Korogwe	11,443,580
16	H/W Tabora	29,134,000
	Jumla	**344,129,357**

Mchanganuo wa manunuzi ambayo hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kwa miaka miwili ni kama ufuatavyo:

Jedwali Na.68 : Mwenendo wa Ununuzi wa bidhaa na huduma uliofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni

Mwaka	Kiasi ambacho hakikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni	Idadi ya Halmashauri
2012/13	344,129,357	16
2011/12	541,013,405	24

Jedwali Na.68, linaonesha kuwa kiasi kisicho idhinishwa na Bodi ya Zabuni kilipungua kwa Sh.196,884,048 kutoka mwaka 2011/12 hadi mwaka 2012/13 sawa na 36%. Hivyo, kiasi kikubwa kinaonesha kuna ongezeko kubwa la idadi ya Halmashauri ambazo zilifanya manunuzi bila kupata kibali cha Bodi ya Zabuni.

Mbali na Halmashauri hizo kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma, vilevile hapakuwa na thamani ya fedha iliyopatikana kwenye manunuzi haya.

7.3.2 Manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanywa kutoka kwa watoa huduma za ugavi wasio idhinishwa Sh.755,813,087

Kifungu cha 67(3) cha kanuni za manunuzi ya Umma, 2005 kinataja kuwa isipokuwa pale ambapo wazabuni, makandarasi au watoa huduma tayari wameainishwa (pre-qualified), taasisi zinazofanya manunuzi ya bidhaa zilizodhibitiwa (restricted) itahitajika kutafuta mzabuni kutoka katika orodha ya watoa huduma za ugavi ambao walipitishwa ili kuleta ushindani zaidi wa bei.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa malipo ya jumla ya Sh. 755,813,087 yahusuyo manunuzi ya bidhaa na huduma katika Halmashauri 26, zililipwa kwa wazabuni mbalimbali ambao hawakuwa katika orodha ya watoa huduma za ugavi waliopitishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Jedwali Na.69 : Manunuzi kwa watoa huduma za Ugavi ambao hawajaidhinishwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/Jiji Arusha	12,748,940
2	H/W Mafia	54,636,100
3	H/W Mkuranga	3,819,412
4	H/M Ilala	118,980,965
5	H/W Bahi	1,581,600
6	H/W Bukoba	17,925,000
7	H/W Ruangwa	12,970,800
8	H/W Bunda	3,315,000
9	H/W Ileje	2,767,600
10	H/W Kyela	65,070,650
11	H/W Rungwe	43,405,000
12	H/W Mbeya	2,262,700
13	H/W Kilosa	7,003,000
14	H/W Morogoro	31,040,000
15	H/W Ulanga	63,313,200
16	H/Mji Masasi	29,525,000
17	H/W Misungwi	8,571,000
18	H/W Sengerema	26,758,800
19	H/Jiji Mwanza	97,927,400
20	H/W Ukerewe	100,130,800
21	H/M Ilemela	16,678,120
22	H/W Sumbawanga	4,200,000
23	H/W Korogwe	17,435,000
24	H/Jiji Tanga	23,991,000
25	H/W Tabora	5,850,000
26	H/Mji Mpanda	13,431,000
	Jumla	**755,813,087**

Jedwali Na.70: Mwenendo kwa miaka miwili wa manunuzi kutoka kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa

Mwaka	Manunuzi yaliyofanywa kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa. (Sh)	Idadi ya Halmashauri husika
2012/13	755,813,087	26
2011/12	375,057,680	18

Jedwali Na.70 linaonesha manunuzi kutoka kwa watoa huduma za ugavi ambao hawajathibitishwa kwa muda wa miaka miwili mfululizo ambapo kutoka mwaka 2011/12 mpaka mwaka 2012/13 kiasi kiliongezeka kwa Sh.380,755,407 sawa na asilimia 101.

7.3.3 Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha zabuni Sh.254,040,434

Mapitio ya kumbukumbu za manunuzi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 uligundua kiasi cha Sh. 254,040,434 zikiwa zimetumiwa na Halmashauri kwa ajili ya manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa na huduma za ushauri bila kufuata mchakato wa kushindanisha zabuni kinyume na kanuni ya 63 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005. Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi kwa kiwango hicho unaweza kuleta shaka hasa upande wa thamani ya fedha na ubora wa bidhaa/huduma zilizonunuliwa na Halmashauri hizo.

Jedwali hapa chini linaonesha kiasi kilicholipwa na kila Halmashauri

Jedwali Na.71: Orodha ya Halmashauri ambazo zilifanya Manunuzi bila ushindani wa wazabuni

Na.	Jina la halmashauri	Kiwango (Sh.)
1	H/ Jiji Arusha	13,095,000
2	H/W Monduli	20,210,300
3	H/ W Mafia	8,482,900
4	H/ W Rufiji	2,510,000
5	H/ W Liwale	13,390,000
6	H/ W Mbulu	12,700,000
7	H /W Rorya	137,913,030
8	H/W Rungwe	9,360,000
9	H/ W Sengerema	10,580,400
10	H/M Ilemela	13,488,224
11	H/W Nkasi	11,453,580
12	H/Mji Mpanda	1,200,000
13	H/M Bukoba	12,752,000
	Jumla	**254,040,434**

Jedwali Na.72 linaonesha ulinganifu wa manunuzi yaliyofanyika bila zabuni za ushindani kwa miaka miwili.

Jedwali Na.72: Mwenendo wa Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni

Mwaka	Zabuni ambazo hazikushinda-nishwa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri husika
2012/13	254,040,434	13
2011/12	443,107,149	25

Jedwali Na.72 linaonesha kwamba manunuzi yaliyofanywa bila kufuata mchakato wa ushindani wa zabuni yamepungua kwa Sh. 189,066,715 kutoka Sh.443,107,149 mwaka 2011/12 hadi Sh.254,040,434 mwaka 2012/13 sawa na 43%

Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kuhakikisha kwamba angalau Nukuu tatu zinashindanishwa kutoka kwa wauzaji wa bidhaa na huduma kabla ya manunuzi kufanyika ili kutekeleza viwango vya taratibu za manunuzi. Kwa upande wa manunuzi yanayofanywa toka chanzo kimoja cha mtoa huduma, inapaswa kuonesha uhalali na uidhinishwaji wa manununzi hayo.

7.3.4 Manunuzi ya bidhaa na vifaa ambavyo havikuingizwa katika leja ya vifaa Sh.665,721,927

Agizo 54(3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linataka kumbukumbu za mapokezi, vifaa vilivyotoka bohari na kiasi halisi kilichobaki kwa kila bidhaa zilizopokelewa ziandikwe katika kurasa tofauti za daftari la vifaa ikionesha taarifa zote za bidhaa zilizonunuliwa kama vile tarehe ya manunuzi, stakabadhi ya kutolea bidhaa, idadi na kiasi kwa kila aina ya bidhaa. Lakini pia, agizo hili linataka kuwe na kumbukumbu juu ya tarehe bidhaa hizo zilipotolewa bohari, idadi iliyotolewa, namba ya hati ya kutolea bidhaa hizo na kiasi kilichobaki bohari. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kuangalia udhibiti na usimamizi wa bidhaa katika bohari ulibaini kuwa Halmashauri 18

hazikuweza kukidhi matakwa ya agizo lililotajwa hapo juu. Orodha ya Halmashauri hizo ni:-

Jedwali Na.73: Orodha ya Halmashauri ambazo vifaa vyake havikuingizwa katika leja

Na.	Jina la halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Karatu	14,394,500
2	H/W Longido	18,609,680
3	H/W Arusha	28,074,744
4	H/W Mafia	18,590,900
5	H/Mji Njombe	18,494,000
6	H/W Mwanga	9,536,000
7	H/W Ruangwa	3,782,550
8	H/W Mbulu	12,300,000
9	H/W Ileje	1,940,880
10	H/W Mbozi	41,097,610
11	H/Jiji Mwanza	7,619,000
12	H/W Ukerewe	23,718,500
13	H/M Ilemela	10,737,040
14	H/W Bukombe	386,788,305
15	H/M Songea	3,750,000
16	H/W Songea	3,674,500
17	H/W Shinyanga	55,938,138
18	H/W Singida	6,675,650
Jumla		**665,721,997**

Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la vifaa na kurekodi vifaa kwa miaka miwili.

Jedwali Na 74: Mwenendo wa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la vifaa kwa miaka miwili

Mwaka	Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja ya vifaa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri zinazohusika
2012/13	665,721,997	18
2011/12	271,711,263	17

Kiasi cha manunuzi kilichobainika kutokurekodiwa katika leja ya vifaa kwa mwaka wa fedha 2012/13 kimeonekana kuongezeka kwa kiasi cha Sh.394,010,734 kutoka Sh.271,711,263 mwaka 2011/12 hadi Sh.665,721,997 ambacho ni sawa na 145%. Hii inaonesha kuna udhaifu katika kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za vifaa vinavyopokelewa na kutoka.

Kwa vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja ya vifaa, inapunguza mawanda ya ukaguzi, kwani inakuwa vigumu kwa mkaguzi kutambua kama vifaa vilivyonunuliwa vimepokelewa vyote na kutumika kama inavyopaswa.

7.3.5 Bidhaa zilizolipiwa lakini hazikupokelewa Sh.150,649,237

Kifungu cha 122(1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2005 kinazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kupata taarifa juu ya mapokezi ya bidhaa ambazo zimenunuliwa kulingana na mikataba ili kuidhinisha malipo mara moja kwa mzabuni. Kinyume na kanuni hii, bidhaa zenye thamani ya Sh.150,649,237 ziliagizwa na kulipiwa katika Halmashauri 9 lakini zilikuwa bado hazijapokelewa kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na.75: Orodha ya Halmashauri ambazo zililipia vifaa lakini bado havijapokelewa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Kibondo	15,906,000
2	H/W Kiteto	15,788,000
3	H/W Ukerewe	11,681,000
4	H/W Bukombe	62,700,000
5	H/W Sumbawanga	5,400,000
6	H/W Manyoni	28,796,437
7	H/W Urambo	4,800,000
8	H/W Tarime	3,500,000
9	H/M Bukoba	2,077,800
Jumla		**150,649,237**

Jedwali hapo chini linaonesha mlinganisho wa miaka miwili wa bidhaa zilizolipiwa lakini hazijapokelewa

Jedwali Na.76: Mwenendo wa Bidhaa zilizolipiwa lakini hazijapokelewa

Mwaka	Bidhaa ambazo zimelipiwa lakini hazijapokelewa (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2012/13	150,649,237	9
2011/12	125,681,000	6

Kutokana na jedwali hilo hapo juu, inaonesha kuwa bidhaa zilizolipiwa lakini hazikupokelewa kuongezeka kwa Sh.24,968,237 kutoka Sh.125,681,000 mwaka 2011/12 hadi Sh.150,649,237 mwaka 2012/13 ambazo ni sawa na 20%.

7.3.6 Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za mikataba na miradi

Mapitio ya usimamizi wa mikataba yamebaini upungufu mkubwa wa utunzaji wa kumbukumbu muhimu za mikataba na miradi kama taarifa/nyaraka muhimu hazikuwa katika mafaili ya mkataba husika ikiwa ni pamoja na mikataba yenyewe, Mchanganuo wa gharama za kazi (BOQ), makadirio ya Wahandisi, hati za madai za kazi iliyofanyika, muhtasari wa vikao vilivyofanyika eneo la kazi, nakala za hati za malipo, ongezeko la kazi (ikiwa lilikuwepo) na manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa mwaka wa manunuzi, vilevile kumekuwa na utunzaji usioridhisha wa rejesta ya mikataba.

Kiwango cha kufuata sheria ya manunuzi si cha kuridhisha. Hivyo mapungufu hayo kuendelea kuongezeka. Katika mwaka huu wa ukaguzi (2012/13), manunuzi ya jumla ya Sh.5,923,884,834 yaligundulika kufanyika kinyume cha taratibu za manunuzi kama inavyooneshwa katika **kiambatisho (xlix).** Ukiukwaji huo wa taratibu katika mwaka unaokaguliwa umeongezeka kwa kiasi kikubwa (79.7%) ikilinganishwa na mwaka 2011/12 ambapo ukiukwaji huo ulihusisha manunuzi yenye thamani ya Sh.660,529,264. Ulinganisho kwa miaka hiyo miwili ni kama unavyoonekana katika jedwali hapo chini

Jedwali Na.77: Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za mikataba na miradi

Mwaka	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
2012/13	18	5,923,884,834
2011/12	16	660,529,264
2010/11	24	4,452,071,069

Menejimenti za Halmashauri kwa mara nyingine tena zinasisitizwa kuimarisha Vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi na taratibu za manunuzi ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za Umma zinazotumika katika eneo hili.

SURA YA NANE

8.0 KAGUZI MAALUM

8.1 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalum

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni ya.79 (1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kutokana na maombi kutoka kwa Afisa Masuuli au mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vyombo vingine. Kanuni pia inampa CAG mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum pale anapoona inafaa. Katika mwaka 2012/2013, kaguzi maalum sita (6) zilifanyika. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyojitokeza katika kaguzi hizo maalum ni kama ifuatavyo:

8.1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Meru

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2011/2012.

- Katika mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2011/2012, Halmashauri haikuomba kibali cha ajira ya nafasi 124 kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- Watumishi wa muda 34 waliajiriwa bila kupata idhini kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- Watumishi 21 walipandishwa vyeo bila kuwepo kwenye ikama ya Halmashauri inayotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- Malipo yasiyo na viambatanisho ya jumla ya Sh.35,893,300 yalifanyika ikiwa ni kinyume na Agizo la

8 (2) (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- Malipo ya posho ya ziada ya Sh.1,170,000 yalilipwa kwa wafanyakazi kwa kutumia viwango visivyo sahihi ikiwa ni kinyume na Waraka Na.AC17/45/03/1 wa tarehe 27 Septemba, 2002 uliotolewa na Ofisi ya Raisi menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- Posho kiasi cha Sh.160,731,000 zililipwa kwa watumishi bila kujaza fomu za madai ikiwa ni kinyume na Agizo la.78 (2) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Posho ya jumla ya Sh.4,100,000 ililipwa kwa watumishi kwa shughuli ambazo hazikufanyika.
- Madai ya posho za kukaimu madaraka yasiyo sahihi ya jumla ya Sh.83,602,830 ambayo iliombwa na watumishi waliokaimu vyeo bila kupata barua za kuidhinishwa kukaimu vyeo hivyo kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- Halmashauri iliingia mkataba na Kampuni ya M/S Damijo Construction Co Ltd wa ajili ya Ujenzi wa Stendi ya Mabasi-Tengeru. Baada ya kupitia nyaraka mapungufu yafuatayo yalionekana:
    1. Taratibu za kutoa zabuni hazikuzingatiwa wakati wa kutoa ongezeko la kazi katika ujenzi wa kituo cha mabasi Tengeru kwa kuwa hakukuwa na ushindanishi wa zabuni kwa kazi hiyo.
    2. Malipo ya Sh.12,166,823 yalifanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.
    3. Stakabadhi za kukiri kupokea malipo zenye mashaka kutoka kwa mkandarasi M/S Damijo Construction Co.Ltd zenye thamani ya Sh.43,280,571 hazionyeshi vitu muhimu kama vile namba ya usajili ya mlipa kodi (TIN) na VRN, hazionyeshi mahali ilipo biashara yake, namba ya

simu na pia hazikuwa katika karatasi ya utambulisho wa kampuni (company's logo).

- Halmashauri iliingia mkataba na Kampuni ya Geometry and Y & P Associates Consultant kama Mshauri katika ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Halmashauri. Baada ya kupitia nyaraka, mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Wajumbe wa kamati ya tathmini ya zabuni walipendekezwa na kuidhinishwa na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi kinyume na Kifungu cha 37(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004.
    2. Wajumbe wa kamati ya tathmini ya zabuni kutosaini hati ya kiapo (Code of ethics) kinyume na Kifungu cha 37(6) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004.
    3. Ongezeko la kazi yenye thamani ya Sh.7,857,600 lilipwa kwa Mkandarasi bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na kifungu cha 69(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004.
    4. Kutokatwa kwa punguzo la Sh.12,798,666 kutokana na kuondolewa kwa kazi zilizopo kwenye mkataba wa awali kutoka kwenye malipo anayolipwa mkandarasi.
    5. Halmashauri iliingia mkataba na mkandarasi kwa kutumia utaratibu wa "Time Based Contract" badala ya "Lumpsum Based" na mkandarasi wa Kampuni ya Geometry and Y & P Associates Consultant kwa mkataba wenye gharama ya Sh.60,030,000 kinyume na mwongozo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ya mwaka 2007 ambayo inataka Halmashauri kuwa na utaratibu wa kusimamia mkandarasi kwa utaratibu wa "Lumpsum Based" ikiwa ukubwa wa kazi,

kiwango cha bei kwa kizio kimoja, muda wa mkataba na gharama za mkataba zinajulikana.

- Lita 5,916 za mafuta ya dizeli zenye thamani ya Sh.12,037,606 zilitolewa kwa magari na pikipiki mbalimbali lakini mafuta hayo hayakuwa yameingizwa kwenye vitabu vya kudhibiti matumizi ya vyombo vya moto (log books), hivyo haikuwezekana kuthibitisha matumizi yake.
- Rimu za karatasi zenye thamani ya Sh.17,050,000 zilitolewa kwa wingi kwa wakuu wa idara mbalimbali bila ya kuingizwa kwenye leja za stoo wala kwenye hati za kutolea, hivyo haikuwezekana kuthibitisha matumizi yake.
- Wakati wa ukaguzi maalum ilibainika kwamba deni la kiasi cha Sh.143,898,525 lilikuwa bado halijalipwa.

8.1.2 Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba katika kipindi cka mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2012/2013:

- Hakukuwa na ushindanishi katika zabuni ya ukusanyaji wa mapato katika gereji ya Manispaa kwa kuwa mzabuni mmoja tu ndiye aliyeomba zabuni. Pia hapakuwa na uthibitisho kutoka kwa Msajili wa Makampuni (BRELLA) unaoonesha kama mwekezaji huyo (ACE Chemicals Ltd) amesajiliwa.
- Kiasi cha Sh.297,000,000 kilikuwa kimewekezwa na Kampuni ya uwekezaji ya ACE Chemicals Ltd katika gereji ya Manispaa ya Bukoba bila ya ridhaa ya Baraza la Madiwani na Kamati ya Fedha.
- Halmashauri ilichukua mkopo wa Sh.470,000,000 kutoka Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) na Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) bila ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya Mamlaka ya Serikali za

Mitaa ikiwa ni kinyume na Agizo la. 51(2)(b) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- Halmashauri iliingia mkataba na kampuni ya Kajuna Investments Co.Ltd wenye Kumb. Na. LGA/034/2011/2012/W/TP/01 wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa Km 17.61 kuzunguka eneo la viwanja na mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Mkandarasi alilipwa Sh.8,826,158 kwa kazi ambazo hazikufanyika.
    2. Mkandarasi alipewa kazi za nyongeza zenye thamani ya Sh.227,989,000 bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
- Halmashauri iliingia mkataba na Kampuni ya OGM Consultants kwa mkataba wenye Kumb.Na. LGA/034/2011/2012/C/05 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, usanifu na usimamizi wa ujenzi wa soko. Mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Mkandarasi hakuwa ameidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
    2. Jumla ya Sh.35,210,520 zililipwa kwa Kampuni (OGM Consultants na APEX Consultants) kama Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), wakati washauri hao wawili hawakuwa wameandikishwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).
- Halmashauri iliingia mkataba na Kampuni ya M/s Deka Enterprises wa ujenzi wa stendi ya mabasi ya Kyakairabwa. Baada ya kupitia nyaraka za malipo, mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Zabuni haikutangazwa kinyume na Kanuni ya 80(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
    2. Jumla ya Sh.31,024,305 zililipwa kwa mkandarasi kwa kazi ambayo haikufanyika.

3. Malipo yote yalilipwa kwa mkandarasi bila ya kukata fedha za matazamio (Retention money).

- Malipo ya Sh.10,965,108 yalifanyika kwa Kampuni Archplan International Limited kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu, kazi ambayo haikuwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2010/2011.
- Katika kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi 2013/2014, kiasi cha Sh.256,218,200 kutoka vyanzo vya ndani vya mapato hakikukusanywa kutoka katika chanzo cha ushuru wa soko.
- Upendeleo katika uteuzi wa wakala wa kukusanya mapato kwa kuwa wakala aliyeomba kukusanya mapato kidogo ndiye aliyepewa uwakala badala ya wakala aliyeomba kukusanya mapato mengi hivyo kupelekea Halmashauri kupata hasara ya Sh.53,400,000.
- Nyaraka za matumizi ya Sh.3,753,300 ikiwa ni marejesho ya gharama za uchapishaji zilizotumiwa na Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo matumizi yaliyofanyika hayakuweza kuhakikiwa.

8.1.3 Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi 2011/2012:

- Jumla ya Sh.109,279,644.60 ziliibwa kutoka katika akaunti ya Halmashauri na watumishi wa Halmashauri kwa kushirikiana na watumishi wa benki ya NMB. Mara baada ya wizi kujulikana, hatua zilichukuliwa na fedha zilirejeshwa.

Fedha za Michango ya Elimu

- Vitabu vya stakabadhi za mapato 127 kwa ajili ya kukusanya michango ya Elimu havikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi wakati vilipohitajika.
- Jumla ya Sh.24,356,087 zilikusanywa na Mkuu wa Wilaya ya Mufindi kutoka vyanzo mbalimbali, lakini fedha hizi zilizokusanywa zilitumika moja kwa moja katika ujenzi wa bweni la Shule ya Sekondari Ilogombe na ununuzi wa madawati 240 kwa ajili ya Shule za Sekondari Sadan na Ilogombe kabla ya kuingiza fedha hizo kwenye akaunti ya Mfuko wa Elimu. Pia, fedha hizi hazikuoneshwa kwenye taarifa ya mapato za matumizi za Halmashauri.
- Michango kiasi cha Sh.4,769,000 iliyokusanywa na Katibu Tawala wa Wilaya (DAS) na Maafisa Watendaji wa Kata (WEOs) haikuwasilishwa Halmashauri.
- Stakabadhi halisi nne (4) ziliondolewa kutoka kwenye vitabu vya stakabadhi za mapato husika ambazo ni stakabadhi namba 031253, 031275, 017065 na 011481. Hivyo kiasi kilichokusanywa kupitia stakabadhi hizo hakikuweza kuhakikiwa.
- Halmashauri ilinunua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh.35,804,900 kutoka kwa watoa huduma mbalimbali bila ya ushindanishi wa nukuu za bei kinyume na Kanuni ya 68 (4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 ambayo inataka taasisi inayofanya manunuzi kutumia nukuu za bei zisizopungua tatu (3) kwa wazabuni ili kupata bei iliyo nafuu na huduma iliyo bora.
- Halmashauri ililipa fedha taslimu Sh.7,416,400 kwa watumishi mbalimbali kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kinyume na Agizo la 68 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linalotaka

malipo yote kutoka Halmashauri yafanyike kwa hundi.

- Baada ya kufanya mapitio ya leja za stoo na hati za kutolea vifaa ilibainika kwamba vifaa vyenye thamani ya Sh.27,236,660 havikuingizwa kwenye leja za stoo kinyume na Agizo la 59 (1) 68 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Mapitio ya leja ya stoo inaonesha kwamba vifaa vyenye thamani ya Sh.2,356,200 viliingizwa kwenye leja ya stoo na kutolewa kwa watumiaji mbalimbali lakini vifaa vinavyoonekana katika hati za kutolea havifanani na vifaa vilivyotolewa kutoka kwenye leja ya stoo, hivyo matumizi yake hayakuweza kuthibitishwa.
- Vifaa vya Ujenzi vyenye thamani ya Sh.12,125,300 viliingizwa kwenye leja ya stoo lakini utoaji wa vifaa hivyo haukuingizwa kwenye leja ya stoo wala havikuwepo stoo wakati wa ukaguzi.
- Lita 4,403 za dizeli zenye thamani ya Sh.7,159,360 zilininuliwa na kuingizwa kwenye leja ya stoo lakini matumizi yake hayakuweza kuhakikiwa kwani vitabu vya kutunzia kumbukumbu za vyombo vya moto (log books) havikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi.
- Wakati wa mapitio ya leja za stoo za mafuta ilibainika kwamba, lita 400 zilitolewa kwa pamoja kwenye gari lenye namba za usajili SM 1031 wakati gari hilo lina uwezo wa kujaza lita 200. Hivyo matumizi ya lita 400 hayakuweza kuhakikiwa.
- Katika mwaka 2007/2008 hadi 2011/2012, Halmashauri iliingia mikataba na wakandarasi mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa shule na zahanati. Wakati wa mapitio ya taratibu za utoaji wa mikataba mapungufu yafuatayo yalibainika:

1. Zabuni zote hazikutangazwa kinyume na Kanuni ya 80 (5) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
2. Utoaji wa zabuni haukuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni ya 80(3) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
3. Mkandarasi mmojawapo (Fredrick Msimbwa) alipewa zabuni nyingi zaidi ya asilimia hamsini ya zabuni zote za Ujenzi wa shule na zahanati.
4. Baadhi ya kazi zilifanywa bila ya kuwa na mkataba wa kisheria kati ya Halmashauri na wakandarasi ambazo ni ujenzi wa nyumba ya mwalimu katika shule ya Sekondari Mgalo.

- Jumla ya Sh.1,200,000 zililipwa kwa S.J.M Construction kwa ajili ya kuweka "door shutters" katika shule ya Sekondari Idunda lakini thamani ya fedha haikupatikana kwa kuwa "Door Shutters" hizo zilikuwa zimeharibiwa na mchwa.
- Halmashauri ililipa jumla ya Sh.1,248,000 kwa mkandarasi Mponela Construction kwa kazi ya kupaka rangi katika dari kwa madarasa mawili ya Shule ya Sekondari Makalala, ambapo kazi hiyo haikufanyika.
- Halmashauri ilinunua vifaa vya Ujenzi vyenye thamani ya Sh.3,181,900 kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa katika Shule ya Sekondari Luganga. Hata hivyo, haikuweza kuthibitika kuwa vifaa hivyo vilipokelewa shuleni.

Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

- Halmashauri ilinunua madawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.14,604,700 kutoka kwa wauzaji binafsi. Wakati wa ukaguzi ilibainika kwamba vifaa hivyo vilinunuliwa bila kuwepo ushahidi wa kutokuwepo kwa madawa na vifaa tiba husika katika Bohari Kuu ya Madawa (MSD).

- Halmashauri ilinunua madawa yenye thamani ya Sh.20,272,200 na kuyahifadhi kwenye stoo ya Halmashauri, lakini matumizi ya madawa haya hayakuweza kuhakikiwa kwa kuwa leja ya stoo na hati ya kutolea havikuwasilishwa wakati wa ukaguzi .
- Halmashauri ilitumia kiasi cha Sh.64,279,941 fedha za Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) kwa ajili ya kugharamia malipo ya Ankara za maji, umeme na ukarabati wa vitanda katika Hospitali ya Wilaya ya Mafinga, malipo ya mishahara, posho za vikao na uhamisho kwa watumishi kinyume na mwongozo wa uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).
- Halmashauri ilinunua meza na kabati vyenye thamani ya Sh.1,010,000 kwa ajili ya Zahanati ya Igombavazi na Ihunga bila ya uwepo wa ushindanishi wa nukuu za bei kinyume na Kanuni ya 68 (4) ya Kanuni za manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 inayotaka taasisi inayofanya manunuzi kutumia nukuu za bei zisizopungua tatu (3) ili kuamua ama kumchagua muuzaji mmoja miongoni mwa waliowasilisha nukuu za bei mwenye bei nafuu na anayetoa huduma bora.
- Lita 12,000 za dizeli zenye thamani ya Sh.24,927,000 zilinunuliwa na kuingizwa kwenye leja za stoo. Hata hivyo, matumizi ya mafuta hayo hayakuthibitika usahihi wake kutokana na kutoletwa kwa vitabu vya kumbukumbu za vyombo vya moto (log books) kwa ajili ya ukaguzi.

Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund)

Kulitokea udanganyifu katika utoaji wa madawa yenye thamani ya Sh.8,359,000 ambao unaonesha kuwa madawa hayo yalikuwa yamepelekwa kwenye Zahanati mbalimbali. Wakati wa Ukaguzi ilibainika kuwa kiasi cha madawa yaliyoonekana kupokelewa na zahanati husika yalitumia hati ya kutolea (Issue voucher) ambayo ilishatumika. Hivyo,

vocha hiyo ya kutolea ilibadilishwa ili kuingiza madawa yenye thamani ya Sh.8,359,000 ambayo hayakuwa yamepelekwa kwenye zahanati tano za Sawala, Ugenzi, Isipii, Igomaa na Ibwana.

8.1.4 Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kwa mwaka wa fedha 2009/2010 hadi 2010/2011:

Mradi wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund)

- Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ililipa Sh.6,808,300 kwa ajili ya uendeshaji wa semina ya Mpango kabambe wa Afya wa Halmashauri (CCHP) na mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Nukuu za Mlinganisho wa bei zilitolewa kwa wazabuni wawili badala ya wazabuni watatu na pia nukuu za bei hazikuwa zimesainiwa na wazabuni.
    2. Malipo yalifanyika kwa jina la Abraham F. Kombe badala ya jina la kampuni New Katavi Hotel.
    3. Hati ya kukiri kupokea huduma haikusainiwa na Afisa mhusika ili kukiri mapokezi ya huduma iliyotolewa.
    4. Karatasi za mahudhurio hazikuletwa kwa ajili ya ukaguzi.
- Manunuzi ya kiasi cha Sh.21,091,269.16 yamefanyika kutoka kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa.
- Madawa yenye thamani ya Sh.1,809,000 yalilipiwa lakini hayajapokelewa kutoka Bohari kuu ya Madawa (MSD).
- Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Halmashauri ililipa madeni ya nyuma ya Sh.24,483,000 ambayo hayapo kwenye bajeti bila ya kuyaorodhesha kama madai kwenye taarifa za fedha za mwaka uliopita,

kinyume na Agizo la 22 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- Matumizi ya mafuta ya dizeli lita 635 yenye thamani ya Sh.1,331,750 hayakuingizwa kwenye vitabu vya kutunzia kumbukumbu za vyombo vya moto (log books). Hivyo, haikuwezekana kuthibitisha matumizi yake.

Mradi wa Maji Safi na Maji Taka Vijijini (RWSSP)

- Fedha kiasi cha Sh.20,000,000 kilipokelewa tarehe 31/03/2010 katika akaunti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maji Safi na Maji Taka Vijijini lakini fedha hizo bado hazijahamishwa kwenda kwenye akaunti ya Maji Safi na Maji Taka Vijijini (RWSSP).
- Halmashauri ilipanga kutumia Sh.30,000,000 kwa ajili ya kuchimba visima viwili katika kijiji cha Kibaoni, lakini Sh.37,088,000 zililipwa kwa mkandarasi M/s Drilling and Dams Construction Agency, hivyo Sh.7,088,000 zililipwa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.
- Halmashauri ililipa malipo ya awali ya Sh.61,433,000 kwa Mkandarasi aitwaye Drilling and Dam Construction Agency kinyume na matakwa ya mkataba Kipengele Na. 5 cha mkataba ambacho kinataka malipo ya awali yasizidi Sh.18,429,900 au 15% ya thamani yote ya mkataba (Sh.122,866,000).
- Halmashauri imepata hasara ya kubadilisha fedha (exchange loss) baada ya kuingia mkataba wenye thamani ya Dola za Kimarekani 173,735 kwa ajili ya kupata huduma ya ushauri ya maji. Mwanzoni mkataba ulikuwa na thamani ya Sh.225,855,500 lakini malipo ya Sh.248,952,056 yalifanyika kwa mkandarasi (O & A) na kusababisha hasara ya Sh.23,096,556.

- Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ililipa Sh.1,050,000 kwa ajili ya gharama za utawala ambazo hazihusiani na fedha za mradi wa Maji Safi na Maji Taka Vijijini na kiasi hiki cha fedha kilikuwa bado hakijarejeshwa.
- Manunuzi kiasi cha Sh.2,000,185 yalifanyika kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa.
- Tozo ya ucheleweshaji wa kazi (Liquidated damages) ya kiasi cha Sh.27,323,700 haikukatwa kutoka kwa mkandarasi (PNR Services Ltd) kwa ucheleweshaji wa kazi zaidi ya mwaka mmoja.

Mradi wa Kilimo (DADPS)

- Manunuzi ya bidhaa na huduma yasiyohusisha wazabuni waliodhinishwa Sh.6,341,777.
- Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 mradi wa kilimo ulikopesha NAEP II kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa posho. Hata hivyo, fedha hizo zilikuwa bado hazijarejeshwa kwenye akaunti ya kilimo.
- Malipo yalifanyika kiasi cha Sh.27,344,000 bila ya kuidhinishwa na Afisa Masuuli.
- Halmashauri ilipokea Sh.2,452,266,909 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Baada ya kufanya mapitio ya taarifa za benki ilibainika kwamba Sh.124,918,000 zilikuwa bado hazijahamishwa kwenda kwenye miradi husika. Hivyo, lengo lililokusudiwa halikufikiwa.
- Jumla ya Sh.6,188,000 zililipwa na Halmashauri katika mwaka wa fedha 2010/2011 kwa wadai wa mwaka wa fedha 2009/2010 bila ya kuorodheshwa kwenye taarifa ya fedha ya mwaka 2009/2010, kinyume na Agizo la 22 (1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- Jumla ya Sh.21,500,000 kwa ajili ya Ujenzi wa ghala katika Kata ya Ikulwe ziliibwa kutoka kwenye akaunti ya Kijiji na Katibu wa mradi (Bwana Peter Deus) ambaye alikuwa mtia sahihi katika akaunti ya kijiji. Aligushi sahihi ya mjumbe mwingine wa kamati ya mradi na kufanikiwa kutoa fedha kiasi cha Sh.21,500,000 kutoka kwenye akaunti. Kitendo hiki cha udanganyifu kinatakiwa kukabidhiwa kwa Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (CID) kwa ajili ya uchunguzi na taratibu nyingine za kisheria.

Mradi wa Mfuko wa Barabara (Roads Fund)

- Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ilifanya manunuzi ya Sh.82,581,205 bila ya kuwemo kwenye mpango wa manunuzi kinyume na Kanuni ya 46 (9) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
- Tozo ya ucheleweshaji kazi (Liquidated damage) ya kiasi cha Sh.3,412,405 hakikutozwa kutoka kwa Mkandarasi (Lupogo Civil Works & Building Contractors) kwa kucheleweshа kazi ya ukarabati wa barabara ya Igagala-Ngomalusambo kwa siku 108.
- Malipo ya rehani ya Utendaji kazi (Performance guarantee) ya kiasi cha Sh.8,219,500 hakikukatwa kutoka kwa mkandarasi RHM Investment kwa ajili ya Ujenzi wa barabara za Utende-Mapili na Inyonga-Ilunde, kinyume na Kifungu cha 54 cha Masharti Maalum ya Mkataba (Special Conditions of the contract).
- Halmashauri iliingia mkataba na Lupogo Civil Works wa ukarabati wa barabara ya Igagala-Ngomalusambo (Km 2) kwa makataba wenye Kumb. Na. RK/MDC/RF/ 2009/2010/05. Mapungufu yafuatayo yalibainika:

1. Hakukuwa na ushindani katika taratibu za zabuni kinyume na Kanuni ya 63 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
2. Wajumbe wa Bodi ya Zabuni hawakusaini fomu ya kukiri kutokuwa na mgongano wa Kimaslahi na wazabuni husika yaani "Code of Ethics declaration form".
3. Kulikuwa na tangazo moja tu la Zabuni kinyume na Kanuni Na.80 (5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 (G.N. Na. 97.

- Katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya Sh.9,737,678.50 zilikopwa kutoka akaunti ya Mfuko wa Barabara ambazo bado hazijarejeshwa.

Mradi wa Maendeleo wa Serikali za Mitaa (LGCDG)

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ilihamisha kiasi cha Sh.4,000,000 kwenda katika kijiji cha Kapanda kwa ajili ya ununuzi wa "Crasher Machine". Wakati wa Ukaguzi ilibainika kuwa fedha hizo zilikuwa hazijapokelewa na kijiji husika hali inayomaanisha uwezekano wa kuwepo kwa udanganyifu kwenye fedha hizi.

8.1.5 Halmashauri ya Wilaya ya Ileje

Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalum katika Halmashauri ya wilaya ya Ileje kwa mwaka wa fedha 2007/2008 hadi 2010/2011:

- Kulikuwa na jaribio la wizi wa fedha kiasi cha Sh.86,210,000 kupitia hundi Na.00100 ambapo hati ya malipo na hundi zinaonesha mlipwaji ni "Commandant School of Infantry" analipwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati mbili za vijiji vya Luswisi na Ibaba.
- Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi 2010/2011 kulikuwa na salio nakisi (overdraft) kiasi cha Sh.52,807,442 bila kuwepo makubaliano na benki kinyume na Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Fedha

Serikali za Mitaa ya 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2000).

- Kulikuwa na tukio la wizi wa 'Gear box' ya gari lenye namba za usajili SM 2598 Toyota Land Cruiser Hadtop yenye thamani ya Sh.8,500,000 ambapo 'gear box' ya gari husika iling'olewa na kupachikwa nyingine ambayo haikuwepo kwenye gari hilo.

Skimu za Umwagiliaji

- Halmashauri iliingia mkataba na kampuni za Katagaito Traders Company Ltd na Summer Communication Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mbebe/Sasenga. Wakati wa ukaguzi mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Tofauti ya gharama kiasi cha Sh.13,549,040 na Sh.12,432,549.50 ililipwa kwa wakandarasi M/s Summer Communication Co. Ltd na M/s Katagaito Traders Company Limited kwa mfuatano bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
    2. Mkandarasi wa kampuni ya M/s Katagaito Traders Ltd aliwasilisha dhamana ya utendaji kazi (performance bond) ya kughushi kutoka benki ya CRDB bila ya Halmashauri kujua.
- Uhamisho wa fedha wa ndani kati ya akaunti mbalimbali za Halmashauri katika mtindo wa mikopo ambazo hazijarejeshwa kiasi cha Sh.294,993,326.
- Fedha kiasi cha Sh.166,823,750 zilizokopwa kutoka akaunti ya Amana kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali ambazo bado hazijarejeshwa.
- Malipo ya Sh.44,454,552 hayakuidhinishwa na Afisa Masuuli na Mweka Hazina wa Halmashauri. Pia malipo haya hayakufanyiwa ukaguzi wa awali kinyume na Agizo la 10(2) (a) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- Malipo kiasi cha Sh.31,502,528 yaliyofanyika bila ya kufanyiwa ukaguzi wa awali (pre-audit).
- Wajumbe wa kamati ya tathmini ya zabuni walipendekezwa na Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni ya 25 (2) ya uundwaji wa Bodi za Zabuni za Serikali za Mitaa ya mwaka 2007.
- Halmashauri ilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh.83,129,550 bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Pia, hakukuwa na ulinganisho wa nukuu za bei kwa ajili ya kuleta ushindani katika manunuzi kinyume na Kifungu Na.58(2) cha Sheria ya Manunuzi ya 21 ya Umma ya Mwaka 2004.

Mradi wa Kilimo (DADPS)

- Halmashauri iliingia mkataba na kampuni ya M/s Sayuni Pet Contractors kwa ajili ya ukarabati wa kliniki ya Mifugo. Mapungufu yafuatayo yalibainika:
  1. Zabuni haikutangazwa.
  2. Ongezeko la kazi la kiasi cha Sh.6,873,978 halikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
- Matumizi ya Sh.21,487,440 yalifanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia maadhimisho ya Nane nane na gharama za shughuli za upimaji wa sampuli za udongo.
- Kutokukatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sh.4,863,060 kwa mzabuni M/s Farm Equip (T) Ltd wakati wa ununuzi wa matrekta madogo “Power tillers”.
- Malipo ya kiasi cha Sh.2,901,000 yalifanyika kwa ajili ya posho ya kujikimu kwa watumishi waliokwenda Dar es salaam kufanya ukaguzi na kupokea matrekta madogo (Power Tillers) bila ya kuwepo kwa barua za uteuzi wa kamati ya ukaguzi na mapokezi. Pia ripoti ya kazi iliyofanywa na kamati hiyo haikupatikana.

- Katika mwaka wa fedha 2009/2010 kiasi cha Sh.429,571,015 kilipokelewa katika akaunti ya Miradi ya maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Kilimo lakini kiasi cha Sh.77,782,015 hakikuhamishwa kwenda akaunti husika ya Kilimo.

Mradi wa Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund) na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM)

- Halmshauri ilinunua madawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.40,579,350 kutoka kwa wazabuni mbalimbali, bila ya kununua au kupata uthibitisho wa kutokuwepo kwa madawa na vifaa tiba hivyo kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD).
- Manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanyika kwa kutumia fedha taslimu kiasi cha Sh.39,521,360 badala ya hundi.
- Katika mwaka wa Fedha 2011/2012, Halmashauri ilifanya malipo kiasi cha Sh.18,970,696 kwa wadai wa mwaka wa Fedha 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011 bila ya wadai hao kuwepo kwenye orodha ya wadai katika taarifa za fedha kinyume na Agizo la 22(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Malipo ya posho kiasi cha Sh.29,849,950 yalifanyika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali lakini ripoti za shughuli zilizofanyika hazikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi.
- Manunuzi ya Sh.5,340,700 yalifanyika bila ya ushindanishi wa nukuu za bei kinyume na Kanuni ya 68(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 ambayo inataka kuwepo kwa nukuu za bei zisizopungua tatu (3) kutoka kwa wazabuni ili kupata mzabuni mwenye bei nafuu na atakayetoa bidhaa au huduma bora.

- Kuwepo kwa manunuzi ya kiasi cha Sh.34,530,700 yaliyofanyika kutoka katika akaunti ya maendeleo ambayo yamekiuka taratibu za manunuzi kwa kuwa yamekosa nukuu za bei kwa ajili ya ushindanishi wa wazabuni na baadhi ya manunuzi ya vifaa yalifanyika bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

Mradi wa Maji Safi na Maji Taka Vijijini (RWSSP)

- Vifaa vyenye thamani ya Sh.7,008,200 havikuingizwa kwenye daftari la vifaa. Hata hivyo, vifaa hivyo havikukaguliwa na Kamati ya Ukaguzi.
- Halmashauri iliingia mkataba na Kampuni ya Drilling and Dam Costruction Agency kwa gharama ya Sh.20,700,000 na mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Hakukuwa na barua za uteuzi wa wajumbe wa kamati ya tathmini.
    2. Hapakuwa na idhini ya Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni Na.80 (3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.
    3. Fedha ya matazamio haikukatwa na kuhifadhiwa kwenye akaunti ya Amana.
- Kiasi cha Sh.21,296,500 kililipwa kwa Mkandarasi Buka Company Ltd kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji katika kijiji cha Mlale. Wakati wa ukaguzi ilibainika kwamba shughuli zenye thamani ya Sh.3,240,000 hazikufanyika.
- Halmashauri iliingia mkataba na Kampuni ya E.A Builders Ltd kwa gharama ya Sh.36,973,600 kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji katika Kijiji cha Ndola. Mapungufu yafuatayo yalibainika:
    1. Hakuna mkataba kati ya Halmashauri na Mkandarasi.
    2. Fedha ya matazamio (Retention money) haikutozwa kwa mkandarasi.

3. Ongezeko katika mkataba la Sh.7,938,000 halikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

- Kutotumika kwa nyumba iliyokamilika yenye thamani ya Sh.306,956,200 hivyo kutotimiza lengo lililokusudiwa.

8.1.6 Halmashauri ya Wilaya ya Geita

Ukaguzi maalum ulifanyika katika Halmashauri ya wilaya ya Geita kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi ni kama ifuatavyo:

- Kulikuwa na ucheleweshwaji wa kuwasilisha makusanyo ya mapato benki kiasi cha Sh.387,553,377 kutoka vyanzo vya ndani vya Mapato ya Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia siku nne mpaka siku tisini na tatu kinyume na Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Mawakala wa ukusanyaji wa mapato, watendaji wa Kata na watumishi wa Halmashauri walishindwa kuwasilisha mapato kiasi cha Sh.83,285,020 kilichokusanywa katika vyanzo mbalimbali vya mapato vya Halmashauri. Pia ukaguzi ulishindwa kuthibitisha uwepo wa makusanyo hayo kwani haikuthibitika kuwa makusanyo hayo yalikuwepo benki au yalikuwepo katika ofisi ya mtunza fedha kinyume na Agizo la 37 (2-3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Vitabu sitini na sita (66) vya stakabadhi za mapato havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo vimezuia mawanda ya Ukaguzi.
- Mapato kiasi cha Sh.50,635,034 yaliyokusanywa na mawakala wa kukusanya mapato kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hayajawasilishwa makao makuu ya Halmashauri kinyume na Agizo la.38(1) la Memoranda

ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 na hakuna hatua iliyochukuliwa na uongozi wa Halmashauri kwa makusanyo ya mapato ambayo hayajawasilishwa.

- Mikataba themanini na moja (81) ya ukusanyaji wa mapato haikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi hivyo kuzuia mawanda ya Ukaguzi.
- Zabuni ya kukusanya mapato ya ndani kwa niaba ya Halmashauri ilitolewa kwa wakala wa ukusanyaji wa mapato bila ya kufuata taratibu za manunuzi na hivyo kupelekea Halmashauri kupata hasara ya kiasi cha Sh.57,564,000.
- Ushuru wa Nyumba ya Wageni kiasi cha Sh.33,559,520 katika mwaka wa fedha 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012 haukukusanywa na wamiliki wa Nyumba za Wageni na hakukuwa na sababu zilizotolewa na Uongozi wa Halmashauri juu ya kutokukusanya kiasi hicho.
- Ushuru wa huduma ambao haujalipwa kwa Halmashauri na makampuni yanayofanya kazi katika mgodi wa dhahabu wa Geita kiasi cha Dola za Kimarekani 2,119,092 kinyume na Sheria ndogo za Halmashauri za mwaka 2004 Kifungu cha 3(1) kinachotaka makampuni (corporate entities) kulipa ushuru wa huduma kiasi kisichozidi asilimia 0.3 ya mauzo baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa bidhaa.
- Kutokusanywa kwa mapato yatokanayo na mauzo ya viwanja katika eneo la Magogoni kiasi cha Sh.1,197,062,220 sawa na asilimia 46 ya mauzo ya viwanja vyote vyenye thamani ya Sh.2,594,606,700.
- Halmashauri kutolipwa na Kampuni ya Ashanti malimbikizo ya ushuru wa “Local Government rates and taxes” kiasi cha Dola 1,400,000 kwa kipindi cha mwaka 1999 hadi 2005 kinyume na kifungu cha. 4.1, 4.2, na 4.3 cha mkataba “Gold Mine Development

Agreement between the United Republic of Tanzania and Samax Resources Ltd and Ashanti Gold Tanzania Ltd an Agreement for Development of Gold Mine at Geita ”

- Kutokulipwa kwa ushuru wa “Prospecting and Mining Fees” wa kiasi cha Sh.1,803,650,000 na Kampuni ya Geita Gold Mine kufuatana na hati ya madai Na.293642 ya tarehe 4/6/2012 iliyotolewa na Afisa Misitu wa Wilaya kinyume na sheria ya misitu Kanuni ya 29(1) kipengele cha (x-xi) ya mwaka 2002.
- Mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu kutolipa kodi (Local Government rates and taxes) ya Dola za Kimarekani 200,000 kwa mwaka kwa Halmashauri. Jumla ya Dola za Kimarekani 600,000 hazijalipwa kwa Halmashauri licha ya kampuni hiyo kufanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri ya Wilaya Geita kwa kipindi cha miaka mitatu yaani mwaka 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012.
- Halmashauri ilifanya manunuzi ya moja kwa moja “Direct contracting” kwa ajili ya uzalishaji wa vitofali vya saruji “pavement blocks” kwa gharama ya Sh.192,000,000 kwa kampuni ya M/S Satellite kinyume na Kanuni ya 90(1), (5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2005, Tangazo la Serikali Na.97 na kifungu cha 25 (1) cha Sheria za Manunuzi za Serikali za Mitaa ya mwaka 2007 (The Local Government Authorities Tender Board (Establishmet And Proceedings).
- Halmashauri ilifanya malipo ya Sh.30,440,850 kwa Kampuni ya M/S Anifa Supplies Co. Ltd ikiwa ni malipo kwa ajili ya kazi za ziada za Ujenzi wa stendi ya mabasi Geita bila idhini ya Bodi ya Zabuni.
- Matumizi mabaya ya fedha kiasi cha Sh.31,605,500 yaliyolipwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Geita kwa lengo la ujenzi wa daraja katika kijiji cha

Nyang'homango ambapo fedha hizo zimetumika kwa shughuli zisizokusudiwa.

- Fedha kwa ajili ya shughuli za mfuko wa barabara kiasi cha Sh.800,030,689.37 kama inavyoonekana katika taarifa ya kupatiwa fedha (Exchequer issue notifications) kutoka Wizara ya Fedha haikuthibitishwa kuwa imepokelewa na Halmashauri kupitia Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza.
- Ujenzi wa dharura wa Barabara ya Kasamwa–Bulela–Busolwa (Km 24) uliofanywa na Kampuni ya Kidagaa Construction Co Ltd ambayo imegharimu Sh.106,042,500 bila ya kibali kilichoombwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali chini ya Kanuni ya 42(1)(c) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2005.
- Halmashauri ilifanya malipo ya Sh.585,155,937.50 ambayo hayakukasimiwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ajili ya shughuli za matengenezo ya maeneo korofi, ya kawaida na maalum yaliyofanyika katika barabara mbalimbali kinyume na Agizo la 18(1) la Memoranda za Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Malipo kiasi cha Sh.96,988,500 kwa Mkandarasi Kaserkandis Construction and Transport Co. Ltd kwa kazi ambazo hazikufanyika kwenye barabara za Bomba Mbili, Block D & E.
- Wakandarasi hawakutozwa tozo ya kiasi cha Sh.46,408,949 kwa ucheleweshaji wa kazi kinyume na Kanuni ya 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (G.N. No. 97) za mwaka 2005 na kifungu Na. 21-22 cha masharti maalum ya mkataba.
- Kutotekelezwa kwa miradi ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) yenye thamani ya Sh.360,502,019 ya mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011 ingawa fedha zilitolewa na Hazina.

- Halmashauri ilifanya manunuzi ya madawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.347,117,115 nje ya Bohari Kuu ya Madawa ya Taifa (MSD) bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (G.N. No. 97) za mwaka 2005. Pia ukaguzi ulibaini kuwa kama unununzi wa madawa na vifaa tiba ungefanyika kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD), Halmashauri ingeokoa kiasi cha Sh.159,998,070.
- Halmashauri haijatekeleza shughuli za miradi kumi (10) yenye thamani ya Sh. 97,855,725 zilizokasimiwa kwenye bajeti ya Mfuko wa pamoja wa Afya kwa mwaka wa fedha 2010/2011 licha ya fedha hizo kutolewa na Hazina. Hata hivyo, fedha hizo hazikuwepo kwenye akaunti na wala matumizi yake hayakuthibitika.
- Manunuzi yenye thamani ya Sh.505,532,032 yaliyozidi kiwango cha kuidhinishwa na Afisa Masuuli yalifanyika bila ya kuwa na idhini ya Bodi ya Zabuni.
- Halmashauri ilifanya malipo ya Sh.167,512,354 bila ya kuwa na nyaraka/viambatanisho vilivyohitajika kuhalalisha malipo hayo, kama inavyoagizwa katika Agizo la 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.
- Hati za malipo zenye jumla ya Sh.722,055,062.05 hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi maalum, hivyo uhalali wa malipo haya haukuweza kuthibitishwa.
- Kulikuwa na miradi ya Halmashauri yenye thamani ya Sh.290,595,550 iliyofanywa na wakandarasi bila ya kufuata taratibu za manunuzi kwa kuwa mihutasari ya vikao vya Bodi ya Zabuni, matangazo ya zabuni, ripoti za tathmini zilizofanyika na mikataba haikuletwa kwa ajili ya Ukaguzi.
- Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Halmashauri ililipa jumla ya Sh.26,342,800 kutoka Mfuko wa Afya

wa Pamoja kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa tiba kwa wazabuni mbalimbali. Hata hivyo, madawa na vifaa tiba hivyo havikufikishwa katika Halmashauri.

- Manunuzi ya kazi za ujenzi kwa kutumia masurufu Sh.155,407,975 ambapo malipo ya fedha taslimu yalilipwa kwa wakandarasi kinyume na Agizo la 39(2) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Pia manunuzi yalifanyika bila ya idhini ya Bodi ya Zabuni.
- Masurufu kiasi cha Sh.7,660,000 yalilipwa kutoka mfuko wa Afya wa Pamoja kwa watumishi wa Halmashauri bila ya kufanya marejesho ya masurufu kinyume na Agizo la 40(3) la Memoranda za Fedha za Serikali za Mitaa.
- Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ilihamisha kiasi cha Dola za Kimarekani 11,000 kwenye akaunti ya Fedha za Kigeni yenye Na. 02J1053615100-CRDB Tawi la Geita kwenda Akaunti ya Mfuko Mkuu (General Fund account). Baada ya mapitio ya taarifa za benki ilibainika kuwa, fedha iliyohamishwa haikuonekana kwenye Akaunti ya Mfuko Mkuu. Hivyo, uhamisho wa fedha kiasi cha Dola za Kimarekani 11,000 haukuthibitika.

Hata hivyo, kuna kaguzi maalum zingine zinazoendelea katika Halmashauri tatu (3) ambazo ni Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa ya Kinondoni, na Manispaa ya Ilala.

Ni matumaini yangu pia kuwa matokeo ya kaguzi maalum katika hizo Halmashauri tatu (3) yatawasilishwa katika ripoti ya mwaka ujao pamoja na matokeo ya kaguzi nyingine zitakazofanyika ikiwa ni njia ya kuwezesha kuimarisha uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Ukaguzi itaendelea kupokea maombi kutoka pande zote kwa kuzingatia sheria zilizopo, lakini ieleweke kuwa

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hana wajibu na hatalazimika kuyakubali maombi yote lakini atazingatia kila ombi kulingana na uzito wake.

8.2 Mambo ya kujifunza katika Kaguzi Maalum zilizofanyika mwaka huu

Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Jukumu la kuanzisha na kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 240 na Agizo 11 hadi 14 ya Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 ni ya usimamizi wa uongozi husika wa Halmashauri.

Ni dhahiri kwamba, kuna udhaifu mkubwa wa usimamizi katika Halmashauri. Hali hii imesababisha menejimenti kushiriki kwa njia moja au nyingine kutawala mfumo wa udhibiti wa ndani, baadhi ya viashiria ni kama vifuatavyo:

- Fedha za Halmashauri za Mufindi na Mpanda ziliibiwa na watumishi wasio waaminifu.
- Upotevu wa hundi na jaribio la wizi wa Sh.86,210,000 kupitia hundi Na.00100 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje.
- Kuna ulegevu mkubwa wa menejimenti za Halmashauri katika kupata na kulinda nyaraka zao muhimu. Hii ina madhara ya kikwazo katika mawanda ya ukaguzi.
- Mweka Hazina wa Halmashauri ana wajibu wa kuhakikisha na kusimamia masuala yote yanayohusu fedha na udhibiti wake pamoja na kusimamia idara ya fedha. Hali hii ilikuwa tofauti katika Halmashauri zilizokaguliwa, kwa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi michango ya Mfuko wa Elimu iliyokuwa inakusanywa haikuwasilishwa Halmashauri kwa ajili ya kupelekwa benki, stakabadhi za mapato za awali (original receipts) zilikuwa zinaondolewa kwenye vitabu vya stakabadhi za mapato husika na baadhi ya

michango ilikuwa inatumika kabla ya kupelekwa benki. Katika Halmashauri ya Geita mapato yaliyokusanywa na wakala wa kukusanya mapato na watumishi wa Halmashauri hayakupelekwa benki wala hayakuwepo katika ofisi ya mtunza fedha.

- Katika Halmashauri ya Geita mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani hayakukusanywa hivyo kusababisha Halmashauri kupata hasara katika kukusanya mapato ya ndani.
- Kwa ujumla kitengo cha ukaguzi wa ndani kimeshindwa kusaidia Halmashauri kikiwa kama chombo muhimu katika kuhakikisha kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani unaimarishwa na kuwa na ufanisi.

- **Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokuwa na ufanisi katika usimamizi wa miradi ya maendeleo**

  Ruzuku ya maendeleo katika Serikali za Mitaa inaweza kuleta faida inayotarajiwa iwapo itafuatiliwa na kusimamiwa vizuri. Miradi mingi ya maendeleo imekamilika katika Halmashauri za Vijiji na Kata. Usimamizi na ufuatiliaji ni muhimu kwa sababu kuna upungufu au hakuna rasilimali watu na ujuzi wa kiufundi wa kusimamia miradi ya maendeleo kama vile ujenzi. Hata hivyo, Halmashauri inalazimika kutoa usimamizi wa karibu wa miradi ya maendeleo ili kupata tija, ufanisi, na ubora wa miradi.

  Ukaguzi maalum uliofanywa katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Halmashauri ya wilaya ya Ileje, wilaya ya Mpanda, wilaya ya Mufindi, wilaya ya Meru na wilaya ya Geita umebaini kuwa, menejimenti za halmashauri hizo hazikuwa na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za chini.

Hakukuwa na ukaguzi kwa wakati wa miradi ya maendeleo na kusababisha kutokuwa na ubora na kuchelewa kukamilika kwa miradi husika. Uzembe kama huu pia ulitokea katika miradi inayotekelezwa katika ngazi za juu za utawala wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- **Mapungufu katika kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi**

  Ukaguzi maalum ulibaini kwamba taratibu za manunuzi zilikuwa hazifuatwi na nyongeza za mikataba zilikuwa haziidhinishwi na Bodi ya Zabuni, hali hii ilibainika katika ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Halmashauri ya Wilaya ya Ileje na Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

  Katika ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Ileje na Geita manunuzi yalifanyika kwa kutumia masurufu na hakukuwa na ushindanishi katika utoaji wa Zabuni.

- **Mapungufu katika usimamizi wa Mali**

  Katika Halmashauri nyingi kumekuwa na usimamizi usiojitosheleza wa matumizi ya mafuta ambapo mafuta yaliyokuwa yanayotolewa kwa watumiaji hayakuwa yanaingizwa kwenye leja za stoo na vitabu vya kumbukumbu za vyombo vya moto (log books). Katika Halmashauri ya Ileje “Gear box” ya gari lenye namba za usajili SM 2598 Toyota Land Cruiser Hardtop iliibiwa kwa kung’olewa na kupachikwa nyingine ambayo haikuwepo kwenye gari hilo.

- **Mapungufu katika kitengo cha Ukaguzi wa Awali**
  Ukaguzi maalum ulibaini baadhi ya mapungufu kwa kitengo cha Ukaguzi wa Awali ambapo malipo yalikuwa yanafanyika bila ya kuidhinishwa na Afisa Masuuli na Mweka Hazina wa Halmashauri. Katika Halmashauri ya Ileje ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya malipo yalilipwa kwa shughuli ambazo hazijafanyika.

SURA YA TISA

9.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Kama ilivyoelezwa katika sura ya utangulizi, ripoti hii ni muhtasari wa yale yaliyobainishwa katika ripoti za ukaguzi zilizotolewa kwa kila Halmashauri. Taarifa hizi zilizotolewa kwa Halmashauri pia zina mapendekezo juu ya kila suala lililobainishwa ambalo linahitaji maboresho. Maafisa Masuuli wa Serikali za Mitaa wanatakiwa kuandaa mipango ya utekelezaji wa mapendekezo ya kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuiwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 na Kanuni ya 86 na 94 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Baada ya kuwasilisha mambo muhimu yaliyotokana na matokeo ya ukaguzi kwa mwaka 2012/2013 kwa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika sura zilizotangulia, sasa nahitimisha kwa kutoa mapendekezo, ambayo kama yatatekelezwa, usimamizi wa fedha katika uendeshaji wa Halmashauri utaimarika.

9.1 MAJUMUISHO YA JUMLA

9.1.1 Udhaifu katika hatua za utayarishaji wa bajeti za Serikali za Mitaa

Mchakato wa bajeti ya Serikali za Mitaa unahitaji maboresho muhimu ili Halmashauri iweze kuongeza makusanyo kutoka katika vyanzo vyao wenyewe, kujitegemea na kutohitaji misaada kutoka Serikali Kuu, kuepuka matumizi yasiyoidhinishwa na kiasi kikubwa cha fedha kisichotumika. Mapungufu yalioonekana katika ukaguzi wa bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

- Kushindwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato kikamilifu na kwa ufanisi kutoka katika vyanzo vyao vya mapato ambapo imepelekea ukusanyaji wa kiwango cha chini kwa asilimia 14 (14%)
- Matumizi yasiyoidhinishwa kutokana na uhamishaji wa fedha bila kibali; hali hii inaathiri utoaji wa huduma kwa mujibu wa malengo ya mwaka ya utendaji na kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa.
- Bakaa kubwa ya fedha zisizotumika mwishoni mwa mwaka kutokana na ukosefu wa uwezo wa kutumia fedha hizo katika shughuli zilizokasimiwa na kuchelewa taratibu za manunuzi. Hii ni ishara ya usimamizi dhaifu wa fedha katika Serikali za Mitaa, hali inayomaanisha kwamba Serikali za Mitaa hazijaweka utaratibu thabiti na mikakati ya kuhakikisha kuwa shughuli zote zilizopangwa zinatekelezwa na kukamilika ndani ya muda uliopangwa aili kutochelewesha manufaa yaliyokusudiwa kwa jamii husika.

9.1.2 Usimamizi wa mapato

- **Udhaifu katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani**

  Imebainika kwamba mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa unapungua kutoka mwaka mmoja hadi mwingine. Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa kutosha na mikakati imara ya Serikali za Mitaa katika kuhakikisha kuwa kiwango cha ukusanyaji wa mapato kinaongezeka mara kwa mara. Serikali za Mitaa hazijaanzisha mikakati imara na endelevu ambayo inaweza kuongeza wigo katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza kiwango cha utegemezi wa fedha kutokana na ruzuku ya Serikali Kuu.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, zimebainika dosari mbalimbali katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa sheria juu ya vyanzo mbalimbali vya mapato, kutowasilishwa kwa mapato yaliyokusanywa kutoka kwa mawakala mbalimbali na wakusanyaji wengine, kukosekana kwa ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato yanayokusanywa na mawakala na kutofanya upembuzi yakinifu wa makusanyo ya mapato. Udhaifu huu unatoa ishara kwamba udhibiti wa ndani wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa ni dhaifu na kuna haja ya kuboreshwa ili maslahi na malengo ya Halmashauri yaweze kufikiwa.

Serikali za Mitaa bado hazijaboresha sheria za ukusanyaji wa mapato ya ndani kuendana na mazingira ya sasa wakati Halmashauri nyingine hazina kabisa sheria hizo. Viwango vya ukusanyaji wa mapato vipo chini mno na havijabadilishwa kukidhi mabadiliko ya kimazingira. Pia, baadhi ya Serikali za Mitaa hazikufanya upembuzi yakinifu ili kuja na mikakati ya namna gani mapato ya ndani yanaweza kuongezeka na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato. Vyanzo kama minara ya simu na ada za matangazo viliachwa bila ya kukusanywa. Aidha, upembuzi yakinifu haukufanyika hata kwa vyanzo vilivyopo kabla ya kufikia maamuzi ya kuvibinafsisha kwa mawakala na kusababisha ugumu katika ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na mawakala, udhaifu katika mchakato wa kuandaa mikataba ya ukusanyaji wa mapato yaliyobinafsishwa, na kutowasilishwa kwa mapato yaliyokusanywa na mawakala. Kwa mfano, ilibainika kuwa ukusanyaji wa mapato kutoka kwa mawakala mbalimbali na wakusanyaji wengine ya kiasi cha Sh.14, 926,757,005.12 (ongezeko la 17% ikilinganishwa na

mwaka uliopita) hayakuwasilishwa kwenye Halmashauri husika. Hii ina maana kwamba Serikali za Mitaa zitaendelea kutegemea misaada kutoka Serikali Kuu ili kufanikisha shughuli zao kutokana na udhibiti na mikakati isiyojitosheleza ambayo ingeweza kusaidia kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani.

9.1.3 Udhaifu katika Usimamizi wa Rasilimali Watu

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, ilibainika kuwa Serikali za Mitaa hazikuboresha taarifa za watumishi wao hali iliyopelekea malipo ya mishahara kulipwa kwa watumishi walioacha kazi, wenye namba za mishahara zaidi ya moja, usimamizi mdogo wa mikopo ya watumishi na kukosekana kwa taarifa mpya za watumishi katika orodha kuu ya mishahara ya watumishi.

9.1.4 Udhaifu katika Usimamizi wa matumizi

Kutofuatwa kwa sheria, kanuni na miongozo kumepelekea malipo kufanyika kabla ya kutolewa vibali ambapo pia inahusishwa na uwepo wa mapungufu katika mgawanyo wa kazi. Udhibiti wa malipo na utunzaji nyaraka za kihasibu haukuwa mzuri hali iliyopelekea malipo kutoambatana na nyaraka na malipo kufanyika katika vifungu tofauti (matumizi yasiyokuwepo kwenye bajeti). Aidha, Serikali za Mitaa hazikuwa na ufanisi katika kutunza nyaraka hali iliyosababisha hati za malipo kutopatikana pale zilipohitajika ili zikaguliwe na vielelezo vinavyothibitisha masurufu yaliyotumika kutorejeshwa na hivyo matumizi ya fedha hizo kutothibitika.

9.1.5 Kuhama kutoka akaunti za zamani kwenda akaunti mpya sita za Seriakali za Mitaa

Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ilitoa agizo lenye kumbukumbu GB.174/389/01/34 la tarehe 30/04/2012, likizitaka Serikali za Mitaa kufunga akaunti zao za zamani

kufikia tarehe 01/07/2012 na kufungua akaunti mpya sita. Agizo hilo lilihitaji Halmashuri husika kusuluhisha mambo yote yaliyokuwa yamesalia katika benki na kuhamisha bakaa zote kwenda kwenye akaunti hizo mpya isipokuwa hundi ambazo zilikuwa bado kuwasilishwa benki kufikia tarehe 30/06/2012. Baada ya uhamisho huo wa fedha kwenye akaunti mpya, menejimenti ya Halmshauri inapaswa kutoa taarifa kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki. Ilikuwa imezuiliwa kufanya malipo yoyote mapya kupitia akaunti za zamani katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Katika kipindi cha kuhama kutoka akaunti za zamani kwenda akaunti mpya, mapungufu mbalimbali yalionekana ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

- Serikali za Mitaa kuendelea kutumia akaunti za zamani kinyume na agizo la Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ikiwa ni pamoja na kuendelea kupokea fedha na kufanya malipo kupitia akaunti hizo za zamani;
- Serikali za Mitaa hazikuhamisha fedha zote kwenda akaunti mpya, na katika hali nyingine fedha zilihamishwa kutoka akaunti za zamani kwenda akaunti mpya zisizojulikana hali iliyoleta ugumu kujua wamiliki wa hizo akaunti za Serikali zilizohamishiwa fedha;
- Serikali za Mitaa hazikufanya maridhiano ya kibenki kabla ya kuhamisha fedha kutoka akaunti za zamani kwenda akaunti mpya na hivyo kuleta ugumu katika kujua kiasi halisi cha fedha kilichotakiwa kuhamishwa kwenda kwenye akaunti mpya hivyo kufanya mapokezi na hundi zilizobaki kutofanyiwa usuluhisho;
- Baadhi ya Halmashauri hazijafunga akaunti zao za zamani ambapo matokeo ya kuchelewa kufunga akaunti hizo ni kuchochea uwepo wa vitendo vya ubadhirifu au matumizi mabaya ya akaunti kama

Halmashauri zitaendelea kupokea fedha kupitia akaunti hizo.

9.1.6 Mapungufu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha

Serikali kupitia Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ilitoa agizo kupitia barua yenye Kumb. namba CA: 26/307/01A/79 ya tarehe 28 Septemba 2009 ikizitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuandaa taarifa zao za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSAs) isiyo ya fedha tasilimu kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009. Ingawa Serikali za Mitaa ziliwasilisha taarifa za fedha katika tarehe zinazokubalika kisheria, mapungufu yafuatayo yaliweza kuonekana:

- Taarifa za fedha zilizowasilishwa zilikuwa na mapungufu mbalimbali kama vile makosa, usahaulifu, kupunguza na kuongeza tarakimu, kutoonesha au kuonesha kwa kupotosha. Kutokana na idadi kubwa ya makosa na usahaulifu, Halmashauri ziliwasilisha upya taarifa zake za fedha, hali iliyoathiti kukamilika kwa ukaguzi kwa wakati uliopangwa. Idadi ya mabadiliko na marekebisho yaliyofanywa inaonesha kiwango cha chini cha uwezo wa wahasibu wa Halmashauri katika kuandaa taarifa za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSAs);
- Taarifa za fedha hazikuandaliwa moja kwa moja kutoka kwenye IFMS kama ilivyopaswa kuwa. Aidha, taratibu za uandaaji wa taarifa za fedha zilikua ngumu kueleweka kwani zilihusisha idadi kubwa ya shughuli zilizofanyika nje ya mfumo;
- Kwa hakika, baadhi ya Serikali za Mitaa ambazo hazikuweka wazi katika taarifa za fedha thamani ya

mali za kudumu zinazomilikiwa, au thamani ya mali za kudumu zilizo chini ya himaya zao hawajaonesha uhalisia kwani Serikali nyingi za Mitaa hazikufanya tathimini ya mali hizo. Pia kuna upungufu katika uandaaji na uwasilishaji wa orodha ya salio la vifaa, tahadhari, madeni sanjari, mali, utoaji taarifa kuhusiana kuwepo kwa uhusiano wa kibiashara na uchakavu kama inavyotakiwa na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSAs vifungu Na.12, 14, 19, 20 na 21.)

9.1.7 Kutofuata sheria za manunuzi

Kiasi kikubwa cha rasilimali za Serikali hutumika kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa, huduma, kazi na ushauri. Kwa hiyo ni muhimu kwa Halmashauri kuwa na nidhamu ya fedha na uwazi katika mchakato wa ununuzi ili kufikia kiwango cha juu cha thamani ya fedha.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa hali ya kufuata sheria za manunuzi ya Umma katika matumizi ya Halmashauri bado hairidhishi. Sehemu kubwa ya Serikali za Mitaa haina rasilimali watu wa kutosha, mikataba inaingiwa na Serikali za Mitaa bila ushindani na tathmini kufanyika, na bidhaa kununuliwa bila kuidhinishwa na Bodi za Zabuni. Kwa ujumla, Serikali za Mitaa hazina usimamizi na ufuatiliaji wa kutosha kuhakikisha kwamba manunuzi na michakato ya kimkataba inakidhi thamani ya fedha kwa kufikiwa malengo yaliyopangwa na Halmashauri.

9.1.8 Upungufu wa Walimu na miundombinu ya shule katika shule za msingi na sekondari

Tangu kuanzishwa shule za sekondari za kata, uandikishwaji wa wanafunzi katika elimu ya msingi na sekondari umeongezeka. Ongezeko hilo linakuja na mahitaji makubwa ya kuongezeka kwa idadi ya walimu na miundombinu ya

shule kukidhi ongezeko hilo la wanafunzi kama vile madarasa, nyumba za walimu, maktaba, zahanati, vyoo, ofisi za utawala, mabweni, madawati, viti, meza, na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Idadi ya kutosha ya walimu katika shule, na miundombinu mingine shuleni ni muhimu katika kuleta mafanikio ya wanafunzi na ndiyo inayoamua ubora wa elimu na matokeo mazuri katika shule za serikali.

Nilibaini kuwa Halmashauri zina upungufu wa walimu na miundombinu takribani katika shule nyingi za msingi na sekondari hali ambayo imeathiri sana ubora wa elimu hapa nchini. Tatizo hili limesababisha kushindwa kufikiwa lengo la uwiano wa kitaifa la 1:45 (wanafunzi 45 kwa mwalimu mmoja). Mwenendo unaonesha kwamba walimu wengi hawafiki katika maeneo yao ya kazi hasa maeneo ya vijijini kutokana na miundombinu na huduma duni kama afya, usafiri, malazi na huduma za kijamii za kutosha katika vijiji. Ukosefu wa miundombinu muhimu mashuleni unaweza kuendelea kuathiri ubora wa elimu na uwezo wa wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao.

9.2 MAPENDEKEZO

(a) Serikali za Mitaa zinashauriwa kutathmini upya mchakato wa mandalizi ya bajeti itakayosaidia kupatikana kwa bajeti halisia ambayo inatekelezeka na kuhakikisha mianya yoyote ambayo inapelekea kupatikana kwa hasara kwenye mapato inaainishwa na hatua stahiki zinachukuliwa. Aidha, Serikali za Mitaa zinatakiwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya matumizi halisi dhidi ya bajeti kwenye matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo ili kuwezesha uaandaji wa bajeti halisia.

(b) Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa fedha za matumizi ya kawaida na Maendeleo zinapelekwa katika Serikali za Mitaa kwa wakati na Serikali za Mitaa zinapaswa kuongeza ufuatiliaji na usimamizi katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kupunguza kiwango cha bakaa mwishoni mwa mwaka. Inasisitizwa kwamba, bakaa ya fedha zisizotumika ambazo zinapelekwa mwaka wa mbele lazima zikasimiwe upya au kuingizwa katika bajeti ya mwaka husika na kutumika kwa shughuli zile ambazo hazikukamilika katika mwaka uliopita.

(c) Serikali za Mitaa zinakumbushwa kuomba vibali kutoka kwenye Mamlaka husika kwa ajili ya kubadili mgawanyo wa fedha kama inavyoelezwa katika Agizo 22(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, 2009 ambayo huathiri utoaji wa huduma kwenye jamii iliyokusudiwa.

(d) Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI wanashauriwa kufanya mara kwa mara upembuzi yakinifu wa upatikanaji wa vyanzo vya mapato na fursa mpya ili kubaini vyanzo vikubwa vya mapato kwa ajili ya mipango sahihi na kuhakikisha kwamba mapato kutoka vyanzo vyote yamekusanywa kwa ufanisi. Pia, Serikali za Mitaa zinapaswa kuanzisha mikakati endelevu ya kuongeza wigo wa mapato.

(e) Serikali za Mitaa zinapaswa kupitisha sheria ndogo za vyanzo vyote vya makusanyo ya mapato ya ndani vilivyo ndani ya mamlaka zao ili kuhakikisha kwamba kuna nguvu za kisheria katika ukusanyaji na ufuatiliaji kwa wale wanaokiuka.

(f) Serikali za Mitaa zinatakiwa kuimarisha udhibiti wa ndani wa mapato yaliyobinafsishwa ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi katika mchakato wa kuandaa mikataba ya ukusanyaji wa mapato yaliyobinafsishwa na kuhakikisha kwamba malengo yaliyopangwa yanafikika. Aidha, Halmashauri zinapaswa kuwa na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu kwenye makusanyo ya mapato yaliyobinafsishwa ambapo ni pamoja na mapitio ya utendaji na shughuli za mawakala kwa njia ya uchunguzi wa mara kwa mara na mapitio ya kazi na taarifa zao za fedha.

(g) Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha udhibiti wa ndani wa usimamizi wa rasilimali watu kwa kuboresha mara kwa mara taarifa za watumishi katika mfumo wa taarifa za usimamizi wa rasilimali watu (HCMIS) kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu sahihi za taarifa ya mishahara.

(h) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI inasisitizwa kupitia changamoto zote zinazoikabili "Epicor" toleo la 9.05 na kuja na majawabu endelevu kwani kuna udhibiti mzuri uliotengenezwa katika mfumo wa "Epicor" kukabiliana na mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi ikiwa ni pamoja na uandaaji wa taarifa za fedha na mgawanyo wa kazi katika matumizi ya fedha za umma. Aidha, Serikali za Mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa hatua za mapatano ya kifedha zimeratibiwa vizuri na kufuata sheria na kanuni ikiwa ni pamoja na ngazi za uidhinishaji na utunzaji wa nyaraka.

(i) Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Serikali Kuu kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali wanatakiwa kuchunguza na kufanya maridhiano na benki husika ili

kuhakikisha kwamba fedha ambazo bado zipo katika akaunti za zamani zinahamishiwa kwenye akaunti mpya kama ilivyoagizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Pia Mlipaji Mkuu wa Serikali anapaswa kuwaelekeza na kuidhinisha kufungwa kwa akaunti zote za benki za zamani ambazo bado ni hai na zinatumiwa na Serikali za Mitaa

(j) Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali zinatakiwa kuongeza uwezo wa Serikali za Mitaa katika uandaaji wa taarifa za fedha zinazozingatia matumizi ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta za Umma (IPSAs) kwa njia ya mafunzo. Mbali na hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali zinapaswa kuweka mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa Serikali za Mitaa ili kuhakikisha na kujiridhisha kuwa Serikali za Mitaa kote nchini zinajiunga katika mfumo mpya wa kuandaa taarifa za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSAs)

(k) Serikali za Mitaa zinapaswa kuanzisha udhibiti bora na taratibu za uhakika kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wake kabla ya kuziwasilisha kwa ajili ya ukaguzi.

(l) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inapaswa kufanya mafunzo ya mara kwa mara ili kujenga uwezo kwa wafanyakazi wanaohusika katika maandalizi ya Taarifa za Fedha kutoka Epicor 9.05 kwani toleo la Epicor ni jipya kwa watumishi wengi wa Serikali za Mitaa na ina matumizi mengi yaliyofungamana katika mfumo huo.

(m) Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma(PPRA) na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatakiwa kuimarisha vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi na pia taratibu za manunuzi ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za umma. Serikali za Mitaa zinatakiwa kuanzisha na kuimarisha vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi kwa kuhakikisha kuwa vina watumishi wa kutosha wenye uwezo na sifa ili kusaidia uzingatiaji wa sheria na taratibu za Manunuzi ya Umma

(n) Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na PPRA wanatakiwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wa kitengo cha manunuzi, wajumbe wa Bodi ya Zabuni; Wakuu wa Idara, Maafisa Masuuli na madiwani ili kuwaongezea maarifa kuhusu sheria za manunuzi na majukumu yao kuendana na manunuzi ya umma.

(o) Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa zinapaswa kuanzisha mikakati itakayoboresha miundombinu ya shule ikiwa ni pamoja na kuwa na idadi ya kutosha ya walimu ili kuongeza na kuimarisha ubora na utendaji wa elimu. Pia, Serikali inapaswa kutenga fedha zaidi katika ujenzi wa miundombinu kama vile afya, usafiri na malazi katika ngazi ya vijiji.

(p) Serikali za Mitaa zinatakiwa kuanzisha mpango wa kutekeleza miradi yenye umuhimu kwanza katika jamii ili kuepukana na tatizo la uhaba wa fedha.

(q) Kupitia kwa Wahandisi, Maafisa mipango, Wakaguzi wa ndani na Kamati za uhakiki za Halmashauri, Serikali za

Mitaa zinatakiwa kuimarisha utaratibu wa mfumo wa ufuatiliaji na tathimini ili kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa ufanisi na wakandarasi wote ambao wanatekeleza miradi chini ya kiwango wanapaswa kutolewa taarifa kwenye Bodi ya Usajili ya Wakandarasi ili wachukuliwe hatua stahiki.

(r) Kiasi cha fedha kinachopelekwa Serikali za Mitaa kinapaswa kutumiwa kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo katika ngazi za vijiji.

(s) Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuepuka uwezekano wa kufanyika kwa shughuli zisizo na uhalali zinazoweza kufanywa na wafanyakazi wasio waminifu.

(t) Mapato kutoka vyanzo vyote vya ndani lazima yakusanywe na kupelekwa benki kama ilivyoainishwa katika Sheria ndogo husika.

(u) Bakaa zote kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato zinatakiwa kuwasilishwa katika Halmashauri husika.

(v) Vitabu vyote vya ukusanyaji wa mapato vinapaswa kutafutwa na kurejeshwa pamoja na makusanyo yake.

(w) Uongozi wa Serikali za Mitaa unapaswa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wafanyakazi ambao watashindwa kufuata sheria ya manunuzi.

(x) Uongozi wa Serikali za Mitaa unapaswa kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha kuwa hati zote za malipo zinahakikiwa kwanza kabla ya kufanya malipo.

(y) Fedha zinazotumika kulipia kazi ambazo hazijafanyika zinatakiwa kurejeshwa kwenye akaunti zake husika. Kinyume na hapo zinaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha za umma.

9.3 Mapendekezo kwa Serikali kupitia kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008

Kwa mujibu wa Kifungu 12 cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ningependa kutoa mapendekezo kwa mambo mengine ambapo kama yatatekelezwa itasaidia kuzuia au kupunguza matukio yasiyo na tija katika matumizi ya rasilimali za serikali. Kwa mujibu wa kifungu hicho cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, napenda kuishauri Serikali katika maeneo wawili yafuatayo:

(a) Ukosefu wa taa za barabarani katika makazi yetu ya mijini na

(b) Mfumo usio na ufanisi wa utoaji wa pembejeo za kilimo

Serikali imetumia kiasi kikubwa cha fedha lakini faida inayopatikana kwa wananchi wa Tanzania haifanani na thamani ya fedha iliyowekezwa na Serikali katika maeneo yaliyobainishwa hapo juu.

9.3.1 Taa za barabarani katika Serikali za Mitaa

Malengo ya Serikali za Mitaa nchini ni pamoja na mambo mengine yanajumuisha uendelezaji wa ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa watu wote waliopo ndani ya maeneo yake ya kimamlaka. Chini ya sera na mipango ya kitaifa iliyopo ya maendeleo ya vijijini na mijini, maendeleo ya kijamii na kiuchumi ndani ya maeneo ya kimamlaka ni pamoja na upatikanaji wa taa za barabarani katika maeneo ya mijini.

Uboreshwaji wa taa za barabarani ni dhana muhimu katika kuzuia uhalifu. Wakazi katika maeneo yenye uhalifu sehemu za mijini na vijijini wanahitaji sana taa za barabarani katika maeneo yao kwa kuboresha katika maeneo yenye taa chache na kuweka taa katika maeneo yasiyo na taa kabisa.

Uboreshwaji wa taa za barabarani katika Mamlaka za Miji unaweza kupunguza uhalifu kwa njia zifuatazo:

1. Kuboresha taa kutawaogopesha wahalifu kwa kuingiwa na hofu ya kuonekana wakati wakipanga mipango ya uhalifu.
2. Polisi katika maeneo yenye taa huonekana vizuri hivyo kuwakatisha tamaa wahalifu katika kufanya matukio ya kihalifu.
3. Kuboresha taa kutasaidia kuwakamata na kuwatia hatiani wahalifu wanaofanya makosa mara kwa mara.
4. Kuboresha taa kunafanya miji kupendeza na kunawatia moyo watu wake kutembea, kuendesha na kufanya kazi hata nyakati za usiku. Mfano, kazi za ufagiaji wa barabara na upakiaji na upakuaji wa bidhaa.
5. Ajali zinaweza kuzuiwa na kupunguzwa kama taa za barabarani zitawekwa vizuri na kufanya kazi.

Faida kubwa ya taa za barabarani ni pamoja na kuzuia ajali na kuongezeka kwa usalama kwa wakazi wa maeneo hayo

pamoja na mali zao. Uchunguzi umeonesha kuwa giza hupelekea idadi kubwa ya ajali na vifo, hasa kwa watembea kwa miguu; vifo vya watembea kwa miguu hutokea zaidi mara 3 mpaka 7 gizani zaidi ya kwenye mwanga. Taa za barabarani zimeonekana kupunguza ajali za watembea kwa miguu kwa kadirio la 50%. Uhalifu kama ubakaji, uporaji, uvunjaji wa nyumba hufanyika mara ngingi nyakati za usiku kuliko mchana.

Aidha, sehemu za makutano na njia kuu za kupishana zenye taa za barabarani huwa na ajali chache ukilinganisha na makutano na njia kuu za kupishana zisizo na taa

Aina zifuatazo za taa za barabarani zinaweza kutumika:

a) Taa nyekundu ambazo hutoa mwanga mkali barabarani.

b) Taa za barabarani ambazo huwaka mara tu giza linapoingia au hali yahewa inapokuwa imeambatana na giza.

c) Pia Kuna taa za barabarani ambazo zinatumia nishati ya jua.

Nimetathmini na kuchunguza hali ya taa za barabarani katika Majiji yetu, Manispaa, Miji, na Makao makuu ya Halmashauri za Wilaya zetu nchini na kubaini kuwa sehemu kubwa hakuna taa za barabarani ambapo Majiji na Miji michache ambayo ina taa za barabarani zimekuwa hazifanyi kazi tangu kuwekwa kwake kwa sababu zifuatazo:

(i) Serikali za Mitaa zina tatizo la kifedha kuweza kulipia gharama kubwa za uendeshaji wa taa hizo zinazowekwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

(ii) Kutofanya kazi kwa miundombinu ya umeme katika baadhi ya mitaa ndani ya miji yetu ambayo imeachwa bila kushughulikiwa na Shirika la umeme nchini kwa muda mrefu.
(iii) Kutobadilishwa kwa taa kwenye nguzo za barabarani
(iv) Madereva wazembe kugonga nguzo za taa barabarani

Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI itoe mazingira mazuri kwa Halmashauri zote nchini kuweza kufunga taa za barabarani. EWURA na TANESCO wanapaswa kushauriwa ili kupunguza gharama za nishati inayotumika kuwasha taa hizo. Huduma hii inapaswa kuonekana kuwa ni huduma muhimu ya kiusalama kwa kuwa kila mtu ananufaika nayo likiwemo Shirika la Umeme Tanzania lenyewe. Serikali za Mitaa zinaweza kutumia gharama ndogo za taa za barabarani kwa kununua taa zinazotumia nishati nafuu. Nazidi kupendekeza kuwa, Serikali za Mitaa ziweke taa za barabarani zitakazoweza kutumia nishati ya nguvu ya jua ikiwa kama njia ya kuondokana na tatizo la umeme barabarani.

9.3.2 Mpango wa Taifa wa mfumo wa vocha za Pembejeo

9.3.2.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania ilianzisha utumiaji wa mbolea tangu mwaka 1970 wakati ilipokuwa inatekeleza Mpango wa Taifa wa Mahindi chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo. Baadaye Mpango huu uliendelezwa na kuanza kama mpango wa pembejeo chini ya Mpango wa Taifa wa mfumo wa vocha za Pembejeo.

Mapema mwaka 2000 utumiaji wa pembejeo za kilimo hasa madawa ya kuulia wadudu na mbolea ulikuwa wa chini kwa sababu ya upatikanaji wake. Hali hii iliilazimu Serikali kuchukua hatua katika kurekebisha. Matokeo ya hali hii ni

kwamba katika mwaka 2003/2004 Tanzania ilianzisha tena utaratibu wa mbolea za ruzuku na kuanza kutekelezwa katika nyanda za juu Kusini katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa na Ruvuma ili kuongeza uzalishaji wa mahindi na baadaye kusambaa katika mikoa yote. Katika mwaka 2004/2005 mpango wa kutoa ruzuku ulifanikiwa kitaifa na katika mwaka 2006/2007 mbegu bora za mahindi na mtama ziliingizwa kwenye mpango na pia mpango huu ulielekezwa katika kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao ya mahindi na tumbaku. Mfumo uliongezwa kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbegu bora za mahindi, alizeti na mtama, madawa ya kuulia wadudu kwenye mikorosho, pamba, miche ya kahawa na chai. Awali mpango wa kutoa ruzuku ulilenga kufidia upatikanaji kidogo wa mbolea na gharama kamili za usafiri hadi maeneo teule yatakayotumika kwa ajili ya usambazaji.

9.3.2.2 Utekelezaji na changamoto katika ngazi ya kijiji

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula ilimtafuta mtengenezaji wa vocha na baada ya kuzitengeneza anazisambaza katika mikoa na baadaye zinasambazwa katika Wilaya, Kata na Vijiji. Katika ngazi ya Wilaya huwa kuna kamati inayoundwa na inaitwa kamati ya vocha ya Wilaya chini ya uwenyekiti wa Mkuu wa Wilaya. Kamati ya vocha inateua mawakala ambao watauza pembejeo kwa wakulima katika vijiji. Katika ngazi ya kijiji zoezi la ugawaji wa vocha lipo chini ya Kamati ya Vocha ya Kijiji. Maelekezo yanaonesha kwamba ni lazima pembejeo ziuzwe na wakala kwa walengwa ambao ni lazima wawe wameshateuliwa na uongozi wa kijiji kupitia mikutano ya vijiji. Ili walengwa waweze kutumia vocha za pembejeo wanatakiwa kuzichukua na kwenda nazo kwa wakala ambao watampatia mlengwa pembejeo za kilimo kama inavyoonekana kwenye vocha na mkulima anatakiwa kusaini alichopewa. Mfumo huu wa vocha za pembejeo za kilimo umekuwa na

changamoto kwa wakulima baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na;

- Mfumo umekosa umiliki wa wakulima wadogo wadogo.
- Wakala wa pembejeo kusambaza mbegu za bandia kwa wakulima.
- Baadhi ya viongozi wa vijiji wasio waadilifu wanashirikiana na wakala wa pembejeo kufanya matumizi mabaya ya vocha kwa faida zao.
- Baadhi ya wakala wasio waadilifu wanashirikiana na wakulima kununua vocha kwa bei ya punguzo.
- Baadhi ya wakulima wasio waadilifu kutochukua pembejeo za kilimo badala yake wanaomba kupewa fedha.

9.3.2.3 Changamoto katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Wizara

Utaratibu wowote unaoonekana kuwa mzuri kuna uwezekano ukakutana na changamoto wakati wa utekelezaji. Mfumo wa vocha za pembejeo unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na zifuatazo;

- Ukosefu wa ufahamu na hivyo walengwa kutokuukubali mfumo.
- Ukosefu wa usimamizi wa karibu na ufuatiliaji katika usambazaji wa pembejeo.
- Makampuni ya mbolea kutopeleka mbolea kwa wakati kwenda sehemu zilizokusudiwa.
- Uchaguzi usio sahihi wa mawakala ambao husambaza vocha za mbolea kwa wakulima.
- Kutofautiana kwa kiasi kikubwa kati ya bei ya soko na ruzuku za pembejeo.
- Kutokuwepo kwa bajeti ya kutosha itakayosaidia upatikanaji wa pembejeo za kilimo.
- Ufahamu mdogo wa baadhi ya wakulima juu ya faida za pembejeo za kilimo.

9.3.3 Mapendekezo

Kutokana na changamoto ambazo mfumo wa pembejeo za kilimo umepitia, ninatoa mapendekezo yafuatayo kwa serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula ambayo kama yatatekelezwa yanaweza kupunguza matatizo yaliyoukumba mfumo huu tangu ulipoanzishwa;

- Wizara ya Kilimo na Chakula isijihusishe na uagizaji wa pembejeo za kilimo na kuacha suala hili lifanywe na sekta binafsi. Hii ina maana kuwa Wizara iteue wakala ambao watasambaza vocha za pembejeo moja kwa moja kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushauriana na Sekretariat za mikoa husika.
- Wizara inatakiwa kudhibiti ubora, aina ya vocha za pembejeo za kilimo, majira ya uzalishaji, muda wa uzalishaji kulingana na misimu ya mvua na gharama zinazohusiana na uzalishaji.
- Serikali ihakikishe kwamba Maafisa Ugani wa Kilimo katika vijiji/kata wanakuwepo katika vituo vyao vya kazi na wawezeshwe vizuri kuhakikisha kwamba mfumo huu unaleta manufaa kwa wakulima wadogo wadogo.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa zipewe fedha ili kuziwezesha kuagiza pembejeo kutoka kwa wakala walioteuliwa na serikali kulingana na mahitaji yao.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwe zinafanya mapitio kila mwisho wa majira ya mvua na kuangalia changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mfumo wa pembejeo na kutoa njia za kutatua changamoto zilizoonekana.
- Katika ngazi ya Vijiji, mfumo wa pembejeo uwe unaratibiwa na kusimamiwa na kamati ya usimamizi ambayo itakuwa na hadidu za rejea zilizo wazi na zinazoelezea majukumu yao.
- Afisa Ugani wa Kilimo katika kata/kijiji awe katibu wa kamati ya usimamizi wa pembejeo.

- Kamati hii inapaswa kuwajibika katika kuchagua aina ya vocha za pembejeo za kilimo ambazo zinafaa kununuliwa.

9.3.4. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

Kutokana na faida zilizo onekana hapo juu za taa za barabarani na changamoto zilizopo za mfumo wa utoaji wa pembejeo za kilimo, ninashauri kama ifuatavyo;

(i) Taa za barabarani katika Serikali za Mitaa

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inapaswa kuitisha mkutano utakaohudhuriwa na TANESCO, Serikali za Miji, Benki na wadau wengine ili kuangalia uwezekano wa kuanza kwa mradi huu. Ni vyema pia kwa Serikali kuhusisha wataalam ambao watashauri juu ya;

- Aina gani ya nishati itumike katika kuwasha taa hizo
- Jinsi gani Serikali inaweza kupata fedha za kulipia nishati itakayotumika ili kuhakikisha huduma hiyo inakuwa ya uhakika
- Kiwango gani kitumike katika kulipia gharama za uendeshaji wa nishati itakayotumika
- Uwezekanao wa kutumia ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi katika kuhakikisha mradi unaendelea vizuri. Mashirika ya simu yanaweza kuingia ubia na Serikali kwa kukubaliana kuweka taa hizo huku wakitozwa kodi ndogo kutoka katika Serikali za Mitaa kufidia huduma hiyo.

(ii) Mfumo wa utoaji wa pembejeo za kilimo

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula inashauriwa kuitisha mkutano na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Serikali za Mitaa, Wadau, Vyama vya Wakulima, Benki na vyama vya Ushirika kujadili suala hilo. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kuboresha uzalishaji wa kilimo nchini, Serikali inashauriwa

kuwatumia wataalamu ambao watafanya tathmini juu ya mfumo mzima na kutoa mapungufu na ushauri juu ya;

- Aina ya vocha zitakazotengenezwa kuendana na mazingira mbalimbali na hali ya hewa.
- Usimamizi wa mfumo mzima.
- Aina ya pembejeo zitakazotumika katika mfumo huo.
- Serikali inaombwa kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo ya uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa lengo la kuimarisha ukuaji katika sekta ya kilimo kwa kutoa mikopo, misaada ya kitaalamu na uwekezaji sawa kwa wakulima kwa kuwa wengi wao hawapo karibu na huduma za kifedha zinazotolewa na benki na taasisi nyingine za fedha.
- Serikali inashauriwa kufanya mazungumzo na Chama cha Wakulima Tanzania - (TFA) ili kupanua huduma zake kwa maeneo mengine ya nchi ambapo kwa sasa chama hicho kina matawi Arusha, Karatu, Babati, Moshi, Morogoro, Tanga, Iringa, Njombe, Mbeya, Dar-es-salaam na matawi madogo Mafinga na Mbozi. Malengo ya Chama cha Wakulima ni pamoja na ununuzi na usambazaji wa pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mashine za kilimo, vifaa mifugo, huduma zote muhimu katika kilimo na kuzitangaza bidhaa zinazotokana na mazao ya kilimo. Katika hali hiyo kuna haja ya Chama hicho kupanua huduma zake kwa maeneo mengine ya nchi kama vile Mwanza, Bukoba, Kigoma, Mpanda, Tarime na Kahama.

VIAMBATISHO

Kiambatisho (i)

Makosa yaliyomo kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa katika mwaka 2012/2013

Na.	Halmashauri	Jumla ya matumizi	Jumla ya Makosa			
			Malipo pungufu	% ya Malipo pungufu	Malipo zaidi	% ya Malipo zaidi
1	H/Jiji Arusha	52,768,511,000	232,486,583	0.4	293,221,495	0.6
2	H/W Karatu	21,526,096,549	1,356,824,507	6.3	0	0.0
3	H/W Monduli	15,190,708,000	6,452,820,771	42.5	5,510,504,000	36.3
4	H/W Ngorongoro	16,670,930,810	648,926,764	3.9	590,649,339	3.5
5	H/W Meru	26,880,092,500	38,618,879	0.1	61,089,368	0.2
6	H/W Longido	12,948,931,000	1,659,670,000	12.8	383,654,000	3.0
7	H/W Arusha	32,758,986,340	3,567,277,632	10.9	767,982,899	2.3
8	H/W Bagamoyo	28,340,312,730	82,966,610	0.3	1,882,431,064.0	6.6
9	H/W Kibaha	11,324,979,530	4,588,092,384	40.5	7,833,519,048	69.2
10	H/Mji Kibaha	19,504,936,552	1,437,611,932	7.4	1,518,587,414	7.8
11	H/W Kisarawe	20,561,032,999	292,634,882	1.4	53,820,799	0.3
12	H/W Mafia	7,951,292,000	1,161,040	0.0	15,159,792	0.2
13	H/W Mkuranga	19,078,081,462	976,480,699	5.1	0	0.0
14	H/W Rufiji	18,696,152,097	0	0.0	9,924,651,382	53.1
15	H/M Temeke	65,206,472,245	113,795,221	0.2	64,941,116	0.1
16	H/W Bahi	15,275,839,346	1,308,805,953	8.6	183,851,532	1.2
17	H/W Chamwino	25,052,067,645	283,035,693	1.1	53,517,698	0.2
18	H/W Dodoma	31,029,376,595	3,469,412,624	11.2	2,056,980,898	6.6
19	H/W Mpwapwa	24,879,417,304	757,524,441	3.0	538,012,816	2.2
20	H/W Njombe	33,252,331,974	758,267,817	2.3	126,796,082.0	0.4
21	H/W Njombe	20,361,592,322	157,927,666	0.8	157,927,666.0	0.8
22	H/W Ludewa	18,349,752,676	0	0.0	9,299,816	0.1
23	H/W Makambako	2,195,850,248	162,145,969	7.4	896,459,023	40.8
24	H/W Biharamulo	14,651,011,247	49,768,831	0.3	0	0.0
25	H/W Bukoba	22,132,612,992	460,519,073	2.1	0	0.0
26	H/M Bukoba	17,899,862,688	146,444,497	0.8	0	0.0
27	H/W Karagwe	26,311,473,667	132,906,400	0.5	68,645,400	0.3

28	H/W Muleba	29,303,148,511	0	0.0	475,596,913	1.6
29	H/W Ngara	20,444,736,754	40,396,673	0.2	0	0.0
30	H/W Missenyi	16,316,962,596	61,721,005	0.4	0	0.0
31	H/W Kasulu	35,791,372,549	1,346,256,150	3.8	0	0.0
32	H/W Kibondo	20,435,402,000	7,945,000	0.0	3,033,147,064	14.8
33	H/W Kigoma	32,658,089,000	79,533,236	0.2	52,376,011	0.2
34	H/M Kigoma/Ujiji	16,389,080,000	254,290,080	1.6	0	0.0
35	H/W Hai	20,917,989,987	303,328,874	1.5	632,153,781	3.0
36	H/M Moshi	24,317,762,483	0	0.0	450,495,918	1.9
37	H/W Siha	11,694,347,954	0	0.0	419,728,794	3.6
38	H/W Mwanga	18,555,947,183	6,268,401,627	33.8	6,492,173,104	35.0
39	H/W Rombo	26,740,749,461	8,300,069,231	31.0	4,014,073,164	15.0
40	H/W Same	29,393,861,207	291,507,675	1.0	1,656,153,258	5.6
41	H/W Nachingwea	16,691,852,000	961,503,000	5.8	114,618,000	0.7
42	H/W Babati	24,156,911,000	3,118,606,000	12.9	4,077,164,000	16.9
43	H/W Hanang'	22,907,341,262	2,281,150	0.0	550,375,000	2.4
44	H/W Kiteto	17,467,994,809	897,485,464	5.1	0	0.0
45	H/W Mbulu	28,785,149,000			13,644,000	0.0
46	H/W Simanjiro	13,036,150,197	4,507,008,720	34.6	1,135,173,495	8.7
47	H/Mji Babati	12,950,816,883			111,431,198	0.9
48	H/W Chunya	16,583,327,052	157,906,244	1.0	219,616,633	1.3
49	H/W Ileje	12,972,222,384	91,804,632	0.7	19,792,250	0.2
50	H/W Kyela	21,349,407,972	401,372,257	1.9	521,466,021	2.4
51	H/Jiji Mbeya	53,342,628,000	1,859,586,321	3.5	216,927,415	0.4
52	H/W Mbozi	45,761,798,662	1,233,086,504	2.7	1,471,055,172	3.2
53	H/W Rungwe	35,874,572,555	108,235,989	0.3	1,329,003	0.0
54	H/W Kilombero	29,616,362,444	2,532,623,648	8.6	0	0.0
55	H/W Kilosa	42,890,749,622	189,668,912	0.4	149,338,033	0.3
56	H/W Morogoro	22,876,035,573	11,292,225,398	49.4	1,342,303,525	5.9
57	H/W Ulanga	22,166,424,560	17,411,224	0.1	0	0.0
58	H/W Mvomero	30,326,700,420	4,641,539,690	15.3	0	0.0
59	H/Mji Masasi	3,287,117,357	28,494,175	0.9	90,734,295	2.8
60	H/W Mtwara	17,559,437,000	2,510,906,000	14.3	1,720,816,000	9.8
61	H/M Mtwara	23,963,467,000	5,845,082,000	24.4	2,742,163,000	11.4
62	H/W Newala	19,653,492,999	0	0.0	7,500,447,617	38.2
63	H/W Tandahimba	20,013,010,463	78,829,203	0.4	2,214,586,559	11.1

64	H/W Kwimba	27,086,681,722	2,767,791,706	10.2	2,349,931,799	8.7
65	H/W Magu	36,563,444,322	6,156,020,094	16.8	27,312,033,246	74.7
66	H/W Misungwi	25,626,506,347	338,727,810	1.3	9,180,000	0.0
67	H/W Sengerema	40,493,159,000	2,305,467,000	5.7	13,794,040,063	34.1
68	H/W Ukerewe	21,826,154,607	164,218,824	0.8	100,808,829	0.5
69	H/M Ilemela	10,007,856,231	743,705,778	7.4	138,183,550	1.4
70	H/W Bukombe	21,785,021,143	146,672,417	0.7	0	0.0
71	H/W Nkasi	16,272,520,096	3,600,000	0.0	2,200,000	0.0
72	H/W Sumbawanga	26,040,848,864	2,944,629,983	11.3	1,742,097,027	6.7
73	H/M Sumbawanga	19,462,127,955	405,074,379	2.1	1,106,619,208	5.7
74	H/W Mpanda	34,462,483,000	205,349,000	0.6	12,207,875,000	35.4
75	H/Mji Mpanda	12,412,150,022	6,288,433,707	50.7	0	0.0
76	H/W Mbinga	39,498,124,230	2,414,134,975	6.1	8,466,886,354	21.4
77	H/M Songea	22,391,381,761	245,902,207	1.1	3,290,736,740	14.7
78	H/W Songea	16,905,837,592	5,582,099,713	33.0	464,363,469	2.7
79	H/W Tunduru	22,278,016,817	12,159,698	0.1	488,713,607	2.2
80	H/W Namtumbo	14,764,634,069	37,163,000	0.3	350,887,395	2.4
81	H/W Shinyanga	14,169,205,628	25,772,764	0.2	4,200,522	0.0
82	H/W Bariadi	44,246,216,366	44,000,000	0.1	95,528,797	0.2
83	H/Mji Bariadi	1,564,889,906	100,269,283	6.4	35,773,849	2.3
84	H/W Iramba	29,825,088,000	2,104,191,000	7.1	1,069,840,000	3.6
85	H/W Manyoni	20,978,868,185	653,588,867	3.1	1,667,875,863	8.0
86	H/W Singida	26,574,892,000	2,458,100,000	9.2	589,195,000	2.2
87	H/M Singida	14,634,429,286	479,381,197	3.3	919,856,449	6.3
88	H/W Handeni	16,616,953,839	1,449,056,495	8.7	0	0.0
89	H/W Korogwe	13,469,916,607	684,367,427	5.1	205,602,094	1.5
90	H/Mji Korogwe	9,968,948,656	1,282,348,876	12.9	365,543,922	3.7
91	H/W Lushoto	35,216,529,005	0	0.0	492,187,985	1.4
92	H/W Muheza	18,739,875,046	2,979,846,150	15.9	292,560,146	1.6
93	H/W Pangani	9,160,985,040	744,781,052	8.1	2,057,994,456	22.5
94	H/Jiji Tanga	44,825,102,704	1,707,275,541	3.8	0	0.0
95	H/W Kilindi	10,677,832,289	3,785,439,740	35.5	0	0.0
96	H/W Mkinga	10,731,347,245	348,496,872	3.2	135,256,031	1.3
97	H/W Igunga	25,782,122,076	4,560,494,000	17.7	2,009,337,000	7.8
98	H/W Nzega	23,364,539,978	3,173,946,416	13.6	129,123,940	0.6

99	H/W Sikonge	14,607,903,603	29,346,173	0.2	1,418,667,611	9.7
100	H/W Tabora	14,728,733,927	3,742,691,034	25.4	31,945,204	0.2
101	H/M Tabora	21,987,684,930	855,782,544	3.9	718,493,813	3.3
102	H/W Urambo	22,518,880,350	1,212,244,929	5.4	1,212,244,929	5.4
Jumla (Sh.)		**2,347,629,365,375**	**149,589,875,934**	**6.4**	**159,706,365,768**	**6.8**

Kiambatisho (ii)

Mchanganuo wa ujumla wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka ya fedha 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013

Mkoa	Jina la Halmashauri	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13
Arusha	H/W Arusha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Karatu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Meru	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Longido	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Ngorongoro	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/Jiji Arusha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
	H/W Monduli	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
Coast	H/W Bagamoyo	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H//W Kibaha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/Mji Kibaha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Kisarawe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Mafia	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Mkuranga	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Rufiji/Utete	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
Dar es Salaam	H/M Ilala	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/M Temeke	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/Jiji Dar	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
	H/M Kinondoni	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
Dodoma	H/W Chamwino	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka

Mkoa	Jina la Halmashauri	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13
	H/W Kondoa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Bahi	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Kongwa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Mpwapwa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/M Dodoma	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
Iringa	H/W Mufindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Iringa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
	H/M Iringa	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Kilolo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
Njombe	H/W Ludewa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Njombe	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/Mji Njombe	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Makete	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
	H/Mji Makambako	-	-	-	-	Hati inayoridhisha
Kagera	H/W Biharamulo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Ngara	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Missenyi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Bukoba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/M Bukoba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Muleba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Karagwe	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
Kigoma	H/W Kasulu	Hati	Hati	Hati yenye	Hati	Hati yenye

Mkoa	Jina la Halmashauri	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13
		inayoridhisha	inayoridhisha	shaka	inayoridhisha	shaka
	H/W Kibondo	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Kigoma	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/M Kigoma/Ujiji	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
Kilimanjaro	H/M Moshi	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Hai	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Moshi	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Mwanga	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Rombo	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Same	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Siha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
Lindi	H/W Kilwa	Hati inayoridhisha	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Lindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/M Lindi	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Liwale	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Nachingwea	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Ruangwa	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
Manyara	H/W Babati	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Hanang'	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/Mji Babati	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Mbulu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Mkoa	Jina la Halmashauri	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13
	H/W Simanjiro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Kiteto	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
Mara	H/W Serengeti	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Musoma	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Bunda	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/M Musoma	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
	H/W Rorya	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
	H/W Tarime	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
